

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Ishirini na Saba – Tarehe 11 Mei, 2018**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaanza na Kikao chetu cha Ishirini na Saba katika Mkutano wetu huu wa Kumi na Moja, Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:-**

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Swali la kwanza ni namba 222 na linaulizwa na Mheshimiwa Martin Masuha, Mbunge wa Mbinga Vijijini na linaelekezwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Na. 222

**Kupitia Mapitio Baadhi ya Maeneo ya Kiutawala**

**MHE. MARTIN M. MSUHA** aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya mapitio ya mipaka ya baadhi ya maeneo kama vile mikoa, wilaya na majimbo ya uchaguzi kwani baadhi ya mipaka ya maeneo hayo yana muingiliano unaoleta ugumu wa utoaji wa huduma za jamii?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuligawa Jimbo la Mbinga Vijijini kwa kuzingatia ukubwa wake wa kata 29?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Mheshimiwa Kakunda.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martin Alexander Mtonga Msuha, Mbunge wa Mbinga Vijijini, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kufanya mapitio ya mipaka kwa baadhi ya mikoa, wilaya na majimbo ya uchaguzi hasa yenye muingiliano unaosababisha ugumu wa utoaji wa huduma za jamii. Hata hivyo, zoezi hilo ambalo linaweza kusababisha mapendekezo ya maeneo mapya ya utawala au

kuyahamisha mengine litafanyika baada ya kukamilisha miundombinu ya majengo ya ofisi, majengo ya huduma mbalimbali na vifaa katika mikoa, wilaya na halmashauri mpya zilizoanzishwa tangu mwaka 2012.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ibara ya 75 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imepewa mamlaka ya kuyagawa majimbo ya uchaguzi kwa kuzingatia vigezo vya idadi ya watu, jioografia, hali ya mawasiliano, ukubwa wa jimbo na uwezo wa ukumbi wa Bunge. Ili jimbo ligawanywe Tume hutoa tangazo kuhusu nia hiyo. Baada ya tangazo, mapendekezo hujadiliwa katika vikao vya halmashauri, Kamati ya Ushauri ya Wilaya na Mkoa na hatimaye huwasilishwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambayo hutangaza Jimbo jipya baada ya kupata kibali cha Rais.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Msuha.

**MHE. MARTIN M. MSUHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Hata hivyo, nitakuwa na maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, wataalam wakati wa kuweka mipaka katika baadhi ya maeneo wamekuwa wakishirikisha upande mmoja badala ya kushirikisha pande zote mbili na hivyo kusababisha migogoro ya mipaka katika maeneo hayo hususani mipaka ya vijiji vyetu. Je, nini kauli ya Serikali ili kuondoka na tatizo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kule Jimboni kwetu Mbinga Vijijini kuna migogoro ya mipaka kati ya Vijiji vya Kilagano, Lugagala na Liganga ambavyo vipo Jimbo la Peramiho, Songea Vijijini. Upande mwingine mgogoro huo unasisha Kijiji cha Litumbandyosi, Mabuni pamoja na Luhugara kwa upande wa Jimbo la Mbinga Vijijini. Je, lini Serikali itashuka ili kwenda kutatua mgogoro huo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kakunda kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza kwamba wataalam wamekuwa hawashirikishi pande zote zinazohusika kwenye maeneo ya utawala, hilo ni tatizo na tumeshawapa maelekezo kwa sababu ya migogoro ambayo imesababishwa na kadhia hiyo. Hapa nchini tunayo jumla ya migogoro 366 ambayo imebuliwa na Kamati ile ya Pamoja ya Wizara mbalimbali ambayo sasa hivi inashughulikiwa. Sasa hivi tumeshawaelekeza wataalam wetu wale wanaoratibu, wakienda kwenye eneo lolote watakapoanza upimaji upya lazima washirikishe pande zote mbili au pande zote zinazohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili kuhusu migogoro inayoendelea chini ya uratibu wa Wizara ya Ardhi kitaifa, migogoro yote nchini imeanza kushughulikiwa tangu mwezi Aprili, 2018 na tunaimani mpaka mwisho wa mwaka huu migogoro yote itakuwa imeshughulikiwa ile ya kijiji kwa kijiji, kata kwa kata, wilaya kwa wilaya, mkoa kwa mkoa, maeneo ya wananchi na maliasili na maeneo mengine yote ambayo yana migogoro tuna imani kwamba mpaka mwisho mwa mwaka huu yatakuwa yametatuliwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Mheshimiwa Mariam Kisangi na Mheshimiwa Nsanzugwanko. *(Makofi)*

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Naomba kuuliza, hivi haionekani kwamba wanapokuja wataalam wa TAMISEMI kugawa upya vijiji na hata vitongoji wanaleta migogoro ambayo haiishi na maendeleo kusitishwa? Je, Waziri anasema nini kwa migogoro ambayo ipo na imewadhuru watu ambao wako kwenye maeneo hayo?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye maswali ya nyongeza ya muuliza swali la msingi, migogoro yote inashughulikiwa isipokuwa kuna baadhi ya maeneo ambayo kulikuwa na matatizo ya usajili wa vijiji na vitongoji ambapo baada ya kupitia upya taratibu imeonekana kwamba kuna baadhi ya maeneo taratibu zilikiukwa.

Kwa hiyo, kule ambako taratibu zilikiukwa, pengine usajili wa kijiji au kitongoji ulipenyezwa bila kufuata utaratibu rasmi wa Serikali, maeneo hayo baadaye yamefanyiwa marejeo ya kufuta usajili wa kijiji au kitongoji. Kwa hiyo, suala hilo likishafanyika inakuwa siyo mgogoro tena. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge kama kuna migogoro ya aina hiyo basi tuwasiliane ofisini kwa Katibu Mkuu wa TAMISEMI ili kuweza kufuatilia vizuri zaidi na kurekebisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mariam Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa matatizo ya Mbinga Vijijini yanafanana kabisa na matatizo ya Jimbo la Mbagala katika Mkoa wa Dar es Salaam. Jimbo la Mbagala sasa hivi lina watu takribani watu 1,100,000. Idadi hii ya watu ni kubwa sana kiasi kwamba utoaji wa huduma katika jimbo hili unakuwa mgumu na miundombinu inaharibika mara kwa mara kutokana na wingi wa watu waliopo katika eneo hilo. Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kuligawanya Jimbo hili la Mbagala ili liweze kufikika na hata Mbunge aweze kutoa huduma zake kwa wakati?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa

Mwenyekiti, kwanza huyu ni ndugu yangu kabisa katika ukoo. Ni kweli Jimbo la Mbagala kwa idadi ya watu ni miongoni mwa majimbo yenye watu wengi ikiwemo Temeke na majimbo mengine hasa ya Dar es Salaam, lakini hivi karibu tumegawa majimbo ya Dar es Salaam. Kwa hiyo, nashauri kwa vigezo vile ambavyo nimevizungumza kwenye jibu la msingi, naomba sasa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke wakae ili waweze kupendekeza, lakini wapeleke mapendekezo yao moja kwa moja Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nsanzugwanko.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nami nina swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugawaji wa maeneo ya utawala ngazi ya kata, tarafa na mitaa yaliyokosewa sana au kusahaulika katika Wilaya ya Kasulu. Unakuta kijiji kimoja chenye wakazi 10,000 ni mtaa mmoja, kijiji chenye wakazi 12,000 ni mtaa mmoja. Nina mifano halisi, kwa mfano wa Kijiji cha Nyantale ni kimoja na mtaa ni huo huo. Je, maeneo yaliyokosewa na kusahaulika ni lini sasa TAMISEMI wanakwenda kurekebisha kasoro hizo kwa sababu hazihitaji miundombinu wala uwekezaji wowote?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ni lini mtasahihisha makosa hayo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kwamba kuna baadhi ya maeneo wakati wa kutenga maeneo hayo yaliyokosewa, vigezo havikuangaliwa vizuri. Kwa sasa hivi kulingana na *payroll* iliyopo Serikalini ambayo bado tunaendelea kuirekebisha itakuwa vigumu sana ndani ya miaka hii miwili kumuahidi kwamba tutarekebisha mwaka ujao au mwaka 2020. Naomba sana wananchi katika maeneo hayo waweze kuwa

na uvumilivu, kwa nchi nzima zoezi hilo litafanyika baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na swali namba 223 na linaulizwa na Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum na linaelekezwa ofisi hiyo hiyo ya Rais, TAMISEMI.

Na. 223

**Ubovu wa Miundombinu ya Barabara  
katika Jimbo la Segerea**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST** aliuliza:-

Jimbo la Segerea ni kati ya majimbo yaliyosahaulika katika miundombinu ya barabara na kupelekea mitaa mingi kuwa na madimbwi sugu na mafuriko kila mvua inaponyesha. Kadhia hii imepelekea barabara za mitaa kupitika kwa taabu na kupelekea foleni kubwa katika barabara ya Segerea mpaka barabara ya Mandela kwa kuwa ndiyo barabara pekee inayotumiwa na wananchi.

Je, ni lini jimbo hili litatengewa bajeti kwa barabara zake za mitaa kwa kiwango cha lami, changarawe na ujenzi wa mifereji?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu tafadhali Mheshimiwa Kandege.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya barabara inayoendelea kutekelezwa kwa kiwango cha lami

sambamba na mifereji katika Jimbo la Segerea ina thamani ya shilingi bilioni 4.6 ambapo Halmashauri ya Manispaa ya Ilala imetoa shilingi bilioni 2.6 na shilingi bilioni 2.0 zimetolewa na Mfuko wa Barabara. Miradi ya barabara inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na barabara za Mnyamani kilometa 2.3 kwa shilingi bilioni 2.5; Tabata Barakuda – Chang’ombe kilometa 0.5 kwa shilingi milioni 744 na Tabata – Kimanga – Mazda kilometa 0.8 kwa shilingi bilioni 1.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Jimbo la Segerea limetengewa shilingi milioni 880 ambapo kati ya fedha hizo shilingi milioni 380 zitatengeneza kwa kiwango cha changarawe barabara za Bonyokwa – Kisukuru- Majichumvi; Tabata – Mawenzi – Kisiwani; Chang’ombe – Majichumvi; Chang’ombe - Mbuyuni, Guest Nyekundu – Jumba la Dhahabu na shilingi milioni 500 zitatumika kufanya usanifu na ujenzi wa madaraja ya Mongolandege na Nyebulu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nadhani waliomwandikia Mheshimiwa Naibu Waziri hawakunielewa vizuri. Swali langu nimeuliza hivi, ni kwa kiwango gani barabara za mitaa ina maana kutoka barabara ya Segerea kwenda *Mandela road* tutaweza kupunguza foleni. Kwa maana tutafungua vipi barabara za mtaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameainisha kwamba wametenga fedha ya ujenzi wa barabara kutoka Barakuda - Chang’ombe, sasa ukitoka Barakuda - Chang’ombe bado hawajapunguza foleni. Wangesema kutoka Barakuda - Chang’ombe - Kimanga ili wananchi wapite Kisiwani wasiingie *Mandela road*. Vivyo hivyo kutoka Kinyerezi - Kimara watu waingie *Morogoro road* wasirudi barabara ya Segerea, tuna changamoto sana ya foleni. Vivyo hivyo ...

**MWENYEKITI:** Swali.



**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali ni lini barabara ya Segerea itapunguziwa foleni kwa kuboresha barabara za mitaa zinazotoka na siyo kurudi barabara kwenye moja? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, wamesema wametenga fedha kwa ujenzi wa daraja wa Tabata Kisiwani. Namwomba Naibu Waziri aje tumuonyesha daraja hilo kwa sababu lina changamoto kubwa. Matajiri wamevamia eneo, daraja haliwezekani kwa sababu mkondo ni mdogo. Ni lini atakuja kuona changamoto ili kuwaondoa wale watu tuweze kujenga daraja pale? Vinginevyo ni kupoteza fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu langu la msingi nimeeleza barabara ambazo zinatengenezwa na tafsiri yake ni nini? Mwananchi ambaye alikuwa anataka kwenda Segerea ana-*option* ya kutumia barabara ya zingine na ambacho kimekuwa kikitokea ni kwamba hizi barabara zikiwa mbovu sana hata ambaye angeweza kupita kwa Mnyamani hawezi kupita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kadri barabara hizi zingine zinavyotengenezwa inampa nafuu mwananchi wa maeneo hayo. Si kwamba gari zote ambazo zinazopita huko wanataka ni kwa sababu barabara za mtaani zinakuwa siyo nzuri. Aidha, kwa Jiji la Dar es Salaam kuna mpango kabambe wa kuhakikisha kwamba tunali-*decongest*, mpango uko vizuri, naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira hilo liko mbioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusiana na daraja ambalo analizungumzia na kuuliza nitakwenda lini, *weekend* iliyopita nilienda nikafika mpaka Mnyamani bahati mbaya tu Mheshimiwa Mbunge hakuwa na taarifa. Mimi niko tayari

kwenda kwa kadri nafasi itakavyoruhusu ili tukatizame *site* kuona nini kilichopo ili tuweze kushauri vile ambavyo inatakiwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mussa Zungu.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mbunge wa Segerea, Mheshimiwa Bonnah Kaluwa kwa kazi nzuri za miundombinu anazofanya kwenye jimbo lake. Hivi karibuni alikuwa na ziara na Waziri wa Ujenzi kutazama miundombinu kwenye jimbo lake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Segerea na Mkoa wa Dar es Salaam, naomba kujua ni lini sasa Serikali itaweka mkazo kwenye barabara za Jimbo la Ilala ambalo ndilo linabeba magari yote kutoka maeneo yote ya Mkoa wa Dar es Salaam? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu tafadhali Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Naibu Waziri, TAMISEMI kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Zungu kwa kufuatilia kwa pamoja na maeneo mengine. Kama alivyosema nimekuwa na ziara Segerea Jumamosi, nimezitembelea barabara ambazo pia ziko chini ya *TARURA* ili kuweza kuona changamoto zilizopo ili kwa upande wa Serikali tuweze kuona namna sahihi ya kuweza kuzitatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme tu kwa maana ya kupunguza msongomano katika Jiji la Dar es Salaam hususani Ilala, kama tulivyopitisha bajeti tunaendelea na ule mkakati wa kupunguza msongomano. Tutakuwa na *BRT III*

na IV lakini pia ipo mbioni BRT V na VI ili hatimaye msongamano katika Jiji la Dar es Salaam uweze kuondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge avute subira na wakati mwingine tunaweza kupeana mrejesho ili aone namna tulivyojipanga. Kwa kweli BRT I na II imefanya vizuri na imekuwa na rekodi nzuri kitaifa na watu na mashirika mengi yapo tayari kuja ku-support tutakwenda mpaka BRT V na VI.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Tatizo lililopo katika Jimbo la Segerea linafanana pia na lililopo katika Jimbo la Temeke ambapo katika Kata za Buza, Tandika na Kata 14 Temeke barabara zimeharibika sana na hasa baada ya mvua hizi. Kwa kuwa kata hizi hazipo katika ule mpango DMDP, nilitaka kujua Serikali ina mpango gani kwenda kukarabati barabara za mitaa katika kata hii angalau kwa kiwango cha changarawe?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kandege.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHATS. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba baada ya mvua kunyesha maeneo mengi miundombinu yake imeharibika na hasa kwa Jiji la Dar es Salaam ambapo mvua zimenyesha nyingi sana.

Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafanya tathmini ya uharibifu uliotokea ili tujue hatua za dharura za kuchukua ili wananchi waendeleo kutumia barabara katika hali nzuri.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata na linaulizwa na Mheshimiwa Frank Mwakajoka, Mbunge wa Tunduma na linaelekezwa kwa Waziri wa Madini.

Na. 224

**Ruzuku kwa Wananchi wa Mji wa Tunduma**

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA** aliuliza:-

Je, ni kwa nini Serikali haiwapatii wananchi wa Mji wa Tunduma ruzuku ya asilimia 0.3 kama ilivyo kwa wananchi wanaoishi katika maeneo yenye kuchimbwa madini?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Nyongo.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Frank George Mwakajoka, Mbunge wa Tunduma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 yaani *Local Government Finance Act, Cap. 290*, kifungu cha 6(1)(u), Halmashauri ulipo mgodi hutoza asilimia 0.3 ya mapato yote kabla ya kuondoa gharama za uzalishaji wa madini kama ushuru wa huduma yaani *service levy*. Aidha, kabla ya kuanza kutoza ushuru huo, Halmashauri husika inatakiwa kutunga Sheria Ndogo ya Halmashauri yaani *District Council By-Laws* ambazo zinaidhinishwa na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa yaani TAMISEMI kwa mujibu wa kifungu cha 153(1) cha Mamlaka ya Serikali Mitaa yaani *Local Government District Authority Act, Cap. 287*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, eneo la Halmashauri ya Tunduma hakuna leseni ya uchimbaji iliyotolewa. Hivyo, tunaendelea kuhimiza wawekezaji wa ndani na nje ili wawekeze katika utafiti na hatimaye kuanza kuchimba madini katika maeneo mbalimbali yenye madini nchini na Tunduma ikiwa mojawapo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa kigezo cha kutoa asilimia 0.3 kwenye Halmashauri ambazo kuna kazi za uchimbaji unaofanywa na migodi inatokana na athari ambazo wananchi wa maeneo hayo wanapata. Katika Mji wa Tunduma kuna forodha ambayo inahudumia nchi karibu nane Kusini na Kati mwa Afrika na kumekuwa na madhara mengi sana kwenye mpaka wa Tunduma ambayo yanafanana kabisa na maeneo wanayochimba migodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, kuna magonjwa ya UKIMWI lakini kuna miongamano mkubwa sana wa magari na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi wangu ambao wanashindwa kutekeleza majukumu yao ya kimaendeleo vizuri.

Je, Serikali haioni kwamba sasa ni muda muafaka kuona na sisi kama Halmashauri ya Tunduma tunaweza kupata asilimia 0.3 ya ruzuku kama ambavyo wanapata katika maeneo ambayo wanachimba migodi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waziri wa Madini, Mheshimiwa Kairuki.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na nipende kujibu swali la Mheshimiwa Mwakajoka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kama ambavyo kifungu cha 6(1)(u) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa kinavyoeleza, fedha hii ya ushuru wa huduma si kwa ajili ya madhara ni kwa ajili ya wao kupata stahiki ya huduma mbalimbali na mapato yaliyotokana na shughuli za uchimbaji. Kama ambavyo tumeeleza, kwa upande wa Tunduma bado hakuna leseni ya uchimbaji madini ambayo ilitolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa ufuatiliaji tumekuwa makini kufuatilia kutaka kujua kwa nini Mheshimiwa Mbunge amekuwa akitaka kuulizia suala hili. Tumefuatilia katika eneo la Mkombozi na Chapwa ambapo katika eneo la Chapwa kulikuwa na shughuli za uchimbaji wa madini ya ujenzi ya kifusi, lakini yalikuwa yakichimbwa kwa ajili ya upanuzi wa barabara. Kwa sasa tunachokifanya tumeanza kurasimisha ili leseni ziweze kutolewa kwa wale ambao waliokuwa wakichimba kwa kificho basi waweze kuingia katika shughuli hizo za uchimbaji kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu na waweze kugaiwa leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge asubiri tu, leseni zitakaporasimishwa kwa wachimbaji wale katika eneo la Chapwa pamoja eneo la Mkombozi basi wataweza kupata ushuru huu wa huduma au *service levy*.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Joseph Mkundi na Mheshimiwa Bilago.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maeneo ambapo shughuli nyingi za uvuvi zinafanyika kunapatikana athari za kijamii za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja. Kama ilivyo kwenye maeneo zinapofanyika shughuli za uchimbaji wa madini ambapo maeneo yanayozunguka migodi hii yanapata mrahaba kama sehemu fulani ya ku-*recover* athari hizi.

Je, Serikali haioni sababu sasa sheria hii iweze kutumika kwenye maeneo ambako shughuli za uvuvi zinafanyika na kusababisha athari mbalimbali za kijamii kwa ajili ya ku-*recover* sehemu ya athari hizi? Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ameulizia suala la kupata *service levy* kutokana na uvuvi katika Ziwa Victoria. Naomba niseme tu suala la uvuvi haliko katika Sheria ya Madini ambayo tunaisimamia sisi. Nadhani ni vema Mheshimiwa Mbunge akaifuatilia Sheria ya Serikali za Mitaa kuona kama kuna stahiki ambayo unaweza ukaipata kutokana na masuala ya uvuvi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bilago kwa kifupi.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilileta swali hapa Bungeni ili kujua maeneo yenye madini katika Wilaya ya Kakonko. Maeneo yaliyoanishwa na Serikali katika majibu yake ni pamoja na chokaa iliyoko eneo la Nkogongwa, dhahabu iliyoko Ruhuru Nyakayenzi na Nyamwilonge. Baada ya kuwa maeneo hayo yametambulika wananchi walichangamkia wakataka kuchimba madini lakini ghafla Serikali ikasitisha leseni za uchimbaji.

Ninachotaka kujua ni lini Serikali itafungua utoaji wa leseni kwa wachimbaji wadogo wadogo wa Wilaya ya Kakonko ili waweze kuanza uchimbaji? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Naibu Waziri, Wizara ya Madini, Mheshimiwa Nyongo, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. STANSLAUS H. NYONGO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mabadiliko ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na mabadiliko yake ya mwaka 2017 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2018, ni kwamba sasa hivi Tume ya Madini ambayo imeundwa ndiyo itakuwa na wajibu wa kutoa leseni kwa wachimbaji wakubwa, wadogo na wachimbaji wote wa kati. Ni juzi tu Mheshimiwa Rais ndiyo ameteua Mwenyekiti wa Tume ya Madini ambayo sasa ndiyo inaendelea na michakato ya kuchakata kwa maana ya kutoa leseni kwa watu wote

walioomba leseni za kuchimba madini. Kwa hiyo, nimueleze Mheshimiwa Mbunge aendelee kuhamasisha wachimbaji wake waombe leseni na sasa Tume imeanza kufanya kazi, watapata leseni walizoomba na wataendelea na uchimbaji. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mbunge wa Mtera na linaelekezwa kwa Waziri wa Maliasili na Utalii.

Na. 225

### **Uharibifu Unaofanywa na Tembo Mtera**

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani juu ya wanyama waharibifu hususan tembo ambao wamesambaa hovy katika Jimbo la Mtera na kufanya uharibifu mkubwa pamoja na kua watu?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu, Mheshimiwa Hasunga, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii napenda kujibu swali la Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, Mbunge wa Jimbo la Mtera kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wanyamapori wakali na waharibifu limekuwa likijitokeza kwenye Wilaya zaidi ya 80 hapa nchini. Wanyamapori wakali na waharibifu ambao kwa kiwango kikubwa wamekuwa wakileta madhara kwa maisha ya binadamu na uharibifu wa mazao yao kisheria ni tembo, mamba, nyati, kiboko, simba, fisi na faru.



*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la watu limesababisha kuzibwa kwa shoroba za wanyamapori pamoja na maeneo ya mazalia na mtawanyiko wao. Kuzibwa kwa shoroba hizo kumeongeza migogoro baina ya binadamu na wanyamapori. Hali hiyo kwa ujumla wake imeongeza ukubwa wa tatizo la mwingiliano kati ya binadamu na wanyamapori hususan tembo na hivyo kusababisha matukio mengi ya uharibifu wa mali na upotevu wa maisha ya binadamu katika maeneo mbalimbali likiwemo Jimbo la Mtera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali itaendelea kufanya doria za kudhiti wanyamapori katika maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Chamwino. Pia Wizara itaendelea kutoa elimu ya njia nyingine za kudhibiti tembo zikiwemo matumizi ya mizinga ya nyuki, uzio wa kamba uliopakwa mchanganyiko wa pilipili na *oil* chafu kuzunguka mashamba na kuchoma matofali ya kinyesi cha tembo kilichochanganywa na pilipili. Moshi unaotokana na uchomaji wa matofali ya kinyesi chenye pilipili ni mkali na hivyo hufukuza tembo mashambani kwa mafanikio makubwa. Njia hizi mbadala zimeonesha mafanikio makubwa pale zinapotumika vizuri na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na mikakati hiyo, Serikali itaendelea kutoa fedha za kifuta jasho kwa uharibifu wa mali, yaani mazao na mifugo na kifuta machozi kwa wahanga waliouwawa au kujeruhiwa na wanyamapori hao. Kwa mfano, mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara yangu imelipa jumla ya shilingi 7,520,000 kwa wananchi 27 wa Wilaya ya Chamwino walioathirika na wanyamapori.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lusinde.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia kuuwawa kwa Ndugu Emmanuel Ernest wa Ilolo na Stefano Ndalwa wa Nhinyi na Amani Joseph Sita wa *Mvumi Mission* kujeruhiwa vibaya na kupata malipo kidogo sana, je, ni lini sasa Serikali itaruhusu vijiji viweze kumiliki silaha kwa ajili ya kujilinda na wanyama hao wakali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, pesa aliyoitaja Mheshimiwa Naibu Waziri kuwa imelipwa kwa watu 27 ukiigawanya ni sawasawa na shilingi 278,518. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kuwatangazia Watanzania kwamba katika nchi yetu tembo wana thamani kubwa kuliko uhai wa watu? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajibu maswali hayo, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Livingstone Lusinde kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya katika kufuatilia na kuwatetea wananchi wake. Kutokana na kazi yake ndiyo maana anajulikana kama kibajaji yaani kwa mambo makubwa anayoyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie nafasi hii kuwapa pole wale wananchi wote ambao wameathirika ama wameuwawa na wanyama wakali, nawapa pole sana. Niseme tu kwamba hili suala alilolileta na kupendekeza kwamba tutoe silaha kwa wananchi na hasa katika vijiji kuweza kumiliki silaha, basi pale tutakapokuwa tunapitia sheria, pamoja na kanuni hizi tutaliangalia kama hilo litawezekana ili kusudi tuone kama linaweza kusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili alilouliza ni kwamba kwa mujibu wa Kanuni za Kifuta Jasho na Kifuta Machozi za mwaka 2011 ndiyo vinatoa viwango vile vinavyostahili. Nataka niseme kwamba tunachotoa siyo fidia, ni kifuta machozi na kifuta jasho. Ndiyo maana imeandikwa kabisa kwamba kifuta jasho kama binadamu

ameuwawa ni shilingi 1,000,000, kama amejeruhiwa ni shilingi 500,000, kama ni mazao yana viwango vyake kufuatana na kilometa. Kwa hiyo, hivi viwango vipo kwa mujibu wa sheria, lakini pale tutakapokuwa tunapitia tutavihuisha na kuona kama kuna haja ya kuvirekebisha ili kusudi vikidhi mahitaji ya wakati uliopo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Vulu atafuatiwa na Mheshimiwa Kalanga.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na napongeza majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nilitaka kujua, je, ni kwa kiasi gani Serikali imejipanga kuhakikisha inatoa pilipili nyingi ili kuweza kuchoma na kukimbiza tembo hao kwenye maeneo wanayoishi watu hasa ukizingatia kwamba kwanza kuchoma moto misitu ni kuharibu mazingira?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulichosema ni kwamba katika maeneo yale yanayozunguka hifadhi zetu au yale ambayo yapo jirani na hifadhi zetu tunajaribu kuwahamasisha wananchi kwamba wapande pilipili na pia pale ambapo pana kinyesi cha tembo tunakichukua kile tunachoma. Nataka niseme kwamba tutaangalia namna na tutazungumza mikakati ambayo tumeiweka katika kuhakikisha kwamba pilipili zinatoshwa katika maeneo hayo hasa pale tutakapowasilisha bajeti yetu hapo tarehe 21 na 22 Mei.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kalanga.

**MHE. JULIUS K. LAIZER.** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Tatizo hili la tembo katika nchi yetu limekuwa likiwasababishia Watanzania umaskini mkubwa sana na mkakati wa Wizara hauoneshi kama kuna jitihada nzuri ya kushughulikia jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nauliza swali hili jana usiku tembo wamevamia mashamba ya wananchi zaidi ya ekari 20 na kumaliza kabisa na ni kilomita zaidi ya 20 kutoka eneo la hifadhi. Je, Serikali ina makakati gani wa haraka katika kipindi hiki cha mvua na cha mazao yetu ili kusaidia wananchi kuwaondoa tembo hao waache kuharibu mazao yetu?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii, majibu tafadhali, ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kumekuwa na matukio ya tembo katika maeneo mengi hapa nchini na hii imetokana na kuimarika kwa uhifadhi katika maeneo mengi na hivyo tembo wameongezeka. Pale ambapo pametokea tatizo la namna hiyo tunaomba tuwasiliane haraka ili kusudi askari wetu wa doria waweze kwenda na kuchukua hatua na kuwafukuza tembo hao ili warudi katika hifadhi pale ambapo wanastahili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Edwin Ngonyani.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Tatizo la Mtera halina tofauti kabisa na tatizo la kata nzima ya Likuyu Sekamaganga na hususan Kijiji cha Mandela. Walioathirika walishafanyiwa tathmini muda mrefu na hakuna dalili ya kuwalipa hicho kifuta jasho na kifuta machozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itatoa hicho kifuta jasho na kifuta machozi kwa wale walioathirika katika Vijiji vya Mandela, Likuyu Sekamaganga, Mtonya pamoja na majirani zao wa Mgombasi?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii, ni lini mtawalipa wananchi hao kifuta jasho?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kumekuwa na matukio mengi katika lile Jimbo la Tunduru na maeneo mengine pamoja na kile Kijiji cha Mandela. Naomba nilitaarifu Bunge lako tukufu kwamba matukio haya ya wanyama waharibifu ni mengi sana katika nchi yetu kwa sasa hivi. Hili inatokana na kwamba uhifadhi umeimarika na wanyama wameongezeka lakini pia kuna changamoto nilizozisema nilipokuwa najibu swali la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kuna matukio zaidi ya 3,509 ambapo wananchi wamepatwa na matatizo mbalimbali. Jumla ya fedha ambazo zinadaiwa mpaka sasa hivi katika maeneo na wilaya mbalimbali ni zaidi shilingi milioni 828. Kwa hiyo, kazi tunayoifanya sasa hivi ni kutafuta hizi fedha ili kuhakikisha kwamba hao wananchi wote walioathirika na wanyamapori na wanyama waharibifu basi waweze kupata kifuta jasho na kifuta machozi kinachostahili. Baada ya kupata fedha hizo tutafanya hivyo mara moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata na linaulizwa na Mheshimiwa Ritta Ernest Kabati, Mbunge wa Viti Maalum na linaelekezwa kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa Kabati.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali langu. Naomba sasa swali 226 liweze kupatiwa majibu na Serikali pamoja na kuwa kuna masahihisho katika jina, naitwa Ritta Enespher Kabati. Sasa naomba Serikali inipe majibu.

**MWENYEKITI:** Jina la katikati unaitwa nani?

**MHE. RITTA E. KABATI:** Enespher.

**MWENYEKITI:** Enespher?

**MHE. RITTA E. KABATI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Wamekosea hapa, ni Enespher.

Na. 226

### **Mradi wa Machinjio ya Kisasa wa Ngerewara**

**MHE. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Mradi wa machinjio ya kisasa wa Ngerewara uliopo Manispaa ya Iringa umekuwa ni wa muda mrefu sana toka umeanza.

Je, ni lini Serikali italeta fedha za kutosha ili kumaliza mradi huo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi na mjukuu wangu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa machinjio ya kisasa wa Ngerewara unatekelezwa na Halmashauri ya Manispaa ya Iringa kwa kushirikiana na wadau wengine. Mradi ulianza kutekelezwa mwaka 2008/2009 na ulikadiriwa kugharimu shilingi za Kitanzania 1,900,000,000. Aidha, mpaka sasa kiasi cha shilingi 928,000,000 zimetumika kugharamia mradi huu kupitia Serikali Kuu, Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, Mradi wa *ASDP* na Shirika la Maendeleo la Viwanda la Umoja wa Mataifa ambalo lilisaidia kuweka vifaa vya machinjio vikiwemo mashine za kuchakata nyama na vyumba viwili vya kuhifadhi ubaridi (*cold rooms*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa sehemu kubwa ya miundombinu inayohitajika kwa ajili ya machinjio imekamilika. Aidha, kiasi cha shilingi 1,090,000,000 zinahitajika

kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa zizi, mabwawa matatu ya maji machafu na maji safi, uzio wa machinjio, tanuru la kuchomea taka kwa maana ya *incinerator*, jengo la ofisi za utawala, vyoo, jiko na kisima cha maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itashirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Iringa kuhakikisha fedha za kukamilisha machinjio ya Ngerewara zinapatikana ili Watanzania wapate ajira na bidhaa abora za mifugo na kuongeza pato la Halmashauri na Taifa kwa ujumla wake.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali madogo ya nyongeza. Kwanza nianze kumshukuru Waziri kwa majibu yake, lakini naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa huu mradi ni muhimu sana na una tija sana katika manispaa yetu na ni mradi ambao kwa kweli toka mwaka 2008 umeanzishwa na ni chanzo kizuri sana cha mapato kama ambavyo amesema kwenye jibu lake. Pia tulikuwa tunategemea kwamba kama ungekamilika, ungeweza kutoa ajira zaidi ya 200 katika Manispaa na katika Mkoa mzima wa Iringa. Katika majibu yake, Serikali bado haijatoa *commitment* ya mradi huu kwa sababu tulikuwa tunategemea kwamba kama mradi huu ungekamilika kwa wakati...

**MWENYEKITI:** Maswali, maswali, Mheshimiwa.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Je, hiyo pesa ambayo inahitajika katika mradi huu Serikali inaji-*commit* vipi maana ni mradi ambao tunategemea kwamba utaweza kusaidia hata miradi mingine katika manispaa yetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, naomba kwanza nimpongeze Balozi wa Comoro, Mheshimiwa Mabumba kwa sababu aliweza kuwaalika wafugaji wanaotoka Tanzania

kwenda kuona fursa zilizoko katika nchi ya Comoro na kwa kweli tuliona kuna soko kubwa sana la nyama, ng'ombe na la mbuzi. Je, Serikali sasa inawasaidiaje wafugaji kuunganishwa na masoko hayo katika nchi hiyo ya Comoro au nchi nyingine ili iweze kuleta tija katika nchi yetu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza amezungumzia juu ya *commitment* ya Serikali katika kuhakikisha kwamba mradi huu wa machinjio ya Manispaa ya Iringa unaweza kupata pesa na hatimaye unakuwa ni chanzo cha mapato cha Halmashauri na kuzalisha ajira. Nimpongeze sana Mheshimiwa Ritta Kabati kwa kazi kubwa anayoifanya kwa ajili ya watu wa Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama yeye mwenyewe Mheshimiwa Ritta Kabati unafuatilia vizuri ataona kwamba hivi sasa Serikali imekuwa ikifanya miradi ya kielelezo ya kusaidia Halmashauri zetu ziweze kujizalishia kipato chao wao wenyewe. Nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi kubwa aliyokwishaianza kwa ajili ya Maispaa za Mkoa wa Dar es Salaam na kwingineko katika Taifa letu. Zimetolewa pesa nyingi kwa ajili ya miradi ya kielelezo ikiwemo ya machinjio kama machinjio ya Vingunguti imepata pesa nyingi ili iweze kufanya vizuri na kuwa na tija. Nina imani kwamba baada ya kumaliza Dar es Salaam vilevile Serikali inaweza ikafanya kazi ya kuelekea katika maeneo mengine ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ameuliza juu ya namna sisi Wizara ya Mifugo na Uvuvi tulivyojipanga katika kuhakikisha wafugaji wetu wanapata masoko. Kama Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine watakuwa wafuatiliaji wazuri wataona kazi kubwa tunayoifanya. Katika kuhakikisha tunatangaza mifugo yetu na tunapata soko nje sisi katika Wizara tuna Idara inayoitwa Idara ya Huduma za



Mifugo na Masoko na tunayo Bodi ya Nyama ambayo kazi yake ni kutafuta masoko nje ya nchi na kuitangaza nyama yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, tunatoa ushauri na kuangalia ubora wa nyama yetu ili iweze kupata masoko nje. Kusema ukweli hivi sasa tumekuwa tukipata masoko makubwa sana. Katika mwaka wa 2004 tulikuwa tunaauza tani zisizozidi tatu, mwaka wa 2016/2017 tumeuza zaidi ya tani 1,000 za nyama nje ya nchi kutoka Tanzania. Mkakati wetu ni kuhakikisha tusingize nyama ndani ya Taifa letu, badala yake sisi tuwe na uwezo wa kutoa nyama nje ya nchi. Kwa hiyo, tunaomba Waheshimiwa Wabunge, watuunge mkono kuhakikisha jambo hili kama Wizara tunaendelea nalo na tunaweza kufanikisha ajenda yetu ya Tanzania ya Viwanda hasa ile inayohusu mazao yetu ya nyama na samaki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ungando, Mheshimiwa Maryam Msabaha na Mheshimiwa Dkt. Kiruswa.

**MHE. ALLY S. UNGANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mji wa Kibiti ina mifugo mingi ya ng'ombe. Je, Serikali ina mpango gani wa kujengea machinjio ya kisasa, malambo na majosho ili kuondoa migogoro baina ya wakulima na wafugaji?  
(Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Mifugo na Uvuvi, lijibu swali hilo vizuri kabisa.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba Halmashauri ya Kibiti ina mifugo mingi sasa, ni ukweli mifugo mingi imehamia katika Mkoa wetu wa Pwani, Wilaya za Mkuranga, Kibiti, Rufiji, Kisarawe zimepata mifugo mingi sana mara baada ya Serikali kukubaliana kuhamishia mifugo kutoka katika Bonde la Ihefu na kuhamia katika Mikoa ya Kusini na sisi tumepata neema

hiyo. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Ungando, kwa namna ambavyo tumejipanga katika Wizara ya Mifugo, tunataka tuhakikishe mfugo hii iende kuwa ni fursa kubwa sana kwetu sisi watu wa Mkoa wa Pwani. Ndiyo maana katika mwaka huu wa fedha wa 2018/2019 ambao bajeti yake tunakwenda kuisoma hapa karibuni ataona haya aliyoyauliza ikiwemo ya malambo na majosho, yatakwenda pale katika maeneo yetu ya Wilaya za Mkuranga, Rufiji na Kibiti, ni kwa sababu ya wingi wa mifugo tuliyokuwa nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tuna mifugo mingi sana na mkakati pia ni kuhakikisha tunapata eneo la uchinjaji na ku-*process* nyama. Hii ni kwa sababu pia tuna *advantage* kubwa ya kuwa karibu na soko la hiyo nyama yenyewe maana nyama kuitoa Kibiti, Rufiji, Mkuranga ama Kisarawe ni rahisi zaidi kuipeleka Dar es Salaam kuliko eneo lingine katika nchi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Maryam Msabaha.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba na mimi nimuulize Mheshimiwa Naibu swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyeiti, kwa kuwa machinjio ya Mazizini ni machafu sana na mazingira yake yako tete na yanahatarisha hata maisha ya watumiaji na Halmashauri pia haipati mapato kutokana na machinjio hayo. Je, Serikali ina mikakati gani kuboresha machinjio haya ya Mazizini ili na Halmashauri nayo ipate kipato?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Ulega.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba naomba tu nijibu kwa ujumla kwa sababu sijafahamu kwamba hayo machinjio ya Mazizini anazungumzia Halmashauri gani, lakini naomba nimhakikishie kwamba Wizara yetu imeendelea kuhakikisha kwamba machinjio yote yawe safi. Ndiyo maana sasa hivi

tuna *operation* maalum ya ukaguzi ya kuhakikisha tunaweka utaratibu mzuri wa tasnia nzima ya mifugo ya nyama kuanzia katika machinjio na hata huko katika minada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili tumekuwa tukilifanyia usimamizi wa karibu kabisa ili tuweze kupata ithibati ya nyama yetu kwa sababu biashara hii ya nyama haiishii kwetu sisi wenyewe, ni sheria za kimataifa zinazoongozwa na Shirika la Kimataifa la Mifugo (*OIE*). Kwa hiyo, tunasimamia vizuri na nataka nimhakikishie tutafika Mazizini na kuhakikisha ya kwamba machinjio yale yanakuwa ya viwango kwa maana ya usafi ili nyama yetu inayotoka pale iweze kuwa bora wa mlaji.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kiruswa.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Longido katika harakati za kujiongezea mapato ya ndani ya kuinua kipato cha wananchi wake walijenga mnada wa mifugo katika Kata ya Kimokouwa inayopakana na Kata ya Namanga iliyoko mpakani mwa Kenya na Tanzania ili pia kuwatengenezea wachuuzi wa mifugo mazingira rafiki ya kuweza kufanya biashara ya mipakani (*cross border trade*) na kwa kuwa baada ya Halmashauri kumaliza mnada ule wakaanza kuhamasisha wananchi waliokuwa wanapitisha ng'ombe maporini kupeleka kuuza katika minada ya Kenya ambayo ndiyo inayutumika katika maeneo ya Longido, jana Waziri akaenda akatoa maagizo ya kuwapangia bei ya kulitumia soko lile kitendo ambacho kimewakera wananchi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, swali.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Naomba Waziri mwenye dhamana aliyekwenda jana kutoa *directives* za bei ya mifugo atoe kauli itakayowafanya wananchi wa Longido na

Halmashauri kuelewa kwamba soko hili ambalo wamejenga kwa nguvu zao wenyewe na wafadhili bila Wizara kuwekeza hata shilingi watatoa *justification* gani ya kwenda kulitwaa na kulipangia bei ambayo sio rafiki ni kandamizi, hii ni sawa na kuvuna usichopanda?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Umeeleweka Mheshimiwa. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tasnia hii ya mifugo inaendeshwa kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni zake. Tunafahamu kwamba Longido kumejengwa mnada kupitia miradi ya Serikali kupitia ule Mradi wa *MIVAF* unaosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnada ule kimkakati uko mpakani na sisi katika tasnia hii ya mifugo kama Taifa kwa mwaka mmoja kwa tathmini tuliyoifanya ng'ombe 1,600,000 wanatoroshwa kwenda nje ya nchi. Pia tunapoteza jumla ya shilingi 263,000,000,000 kama Taifa ikiwa ni mapato yetu yanayotokana na tasnia hii ya mifugo hasa *export royalty*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwambie Mheshimiwa Kiruswa kwa sababu nafahamu kwamba ni Mbunge makini na ana timu makini iliyoko kule ya *DC* na Mtendaji kwa maana ya Mkurugenzi, watupe ushirikiano. Hatufanyi jambo hili kwa ajili ya kuwakomoa, tunafanya jambo hili kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni za nchi yetu lakini tunafanya jambo hili kwa ajili ya kuhakikisha Taifa letu linanufaika na rasilimali zake. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, Mbunge wa Liwale, linaulizwa kwa Waziri wa Katiba na Sheria.

Na. 227

## Hitaji la Jengo la Mahakama – Liwale

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA** aliuliza:-

Liwale ni Wilaya ya zamani hapa nchini lakini hadi leo haina jengo la Mahakama zaidi ya jengo lililorithiwa toka iliyokuwa Mahakama ya Mwanzo Liwale.

Je, ni lini Serikali itajenga jengo la Mahakama Liwale sambamba na nyumba za watumishi?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu tafadhali Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mavunde.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakiri kwamba ni kweli Wilaya ya Liwale haina jengo la Mahakama ya Wilaya. Aidha, kama alivyoainisha Mheshimiwa Mbunge ni kweli jengo la Mahakama ya Mwanzo ya Liwale Mjini ambalo linatumika sana kutolea huduma za Mahakama ya Wilaya na ya Mwanzo ni chakavu na hivyo kuhitaji kujengwa upya. Katika mpango wa ujenzi, tumepanga kujenga kujenga Mahakama ya Wilaya ya Liwale kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambalo pia litatumika na Mahakama ya Mwanzo Liwale Mjini, sambamba na ujenzi wa nyumba ya Hakimku kutegemea upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Awali naomba uelewe kwamba haya maswali tunayoyauliza hapa

na sisi wawakilishi yanaulizwa kwa niaba ya wananchi wetu, kwa hiyo, hii ni kero ya wananchi. Sasa tunapopata majibu yasiyoridisha na majibu ambayo yana mkanganyiko, tunapata mashaka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi wa Septemba, 2017 niuliza swali hili na Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana alitumia sekunde zisizozidi tano akaniambia Mahakama ya Wilaya ya Liwale itajengwa mwaka 2018. Sasa leo hii naambiwa itajengwa kwenye bajeti ya 2018/2019. Kwa nini wanakuwa na majibu ya kudanganya wananchi wakati sisi ni wawakilishi wao na hizi ni kero wanatupa ili wapate majibu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza...

**MWENYEKITI:** Umeshauliza hilo la kwanza, la kwa nini?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, sambamba na Mahakama ya Wilaya ambayo nadanganywa kwamba itajengwa kwenye mwaka ujao wa bajeti, je, Serikali ina mpango gani kujenga Mahakama za Mwanzo katika Tarafa za Kibutuka na Makata? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa niaba.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba huduma za Mahakama zinawafikia wananchi wote nchi nzima kwa ukaribu na pasipo upendeleo wowote na ndiyo maana katika bajeti ambayo Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ameisoma hapa tumeelezea mahitaji yaliyopo na mpango wa Serikali katika kuhakikisha kwamba Mahakama hizi zinajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuondelee hofu Mheshimiwa Kuchauka kwamba Serikali hii si Serikali ya

kudanganya kama alivyokuwa ameanisha awali Mheshimiwa Waziri na mimi pia nimesema hapa leo ni kwamba Mahakama hii itajengwa na ipo katika mpango huo kwa sababu hivi sasa tumepata nafasi ya kuwa na ushirikiano mzuri na Chuo Kikuu cha Ardhi na Baraza la Nyumba la Taifa ambapo tunatumia teknolojia rahisi sana ya ujenzi wa Mahakama kupitia teknolojia ya moladi. Nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba kama Serikali ilivyoahidi, Mahakama ya Wilaya ya Liwale itajengwa. Hivi sasa navyozungumza katika mpango wa bajeti ya mwaka huu tuna mpango wa kujenga takribani Mahakama za Wilaya 29. Kwa hiyo, Mheshimiwa atupe imani, Mahakama hiyo itajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuhusu Mahakama za Mwanzo, ni kweli ni dhamira ya Serikali kuendelea kuzijenga Mahakama za Mwanzo nyingi kadri ya upatikanaji wa fedha kwa sababu kwa hivi sasa tuna upungufu wa Mahakama za Mwanzo takribani 3,304 nchi nzima. Kwa hiyo, nimuondolee hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba pindi pale bajeti itakaporuhusu na fedha zitakapopatikana Mahakama hizo pia zitajengwa ili kuwafanya wananchi wa Jimbo la Liwale waweze kupata huduma ya Mahakama kwa urahisi zaidi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Fletei na Mheshimiwa Hongoli.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Jimbo la Liwale linafanana kabisa na Jimbo Mbulu Vijijini; katika Mji wa Haydom hakuna Mahakama ila kuna kituo kikubwa cha polisi, kwa hiyo, mahubusu inabidi wapelekwe kilometa 86 kutoka Haydom mpaka Mbulu. Je, ni lini sasa pamoja na maombi niliyoleta watajenga Mahakama katika Mji wa Haydom?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, ni lini Haydom mtajenga Mahakama ya Mwanzo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa

Mwenyekiti, nisiweke *commitment* ya ni lini lakini nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba ni mpango wa Serikali kuhakikisha tunaendelea kujenga Mahakama nyingi za Mwanzo katika nchi yetu. Kwa hiyo, pindi pale fedha zitakapopatikana pia Mahakama ya Mwanzo Haydom itaingizwa kwenye mpango ili wananchi waweze kupata huduma ya mahakama.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hongoli.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Lupembe, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ina Mahakama ya Lupembe ambayo ni Mahakama ya muda mrefu sana, jengo lile lilijengwa na wakoloni na mpaka sasa hivi karibu linaanguka. Tayari tulishaleta mihtasari ya kuomba ujenzi wa Mahakama eneo lingine ambalo tayari wananchi wameshatoa na nimeshaandika barua ya kuomba. Nataka kujua ni lini sasa Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama hii ambayo sio muda mrefu itaanguka?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ni lini mtanusuru kabla jengo halijaanguka?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika majibu yangu yote ya awali ya kwamba Serikali inayo dhamira ya dhati ya kwanza kabisa kuhakikisha kwamba wilaya nyingi zinapata Mahakama za Wilaya pamoja na Mahakama za Mwanzo vilevile na kufanya ukarabati wa majengo chakavu ya zamani.

Kwa hiyo, nimuahidi tu kwamba maombi yao yameshawasilishwa Wizarani, tunaendelea kuyafanyia kazi, pindi pale fedha zitakapopatikana basi tutawasiliana na mamlaka husika ili tuone namna bora ya kuweza kufanikisha ujenzi wa Mahakama hiyo katika Wilaya ya Njombe pia.



**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali namba 228 linaelekezwa kwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na linaulizwa na Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini.

Na. 228

**Kujenga Barabara Mpya ya Kuelekea  
Nchi Jirani ya Zambia**

**MHE. ORAN M. NJEZA** aliuliza:-

Barabara Kuu ya kwenda nchi jirani ya Zambia imepita katikati ya makazi ya watu na sehemu za biashara hasa katika Mji Mdogo wa Mbalizi na barabara hiyo inatumiwa na magari ya mizigo ambayo mara nyingi huwa ni chanzo cha ajali.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara mpya ili kuhakikisha ajali zinapungua?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA  
MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya *Tanzam highway* inayoelekea nchi jirani ya Zambia ni barabara inayopita katika maeneo yenye makazi ya watu. Aidha, kutokana na tabia ya watu kupenda kufanya biashara ndogondogo kandokando ya barabara, kumekuwepo na msongamano mkubwa wa watu katika sehemu zinazopitiwa na barabara hii. Hali hii imejitokeza hasa katika

maeneo ya Mbeya Mjini, Mbalizi, Uyole, Mlowo, Vwawa, Tunduma, Igawa, Chimala na Igurusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipo kwenye mpango wa kuikarabati barabara kuu ya Tanzam kuanzia Igawa hadi Tunduma ambapo katika mradi huo maeneo yenye matukio mengi ya ajali, ikiwemo eneo la mteremko wa Mbalizi, yataboreshwa ili kupunguza ajali. Mradi huu utajumuisha ujenzi wa barabara ya mchepuo kuanzia Uyole hadi Songwe na kazi hii ipo kwenye hatua ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, nina imani wahanga wengi akiwemo ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa atakuwa amefurahishwa sana na majibu haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari yetu ya Dar es Salaam ina ushindani mkubwa sana kutoka Bandari za Angola, South Africa pamoja na Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itajenga Bandari ya Inyara ikiwa ni pamoja na reli ya kutoka Mbeya kwenda Ziwa Nyasa ili kukabiliana na ushindani huu wa kibiashara ambao ni karibu asilimia 70 ya biashara ya nje kutoka Bandari ya Dar es Salaam kwa mizigo inayokwenda nchi za nje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya Mbalizi - Shigamba - Isongole na barabara ya Mbalizi - Makongorosi ambazo ni barabara za kimkakati na ilikuwa ni ahadi ya Rais wa Awamu ya Nne na Rais wetu wa Awamu ya Tano?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa kifupi Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niruhusu nimpe pongezi nyingi Mheshimiwa Mbunge Oran kwa kufuatilia mambo mbalimbali kwa sababu nafahamu anafuatilia masuala ya barabara, Uwanja wa Ndege wa Songwe, bandari kavu kama alivyouliza, lakini mambo muhimu kama ya kilimo na wachimbaji wake wadogo wadogo na mara nyingi tunapokea ushauri wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujibu swali lake la kwanza kuhusu ujenzi wa bandari kavu hususan eneo la Inyara, niseme tu kwamba Serikali inafanya maandalizi muhimu kwa ajili ya ujenzi wa hii bandari kavu ikiwa ni pamoja na kutenga eneo la heka 108 kwa ajili ya ujenzi huo. Eneo hili tumelitazama kimkakati kwa kweli kwa maana ya kuangalia ile *chain supply* yaani kuwa na mnyororo wa muunganiko kwa maana kwamba eneo hili linapakana na barabara inayotoka Mbeya au Kyela kwenda Malawi pia iko kandokando ya reli ya *TAZARA*.

Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tumejipanga kwa ajili ya kuboresha bandari hii na hatua ambayo tuko nayo ni kufanya tathmini ya maeneo ya wakazi wanaopitiwa na mradi huu ili tuweze kuwalipa fidia na harakati zingine zitakazofuata kwa ajili ya ujenzi wa bandari hii kavu ziwezi kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusu barabara ya Mbalizi - Shigamba na barabara ya Mbalizi - Makongorosi ni barabara ambazo tumezizingatia pia katika bajeti yetu hii kwa maana ya kuziboresha. Mheshimiwa Mbunge anatambua kwamba tumetenga fedha nyingi kuboresha barabara hizi ili ziendeleo kupitika wakati wote, wakati tunazitazama kwa ajili ya kuziboresha kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Richard Ndassa na Mheshimiwa Mbatia.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri kwamba barabara ya kutoka Magu (Ilungu) – Nkalalo – Ngudu - Hungumalwa ni barabara muhimu sana katika kuleta uchumi kwa maeneo yale na imeshafanyiwa usanifu wa kujengwa kwa kiwango cha lami. Je, ni lini sasa barabara hiyo itajengwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, ni lini itajengwa kwa kiwango cha lami, majibu unayo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwani amekuwepo katika Bunge hili muda mrefu na naamini kabisa hata hii hatua ya barabara hii kusanifiwa na kupata michoro ni pamoja na juhudi zake mwenyewe. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Ndassa tuendelee kuwasiliana kuifuatilia barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme kwamba Serikali ilikuwa inafanya juhudi kubwa sana za kuunganisha mikoa. Baada ya kuwa sasa tumekuwa na hatua nzuri, naamini tutaendelea kutafuta fedha na muda siyo mrefu barabara hii ya Ilungu – Ngudu – Hungumalwa tutaweza kuitafutia fedha ili tuweze kujenga kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, nimuombe tu uvute subira yeye na wananchi wake muda siyo mrefu tutaipatia ufumbuji barabara hii.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbatia.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Swali la msingi linasema pia vyanzo sababishi ni ajali na ajali nyingi zimekuwa zikitokea kwa uzembe. Sasa niulize Serikali, Kitengo cha Kupambana na Majanga yaani *Risk Management* katika Wizara ambapo kuna *known risk*, *known-unknown risk and unknown-unknown risk* lakini ajali nyingi zinasababishwa na *known-known risk* ambazo tunajitakia sisi binadamu. Sasa Serikali ni kwa kiasi gani inaimarisha Kitengo cha *Risk Management* kitaalamu na

kibajeti ili kiweze kupunguza vyanzo vya ajali hizi ambapo maisha ya binadamu hayana thamani?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali tunatambua kwamba kumekuwa na ajali nyingi na hizi tumezizungumza sana kwenye Baraza la Usalama Barabarani. Ziko hatua kabambe nyingi ambazo zinachukuliwa na Serikali ili kuhakikisha kwamba ajali hizi zinapungua. Kwa kipindi hiki kifupi ajali zimepungua lakini tunapenda tuendelee kuzipunguza zaidi na zaidi. Nafikiria tunajaribu kutazama muundo wa Baraza hili sasa ili kuwa na *mechanism* nzuri ya kuhakikisha kwamba tunazitambua vizuri hizi *risk* ambazo zipo ili tuweze kuzishughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu suala la kupunguza ajali ni letu sisi wote. Kwa hiyo, nitoe tu ombi kwa Waheshimiwa Wabunge tuendelee kushauri wanaotumia vyombo, madereva wetu, madereva wa bodaboda ili wakati Serikali inachukua hatua ni vyema wote tuwe pamoja ili kuhakikisha kwamba tunatoa hamasa, tunatoa elimu na kuwafanya watumiaji wote wa vyombo waweze kutumia barabara vizuri. Pamoja na watumiaji wa miguu, hatari ziko nyingi tunazona katika majiji na maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tushirikiane ili tuhakikishe kwamba ajali zinapungua na kama ikiwezekana tuziondoe kabisa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na swali Na.229 na linaulizwa na Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi na linaelekezwa kwa Waziri wa Nishati.

Na. 229

**Umeme wa REA kupelekwa Vijiji vya Itigi**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE** aliuliza:-

Je, ni lini Vijiji vya Jeje, Kashangu, Idodyandole, Mbugani, Aghondi, Mabonden, Kitopeni, Ipande, Muhanga, Damwelu, Kitaraba, Kazikazi, Kintanula na Rungwa vitapatiwa umeme katika Mradi wa REA?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Naibu Waziri, Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Subira Mgalu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) inaendelea kupeleka umeme katika vijiji vyote vya Tanzania Bara ambavyo havijafikiwa na miundombinu ya umeme ili vifikiwe na umeme ifikapo mwezi Juni, 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Manyoni Magharibi lina vijiji vipatavyo 39 ambapo vijiji 11 vimefikishiwa miundombinu ya umeme. Vijiji 10 vya Kamenyanga, Kayui, Jeje, Songa Mbele, Njirii, Kashangu, Idodyandole, Sanjaranda, Ziginali na Ipanga vimewekwa katika mradi wa REA Awamu ya Tatu mzunguko wa kwanza. Utekelezaji wa mradi huu umekwishanza na mkandarasi anayefanya kazi hii katika Mkoa wa Singida aitwaye *CCCE-ETERN Consortium* anatarajia kukamilisha kazi Juni, 2019. Kazi za ujenzi zinajumuisha ujenzi wa kilometa 22.4 za njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 na kilometa 36 za njia za umeme wa msongo kilovoti 0.4/0.23, ufungaji wa transfoma 18 na uunganishwaji wa wateja 662. Gharama ya mradi huu ni shilingi bilioni mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji 18 vilivyobaki vikiwemo vya Mbugani, Aghondi, Maondeni, Kitopeni, Ipande, Muhanga, Damwelu, Kitaraba, Kazikazi, Kitamula na Rungwa vitaanza kupelekewa umeme kupitia mradi huu mzunguko wa pili kuanzia Julai, 2019 na kukamilika Juni, 2021.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Massare.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri yenye kutia moyo wananchi wa Jimbo la Manyoni Magharibi, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Kalangali kimepitiwa na umeme ukaenda kutua kijiji cha pili cha Mkoa wa Tabora, Kijiji cha Kipili. Wananchi wa Kalangali wanasononeka sana na kupitwa na umeme huu. Je, sasa Wizara hii iko tayari kuingiza kijiji hiki katika mzunguko huu wa kwanza, Awamu ya Tatu ya *REA*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii alipokuwa Naibu Waziri alikuja Itigi na alifanya mkutano mzuri sana na wananchi. Sasa yuko tayari kwenda kufanya mkutano na wananchi wa Rungwa kuwahakikishia kwamba Awamu ya Tatu mzunguko wa pili umeme utaenda hadi Rungwa?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza lilihusu Kijiji cha Kalangali ambapo kwa maelezo yake kijiji hiki kimepitiwa na miundombinu ya umeme ambayo imeelekea Mkoa wa Tabora na wananchi wa kijiji hiki hawajapa umeme huo.

Napenda nikubali maelezo ya Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kuwa kuna maelekezo ya Serikali maeneo yote yaliyopitiwa na miundombinu ya umeme mkubwa na ambayo hayajapata umeme yapatiwe. Kwa kuwa kazi

katika kijiji hiki ni kushusha transfoma na kuwaunganisha wateja, napenda nimthibitishie nitatoa maelekezo kwa mkandarasi na REAwafanyie kazi kijiji hiki na kipatiwe umeme katika awamu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ombi la Mheshimiwa Waziri kufanya ziara katika Wilaya ya Itigi, Kijiji cha Rungwa, naomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ombi hilo limekubaliwa na ziara itafanyika kama ilivyo utaratibu wetu kutembelea maeneo mbalimbali. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tumekula muda wetu kidogo. Matangazo, nianze na wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Wageni waliopo Jukwa la Spika ni wageni wa Mheshimiwa Spika ambao ni Mheshimiwa Onyango Kakoba - Katibu Mkuu wa Sekretarieti za Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu na Msaidizi wake Ndugu Jenny Mbodi na wageni wengine ni Shekhe Othman Kaparo, Bwana Saleh Omar Saleh na Bwana Abdul Manare, karibuni sana kwetu. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni watatu wa Mheshimiwa Japhet Hasunga, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii ambao ni watumishi kutoka shule ya sekondari ya Iyula Malaika, Mkoani Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 30 wa Mheshimiwa Antony Mavunde, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri ya Mkuu Kazi, Vijana na Ajira ambao ni wanafunzi kutoka Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini cha hapa Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Jumaa Aweso, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji ambao ni wapiga kura wake kutoka Pangani, Mkoani Tanga, karibuni sana wageni wetu kutoka Tanga. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Mbarouk Ali ambao ni watoto wake kutoka Jijini Dodoma, karibuni. *(Makofi)*



Wageni 54 wa Mheshimiwa Esther Matiko ambao ni wanafunzi wanaosoma vyo mbalimbali vya hapa Jijini Dodoma wanaotokea Jimbo la Tarime, Mkoani Mara, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 32 wa Mheshimiwa Willy Qambalo ambao ni wanafunzi 25 na walimu saba wa shule ya sekondari ya Welwel kutoka Karatu Mkoani Arusha, karibuni sana na someni kwa bidii sana. *(Makofi)*

Wageni 36 wa Mheshimiwa Mary Chatanda ambao ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi kutoka kata 38 za Jimbo la Korogwe Mjini, Mkoani Tanga. Karibuni sana viongozi wetu, hiyo ndiyo nguvu ya Mheshimiwa Chatanda huko. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Sabreena Sungura ambaye ni Ndugu Kuruthum Msafiri ambaye ni mdogo wake kutoka Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Seif Gulamali, Mbunge wa Manonga ambaye ni Ndugu Joseph Gimbuya, mpiga kura wake kutoka Manonga, Mkoani Tabora, karibu sana ndugu yetu. *(Makofi)*

Wageni 14 wa Mheshimiwa Maria Kangoye ambao ni wanafunzi kutoka Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini cha hapa Dodoma. Wageni wa Mheshimiwa Kangoye, karibuni wanafunzi. Nawahimiza someni, someni, someni mpaka mwisho wa *black board*. *(Makofi)*

Tunaendelea, wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunao wanafunzi 25 na walimu wawili kutoka shule ya sekondari ya Shamsiya ya Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana wanafunzi na walimu mjifunze shughuli za Bunge. *(Makofi)*

Wanafunzi 120 kutoka Chuo cha Uhasibu Tanzania *(Tanzania Institute of Accountancy)* cha Jijini Dar es Salaam, mko wapi? Karibuni sana. *(Makofi)*

Tangazo la semina muhimu; Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa kutakuwa na semina kwa Wabunge wote, kama ifuatavyo:-

Kwa Wabunge wote kesho Jumamosi tarehe 12 Mei kutakuwa na semina kuhusu kazi na majukumu ya Idara ya Usalama wa Taifa. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Rudia.

**MWENYEKITI:** Kutakuwa na semina kuhusu kazi na majukumu ya Idara ya Usalama wa Taifa, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Semina hii itafanyika katika Ukumbi wa Msekwa kuanzia saa 4:00 asubuhi. Nawaombeni sana Waheshimiwa Wabunge, hata ambao mmepanga safari muahirishe kidogo muondoke baadae. Ni semina muhimu sana hii. *(Makofi)*

Siku ya Jumapili, tarehe 13 Mei, kutakuwa na semina kuhusu mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja, mmeisemea sana hii. Semina hiyo itafanyika katika Ukumbi wa Msekwa kuanzia saa 05:00 asubuhi. Mnahimizwa sana muhudhurie. *(Makofi)*

Sasa mnisikilize sana Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima naleta mbele yenu taarifa ya kuchaguliwa kwa Mheshimiwa Stephen Julius Masele kuwa Makamu wa Rais wa Kwanza wa Bunge la Afrika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, huyu ni Katibu wa Bunge; napenda kuwajulisha kuwa katika mkutano wake unaoendelea hivi sasa huko Midland Afrika Kusini, Bunge la Afrika *(PAP)* limumchagua Mheshimiwa Stephen Julius Masele, Mbunge wa Shinyanga Mjini kuwa Makamu wa Rais wa kwanza wa Bunge hilo. Bunge la Afrika lina Makamu wa Rais wanne, huyu ni Makamu wa Rais wa Kwanza kwa sababu ndiye ambaye ameongoza kwa wingi wa kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Masele amechaguliwa jana tarehe 10 Mei, 2018 na kwa niaba yenu sasa napenda kumpongeza

sana kwa kuchaguliwa kushika wadhifa huo mkubwa ambao umelipa Bunge letu sifa na Tanzania kwa ujumla na pia nafasi hii ni inaitangaza nchi yetu na Bunge hili linamtakia Mheshimiwa Masele utekelezaji mwema wa majukumu yake katika Bunge hilo la Afrika. Hilo ndio tangazo kuhusiana na taarifa hiyo muhimu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, na mimi niwapongeze sana, niipongeze sana timu ya Wabunge ambayo imekuwa kule Afrika Kusini wakifanya shughuli hii, lakini na yeye mwenyewe huyu kijana kwa jitihada zake, lakini na Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, mambo haya niwaambieni huwezi kuyapata kama hujaungwa mkono na Serikali yako. Kwa hiyo, napongeza sana *Foreign Affairs* kwa *facilitation*, lakini pia na uongozi wa nchi hii na Rais Magufuli, kwa hayo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nifanye sahihisho, nilisikia mtu fulani upande wangu wa kushoto akisema mbona mwenye Wizara hiyo hasemi? Mwenye Wizara ameniambia nifanye sahihisho na ndio maana nawasihi tena mnaotaka kusafiri, msafiri baada ya semina hii. Amesema hivi kwa sababu ya umuhimu wa semina hii kesho tufanye tu ya *TISS* hiyo ya Idara ya Usalama wa Taifa. Yale mengine tutafanya siku nyingine ili mshibishwe vizuri ninyi kama viongozi wa Taifa hili. Hilo ni sahihisho zuri tu. *(Makofi)*

Mimi haya mambo, lakini nilazimike tu kusema; Mheshimiwa Rashid Shangazi ameniomba nitangaze kwamba Simba ni Bingwa wa Soka Tanzania kwa mwaka 2018. Kwa hiyo, tunawapongeza sana Klabu yetu ya Simba na wengine tuendelee kujipanga vizuri kwa msimu ujao. Hayo ndiyo matangazo niliyonayo. *(Makofi)*

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Ngoja tuwachukue majina. Nianze na mkono wangu wa kulia.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** ...jibu, jibu langu lilikuwa kwenye nani.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mlinga

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo, nianze moja kwa moja.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Hapana, nachukua tu majina. Mlinga, nimemaliza, nahama. Mheshimiwa Bilago.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwakajoka.

**MHE. ANATROPIA L. THEONES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Anatropia.

**MWENYEKITI:** Haonga! Alaa!, nimezoa wale ambao wana miongozo kila siku, samahani sana Mheshimiwa Mwakajoka, Mheshimiwa Kalanga; kaa tu wewe.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nasimama kwa Kanuni ya 68(7), sitaisoma. Wakati Mheshimiwa Naibu Waziri akijibu swali langu namba 223; nitaeleza alichokisema nikiunganisha na

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la 2005. Anasema...; ngoja niende tu kwenye hoja nitarudi baadae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Naibu Waziri anajibu swali langu nilimuomba afanye ziara katika eneo la Kisiwani ambalo liko katika Halmashauri ya Ilala, akasema kwamba ameshafanya ziara katika Jimbo la Segerea na maeneo mengine, kitu ambacho ni kizuri. Mwongozo wangu umekuja hapa au naomba mwongozo kwamba Mawaziri wamekuwa wakifanya ziara katika mikoa, wilaya na majimbo mbalimbali bila kuhusisha Wabunge wa Viti Maalum katika wilaya na mikoa husika, ilhali wakijua Wabunge hao ni wawakilishi na wanakuwa na jukumu pia la kusemea kero za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea leo, kwamba Naibu Waziri ameshafanya ziara katika Jimbo la Segerea, pengine Ilala na Ukonga ambako pia mimi nawakilisha na ninamuomba vile vile arudi kwenye eneo lile lile. Hauoni ni busara hawa watu wakiwa wanakuja kwenye wilaya zetu tuwe tunapewa taarifa, ili tuwe na uelewa wa pamoja tuweze kuwasemea wananchi wetu kwa pamoja. Na hiyo ni kwa sababu, Wabunge wa Viti Maalum hawaji katika Bunge hili kwa hisani ni takwa la Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mwongozo wangu nilikuwa naomba, kuna jambo limetokea, limetikisa sio Bunge tu, bali ni hata na nchi. Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu jana ilizindua udahili, ilifungua dirisha la udahili wa wanafunzi kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu, lakini sharti mojawapo walilolitoa ni kuwa ili uweze kuomba mikopo inatakiwa mzazi wako asiwe anamiliki leseni yoyote ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu ilikuja na hoja kuwa kama umesoma shule ya *private* haupati mkopo, tumepiga kelele tukanyamaza. Ikasema watoto wa

Wabunge, tukanyamaza; imesema watoto wa Wakurugenzi, tumenyamaza; watoto wa Wakuu wa Wilaya tumenyamaza na Maofisa mbalimbali wa Serikali tumenyamaza. Sasa hivi inasema kuwa, kama mzazi wako anamiliki leseni ya biashara hupati mkopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara pekee ambayo haina leseni ni wamachinga. Sasa hivi Serikali yetu inafanya uhakiki na kuwapa *TIN Number* wamachinga, tunajua mkiwapa *TIN Number* mtakuja kuwapa leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi Mwongozo wangu ulikuwa huu, nilikuwa nataka majibu ya Serikali kuwa, ina mkakati wa kuifuta Bodi ya Mikopo? Maana tunapoelekea watu wote wa Tanzania watakuwa na *disqualification* ya watoto wao kutopata mikopo. Nilikuwa naomba Mwongozo wako. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea, Mheshimiwa Kalanga.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi ya kuuliza Mwongozo, sawasawa na Kanuni ya 68 ambayo Mheshimiwa Mlinga ameshaisemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu Kiti chako kikatoa Mwongozo katika suala hili, kwa sababu inaonekana sasa Bunge hili tumepitisha sheria kuhusu mikopo na haki na taratibu za kupata, lakini siku za karibuni imetokea ule utaratibu wa kikanuni na wa sheria ambao tumepitisha umebadilishwa, kila mtu anakuja kwa mapendekezo yake na kwa utashi wake na kutoa maelekezo. Bodi ya Mikopo inaongeza kila mwaka sharti la kuwafanya Watanzania wasipate mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako Bunge hili, hili jambo ni haki ya Mtanzania kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania? Ni nini sasa kinasimamia mikopo, ni sheria ambayo Bunge limepitisha au

ni matamshi na matakwa ya Bodi wanavyotaka kubadilisha kila siku na kuwafanya Watanzania wengi wasipate mikopo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana jambo hili Kiti chako kikaitaka Serikali itoe maelekezo ambayo ni haki na ambayo hayabagui na ambayo yanasimamiwa na sheria na utaratibu wa nchi yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Na mimi naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) ikisomwa sambamba na Kanuni ya 46(1).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati swali langu linajibiwa hapa leo na Naibu Waziri na Waziri pia wa Madini, swali langu halikuhusu kabisa Wizara ya Madini, mimi swali langu lilikuwa linahusu Wizara ya Fedha na ndiyo maana ukiangalia swali langu linasema kwamba je, kwa nini Serikali haiwapatii wananchi wa Mji wa Tunduma ruzuku ya asilimia 0.3 kama ilivyo kwa wananchi wanaoishi maeneo yenye migodi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, swali langu lilikuwa halihusu kabisa Wizara ya Madini. Kwa hiyo, swali langu halijajibiwa ipasavyo. Mimi najua kabisa kwamba Tunduma hakuna mgodi na kwa hiyo sikuiuliza Wizara ya Madini nilikuwa nauliza kwa sababu pale tuna forodha na matatizo yanayopatikana kwenye maeneo ya forodha kwenye mpaka wetu wa Tunduma yanafanana sana na matatizo mbalimbali ambayo yanapatikana kwenye migodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa nataka nijue kutokana na athari ambazo tunazipata kwenye Mji wa Tunduma ni namna gani Serikali inaweza ikatupa pia hiyo asilimia tatu Halmashauri ya Mji wa Tunduma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningepomba swali langu kwa kweli, lijibiwe upya. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba Mwongozo unaofanana fanana na Mheshimiwa Mlinga pamoja na Mheshimiwa Kalanga ikizingatiwa kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ambayo Wizara ya Elimu iko chini yake, iko ndani ya Kamati hii na Bodi ya Mikopo nayo iko ndani ya Kamati yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa vigezo hivi vinavyoongezwa kila kukicha kwa ajili ya wakopaji wa fedha ambazo ni kodi ya Watanzania inaonesha moja kwa moja ni ubaguzi. Sasa hiki kitu mwaka jana kwa mfano, waliongeza kigezo cha kila anayejaza fomu ya maadili haruhusiwi kupata mkopo wa kusomesha mtoto wake. Sasa na Madiwani wanajaza hizi fomu za maadili, hivi Diwani anaweza akamsomesha mtoto wake elimu ya juu? Sasa hivi magenge, genge lina leseni, mama ntilie wana leseni, hivi hawa wana ubavu wa kumsomesha mtoto elimu ya juu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tupate Mwongozo wa Serikali, hii Bodi iendelee iwepo au isiwepo au tufanyeje, ili itende haki kwa Watanzania watakaolipwa fedha za mikopo ambazo zinatokana na jasho la Watanzania? Naomba Mwongozo wako, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa hiyo Miongozo sita na Waheshimiwa Wabunge; lakini kama mlivyosikia ninyi wenyewe Mwongozo unaoombwa na Mheshimiwa Mlinga unafanana na ule wa Mheshimiwa Laizer Kalanga pamoja na Mheshimiwa Bilago ambayo imeelekezwa kwenye Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu.

Sasa nianze na Mwongozo ulioombwa na Mheshimiwa Anatropia, ni kweli aliuliza swali hilo 223. Sasa mimi nitaendelea kuwakumbusha tu Kanuni hizi, kwamba jambo ambalo halijatokea mapema humu pamoja na heshima zote msiwe mnachukua muda wetu mwingi. Halijaangukia kwenye kanuni ambayo umeiombea mwongozo. Huo ndio mwongozo wangu halijaangukia katika kanuni hiyo, lakini nitasema tu maana tusiwe



tunachanganya sana haya mambo. *Extension* ya mwongozo wangu kwa Wabunge wa Viti Maalum kama wewe, maana swali lako limejibiwa vizuri tu na Naibu Waziri amekuja akaeleza vizuri, *is a fact* kwamba Waziri alitembelea Jimbo la Segerea *is a fact*, ni ukweli.

Sasa wewe kama unataka kuuliza nafasi ya Mbunge wa Kiti Maalum au wa Viti Maalum wa eneo husika ambako kuna Mbunge wa Jimbo, Mawaziri wanapotembelea *angle* yenu unataka kuona kwamba lazima na Wabunge wengine wa Viti Maalum wa eneo hilo wawepo, ndiyo hoja ambayo mimi naiona. Sasa uliza swali *specific* kwa hilo, lakini majibu yangu naendelea kusisitiza Mbunge wa Jimbo yupo, ndiye amechaguliwa na wananchi wote wa Jimbo hilo. (*Makofi*)

Wabunge wa Viti Maalum ni utaratibu ndani ya Katiba yetu wa kuongeza uwakilishi wa kundi maalum muhimu katika jamii ndani ya Bunge hili na vyombo vingine vya uwakilishi. Lakini Mbunge wa Jimbo husika yupo na ndiyo maana Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Zungu nimemsikia anasema Mheshimiwa Naibu Waziri alienda Jimbo la Segerea na mwenye jimbo aliyechaguliwa na wananchi naye alikuwepo. Wameangalia hali ya miundombinu ya jimbo hilo, lakini mwongozo wangu, narudia hili suala halijatokea mapema hapa.

Mheshimiwa Mlinga, Mheshimiwa Bilago na Mheshimiwa Kalanga, *again*, narudia hapa hayajatokea hapa mapema. Hata hivyo kwa vile suala hili linahusu kwamba inadaiwa Bodi inaibua masharti mapya ambayo kila kukicha na Serikali imo, mmesikia lakini na nafasi ya kamati husika ya kisekta ipo. Kwa hiyo, mimi nasema mwongozo wangu kwa hili halikutokea hapa lakini Serikali ipo mnaweza mkalitolea maelezo wakati unaofaa, lakini na kamati ya kisekta iendelee kutekeleza majukumu yake katika kuishauri na kuisimamia Serikali maana Bodi iko chini ya Wizara mnayoismamia.

Mheshimiwa Frank Mwakajoka, yeye anasema hakufurahishwa na kujibiwa na Serikali kupitia Wizara ya

Madini. Alitaka angejisikia vizuri kama angellibiwa vizuri na Wizara ya Fedha na Mipango.

Sasa umesema wewe hukujibiwa kikamilifu, mimi mwongozo wangu nione acha tukajiridhishe na majibu ambayo yametolewa na Serikali na jinsi swali lako ulivyoliuliza kama lilielekezwa na Sekretarieti yetu ya Bunge kwenye wizara, wao kazi yao ni kupeleka kwa Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo inaratibu shughuli zote za Bunge ili Ofisi ya Waziri Mkuu ione ni nani ambaye anapaswa kujibu. Wizara ipi inapaswa imjibu Mheshimiwa Mbunge. Acha tukaliangalie na nitakuja kutoa mwongozo wangu baadae kama kweli linahitaji kurudia kujibiwa siku za usoni.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo mwongozo wangu kwa leo, ahsanteni sana. Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, ninayo orodha ya wachangiaji kwa siku ya leo ambayo imeletwa na pande zote za vyama humu Bungeni. Nianze na Mheshimiwa Sixtus Mapunda atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Ditopile na Mheshimiwa Omary Mgumba ajiandae. Hawa ni dakika kumi, kumi.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia asubuhi hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sio muumini wa ushirikina ingawa kuna wengi wanaamini katika ushirikina. Kila nikiangalia mazingira rafiki yenye kuvutia, yenye uwezo wa kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda kuanzia ukubwa

wa ardhi yenye uwezo wa kustawisha mimea ya kila aina, aina ya mifugo tuliyokuwa nayo, idadi ya watu, kwa maana ya soko la ndani, malighafi muhimu kwa maana ya chuma, makaa ya mawe na madini utayataja kadri utakavyoweza, uwepo wa bandari kubwa tatu zenye uwezo wa kufanya kazi katika *standard* za kimataifa na bandari nyingine ndogo ndogo kwenye maziwa na bahari isiyokuwa na idadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi imekaa vizuri kimkakati, inazungukwa na nchi nane ambazo zote zinatutegemea. Tuna mtandao mzuri wa barabara za lami ambao nchi za Afrika Mashariki na Kati hakuna nchi hata moja iliyounganishwa vizuri kwa mikoa na wilaya kama nchi yetu, na bado tuna reli na tunaendelea kutengeneza reli ya kisasa ya *standard gauge*. Kwa hizi sifa zote nzuri tusipokuwa na viwanda vya uhakika napata shida na ndiyo maana ninasema huenda tumerogwa. Kama huyo aliyeturoga sijui ni nani na kama kuna mganga wa kutugangua huko tulikorogwa basi atusaidie. Haiwezekani tukawa na nchi nzuri kama hii, yenye haya mambo mazuri yote leo hii tunasua sua kwenye viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zote zilizokua kiviwanda dunia nzima zilianza na mahitaji ambayo wananchi wake wanayahitaji sana. Nchi ya Ujerumani ilipoanza viwanda ilianza na makaa ya mawe na chuma; nchi ya Uswisi ilipotaka kukua kwa viwanda ikaanzisha viwanda vidogo vidogo vya jibini, maziwa pamoja na mboga mboga; nchi ya Uholanzi ilipotaka kukua kwa viwanda ilianza kwenye maua na mboga mboga; nchi za China na India zilipotaka kukua kiviwanda zilijielekeza kwenye viwanda vya nguo. Kila nchi inakuwa na ajenda mahsusi inapotaka kwenda kwenye viwanda kulingana na mahitaji halisi ya watu wake, lakini vilevile kwa soko linalowazunguka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina bahati ya kuwa na ajenda mahsusi ya viwanda. Tanzania ya viwanda ni *national strategy* ambayo wimbo huu ukipigwa unapaswa uchezwe na kila Mtanzania na katika *tune* ya ule muziki

uliochezwa. Tunachokiona kwenye huu mkakati mkubwa wa kitaifa wa kuifanya Tanzania ya viwanda ni kana kwamba Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji inacheza muziki wake na wengine hao ambao inabidi waifanye hii Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji iende vizuri nao wanacheza muziki wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mwaka wa tatu sasa ta Tanzania ya viwanda. Sikilizeni bajeti zote hapa, tutaanza na Wizara ya Kilimo, wapi mtu wa kilimo ana-*link* mipango yake ya kilimo na viwanda tangu mwaka 2016 wapi ana-*link*, anakuja na mkakati wa kilimo unaoenda sambamba na Tanzania ya viwanda. Twende kwenye Wizara ya Mifugo na Uvuvi yote watakatayosema na hotuba zao watakazozitoa wapi wana-*conclude* kwa kufanya moja, mbili, tatu kwenye kilimo, mifugo na uvuvi. Hapa sasa ndipo dirisha la kutokea kwenye viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye Ardhi. Mikakati ya mashamba, mikakati ya kurasimisha maji, wapi tuna-*link* ardhi na viwanda. Twende kwenye elimu, tutakwenda kutengeneza viwanda nchi nzima, mafundi michundo wako wapi? Wapi tume-*link* VETA na Tanzania ya viwanda? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa haya yote hayawezi kwenda bila fedha. Ili twende kwenye Tanzania ya viwanda namba moja sasa mwezeshaji huyu fedha ndiye a-*pump* pesa kwenye haya maeneo manne niliyoyatoa ndipo hatimaye mtapata viwanda. Waziri wa Fedha asipoelekeza nguvu zake kwenye kilimo, asipoelekeza nguvu zake kwenye mifugo, asipoelekeza nguvu zake kwenye elimu hiyo Tanzania ya viwanda haiwezekani. Nilianza kwa kusema mwanzoni zile sifa nne/sita za Tanzania zina kila kitu kizuri, kwa nini hatuendi? Ndipo tunaishia kusema kwamba pengine tuanze kuamini na ushirikina, pengine tumerogwa na kama kuna mganga aje atugangue, sitaki kuamini hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchawi wa Mtanzania ni Mtanzania mwenyewe na mganga wa Mtanzania ni

Mtanzania mwenyewe. Tunachohitaji sasa hivi ni kuthubutu kwa dhati, Watanzania wote tucheze *tune* moja, Watanzania wote tupate uelewa. Leo hii tunaongelea Tanzania ya viwanda, leo hii tunaangalia Tanzania ya viwanda yenye changamoto nyingi, lakini mahitaji yetu sisi hatukuwahi kujitosheleza kwa kila kitu. Tuanze tu na sembe, tunalima mahindi kule Kusini, tunalima Rukwa mahindi, mahindi yanafika yanatujalia hatuna uwezo hata wa kuyafanya yale mahindi angalau yasubiri misimu miwili kuangalia soko linakwendaje au tunasaga kwa kiasi gani kuwasaidia na majirani zetu. Kwa hiyo, tutakwenda kwa mwaka mmoja hatuna maghala, mahindi yataoza mwishowe tunaharibikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachotaka kukisema, sisi tuna changamoto nyingi lakini zote zinatibika. Tulivyotaka kutengeneza *standard gauge* hatukujadiliana na mtu tukaanza tu kwenda, hali kadhalika viwanda tunavyotaka kuweka. Tunapozungumzia Mchuchuma na Liganga hatuhitaji tena maneno kwa sababu tuna uhakika Tanzania ya viwanda inahitaji umeme wa kutosha, inahitaji chuma cha kutosha. Sasa Mchuchuma na Liganga tuna yote mawili kwa wakati mmoja. Una-*caa*/hapo hapo na una-*steel*/hapo hapo na ukienda kusoma kwenye historia za nchi zilizokuwa kwa viwanda unakuja kukuta Ujerumani walianzia hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii huu ukanda wetu huu tunaongelea ile *story* ya mafuta, sijui mchikichi, sijui alizeti, hivi tunashindwaje leo kuwaambia jamani JKT hebu kaeni, Magereza kaeni, wataalamu wa *SUA* hebu fanyeni *breeding* nzuri ya mbegu ya alizeti au mbegu ya mchikichi tuiweke ndani ya miaka mitatu/minne tusiwe na tatizo la mafuta au tunaongelea mambo ya sukari? Sitaki kuyasema haya, yamesemwa sana. Tanzania ya viwanda ianze na yale mahitaji. Tunakwenda kwenye nyama Tanzania yetu ni nchi ya pili kwa kuwa na ng'ombe wengi Afrika, lakini tujiulize maeneo yote ambayo wanahitaji nyama kwenye mahoteli nyama zinatoka wapi? Sasa hivi tunaongelea suala la maziwa, hatuna sehemu ya ku-*process* maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tutakwenda kwenye msimu wa nyanya, Waheshimiwa Wabunge, ninyi ni mashahidi mnapita hii njia mnaifika pale Dumila, mnaikuta nyanya zimemwagwa pale chini, nyanya zinazuzwa mpaka shilingi 200 na hakuna mnuunaji. Hivi kweli tumeshindwa hata kuwasaidia kuwapa mawazo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kitu kimoja, Mheshimiwa Mwijage usidhani kwamba Watanzania unaposema viwanda wanaelewa kama unavyoelewa wewe. Wenzako wanaelewa kwamba wewe ndiye mwenye ajenda ya viwanda, wewe utawapelekea mashine na si kwamba wao wafikiri kulingana na mazingira yao. Hata hivyo ukitoa tafsiri ya viwanda, kama ulivyotuwekea, kwamba viwanda vinatokana na ile hali halisi ya watu kuyaona mazingira yao, wakazona fursa, wakatatua shida zao kulingana na mazingira yao jinsi walivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sasa hivi ukiondoa hizo *efforts* zako unazozifanya kwenye viwanda, tengeneza timu maalum ya kufanya *industrial mapping*. Hiyo *industrial mapping* itanguliwe na *research*. Uwe na kitengo maalum kifanye tafiti eneo gani yanastawi mazao gani, eneo gani tukiweka kiwanda cha aina gani kitakwenda vizuri. Tukifanya hivi mambo yetu yatakwenda vizuri, bila kufanya *research* sasa na kujua ajenda ya viwanda si ajenda ya hiari. Hii ajenda ya viwanda ni ajenda ya lazima kwa sababu ndiyo *National Agenda*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi leo tunasema Awamu ya Tano tuna ajenda gani, ni Tanzania ya viwanda hatuna ajenda nyingine. Sasa Tanzania ya viwanda ambayo hatuna mkakati wa viwanda, hatuwezi kwenda, uwe ni wimbo wa nchi nzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikupe mfano tu Tanzania tuna uzoefu wa kuamua na kufanikiwa. Mimi nina mifano miwili ambayo najua kabisa tuliwahi kuamua na tukaenda. Siku tulipoamua kuweka *standard gauge* hatukuulizana na mtu tukaweka ikaenda. Siku tulipoamua

kuifanya *UDOM* iwe *university* tukaamua tukaenda. Mimi nina imani mambo haya yote yanachohitaji ni kitu kimoja tu kuamua, kutenda na kutekeleza. Tunachokosa sasa hapa ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana, tunaendelea, Mheshimiwa Mariam Ditopile, atafuatiwa na Mheshimiwa Omary Mgumba.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi kuweza kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja naomba nilitolee ufafanuzi. Serikali iliyokuwepo madarakani ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi; Serikali ya Awamu ya Tano ya Chama cha Mapinduzi na inatekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015/2020. Sasa leo hii unatofautishaje Serikali ya Chama cha Mapinduzi na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Awamu ya kwanza ilikuwa ni ya CCM, ya pili ya CCM, ya tatu ya CCM, ya nne ya CCM na ya tano ya CCM. Leo hii Mheshimiwa Rais Magufuli akizindua kiwanda ambacho jiwe la msingi liliwekwa na Kikwete hapo kuna tatizo gani? Maana watu wanaleta hoja ambazo hazina mashiko. Tumepewa nafasi hii kutoa michango naomba tutoe michango ambayo inaleta tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mdogo tu mimi Mzaramo nitatoa mfano, leo hii kaka yangu Kubenea ameenda kuo baada ya harusi akitembea na mke wake watu watamsifu, Kubenea una mke mzuri, alimlea yeye? Ni kwa nini wasisifie wazazi waliomlea yule mke. Nimetolea

mfano, utapewa sifa wewe mume wa yule mke ingawa hujamzaa wala hujamlea wewe. Kwa hiyo, mafanikio ambayo leo hii tunajivunia ya awamu ya tano yanatokana na misingi mizuri ya Chama cha Mapinduzi na Serikali zake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alivyokuwa anaomba ridhaa ya kuongoza nchi hii wimbo wake mkubwa ulikuwa kwamba tutajenga Tanzania yenye viwanda na ninampongeza. Mheshimiwa Rais ameanza kuweka mikakati ya kitaifa ambayo itatupeleka kwenye uchumi wa viwanda. Uwekezaji kwenye reli ulio kwenye kiwango cha *standard gauge*, kinaenda kuwekeza kwenye uchumi wa viwanda. Ununuzi wa ndege ambao tunafufua Shirika letu la ATCL leo hii lazima tutambue tunasafirisha minofu ya sangara kwenda nje ya nchi, tunasafirisha maua, tunasafirisha mboga mboga. Leo tumeanza kununua ndege za abiria ndogo mpaka kubwa, najua huko mbele tutaenda kununua ndege za kusafirisha mizigo. Kwa hiyo, zile bidhaa zetu tutazisafirisha kwa shirika letu, tuta-*enjoy economies of scale*. Kwa hiyo, lazima tutambue kwamba uwekezaji huu kwamba Mheshimiwa Rais anasimamia kauli yake na kwa *level* yake ya juu kabisa ameonesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye uwekezaji wa *Stiegler's Gorge* kwenda kuzalisha umeme yote hii tunaona kwamba tunaenda kuelekea kwenye uchumi wa viwanda. Waliokuwepo chini ya Mheshimiwa Rais, Waheshimiwa Mawaziri hususani Waziri Mwijage, kama uthubutu wa Mheshimiwa Rais kuwekeza kwenye haya mambo je, wewe unaendana naye? Kila saa anasimama Mheshimiwa Rais kuwaambia wasaidizi wake hivi kweli mnaelewa mimi ninayoyahitaji? Je, mnasoma mimi nini ninachokitaka? Tunakuomba Mheshimiwa Mwijage lazima ujiulize mtu akikusifia makofi matatu hayazidi. Kwa hiyo, je, unaendana na ajenda? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba, mimi nina neno moja kwa Mheshimiwa Waziri naomba uwe *serious* kwenye hii ajenda ya viwanda na uwekezaji. (Makofi)



Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu tunaenda kujenga viwanda na viwanda tayari vipo vya ndani tunavilindaje? Maana kuanzisha kiwanda ni jambo moja, lakini kuvifanya viwanda hivi viwe endelevu na vizidi kukua lazima tuweke ajenda muhimu je, Mheshimiwa Waziri naomba ukiwa unakuja kujibu hoja utuambie una mipango mikakati gani gani ya kulinda hivi viwanda ambavyo tunavianzisha? Unaweza ukaanzisha viwanda vikatoa bidhaa visinunulike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunawaambia wananchi wetu tuwe wazalendo tununue bidhaa za ndani, lakini unaweze ukakuta nguo kutoka China ina bei nafuu kuliko nguo iliyotengenezwa *Mwatex* na haya matatizo tunasababisha wenyewe, viwanda vya ndani vinaonewa, urasimu ni mwingi, umangimeza umejaa, utitiri wa kodi na usumbufu ambao hauna sababu. Mwenye kiwanda atafuatwa Halmashauri, atafuatwa na Mbunge, Diwani, OSHA na Wizara, yaani imekuwa ni usumbufu. Tunawaambia wawekeze hela, tunawapa *pressure* katika kurudisha mitaji yao na kuweza kujiendeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano mdogo, leo hii mtu akileta nyuzi ama nguo kutoka nje ya nchi, ataleta *estimates* za uongo atawekewa kodi ndogo, lakini huyu mwenye kiwanda ndani atakuwa *charged* kodi nyingi, hatimaye *cost of production* inakuwa kubwa anashindwa kufikia *break even*, anafeli. Kwa hiyo, lazima tuangalie na tuwe na mikakati. Naomba na nasisitiza ukiwa unajibu hoja unijibu kwamba una mikakati gani katika kulinda hivi viwanda na uwekezaji wa ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu chochote lazima kiwe na washika dau. Waheshimiwa Mawaziri wote kwa ujumla hasa Waziri wa Viwanda, jamani msiwaogope wafanyabiashara na wawekezaji, hii inaenda kwenu Waheshimiwa Mawaziri na watendaji, mfanyabiashara ataomba *appointment* na kuonana na Waziri au mtendaji mtamkwepa, mnamkwepa nini. Yule ndiye mdau wako, kaa naye ujue changamoto zake na yeye umueleze mambo na

mikakati ya Serikali. Utapigiwa simu na mwekezaji aah naogopa, hutaki kumuona wa nini? Utapata wapi *information* za kukusaidia? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mtu mla rushwa atakuwa mla rushwa tu, rushwa zina aina nyingi sana kupatikana, kwa hiyo, tusiwekewe hawa watu. Pia nikupongeze MheshimiwaMwijage maana naona jana ulialika wadau wako wamiliki wa viwanda akiwemo Mzee wangu Kilua mmiliki wa *Kilua Group*. Kwa hiyo, hilo nalo nikupongeze, lakini wengine wote tusiwaogope hawa ni wenzetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema *when government walks, business community runs*. Kwa hiyo hawa ni wadau wetu tusiwakwepe, tukae nao tujue changamoto tuweze kusaidiana kupeleka gurudumu la maendeleo mbele. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala naomba niliweke vizuri na *na-declare interest* kwamba mimi ni mkulima na ni mchuuzi wa mazao. Kwa hiyo, nikiongelea natafuta soko la ufuta nafuatilia kwenye soko la dunia na vilevile nchi za wenzetu hali yao ya kuvuna, maana lazima tuelewe si Tanzania peke yake duniani ndiyo inayolima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa tu mtambue kwa mujibu wa *FAO*, India ndiyo nchi ya kwanza inayolima mbaazi duniani, lakini India ndio nchi ya kwanza ambayo pia inanunua mbaazi duniani. Yote ni kwa sababu India ndiye mtumiaji wa kwanza wa mbaazi, tofauti na chakula India anakamua mbaazi mafuta. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea msimu wa mwaka 2017/2018 kuhusu mbaazi maana shutuma nyingi zinakwenda kwa Serikali, penye kushauri tushauri ukweli, penye kukosoa tukosoe ukweli na kwenye kusifia tusifie ukweli. *I am talking because I know*. Mimi nilikuwa nafuatilia suala la mbaazi, kilichotokea msimu uliopita India ili-over produce mbaazi. (Makofi)

Mimi nilikuwepo kule na nikaenda *Lower House* Bungeni kwao na siku hiyo nilikuta mjadala Wabunge wa Upinzani wamewachachamalia Serikali wakiwaambia najua mmeenda nchi za Afrika ikiwemo Tanzania mmekubaliana kwamba mta-*import* mbaazi kutoka kwao, sasa wakulima wetu wamelima hawana soko, tunaomba muweke *ban* kwenye *importation* ya mbaazi kutoka nchi za Afrika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tuliaothirika sio Tanzania peke yake ni pamoja hata na jirani zetu Malawi ambao wanalima kuliko sisi. Kwa hiyo, sasa usiwe wimbo wa kuikosoa Serikali; mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ndiyo maana naunga mkono jibu la Naibu Waziri alilosema kwamba hata na sisi tujifunze kula mbaazi, sisi ni Wabunge tumeaminiwa lazima tujiongeze kwenye kudadavua mambo, hajamaanisha ukapike nyumbani kwako, tu-*cultivate* tabia ya sisi wa kwanza kutumia bidhaa tunazozialisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikaenda mbali nikasema ili Serikali muwe mfano, basi kule magerezani na mashuleni tunapeleka vyakula tuwafundishe kule kula mbaazi *instead of* maharage ili ninyi muanze kama mfano. Sisi tunapoenda Mjimboni mwezi mtukufu wa Ramadhani watu mnaongelea mafuta, sukari tuseme na mbaazi, hata kiafya ni nzuri. Kwa hiyo, lazima sisi tuwe mfano, bidhaa zetu sisi tuwe watumiaji wa kwanza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ndicho kinachotukuta, ufuta wote tunautoa nje kwa sababu hatujui umuhimu. Unaambiwa duniani hata hii alizeti tunaongea *cholesterol free it's not true*, mafuta ambayo hayana rehemu kabisa ni mawili, mafuta ya ufuta na mafuta ya nguruwe (*pig fat*), *that is the truth*. Kwa hiyo, leo hii tunasafirisha ufuta wote kwenda nje kwa sababu hatupo *aware* kuhusu... (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naunga mkono hoja nawashukuru sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, huyo ndio Mariam Ditopile, ahsante sana. Mheshimiwa Munde Abdallah atafuatiw ana Mheshimiwa Omary Mgumba na Mheshimiwa Bashe ajiandae. *(Kicheko)*

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa mimi nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa makusudi na dhati kubwa anayoifanya ya kuendeleza viwanda vya ndani. Anapambana kwa nguvu zake zote, na kweli Rais wetu ni mzalendo; na mimi niwaambie tu wale wanaobeza wanaosema hovyoy, viwanda hivi siku vikija ku-*achieve* Magufuli atakuwa kamaliza muda wake, tutafaidika sisi, watoto na wajukuu zetu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais anafanya kazi hii kwa ajili ya watanania, ni wajibu wetu kumuunga mkono Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niungane na Wabunge waliotangulia kusema, lazima Serikali hii iwe na mkakati maalum. Tumechoka sasa kuagiza mara mafuta mara sukari, kama Mheshimiwa Rais anavyotaka viwanda vya ndani vifanye kazi basi na Waziri na viongozi wote wa Serikali waungane na Mheshimiwa Rais kwa vitendo. Tujiwekee labda miaka miwili au mitatu tusiagize tena mafuta wala sukari nje ya nchi, tunaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano sasa hivi *NSSF* wana shamba kubwa la miwa, ni kuhakikisha tunaongeza uwezo mkubwa kwa wafanyabiashara wengine wa viwanda, lakini *NSSF* tuweke nguvu zetu zote, wafanye bonde lingine na bonde lingine, tuwaongeze nguvu hatimaye miaka miwili tusinunue sukari nje ya nchi. Tuna uwezo mkubwa wa kufanya hivi kama tutaamua. Tuna Mkurugenzi mzuri sana pale *NSSF* mkimpa nguvu anaweza kufanya hili jambo, lazima tuwe na mikakati, lazima tuamue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri Mkuu kwa kauli yake nzuri aliyotoa juzi kuhusu sukari na mafuta, kwamba ndani ya siku tatu vitu hivyo viwe vimetoka. Nasema hivyo kwa sababu mahitaji ya mafuta ni tani 28 hadi 30 kwa mwezi, Januari, Februari na Machi tumeingiza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Aprili mafuta hayo waliyoleta nyaraka hazitimii, Serikali haiwezi kukuingizia bila nyaraka, hivi vitu ni mafuta/ni chakula, hauna *TBS* ya Malaysia tukuingizie kama, kuna sumu. Hakuna *code* iliyoonesha mafuta ghafi yameliwa Malaysia, Malaysia hawatoi mafuta ghafi bila kulipia kodi, nyaraka hazitoshelezi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii isiwe sababu ya kuwaadhibu Watanzania kwa kuficha mafuta haya. Nasema hivi nina maana yangu, haya mafuta waliyoingiza wanaita wameingiza *crude oil* (mafuta ghafi). Haya mafuta ghafi ya mwezi wa nne kwa mfano yangeingia mpaka *process* kila kitu labda tarehe nne au tano yangukuwa yameingia, lakini mafuta haya ni lazima waende kuya-*refine* kuyasafisha ili yaje kuingia sokoni. Mpaka waya-*refine* ina maana sokoni mafuta haya yangeingia kwenye tarehe 12, 13 na 14; leo vipi mafuta hakuna nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, watu hawa wameficha mafuta ku-*demand* bei ipande na kuikomesha Serikali. Nakupongeza sana Waziri Mkuu kwa kauli yako ya watoe mafuta, kwa sababu mafuta ya Aprili hata kama yangukuwa yameingia wangukuwa hawajamaliza kuya-*refine*, kuyasafisha na kuyaingiza sokoni, iwaje leo mafuta yapotee kabisa ndani ya soko la Tanzania. Mheshimiwa Waziri Mkuu mafuta yapo, Serikali iweke nguvu mafuta yatoke na Watanzania wauziwe kwa bei inayostahili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa tuamue kabisa, tuna asilimia 30 ya mafuta tunayolima mbegu hapa Tanzania, tuamue kuwekeza. Serikali juzi iliamua kuwekeza nguvu zake zote kwenye pamba, TAMISEMI, Waziri wa Viwanda, Waziri wa Kilimo, Mkuu wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya

hatimaye mwaka huu pamba imekuwa nyingi sana Mwanza. Tuamue kwenye alizeti, michikichi. Hatuwezi kuamua kwenye vitu vyote kwa wakati mmoja, tuchague mazao yetu ambayo tuamue, kwa mfano uchukue Dodoma, Singida, Tabora useme ni *zone* ya alizeti, hii ni *zone* ya alizeti. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwijage nimepitia hotuba yako kuna sehemu umesema una matrekta 148 unauza, nikwambie kwa hali ya sasa hivi kununua *cash* yale matrekta watu wengi hawatamudu. Sasa lazima Serikali itusaidie. Mimi niombe tuanzie Mkoa wangu wa Tabora, nina wilaya saba, kila Halmashauri moja mtupelekee matrekta matatu mtukopeshe, mdhamini atakuwa Halmashauri, Mkuu wa Mkoa, *DC* na mimi Mbunge wa Viti Maalum pamoja na Wabunge wa Majimbo yangu ya Mkoa wa Tabora. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapewe matrekta matatu matatu, haya matrekta yawe mali ya Halmashauri, mtu akienda Halmashauri aandikiwe mkataba utajaza mafuta, utalipa posho, ukiimbua utalipa pesa za gharama ya kulimia. Zile pesa zitakuja kulipwa kwako Mwijage, lakini hutapata *cash* lakini utakuwa umesaidia Watanzania. Wakati huo huo mtafute mbegu za kisasa za alizeti, zilizopo hazitoi mafuta mengi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwijage hata mchikichi pia tufanye vivyo hivyo. Mchikichi unaweza kupeleka Kigoma, Mbeya kwa maana ya Kyela pamoja na Katavi na ukaita *mchikichi zone* na akili zote, viongozi wote wakaelekezea kwenye haya mambo, inawezekana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumechoka kunyanyasika Mheshimiwa Mwijage, watu wanaficha mafuta demand inapanda, Serikali nzima inapata *stress* mnashindwa kufanya vikao na vitu vingine, mnakaa kwenye vikao mpaka saa saba za usiku, hivi vitu tunaviweza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona Rais ameamua tutajenga *standard gauge*, Afrika nzima hakuna anayejenga *standard gauge* kwa hela yake, mbona ameweza? Mbona

ameamua kununua ndege na kusomesha elimu bure ameweza; watu wamepiga kelele haiwezekani, imewezakana. Nina amini tukifanya hii *alizeti zone* na *mchikichi zone* tukawekeza tunaweza Mheshimiwa Mwijage. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi trekta zikipelekwa Halmashauri wakabidhiwe wakurugenzi ma-DC, RC na Wabunge watu wakakope pale kwa mikataba wakalime baadae watalipa kwenye Halmashauri, tutaenda mbali sana. Pia mtusaidie viwanda vidogo vya kukamulia hizi alizeti, kila Halmashauri ikopeshwe. Serikali bado ina uwezo huo, Halmashauri zetu zina uwezo wa kununua viwanda vidogo, ni maelekezo tu. Kama kweli tumeamua kumsaidia na kumuunga mkono Mheshimiwa Rais naamini hivi vitu vinawezekana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee sasa kuhusu suala zima la viwanda, nianze na Kiwanda cha Tabora. Tabora kule tuna kiwanda cha nyuzi, kiwanda cha nyuzi cha Tabora kinazalisha pamba, tumekuja kuomba mara kadhaa pamoja na mwenye kiwanda tuiombe Serikali inunue pamba za hospitali kutoka kwenye kiwanda cha nyuzi cha Tabora; tuwasaidie wenye viwanda vyetu, kwa mfano mtu ana kiwanda cha kutengeneza kitu ambacho kinawezekana Serikali kinaitaka, Serikali inunue kwake kumpa support. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais kila siku amekuwa akisema jamani tengenezeni hata *syringe* za hospitali tutanunua kwenu, kwa hiyo tum-*support*. Kule Tabora hamji kununua pamba kwa ajili ya matumizi ya hospitali, mnaagiza nje ya nchi. Tunaomba Mheshimiwa Mwijage mje mnunue kule kwetu Tabora. (Makofi/kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niendeleo kuongelea viwanda vidogo, kumekuwa na kebehi zinafanyika hapa Bungeni kwamba cherehani si viwanda, hakuna viwanda 3000; mimi naomba ni-*declare* kuhusu cherehani, nitoe ushuhuda. Kuna ndugu yangu ni fundi cherehani, alishindwa

kusoma akaishia *form three* akajisomesha cherehani akaendelea akanunua cherehani nne, huyu akaenda kukopa benki, wakamwambia huwezi kukopeshwa bila leseni wala *TIN*, akapata. Baadae akapata *tender* ya kutengeneza mashati ya taasisi X, siwezi kuitaja hapa, wakamlipa shilingi milioni 70; sasa hivi amenunua cherehani 45. Mheshimiwa Mwijage nifuate nitakuonyesha na amenifuata mimi, dada nitafutie eti tenda ya kushona nguo za jeshi nikamwambia eeh umefikia huko mwenzetu? Kwa hiyo, wale wanaodharau hizi cherehani nawaambieni hivi watu wanatoka kwa hizi cherehani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sasa Serikali kwa sababu Serikali mmekubali cherehani ni viwanda vidogo hakikisheni taasisi zenu, wenye viwanda hivi vya cherehani wapeni kazi. Kwa mfano *uniform* za *TPA*, *TANAPA* na *uniform* sijui za nini wapeni washone, wapeni uwezo, watu wasiende kushona hizi *uniform* nje, Serikali hii inaweza ni kiasi cha kujipanga tu. Kwa hiyo, mimi bado naitia moyo Serikali kwamba tunaweza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *A to Z* ya Arusha ni kiwanda kikubwa sana, Kamati tuliwahi kwenda kutembelea mwaka 2013. Historia yake mwenye *A to Z* alikuwa na cherehani moja, alianza na cherehani moja, mwenye *A to Z* ya Arusha, anayebisha akamuulize. Leo hii ni kiwanda kikubwa duniani, hata huu mchakato wa malaria amepata *tender* viwanda vitano duniani na yeye amepata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anatengeneza mashuka, *uniform* na kila kitu. Kwa hiyo, tusidharau hizi cherehani watu wanaponda viwanda gani kama cherehani, mimi nasema hivi ni viwanda na vinafanya kazi na watu wananufaika kutokana na hizi cherehani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani...

(*Hapa kengele ililia kuashira kuisha kwa muda wa Mzungumzaji*)



**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Omary Mgumba atafuatiwa na Mheshimiwa Bashe na Mheshimiwa Maria Kangoye ajiandae.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na mimi kupata nafasi ya kuchangia mjadala huu kuhusu Hotuba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa afya na uzima tumekutana asubuhi ya leo kuchangia Wizara hii muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutupatia viwanda vitatu vipya katika Jimbo letu la Morogoro Kusini Mashariki, *Mkulazi One*, *Phillip Morris* na *Mahashree* cha kuchakata mbaazi, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa sababu kama Magufuli asingekuwa Rais, *Mkulazi One* isingekuja Mkulazi, kiwanda kile cha sukari kisingekuja pale na leo nitazungumzia hoja hii tu moja mwanzo mwisho, nikipata muda nitazungumzia ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tulikuwa na ziara na Mheshimiwa Rais pale Morogoro na nilimweleza hili, nilimwambia mchakato wa kujengewa Kiwanda cha Sukari Mkulazi kilianza tangu mwaka 2016 mpaka leo Serikali yako ina mchakato, kiwanda hakijaanza kutengenezwa. Nilimwambia wanaokukwamisha wapo ndani ya Serikali na chama chako, tupo Bungeni na sehemu nyingine kwenye taasisi za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo habari zilikuwa za mtaani, leo nimezipata rasmi kwenye ukurasa wa 32 wa kitabu cha Mheshimiwa Waziri; anasema kiwanda cha kutengeneza sukari cha *Mkulazi One* kilichokuwa pale Morogoro Jimboni kwangu kitaanza kuzalisha mwaka 2025, miaka saba kuanzia sasa. Kiwanda cha *Mkulazi II* ambayo

ni Mbigiri anasema kitaanza kuzalisha mwaka 2022 baada ya uchaguzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nilimwambia Dkt. Magufuli juzi kwamba lengo viwanda hivi vianze kuzalisha baada ya uchaguzi ili watu waje na ajenda wakwambie ulisema wewe Tanzania ya viwanda, viko wapi na leo inatimia kwa ushahidi wa kitabu hiki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa simuelewi Mheshimiwa Rais siku zote anaposema wasaidizi wangu wengine hawanielewi, leo ndiyo nimemuelewa. Tunafahamu siyo wote walifurahia kiwanda hiki kujengwa Morogoro, kuna watu walitaka kijengwe sehemu nyingine. Vilevile tunafahamu kuna wengine hawakupendezwa kiwanda hiki kupewa *NSSF* na *PPF* kwa sababu kuna wengine washindani wa hiyo biashara ya sukari walitaka shamba lile waliendeleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wanapitia mlango wa nyuma kukwamisha kiwanda hiki kuanza kwa wakati ili kutoa ajira kwa Watanzania, kuongeza uchumi wa Watanzania na kuondoa tatizo la sukari nchini. Mungu anawaona. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi, walikuja na sababu zote, sababu ya kwanza walisema kwamba wakati Mheshimiwa Rais anaiomba mifuko ya jamii ijiingize kwenye viwanda, wanasema mifuko haina uzoefu wa sukari kwa hiyo kujiingiza kwenye viwanda ni kupoteza hela za wanachama, hilo limepanguliwa limekwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadae wanasema kwamba hapana, mkataba umesainiwa na mtu ambaye ni tofauti, kwenda wakagundua aliyesaini ni mtu sahihi. Mara nyingine wanasema kwamba hapana *raw material* haijakuwa tayari, hivi kiwanda na *raw material* kinaanza nini? Tulikuwa na Mheshimiwa Rais juzi Kilombero, wananchi wanalalamika soko la miwa halipo, Mtibwa, Turiani wanalalamika soko la miwa yao halipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wawekezaji wako tayari, walishasaini mkataba tangu mwaka jana na mtengenezaji wa kiwanda kile, kile Kiwanda cha *Mbigiri II* kilitakiwa kifike mwezi wa kwanza mwaka huu. Kiwanda cha *Mkulazi I* kilitakiwa kifike Juni mwaka huu na Kiwanda cha *Mkulazi II* kilitakiwa uzalishaji kianze mwezi huu, lakini mpaka leo Serikali haijatoa kibali kwa mwekezaji. Ndiyo maana tunasema tatizo si pesa wakati mwingine, tatizo ni uzalendo na dhamira ya dhati ya kuwatumikia Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua, ni kweli kabisa mbuzi hula kwa urefu wa kamba yake, lakini si lazima kila jani lililopo pale atakula. Tatizo la watumishi wengi huko ndani ya Serikali wanataka kila jambo lazima kuwe na cha juu ili na yeye anufaike, kama jambo hilo hanufaike yeye yuko radhi lichelewe hata miaka kumi, hata mradi upotee kwa sababu tu yeye hajanufaika, hili halikubaliki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wekeni maslahi yenu pembeni, tangulizeni Tanzania kwanza, wekeni uzalendo kama alivyouonesha Dkt. John Pombe Magufuli. Ninayasema haya, nafikiri ananisikia, ajue namna gani kwamba kuna watu wanamkwamisha katika Sera hii ya Viwanda. Nilimwambia na leo nimelirudia baada ya kuona kwenye kitabu hiki kwamba viwanda hivi vitaanza kutekelezwa baada ya uchaguzi 2020. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana watumishi wa Serikali, sisi tulitoka sekta binafsi tulikua tunapimwa kutokana na matokeo, wenzetu wanapimwa kutokana tu na chochote ambacho hakina tija wakati mwingine.

Naomba majibu ukija kufunga hoja yako, kiwanda hiki tayari hela zipo na mwekezaji ameshawekeza, Kiwanda cha *Mbigiri II* mwekezaji ameshalima zaidi ya hekta 1000 za miwa, tunavuna kuanzia Juni, 2018. Lakini pia *outgrowers* (wakulima wadogo) walishapata mkopo kutoka Benki ya Azania zaidi ya *4.9 billion* na wameshalima zaidi ya hekta 600, hawa wote baada ya kuvuna watapeleka wapi bila kiwanda hiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali toeni kibali haraka iwezekanavyo, kiwanda hiki kiagizwe kianze uzalishaji *Mbigiri II* mwaka huu na *Mbigiri I* mwakani; zaidi ya hapo hatutaelewana, nafuatilia mradi huu kwa karibu sana. Siku ile nilimwambia kama hatutapata kibali haraka nitaenda tena Ikulu kwenda kumueleza Mheshimiwa Rais na tutawataja hata kwa majina wale wanaomkwamisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya pili, Morogoro ndio uliokuwa mji wa viwanda na ninataka nimwambie Dkt. John Pombe Magufuli, nampongeza sana kwa sababu anatekeleza ndoto zote za Mwalimu, anajenga *Stiegler's*, anajenga Kidunda, amehamisha Makao Makuu kuja Dodoma, lakini sasa kama alivyosema juzi, kuwa katikati kuna raha yake, lakini katikati hiyo Mwalimu Nyerere alimaanisha Morogoro ndiyo uwe mji wa viwanda. Na wakati ule aliunganisha na Pwani kwa sababu sehemu kubwa ya Pwani ilikuwa ni sehemu ya Mkoa wa Morogoro, hatukuwa na Mkoa wa Pwani, tulikuwa na Dar es Salaam na Morogoro na ndiyo maana alisema kwamba Morogoro uwe mji wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tulikuwa na viwanda vyetu zaidi ya 11 vile vya kimkakati, leo vinavyofanya kazi ni vinne tu. Vinavyofanya kazi ni *Kilombero Sugar*, Mtibwa pamoja na kile cha tumbaku, pia kinachechemea hiki cha *21st Century* ambacho kinafanya kazi na Moproko imeanza.

Nataka majibu ya kina, nini hatima ya viwanda saba vilivyobaki? *Morogoro Ceramic* ambayo *raw material* lilikuwa inatumia mchanga tu, lakini mnafahamu mmewauzia watu kwa bei ndogo kwa kupeana kiujoba ujomba, matokeo yake wale waliochukua viwanda vile wakang'oa mashine kwenda kuuza kama *scraper*, naona kwa sababu wamenunua kwa bei rahisi, hata akiuza *scraper* yeye anapata faida kuliko ku-*run* kiwanda. Nataka mniambie *Morogoro Ceramic* iko wapi, Kiwanda cha Magunia kiko wapi? Mniambie Kiwanda cha Ngozi kiko wapi na mna mkakati gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mpaka kile la Mang'ula, kiwanda ambacho ndiyo uhai wa Reli ya TAZARA, na mnafahamu mpaka leo, Mang'ula hakipo, leo TAZARA tutaiendeshaje? Ilikuwa chuma chochote, *spare* yoyote ya gari au ya namna gani usipoipata mahali popote unaenda kuchongesha pale Mang'ula, leo Serikali kama hamuoni lolote, hamuoni umuhimu huo Wachina tafuteni namna gani ya kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana mlete majibu mazuri. Nilisikitika sana, nilitamani kulia siku ile wakati anaongea Mzee Kasori kuhusu historia na umuhimu wa kiwanda kile. Leo tupo tumepata Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, mzalendo, msaidieni. Kiwanda hiki ndio uhai wa TAZARA, nchi maskini kama hii Tanzania haiwezi kununua kila *spare part* kutoka China bila kukifufua kiwanda hiki kukirudisha katika hali yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya najua mpaka uwe na roho ngumu kuyasema, na watu watanichukia lakini lazima ukweli niyazungumze kwa sababu mimi natoka Morogoro, viwanda hivi viko Morogoro, vina faida kubwa sana kwa watu wa Morogoro, kwa taifa, lazima tuambiane ukweli. Bila kuambiana ukweli hatutoki hapa tulipokwama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kuhusu suala la mbaazi, dada yangu ameliongelea vizuri sana... *(Makofi)*

*Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana na mbaazi, hayaa! Ahsante. Mheshimiwa Hussein Bashe atafuatiwa na Mheshimiwa Maria Kangoye na Mheshimiwa Lucy Mayenga ajiandae.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nitumie nafasi hii kwanza kusema mambo machache; mwaka 2016 wakati tunachangia bajeti ya kwanza ya Wizara ya Viwanda na Biashara nakumbuka nilimwambia kaka yangu Mheshimiwa Mwijage kwamba nasubiri nione muujiza na nilitaja miujiza ambayo nilikuwa naisubiri na leo haijatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muujiza wa kwanza niliokuwa nausubiri ni kuona namna gani Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji inaweza kuunganisha mambo matatu ambayo Waziri amekabidhiwa. Mheshimiwa Rais alivyokuja na *vision* ya ku-*revive industrialization* aliamua kwa makusudi kuunganisha biashara, uwekezaji na viwanda ili kuweza kufikia lengo la *industrialization*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka leo bado tunazungumzia *General Tyre*, mpaka leo tunazungumzia Liganga na Mchuchuma, mpaka leo tunaongelea matatizo ya msingi ya biashara na huoni yakijadiliwa katika hotuba za Waziri na hata kwenye mpango wetu wa mwaka mmoja, miwili na huu ni wa tatu. Tusome ukurasa wa 138 wa hotuba ya Waziri. Waziri ametaja vipaumbele na malengo ya mwaka 2018/2019. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri ametaja vipaumbele kushirikiana na taasisi kutunisha mtaji wa *NEDP*, kuendeleza miradi ya kieleleza ya Mchuchuma na Liganga, Engaruka Kiwanda cha Matairi, utekelezaji wa eneo la *TAMCO*, mradi wa kuunganisha matrekta, uendelezaji wa maeneo ya viwanda ya *SIDO*. *This is a hundred percent* kwa miaka mitatu tunajadili *the hardware part of business*, hatujadili *the software part of the business*. Ili tuweze kuona matatizo tuliyonayo kwenye *software part of the business* naomba nitaje haya mambo. *The software part of business* ni *regulations* na sheria na mfumo wetu wa kodi, huu ndiyo utachochea haya mambo mengine yote kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania katika kufanya biashara *according to the World Bank Report* ni ya 137 kati ya nchi 190 katika mazingira ya kufanyia biashara, Tanzania

ili uanzishe biashara ni nchi ya 162 kati ya nchi 190; Tanzania ni ya 150 kwa ajili ya kutoa vibali vya kufanyia biashara. Kama kweli tunataka ku-*break through* ni lazima Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Fedha wakae kwa pamoja kwa ajili ya kutengeneza *the software part* ya kufanya biashara katika nchi, tusipofanya namna hii tutakuja hapa tutaimba kila siku. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikupe mfano wa *leather sector*; na ndugu yangu Mheshimiwa Mgumba, ameongelea Kiwanda cha Ngozi cha Morogoro. Kwa takwimu kwa mwaka sisi tunazalisha vipande milioni tatu vya ngozi katika nchi. Sasa ili kiwanda chetu cha ngozi kiweze kuzalisha, na nimeona kwenye mpango tunatenga *10 billion* kwa ajili ya kuandaa eneo la viwanda vya ngozi, tuna viwanda saba ama vinane havifanyi kazi, halafu tunataka kutenga bilioni kumi nyingine kwa ajili ya kuandaa eneo la viwanda hapa nchini, *this is wastage of resources*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikupe mfano, katika uzalishaji wa *leather sector* tuna-*process* ngozi kutoka katika hatua ya *raw material* kwenda kwenye *wet blue*, kutoka *wet blue* kwenda kwenye *crust* na kutoka kwenye *crust* kwenda kwenye *finished*, hizi ni *levels* tatu. *Level* ya kwanza *investment* inayohitajika kwa kiwanda cha kati ni *15 million US dollars*; kutoa kwenye *wet blue* kwenda kwenye *second level* ambayo ni *crust* unahitaji *five million dollars*; kutoka kwenye *crust* kwenye *level* ya *finished* unahitaji *another five million dollars*, *this is 25 million dollars*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini angalia kodi za mzigo. Ukizalisha *wet blue* ili ui-*export* kwenda nje unalipa *ten percent export levy*, unalipa *wharfage* dola 40, unalipa *MoFED* dola 100 halafu uki-*import chemicals* unalipa dola 190 kwa ajili ya *import duty*, lakini bado utalipa *18 percent VAT*. Huyu mtu atahitaji apate *chemical permit*, alipe dola 667, atalipa *railway development levy* ya 1.5, atalipa, wanaita *corridor levy* ya *4.9 dollars*; lakini bado ana *Government taxes*, kuna *workers' compensation*, kuna *municipal levy*, kuna *tax*, kuna *Government chemistry fee*, kuna *OSHA*, *NEMC*, *other crises*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hebu *compare leather sector* na nchi zilizotuzunguka; hakuna *export duty* ya 10 percent ya *wet blue* ukienda Kenya na Uganda. Halafu ngozi zetu zinazozalishwa ndani ya nchi huyu mwenye kiwanda hawezi ku-*process* kwa sababu atakapozalisha kwenda kuuza nje, *the cost of processing wet blue square feet* moja ni dola 30, na soko la dunia ni dola 30 anauza wapi? Hata tujenge viwanda milioni *we cannot*. Ni lazima Serikali itambue kwamba *number one principle* ya biashara ni kutengeneza mazingira *condusive* ya watu wetu waweze kuzalisha *at a competitive rate*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mfano mwingine, nchi ambayo ilifungua soko lake pamoja na sisi ni Vietnam na Waziri ameshawahi kwenda mwaka 1986. Na Waheshimiwa Wabunge tuelewe, viwanda ni vya aina tatu; tunazungumzia *manufacturing, processing and assembling*, hivi ndivyo viwanda tunavyovizungumzia. *Manufacturing and processing* kuna *technological advancement* kila siku, leo tunazungumzia *textile industry*, je, tuna *raw material* ya kutosha kulisha viwanda vyetu tulivyonavyo? Je, tumeweka mpango gani wa ku-*invest* katika uzalishaji wa *raw material*? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunazungumzia mafuta, nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, kwa mwaka tunatumia dola milioni 240 ku-*import* mafuta ya kula katika nchi yetu. Lakini tunahitaji shilingi ngapi kuondoa hili tatizo? Mpango uliopo kwenye *African Development Bank* wa *African Edible Oil* ili sisi tuondokane na *importation* ya mafuta ya kula katika nchi *we only need 45 million US dollars* ili tuweze kulima michikichi ambayo tutazalisha mafuta, tutaondokana na tatizo la ku-*import* mafuta, *where is the plan*? Hakuna! Hela ipo kwenye *ADB*, ni *accessible*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani, Dkt. Magufuli ataimba, ndiyo maana kila siku anabadilisha sheria huko *State House*, *because the old man is frustrated*. Anaongea hivi *it seems like yeye yuko mbingu ya saba wengine tuko kwenye ardhi*, *what is the problem*? Wizara ya Viwanda na



Biashara *what is the problem?* Wizara ya Fedha *what is the problem?* Wizara ya Kilimo *what is the problem?* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia hapa ndugu yangu Mheshimiwa Ulega anazungumzia *exportation* ya nyama. *70 percent* ya ngozi tunayoizalisha katika nchi yetu ni *grades four, five, six and seven*, hatuna ngozi ya *grades one, two wala three* katika nchi yetu. *Why? Because* hatujafanya *proper breeding* ya mifugo. Hakuna mpango, Wizara ya Mifugo ukisoma huu mpango wa mwaka mmoja Waheshimiwa Wabunge Serikali inapanga eti kutafuta madume kumi ya kupanda ng'ombe, hivi mnajua madume kumi ni shilingi ngapi, ni *20 million shillings, this is the plan, it is here*, iko humu kwenye mpango. *There is no seriousness.* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naendelea kusema, ili tutoke hapa mimi natoa ushauri tena, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara kama hautaamua...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Bashe, kwa mchango wako.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maria Kangoye, Lucy Mayenga na Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ajiandae.

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa uthubutu mkubwa wa kuwa na nia ya kujenga Tanzania ya viwada. Vilevile

niipongeze sana Wizara kwa jitihada zake chini ya Waziri, Mheshimiwa Mwijage, Naibu wake, Mheshimiwa Stella Manyanya, pamoja na Katibu Mkuu, Profesa Elisante, kwa kweli jitihada zenu zinaonekana. Hivyo basi, tunazidi kuwatia moyo, tupo nyuma yenu, tutazidi kuwashauri kadri tuwezavyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote nipende kumkumbusha Mheshimiwa Waziri kwamba Mkoa wa Mwanza uko tayari kwa ajili ya uwekezaji mpya wa viwanda vipya. Kila Wilaya imeshatenga maeneo kwa ajili ya viwanda. Kwa mfano Magu imeshatanga maeneo Isangijo, Bundirya; Wilaya ya Ilemela imeshatenga Nyamongolo na Sangabuye, na Wilaya nyingine hivyo hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyojua kwamba Wanamwanza ni wakarimu, hali ya hewa ya Mwanza ni nzuri, lakini vilevile tupo tayari kuwakaribisha hawa wafanyabiashara wawe wadogo ama wakubwa. Kwa hiyo tunaomba Mheshimiwa Waziri utusaidie sana kutukaribishia na kutupa ushirikiano katika kuwaalika wawekezaji hao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ilemela ina Kiwanda cha Ngozi cha *Mwanza Tanneries*. Mwaka jana nilisimama hapa nikaomba Serikali izeze kumnyang'anya yule mwekezaji aliyekuwa amepewa kwa sababu alikuwa amekitelekeza. Ninaishukuru sana Serikali, kupitia Mkuu wa Mkoa wa Mwanza imeweza kukiridisha mikononi mwake. Sasa ninachoomba ni kwamba mtuletee mwekezaji katika kiwanda kile kwani maeneo yale kuna chuo na wanachuo wale wanakosa sehemu ya kufanya *field*. Kwa hiyo, vilevile itasaidia wanafunzi kupata *field* na itatoa ajira kwa akina mama na vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyojua, pamba ni ajira lakini ni uchumi hususani katika Mkoa wetu wa Mwanza, na wanawake na vijana wanategemea kipato kutoka katika zao hili. Hivyo basi, nichukue fursa hii kumkumbusa Mheshimiwa Waziri kuhusu ule mpango wa kuvifufua viwanda

vya kuchambua pamba vya *Nyambiti Ginnery* na *Ngasamo Ginnery* ambavyo tunaamini kabisa vitaongeza ajira kwa vijana lakini pia pamba yetu itaweza kuchambuliwa pale pale na kutengeneza nyuzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Waziri, kwa sababu hili suala lipo mezani kwake kwa muda mrefu, atakapokuja ku-*wind up* atueleze ni lini viwanda hivi vitafufuliwa, kwa sababu wananchi wa Kwimba wamekuwa wakihangaika kupeleka pamba yao mbali wakati viwanda vipo pale na vina uwezo wa kufufuliwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme Wizara hii ya Viwanda imekuwa ikionesha nia nzuri na imekuwa ikifanya kazi nzuri, lakini nashindwa kujua ni kwanini Mheshimiwa Waziri anashindwa kuwa muwazi? Yapo masuala ambayo yanawakwamisha na sisi tunayaona lakini kwa namna moja ama nyingine yeye inabidi *admit* na aseme na awe *aggressive* juu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano zipo hizi *associates* za Wizara yake kwa ajili ya kujenga viwanda. Kwa mfano iko *TRA, TFDA, NEMC, TBS, OSHA* na mengineyo kama yapo; hizi taasisi ni muhimu sana katika ujenzi wa viwanda. Pia zimekuwa zikiangusha sana Wizara hii. Kwa nini nasema hivyo zimekuwa na mlolongo mrefu, urasimu mrefu sana wa kutoa vibali. Vilevile kwa namna hiyo tumekuwa tukiwakatisha tamaa wafanyabiashara na wawekezaji wengi sana. Hivyo basi Mheshimiwa Mwijage simama kifua mbele uzikemee na uwe *aggressive* kama navyosema. Ni lazima useme ili yaweze kusunga mbele kama kweli tuna nia ya kumsaidia Mheshimiwa Rais kutimiza azima yake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa mfano leo hii unataka kufungua kiwanda na unapaswa kupata *certificate* ya *TFDA* utaambiwa lazima uje ukagulie *premises* zako. Kitendo cha kumpata afisa kuja kukagua *premises* inaweza ikachukua miezi miwili/mitatu na bado akifika pale atasema sawa naomba urekebishe hiki na hiki na hiki ukimaliza niite. Kitendo cha kumuhitaji tena inaweza ikachua miezi kama ile ile bado

bidhaa yako umeipelekea *TFDA*, ipo kule inakaguliwa, kitendo hicho nacho kinaweza kikachukua miezi mingi. Mimi napenda ku-*declare interest*, kwamba mimi ninakiwanda changu ndiyo, lakini leo ni miaka miwili ninashughulikia kupata leseni na mpaka hivi naambiwa leseni yangu nembo yangu ya *TBS* ipo tayari lakini mpaka leo hivi sijaipata na hapo mimi ni Mbunge, je, wale wananchi wa kaaida wanafanyaje? Ni lazima tutafakari haya masuala ili tuweze kuisaidia nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masoko, bado Serikari haijaonesha nia ya kulinda bidhaa za Kitanzania kwa sababu kumekuwa na mambo ambayo yanakwamisha bidhaa hizi. Tukianza katika kodi nyingi ambazo zinatozwa juu ya bidhaa hizi, tukiangalia malighafi ambazo zinaletwa ndani ya nchi zinatozwa kodi nyingi katika bandari yetu. Leo hii bidhaa za kitanzania ni gharama kuliko hata bidhaa zinazotoka nje, hivi unategemea nini? Kwa na namna hii tunauwa viwanda na tunawakatisha tamaa wawekezaji wadogo kwa wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshauri Mheshimiwa Waziri, lakini si ushauri kwa sababu ni jambo ambalo nalifahamu, nikukumbueshe kwamba tunao mabalozi wetu nje ya nchi unaweze kuwatumia kututafutia masoko. Vilevile mkae muangalia namna ya kuweza ku-*regulate* hizi kodi ndogo ndogo ili tuweze kumwezesha Mtanzania kuuza katika bei nzuri na bidhaa zao ziwe katika soko. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko mengi sana juu ya *TRA*, hasa pale inapojipangia bei ya bidhaa za wafanyabiashara wanazoagiza kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii wafanyabiashara wengi wamekuwa *forced* kususia bidhaa zao bandarini kwa sababu wana-*estimate* bei kubwa ambazo wanajua wao lakini kodi pia inakuwa kubwa. Kwa hiyo, kunakuwa hakuna haja ya mfanyabiashara yule kutoa kodi kubwa na bidhaa ile isiwe na faida. Kwa hiyo, iko haja ya Serikali kukaa na kutathmini ufanyaji kazi wa hizi taasisi. Tunazipenda sana,

tunafahamu umuhimu wake katika kuijenga Tanzania ya viwanda. Hata hivyo kama haitafanya kazi zake kwa ufasihi ni lazima tuzirekebishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa machache hayo naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba na Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii walau na mimi ya kuweza kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutoa pongezi nyingi sana kwa Waziri huyu wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, pamoja timu nzima katika Wizara ya Viwanda, Katibu Mkuu, Watendaji wote *FCC, TBS, TRA* na wengine wote huko chini ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze tu yaani kwa kusema maneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ukianza Waziri pamoja na watendaji wako ichukuliwe kwa umuhimu wa kipekee, mtoke nje. Jana iligusiwa kidogo na Mheshimiwa Spika wetu, na mimi kitu ambacho nimekuwa nikikifikiria sana Wizara hii kuna baadhi ya watendaji kule chini ambao vitu vingi sana wanavifanyia mezani, hawajui *on the ground*, kwenye hali halisi kule mambo jinsi yalivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi ninaomba na biashara ni ushindani na baishara msingi mkubwa wa biashara ni *connection*. Kwa hiyo, Waziri wetu pamoja na watendaji wote, Wakurugenzi yaani mimi nitafurahi sana endapo kama nitaanza kusikia Mkurugenzi wa *FCC*,

Mkurugenzi wa *TBS* wamekwenda huku na huku, wasikae ofisini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi kazi zao si kazi za kusubiri tu kwamba mtu amefanya makosa ndipo aje huku kuja kmsughulia, inatakiwa na wao waende *on the ground*, waende kule kujifunza. Ninasema hivyo kwa sababu gani, kuna nchi jirani zawenzetu ambazo tunapakananazo, haiwezewekani sisi tukawa na urataibu mwingine nchi za wenzetu zikawa na utaratibu mwingine, Serikali inakosa mapato. Mfanyabiashara yoyote duniani hata kama mtu mkiwa mama ntilie nia yake anataka apate faida na sio tu faida akipa upenyo wa kuongeza faida kubwa yeye kwake ndiyo anaona ndiyo mafanikio ya baishara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokaa kuzungumzia uchumi, uchumi ni biashara, hauwezi kutenganisha uchumi na baishara. Sasa basi nikupe tu mfano kwa mfano sisi kama Watanzania kwa wezetu ambao ni wafanyabiashara kuna bidhaa ambazo kwa nchi za wenzetu kule kwao ni *zero tariff*. Lakini hapa kwetu tumeziwekea *tariff*, lazima na sisi tuweze kuangalia kwa nini wale wenzetu kule wamefanya hivyo ili nasi huku tuweze ku-*react* haraka. Kwa sababu kwa mfanyabiashara ambaye anajua biashara ataona kwamba nikiingiza Tanzania nitapata hasara, kwa hiyo atakachokifanya ataenda kukimbilie kuingiza huko jirani kwenye nchi za wezetu jirani ambako kule zinaingia kwa bei ya chini alafu baadae zitakuja kuigia huku Tanzania. Kwa hiyo mimi nilikuwa naomba sana Serikali iweze kuangalia kuhusu hili suala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ninapongeza sana hii Wizara na ninampongeza sana Mheshimwa Rais. Hata leo hapa tunavyozungumza ni miaka takribani miaka miwili na wala si miaka mingi sana, lakini wamefanya kazi kubwa sana wanajitahidi sana. Mheshimiwa Waziri usijali baadhi ya madongo unayopigwa pamoja na wenzako, madongo hayo unayopigwa mimi huwa wakati huwa najjuliza natamani na huwa mara nyingi sana nasema kwamba natamani yaani huwa wakati mwingine nasema

kwamba ndiyo maana sasa nailewa baadhi ya nchi duniani viongozi waliopita kwenye nafasi mbalimbali kama Mawaziri, Makatibu Wakuu na kadhalika kuna baadhi ya nchi huku Mawaziri walikuwa wanapigwa mawe na wanafanyiwa hivi kwa sababu ya mambo waliyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hi inapata matatizo mengi sana na Serikali hii imekuwa ikipata mataizo mengi sana kwa sababu ya *system* ambayo ilikuwa imeoza iliyopita. Nitoe mfano, utaratibu wa *TRA* wa zamani maana na mimi si mfanyabiashara mkubwa, lakini walao nakaaka karibu karibu na wafanyabiashara, utaratibu wa *TRA* wa zamani ilikuwa ni kwamba mtu lazima utoe rushwa ili mambo yaende, ilikuwa ni kwamba lazima utoe rushwa huku na huku ndipo mambo yako yaende. Sasa basi mfanyabiashara/mtu yoyote ambaye anataka biashara yake na apate faida alikuwa anaona kwamba huo ndiyo utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa sababu huo ndio utaratibu wafanyabiashara walikuwa wanalazimika kufanya vitu ambavyo vilikuwa wakati mwingine ni kinyume na maadaili.

Sasa ninachoiomba Serikali kwa sasa hivi tujaribu kukaa chini kuangalia, hawa wafanyabiashara si watu wa mataifa mengine, baadhi yao ni Watanzania wenzetu. Hata kama mtu akiwa pengine labda ana rangi tofauti lakini bado pia ni Mtanzania mwenzetu, wapo hapa Tanzania wanataka kuendelea kufanya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tusiendeleo na yale mambo ya kukaa kuangalia yaani wao ni kwamba kama sheria imekaa, kama kanuni na taratibu tumekaa, tumesema kwamba hawa watu walifanya mambo mabaya tukae nao, najua kwamba Serikali kamba imekaa nao imewasikiliza, imeweza kuangalia kwamba wewe ulikwepa kodi mwaka fulani, lakini baada ya hapo tujiulize huyu mtu anaendelea na biashara au haendelei? Kama anaendelea Serikali iweze kumwangukia kwa macho mawili na kwa ukaribu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile isichukuliwe sasa kwamba mfanyabiashara kwa sababu miaka ile ya nyuma alikuwa labda pengine inasemekana kwamba aliwahi kukutwa tuhuma za kufanya jambo fulani, kwa sasa hivi anaendelea kuzibiwa kwa asilimia 100. Tusiendeleo kufanya namna hivyo sisi tunachotaka hizi kodi zitusaidie kwenye nchi yetu nchi yetu ili nchi ipate pesa. Hawa wafanyabiashara hawajakimbia nchi, wapo wengine ambao si wazalendo wameamua kukimbia nchi, lakini hawa wafanyabiashara kama walikuwa na madeni yao kaeni nao huko mkubaliane nao kwamba watalipaje hizo pesa walipe Serikali ipate pesa. Lakini tusiendeleo kusema kwamba wafanyabiashara fulani, kwa mfano labda Lucy Mayenga huyu inasemekana kwamba alikuwa anafanya jambo fulani basi ndo anakuwa ameharibika kiasi kwamba mpaka sasa hivi hata akiingiza mizigo yake anapata usumbufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiendelea kufanya namna hiyo biashara za watu zitakufa, kodi ambazo sisi kama Serikali tumekuwa tukifikiria kuendelea kuzipata hatutaendelea kuzipa kama inavyotakiwa. Pamoja na hayo ninataka kwamba Serikali iendeleo kufanya utaratibu kama inavyotakiwa. Kinachotokea sasa hivi kwa hilo ambalo linaendelea ni nini, kwa mfano mimi kama mfanyabiashara nina kampuni yangu inaitwa X inaonekana kwamba labda inasakwama sana kutokana na mambo ambayo labda pengine nilifanya huko nyuma, labda pengine tumekaa chini tumekubaliana kwamba jamani nilikuwa nadaiwa nitalipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anaamua sasa, kwa mfano Mheshimiwa Waziri nikupe mfano mmoja, mfano tu mdogo *TIN Number* mpaka mwendesha boda boda anayo. Mimi nikileta leo hii makontena kumi kwa ajili kampuni yangu ninyi kama Serikali mtu akija akanikanidiriya makadirio ya juu natafuta watu wa bodaboda kumi kila mtu pale na *TIN Number* yake anaingia ule mzigo kama vile kwamba ule mzigo ni wa kwake. Kwa maana hiyo sasa Serikali itakosa *income tax* na itakosa *VAT return*. Kwa hiyo, lazima tukae tuangalie, biashara ni vitu lazima wakati wewe unafikiria (a) uangalie (b), (c) na (d). *(Makofi)*



Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niongezee tu hapo; kama sisi tunafahamu Serikalini kwamba asilimia 30 ya pato la Taifa linatokana na wafanyabiashara wakati na wadogo lazima tuangalie kwamba tunawezaje kuweka mazingira mazuri. Mheshimiwa Rais amekaa na wafanyabiashara, uamuzi wa Mheshimiwa Rais kukaa na wafanyabiashara si uamuzi mdogo. Ameamua kukaa na wafanyabiashara kwa sababu anachotaka haya mambo na malalamiko anataka kwamba watu wakae tuanze upya, kazi zianze kufanyika upya na mabo yakae yawe sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabla sijagongewa kengele ninachoomba kusema, ninaomba kusema ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara, ninaomba na sisi wanasiasa kwa ujumla na hasa sisi Wabunge tusiwe madalali wa wafanyabiashara. Sisi kwenye Kamati yetu tulikuwa na Mheshimiwa Munde Tambwe, tumekaa kuna baadhi ya vitu tulikuwa tumekaa tukasema hivi hatuvikubali. Kuna mtu mmoja ambaye alikuwa ni mfanyabiashara anadiriki mpaka kiwango cha kuongea lugha mbaya na bahati yake ni kwamba sisi hatukuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kusema kwamba kwenye mambo ya msingi, mambo ya uchumi mambo ya kulitakia mema Taifa letu lazima sisi wana siasa tuanze kwanza, hata kama ukiongea uongee yale ambayo unaona kabisa kwamba haya ni mambo ya ukweli ili kuweza kulisaidia Taifa letu. Tusikae tu kwa sababu sisi tuna *interest*, una *interest* zako binafsi huko pembeni unataka watu wote wakukubalie waseme ndiyo, *for what?* Ni kitu ambacho hakiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho kabisa kabla sijagongewa kengele, shilingi bilioni kumi na tatu za kulipa fidia Liganga na Mchuchuma Mheshimiwa Waziri nilikuwa naomba hizi pesa ni nyingi sana. Kabla ya kulipa hizi pesa

bajeti yako ikishapita nenda kajiridhidhishe uangalie pesa hizi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Shukuru Kawambwa ajiandae.

**MHE. LOLESIA M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara kwa kazi kubwa ambayo wamefanya katika Wizara hii ninasema hivyo kwa sababu kuna ongezeko katika pato la Taifa kwa asilimia 0.6 ambalo limechangiwa na sekta ya viwanda. Kwa hii inaonesha jinsi ambavyo Wizara hii inafanya kazi kubwa zaidi katika kuhakikisha kwamba uchumi wetu unaimarika siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nikiangalia malengo yenyewe ya Wizara yenyewe ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwanza kabisa inahakikisha viwanda vilivyopo vinafanya kazi zake vizuri, kwa uhakika na kuweza kuongeza zaidi mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kuhakikisha kwamba viwanda vyote ambavyo vimebinafishwa ambavyo havifanyi kazi vinafanya kazi vizuri. Vilevile kuhamasisha wananchi ili waweze kushiriki katika kuwekeza na kuanzisha viwanda vipya. Hayo ni malengo matatu ambapo Wizara imejiwekeza.

Mimi nitazungumzia zaidi kwenye kuanzisha viwanda vipya. Lazima Wizara sasa pamoja na Serikali kwa ujumla iweke mikakati ya dhati na kuhakikisha kwamba kupitia

mikakati hii itawezesha uwanzishwaji viwanda hivi. Kwa mfano lazima kuwepo na mazingira wezeshi ya uwanzishwaji wa viwanda; kwanza ni kuhusu umeme. Haiwezekani kuanzisha viwanda tusipokuwa na umeme wa uhakikika. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kusimamia msimamo wake wa *Stiegler's Gorge*, ule mradi mkubwa wa umeme; kwa sababu anakusudia tuweze kupata umeme wa uhakika. Vile vile mpango wa Serikali wa *REA* wa kuhakikisha kwamba watazania mpaka vijiji wanapata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Wizara inayohusika ya Nishati kuhakikisha kwamba suala la umeme linakuwa ni kipaumbele cha umuhimu kabisa kwa sababu wananchi vijijini hawawezi kuanzisha viwanda bila ya kuwa na umeme wa uhakikika. Katika mpango wa Serikali wa kwamba kufikia mwaka 2020 na 2021 vijiji vyote vya Tanzania vitakuwa vimepata umeme, niombe Serikali hasa kwa *REA* iweze kuwekeza zaidi fedha nyingi kwenye *REA* ili kuhakikisha umeme wa uhakika unafika vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wananchi wameitikia sana na hii Tanzania ya viwanda wengi hasa walioko vijijini wameitikia sana kuanzisha viwanda. Hata mimi katika Mkoa wangu watu wengi wanafuata wanataka kuanzisha viwanda, lakini changamoto kubwa ni upatikanaji wa uhakika wa umeme hasa vijijini ambako wanataka kuanzisha viwanda. Kwa hiyo niombe Serikali sasa kwamba mwaka huu 2018 itenge bajeti kubwa, hasa kwenye Wizara ya Nishati, kwenye *REA* ili wananchi hasa wa vijijini waweze kupata umeme wa uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia jambo la pili la kimkakati ni suala la elimu. Haiwezekani kuanzisha viwanda ikiwa vijana wetu hawana uwezo, hawana ujuzi wa kutosha wa kuweza kufanya kazi viwandani. Kwa hiyo niombe katika sekta ya elimu pia tuangalie hili suala la kuwa na *VETA* kwenye kila Wilaya kama sera ya taifa inavyosema katika upande wa elimu. Kuna Mikoa mingi ambapo mpaka sasa hatujafikia hatuna vyuo vya *VETA* na Wilaya nyingine hakuna vyuo vya *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niimbe Serikali ijielekeze katika kuhakisha kwamba ile Mikoa na Wilaya ambayo mpaka sasa hawajapata vyuo vya *VETA* wahakikishe vyuo hivi zinajengwa kwa haraka ili kuwezesha wanachi hasa vijana kuweza kupata elimu ya ujuzi katika ufundi ili hatimaye waweze kushiriki vizuri katika viwanda kwa sababu Tanzania ya viwanda haitawezekana bila kuwa na ujuzi wa uhakika.

Vilevile niimbe Serikali iweke pia fedha kwa ajili ya kusomesha vijana wetu nje ya nchi. Kwa sababu kuna ujuzi mwingine tunaupata kutokana kupata kwa wenzetu, nilikuwa nikianagalia katika Awamu ya Kwanza ya Mheshimiwa Rais Marehemu Nyerere watu wengi sana walikuwa wanapelekwa nje kwa ajili ya kujifunza teknolojia na ndiyo maana pia hii sekta ya viwanda ilikuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niimbe katika awamu hii Serikali itenge fedha ipeleke vijana hata kama ikiwezekana vijana wapelekwe nje ya nchi ili waweze kujifunza mbinu na ujuzi mbalimbali ili kuweza kufanya kazi na kuweza kuleta teknolojia mpya katika nchi yetu ili kuwawezesha vijana hao kuweza kufanya kazi zao vizuri, la sivyo viwanda hivi ambavyo vinaanzishwa hasa na wageni kama vijana wetu hawatakuwa na teknolojia wanayojua na ujuzi itakuwa si rahisi kuweza kupata ajira za hali ya juu, watakuwa wanafanyakazi za kada ya chini kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niimbe Serikali katika sekta ya elimu iendeleze zaidi Vyuo vya *VETA* ikiwezekana tufanye kila hata Jimbo, sasa hivi sera ni kila Wilaya lakini niimbe Serikali yaani iwezeshe kila Wilaya sasa ambazo hazijapata *VETA* ziweze kupata Vyuo vya *VETA*. Lakini hapo baadae pia ikiwezekana tuangalie hata kila Jimbo liweze kupata Chuo cha *VETA* kwa sababu vijana wengi sana wanamaliza sekondari, hawana ujuzi yaani hawana uwezo wowote, hawana ujuzi wowote lakini wanapokuwa na stadi za maisha hasa katika Vyuo vya *VETA* mimi nina uhakika vijana hawa wataweza kushiriki vizuri hasa katika Tanzania ya viwanda katika ujuzi waliokuwa nao. (*Makofi*)

## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ni muhimu Serikali iwekeze hasa katika kuwezesha mazao ya kiuchumi. Kuna mazao mengi sana na wakulima asilimia 70 ya Watanzania wanaishi vijijini na ndiyo ambao wanashughulika na suala la kilimo. Tunaiomba sasa Serikali iangalie sana suala la kilimo kwa sababu haiwezekani kuweza kupata malighafi tusipowekeza katika suala zima la kilimo. Kwa hiyo, niombe Serikali iangalie kabisa hata katika maeneo ambapo tumezungukwa na maziwa kwa mfano, Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika na maziwa mengine tuweke hata kilimo cha umwagiliaji ili kuwezesha upataikanaji wa mazao ya malighafi kwa ajili ya viwanda vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kikubwa zaidi wananchi wengi wa Tanzania wamehamasika sana katika hii sera ya Tanzania ya viwanda, watu wengi wamehamasika, wanataka kuanzisha viwanda, changamoto tu ni hizo, mambo muhimu kabisa hilo suala la elimu naomba Serikali izingatie na suala la umeme iwe ni kipaumbele cha uhakika ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanashiriki kikamilifu katika suala zima la viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la biashara, katika biashara ni kweli wafanyabiashara wengi wanazo changamoto nyingi sana. Nilikuwa ninaomba Wizara kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara tuwe na muda wa kwenda kukaa na wafanyabiashara hata katika maeneo yao vijijini. Tumezoea tu mikutano mingi inafanyika mijini, tuombe na vijijini pia wako wafanya biashara ambao wanahitaji pia tukae nao, tuangalie changamotoyo zao hatimaye tuweze kutatua kero zao walizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwasababu nimekuwa na *experience* katika Jimbo langu kuna sehemu kubwa kuna *centre* ya biashara kunaitwa Katoro kulikuwa na changamoto kubwa watu wengi wanafanya biashara nyingi lakini sasa kumekuwa na changamoto za hapa na pale, *TRA* inasumbua, sijui zimamoto yaani wanakuwa na changamoto nyingi sana lakini Serikali kupitia Wizara husika ikipata fursa kwenda kukaa na hao wafanyabiashara itaweza

kusikiliza kero zao na hatimaye watakuwa na mazingira mazuri kabisa ya kuweza kufanya biashara na hatimaye sasa tutaweza kufikia lengo la taifa la kufikia uchumi wa kati kama ambavyo tumejipangia.

Kwa hiyo, niombe, nituie fursa hii kuomba Wizara tutoke nje kama wezangu walivyosema, tusijifungie tu ofisini, twende *field*, twende vijijini, twende mijini, tukae na wafanyabiashara tusikilize kero zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia changamoto nyingine katika biashara nimeona kwa sasa hivi watu wengi wamejikita kuchukua bidhaa kutoka Uganda. Sasa nilikuwa najjuliza kwamba kwanini hapa Kariakoo sasa watu hawaendei kuchukua bidhaa? Siku za nyuma tulikuwa tumezoea watu walikuwa wanatoka Zambia na sehemu mbalimbali wanakuja Kariakoo wananunua bidhaa wanakwenda kuuza kwao lakini sasa hivi imekuwa tofauti. Watu wengi wanakwenda kununua bidhaa Uganda kwa hiyo, ninaomba Wizara pia iangalie hili ni kwanini sasa watu wanakwenda Uganda kuliko kwamba watu wa Zambia na watu wa Uganda waje Tanzania kununua bidhaa ili waende wakauze huko kwao.

Kwa hiyo, niombe jambo hili Serikali ilifanyie kazi, ilifanyie utafiti wa kutosha kwamba ni kwanini bidhaa nyingi watu wanakwenda Uganda isiwe Tanzania ambapo Tanzania tuna bandari, tuna kila kitu, tunajenga *standard gauge* yaani tunafanya vitu vingi. Sasa ni kwa nini badala ya watu kuja Tanzania kununua bidhaa sasa wanakwenda Uganda kununua bidhaa kwa ajili ya kuuza katika nchi yetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu maana yake tunapoteza pato la Taifa, tunapoteza uchumi...

## T A A R I F A

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Tusipolifanyia kazi jambo hili pengine tunaweza tukapoteza watu wengi,...

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** ... tunaweza tukapoteza biashara...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa subiri kidogo, taarifa! Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka nimpe taarifa mchangiaji, anashangaa anasema kwa nini watu wananunua bidhaa Uganda badala ya kununua bidhaa zetu. Kwa kweli kusema ukweli bidhaa zetu Watanzania gharama za uzalishaji ni kubwa sana, hakuna katika nchi za Afrika Mashariki ambapo kuna bidhaa ghali kama Tanzania hiyo ndiyo sababu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lolesia.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante...

**MWENYEKITI:** Na wewe mjibu tu hapo hapo.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kama yeye sababu yake ndiyo hiyo lakini ninatoa ushauri kwa Serikali waende walifanyie kazi jambo hili kwa sababu tunaona changamoto ipo na watafute namna sasa kujua, kufanya utafiti wa kutosha ili hatimaye wajiridhishe kwamba ni sababu gani na hatimaye hiyo sababu waweze kuifanyia kazi mwisho wa siku Tanzania basi tuwe *hub*, tuwe soko ambapo watu wengi watatoka sehemu mbalimbali nje ya nchi kuja kununua bidhaa katika nchi yetu ya Tanzania kama ilivyokuwa zamani. Kariakoo ilikuwa inajulikana ni sehemu ambapo watu walikuwa wanatoka Congo, wanatoka Zambia, wanatoka sehemu mbalimbali kuja kariakoo kwa ajili ya kununua bidhaa mbalimbali.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Kwa hiyo, niombe Serikali jambo hili ilifanyiekazi na Mheshimiwa Waziri pengine uunde *task force* ya kuweza kulfanyiakazi jambo hili ili kuhakikisha kwamba uchumi wa Tanzania uendelee kwenda juu pamoja na kwamba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa atafuatiwa na Mheshimiwa Cecil Mwambe na Mheshimiwa Devotha Minja ajjandae.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa fursa hii ya kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara. Nitangulize kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na kwa utekelezaji mzuri wa ilani, nampongeza yeye, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na watendaji kwa utekelezaji mzuri wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa utekelezaji wa mkakati huu wa ujenzi wa viwanda. Hili jambo ni jambo adhimu, ni jambo zuri ambalo litaweza kutupelekea sisi mwaka 2025 kufikia hadhi ya nchi ya uchumi wa kati na hili ni jambo la ukombozi pia kwa vijana wetu wa kike na kiume wa Tanzania kwa sababu katika matatizo makubwa ambayo vijana wanayapata ni tatizo la ajira, hili ni tatizo namba moja. Kila kijana awe wa chuo, awe wa shule ya msingi, awe wa sekondari na kadhalika shida yake kubwa ni ajira na viwanda ni ajira kwa hivyo tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa mkakati huu wa ujenzi wa viwanda katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepanga vizuri na kutenga maeneo ya *EPZ* na *SEZ* na maeneo haya ni maeneo



## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

muhimu sana yanatoa fursa moja nzuri sana, yanatoa fursa ya kujenga viwanda katika mpangilio mzuri na katika hali ambayo mazingira yanalindwa vizuri kwa maana unaweza mkaamua kwamba hapa ni viwanda vya madawa, hapa vya nguo, kule vya chuma na kule vya chaki bila muingiliano usiokuwa na mpangilio kwamba mtu anaamua huyu anaweka hapa cha tofauli na mwingine anakuja hapo hapo anaweka cha *battery*, mwingine anakuja hapo hapo anaweka kiwanda cha alizeti, kwa hiyo inakuwa shaghala baghala hakuna mpangilio mzuri. Naiomba Serikali yetu iweke mkazi mkubwa iweze kuhakikisha kwamba maeneo maeneo haya ya *EPZ* na *SEZ* yanafanyiwa kazi kwa umuhimu na kwa haraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1979 China iliamua kwamba itenge eneo la mfano la viwanda ikachangua *SEZ* ilikuwa na watu 30,000 tu pale sasa hivi ina watu zaidi ya milioni 11 na viwanda ambavyo vina mpangilio mzuri na vinatoa tija kubwa sana na huo ndiyo mfano ambao inabidi twende nao na kwa haraka. Tumechukua muda mrefu sana, tumezungumza sana lakini vitendo vimekuwa nyuma, kwa hivyo sasa ni wakati ambao Mheshimiwa Rais ameshaweka nia yake lazima tufanye sasa huu ndiyo wakati sasa wa kuweza kutekeleza jambo hili kimakini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Bagamoyo Serikali imetenga eneo la *EPZ*, imetenga kwa awamu mbili, awamu ya kwanza jumla ya hekta 5,742 kwa ajili ya ujenzi wa viwanda na mpaka hivi sasa tayari imeshalipia hekta 2,399 isipokuwa kuna wananchi 1,025 ambao mpaka hivi sasa hawajalipwa fidia zao katika maeneo hayo, kwa maana ni miaka 10 sasa tangu eneo hili limetengwa na wananchi wakatathminiwa lakini hawajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale ninaposema kwamba tufanye uharaka, basi uharaka unaanzia kupata ardhi ambayo iko *free*, haina tatizo na mwananchi yoyote kwamba walipwe hawa mapema iwezekanavyo ili eneo hili sasa wawekezaji waanze kulitumia kwa ajili ya kujenga viwanda ambavyo viko katika mpangilio mzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba sana Mheshimiwa Waziri, juhudi kubwa najua anaifanya lakini kwa sisi kule Bagamoyo nguvu zake tutazona tu kwamba zimekuwa za kutosha kama pale ambapo tutakuta kwamba fidia hizi zimelipwa kwa haraka ili eneo hili liweze kuwa *free* na viwanda vianze kujengwa bila hivyo ujenzi wa viwanda unakuwa mgumu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na stahiki ya fidia hii na hasa kwa sababu najua kwamba sasa hivi mwekezaji ana jukumu la kulipa fidia na kwa hiyo wawekezaji hawa wapo tayari kulipa fidia, basi niombe Serikali ifanye haraka sana kuweza kuwapa ruhusa au kuwasukuma ili waweze kulipa fidia zao mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili la *EPZ*, eneo la Awamu ya Pili la *EPZ* jumla yake ni hekta 3,338 hili eneo hili linajumuisha maeneo yenye makazi makubwa ya wananchi na limeingia kwenye *EPZ* bila ya wananchi kuridhia kwamba liingie kwenye *EPZ*. Linajumuisha Kijiji cha Zinga, Kijiji cha Mlingotini, Kijiji cha Pande na Kijiji cha Kiromo na Kijiji cha Kondo. Vijiji hivi ni vya zamanai na vimejengwa, vina wananchi wengi sana wamejenga kwa miaka mingi wako mle tayari wameshatoa eneo la zaidi ya hekta 5,000 kwa ajili ya *EPZ*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaomba chonde chonde tafadhali Mheshimiwa Waziri wananchi hawa waruhusiwe kuishi katika maeneo yao haya kwa amani na usalama na hasa kwa kuzingatia kwamba wameshatoa maeneo ya kutosha kwa ajili ya *EPZ* eneo ambalo ni mji mzima kabisa tunaweza tukapata *SEZ* nyingine katika Jimbo la Bagamoyo kwa kuchukua tu eneo lile ambalo tayari limeshakubaliwa katika awamu ya kwanza. Naomba kwa heshima na taadhima Serikali ikubali kuwaaachia wananchi hawa jumla ya kaya 3,381 kwa sensa ya mwaka 2012 ama wananchi 12,797 hawa wataathirika maeneo yao ambayo tayari yameshajengwa, ni vijiji vinavyojulikana kuingizwa kwenye *EPZ* na kuambiwa kwamba waweze kuondoka kwa ajili ya kujenga viwanda.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Waziri utakuwa umefanya jambo zuri sana na la muhimu sana kwa wananchi hawa kama utaweza kusimamia kuhakikisha kwamba wananchi hawa wanaweza kuendelea na maisha yao kwa amani na usalama katika maeneo haya bila kubughudhiwa tena kuweza kuhama kupelekwa maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili la *SEZ* Bagamoyo kuna eneo la ujenzi wa bandari ambalo waziri anahusika moja kwa moja na analisimamia kwa uzuri na alifuatilia, ameshafanya safari mpaka China kwa ajili ya kufuatilia ujenzi wa bandari hii, lakini wananchi hawa wanaopisha ujenzi wa bandari, jumla ya kaya 460 wao wananchi hawa mpaka hivi sasa hawana eneo mbadala la kwenda kuishi na kwa bahati Serikali iliwahi kuahidi kwa maandishi kwamba watapewa eneo mbadala la kwenda kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu tukufu, namuomba Mheshimiwa Waziri chonde chonde ahakikishe wananchi hawa wa Kijiji cha Pande na sehemu ya Kijiji cha Mlingotini ambao wanapisha ujenzi wa bandari wapatiwe eneo lile la makazi mbadala ili waende wakaanze maisha mapya katika eneo hilo ama sivyo watakuwa ni watu ombaomba tu ambao tutakutana nao miaka inayofuata hawana mahali pa kuishi, wako hovyoy, wanamuangalia Mbunge wanamuona hafai, hana maana kwa maana kwamba wao walikuwa wamekaa mahali pazuri, wanapopapenda lakini sasa leo imekuja bandari imewafanya wawe watu ombaomba, watu masikini wa kutupa. Naiomba Serikali chonde chonde ihakikishe kwamba suala la *resettlement* kwa wananchi hawa wa Pande na Mlingotini ambao tayari walikuwa wameshaahidiwa na Serikali basi waweze kupatiwa maeneo yao waweze kuanza maisha mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo ninashukuru sana, ninaunga mkono hoja, ahsante sana.  
(*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Mheshimiwa Cecil Mwambe atafuatiwa na Mheshimiwa Minja na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hotuba iliyoko mbele yetu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na uwekezaji. Nianze moja kwa moja kwa kumshauri Mheshimiwa Waziri...

**MWENYEKITI:** Wewe una dakika kumi.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kumshauri Mheshimiwa Waziri kwamba aliyetufikisha hapa ni yeye mwenyewe Waziri kwa sababu mara nyingi anapoongea na kutaka kuli-*address* Bunge au hata ku-*address* Taifa amekuwa akitumia neno moja anasema mimi ni mzee wa *sound*. Hili jambo linamharibia yeye, lakini pia linatuharibia na sisi kama nchi. Hata hivyo wanaotakiwa kumsaidia nao wanapata akili ile ile kwamba tunatakiwa tupige *sound* ili tuweze kufika mahali fulani, sasa athari zake ndiyo hizo ambazo tunazona leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa tu mifano michache, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara lakini pia ni Waziri Kivuli kutoka kwenye Serikali yetu ambayo tunategemea Mungu akitujaalia tutakuja kuiongoza hii nchi, nitakuwa Waziri wa Viwanda na Biashara na sitegemei kama nitafanya kama ambavyo kaka yangu Mheshimiwa Waziri hapa anafanya kwa sababu kwa vyovyote vile tunataka kulisogeza hili Taifa letu mbele. Ndiyo maana juzi wakati ninatoa mchango wangu nilijaribu kuwakumbusha ndugu zangu Wabunge kwamba lazima tuangalie kwanza uzalendo na kulitetea Taifa letu ili tuweze kujua tunakwenda wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Chama cha Mapinduzi ndiyo ambayo sasa hivi kaulimbiu yake ni masuala ya viwanda kwamba tutakapofika mwaka 2020/2025, basi nchi yetu iwe ya viwanda. Lakini nimwambie tu Mheshimiwa Waziri kwamba ameanza vibaya jukumu hili. Tukiwa kwenye

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Kamati tuliletewa taarifa kwamba mpaka sasa Tanzania kuna viwanda 53,050 viwanda hivyo ambavyo Tanzania tunavyo mpaka sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Jimboni kwangu sina kiwanda kile ambacho kipo wananchi wanakifahamu kwamba hiki ni kiwanda na ile tafsiri ya viwanda iliyozoeleka kwenye mitaa yetu, lakini tumeona wamezidi kuwapa jukumu pia sasa hivi kutoka TAMISEMI wamekwenda kuwapa majukumu Wakuu wa Mkoa na wengine kwamba kila Mkoa lazima wamhakikishe wamepata viwanda 100. Wanachokifanya sasa hivi ni kwamba Mkuu wa Mkoa anaamua, anatafuta watu 25 wenye uwezo wa kuwa na cherehani nne, nne halafu analeta taaifa kwamba tumefanikiwa kupata viwanda 100. Sasa hii hatuwezi kwenda vizuri. Tunachotaribu sisi kuangalia ni vile viwanda vya kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuomba ile taarifa kwamba nchi yetu ina viwanda 53,000 na mimi nilitamani nivijue ili kama inawezekana basi niweze kufahamu Jimboni kwangu kuna viwanda vingapi, lakini bahati mbaya kabisa na Mheshimiwa Naibu Waziri nilimkumbusha kwenye kikao chetu cha mwisho cha Kamati mpaka tunaingia hapa hiyo taarifa sijaipata, sijui kama wajumbe wenzangu, Mwenyekiti au Makatibu wa Kamati kama walipata hiyo taarifa inayoonesha Tanzania tuna viwanda 53,000 kwa sababu nilitaka tuvifahamu kwa majina ili tuweze kuwasaidia ndugu zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tena sasa kiti chako watuambie hizo taarifa, walisema ni *document* kubwa sana tukaomba basi tupate *in software* ili iweze kutusaidia kuvitambua hivyo viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wanapoongelea habari ya viwanda, ukienda kwenye kitabu chao cha hotuba, ukienda ukurasa wa 13 kwenye taarifa ya Mheshimiwa hapa waziri anasema miradi mipya ya viwanda, sasa sehemu ambayo sijaielewa na nitaisoma kidogo kama alivyoelezea

yeye; kuanzia Julai, 2017 mpaka Machi, 2018 jumla ya miradi 243 yenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 4,169.11 inatarajiwa kuajiri watu 49 ilikuwa imesajiliwa, wanaiongeza hiyo wanasema kwenye miradi mipya ya viwanda. Mimi nilitegemea kama Bunge au kama sisi Watanzania tulikuwa tuna *interest* ya kusikia bada ya kusajili nini kimefanyika, usajili tu peke yake haitusaidii, kwa hiyo, tumeleta hapa habari ndefu sana lakini kimsingi tunataka tusikie mwishoni nini kimefanyika baada ya usajili huu. Hii ndiyo maana tunasema tunakwenda mbele na tunarudi nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kuangalia pia kwenye kitabu chao hiki hiki, tunajaribu kuongelea hapa wanasema viwanda mama na miradi ya kielelezo. Tumeona hapa wabunge wengi sana wanaongea habari ya Mchuchuma karibia asilimia 50 ya Wabunge walioongea kuchangia kwenye hii Wizara wanaongea habari ya Mchuchuma. Huko Mchuchuma tunakoongea sasa hivi pesa ya Mchuchuma na Liganga pesa iliyotengwa ni karibia shilingi bilioni 10 ambayo inakwenda kufanya nini kimsingi bado haijasemwa moja kwa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania hii ni nchi ambayo kwa vyovyote ili tuweze kwenda sawa sawa lazima tuangalie wenzetu walivyopita waliopita walikuwa wanafanya nini kama ambavyo Mheshimiwa Mariam Ditopile pale alijaribu kushauri kwa sababu hizi *regime* lazima zipokee kijiti kutoka kwenye *regime* iliyopita. Tumeona sasa hivi kulikuwa kuna utaratibu wa *Mtwara corridor*, Serikali ya Awamu hii ya Tano imesahau kabisa habari ya *Mtwara corridor* na hii inajithibitisha wazi wazi tunapokwenda kuongea habari ya Mchuchuma, tunakuja hapa tunaita Mradi wa Mchuchuma na Liganga ambao ni mradi mama na mradi kielelezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kwenda kuchimba chuma, nchi za Ulaya pamoja na china walipofanya mapinduzi ya kiviwanda wao walitegemea sana chuma. Chuma ndio kiwanda mama ili uweze kujenga kitu kingine chochote unahitaji kupata chuma. Unaambiwa pale

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mchuchuma na Liganga tukiamua ile kuchuma chuma yetu tuna uwezo wa kujitoshleza chuma kama sisi wenyewe kama nchi, lakini pia tuna uwezo wa kuichukua hii chuma tukaipeleka nchi za nje kwenda kuuza tukajiingilia sisi *forex* matokeo yake sasa hivi pesa nyingi za kigeni Serikali hii imeamua kuzitumia kwenda kununa chuma nje kwa ajili ya kuja kufanya miradi mikubwa hapa kwetu badala ya kuwekeza kwetu baada ya miaka mitano au 10 mbele tukahakikisha na sisi tunapata chuma hapahapa nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kuisikitisha kabisa ni kwamba ili chuma iweze kufika bandarini na tunategemea bandari itakayosafirisha chuma ni Bandari ya Mtwara hakuna mpango mkakati mzuri unaoonesha namna ya kusafirisha chuma hii. Bado tunataka turudi miaka ya 40 kwa kusafirisha chuma kutoka Mchuchuma na Liganga kuleta kuileta Bandari ya Mtwara kwa kutumia barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara za Mtwara, Songea tumezipata kwa shida kubwa sana, leo hii tunataka kurudi kulekule badala ya kufikiria kujenga Reli, ambao mkakati wake hauonekani. Sasa hivi karibia mwaka wa 20 kule kuna watu walioekewa X kuonyesha kwamba kunatakiwa kupita reli inayotoka Linganga na Mchuchuma hiyo Reli inakwenda mpaka bandarini Mtwara imepita Jimbo la Mtama, imepita baadhi ya maeneo la Jimbo Ndanda, imepita Songea, Tunduru na kuelekea kote mpaka kufika Liganga na huko Mchuchuma lakini Serikali haijaonesha kwa namna yoyote jinsi gani inataka kufanya kazi kwenye hii Reli ya Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hii Reli ya Kusini kihistoria ilikuwepo toka mwaka 1949 lakini mara tu baada ya uhuru Reli ya Kusini iling'olewa. Tulitegemea leo tunakwenda kuendeleza ile Reli ya Kusini ili iweze wale wananchi pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye kitabu cha Kamati hapa, matatizo yaliyopo kwenye hii na ninaomba

Mheshimiwa Waziri akasome ili kuboresha kwenye majibu yake atakapokuja hapa. Wenyewe wanasema kwenye ukurasa wa sita na Kamati inaishauri Wizara. Inasema hivi, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa kiwango kikubwa unaonyesha kuwa Serikali inapanga matumizi makubwa yasioakisi uhalisia wa vyanzo vya mapato, hali hii imeathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni ushauri wa Kamati, na Mheshimiwa Mwijage naomba hii uingalie sana, ndugu zetu wa Wizara ya Fedha hawana nia njema na wewe. Hawana nia njema na Naibu wako Waziri kwa sababu ndio wanaokwamisha. Haiwezekani bajeti iliyopitishwa kwenye pesa za maendeleo wawape nyinyi asilimia tisa tu, na wakati mwaka uliopita 2015/16 waliwapa asilimia tano na bado tunasema nchi yetu tunataka kuisogeza kwenda kuwa nchi ya viwanda. Nchi ya viwanda inapewa pesa za maendeleo, Wizara inayosimamia masuala haya asilimia tisa Wizara inayosimamia maswala haya asilimia tano. Kwa hiyo, katika hii miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Tano pesa pekee ambayo imepata kwa ajili ya maendeleo kwenye Wizara yako ni asilimia 14 pekee. Ni kweli tuna nia ya kutekeleza hiyo Ahadi ya viwanda kwa wananchi? Na lazima watu tuwaambie ukweli kwa sababu tusipofanya hivyo hatutaweza kufika kokote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeendelea kwenda mbele, kwenye changamoto zilizopo wanasema hivi kumekuwa na ucheleweshwaji wa fedha za maendeleo, jambo linalokwamisha utekelezaji wa miradi hiyo kwa wakati na hatimaye kupanda kwa gharama hizo mwaka hadi mwaka. Hayo ndio matataizo na umeangalia hapa Wizara zote wamejaribu kuongelea suala hilo hilo. Ukienda Wizara ya Maji kuna matatizo ya ucheleweshwaji wa pesa, ukienda Wizara ya Nishati na Madini yaani ni kote kuna matatizo ya ucheleweshwaji wa pesa unaofanywa labda kwa makusudi kabisa na Waziri kwa maana ya kutokutaka kuwasaidia wenzie ili ikiwezekana yeye ndio aonekane anafanya vizuri kuliko Mawaziri wote, jambo hili msipolikemea haraka katika



*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

vikao vyenu vya Baraza la Mawaziri niwaambie Hazina Wizara ya Fedha inawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyofahamu kwa uelewa wangu mdogo tuu wa masuala ya mahesabu mimi ni mtaalam wa hesabu pia, kwamba mara baada ya kupitisha bajeti kinachofata kunakuwa kuna *cash flow* hazina wanatakiwa watoe pesa kutokana kwenye *cash flow* kwenye matukio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 10 wanatakiwa wawe wamepata shilingi milioni mbili kwa ajili ya kugharamia shughuri fulani. Lakini sasa hivi kuna utaratibu mpya hata sijui hata unapotokea. Bunge likishapitisha hapa kuna watu wengine nawasikia hapa kwenye taarifa wanasema kutoka juu ya Mheshimiwa Waziri mwenyewe hapa kuna sehemu ameandika wakati anajadili hilo suala la Liganga na Mchuchuma yaani ni robo tu ya ukurasa kwenye kitabu chake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwishoni kabisa anamalizia kwamba huu Mradi wa Liganga na Mchuchuma unakwenda vizuri anasema; taarifa ya awali ambayo inatakiwa kutolewa maamuzi na mamlaka husika. Sasa mamlaka anayopewa Waziri na Bunge hili halafu naye anatafuta mamlaka nyengine husika kwa nini hiyo sasa isije hapa ikajibu maswali ya Wabunge kwamba Mchuchuma na Liganga itaanza kufanya lini shughuli zake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nikuombe jambo moja, mama yetu Mheshimiwa Lulida hapa ameongea kuhusu viwanda vya korosho kule Mtwara ambavyo sisi tumeshakata tamaa moja kwa moja wa sababu hatuoni juhudi yoyote ile ikifanywa ili kuweza kufanya, kwa hiyo tunakuomba sana ujitahidi ili vile viwanda ziweze kuanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine jaribu kufungamaana na Wizara ya Kilimo, kwa sababu ili uweze kufanya kazi vizuri lazima ushirikiane na Wizara... *(Makofi)*

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha muda wa mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Minja hapana nitaenda kwa Joseph Haule alafu atafuatiwa na nitasema baadaye. Mheshimiwa Joseph Haule.

**MHE. JOSEPH L. HAULE.** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, awali ya yote nitoe pole sana kwa Mbunge mwenzangu Mheshimiwa Jesca David Kishoa, ambaye amepata ajali mbaya sana asubuhi hii tunamuomba kwa Mungu aweze kumpa nguvu na uponyaji wa mapema aweza kurudi kuendelea kulitumikia Taifa. Lakini pia nitoe pongezi kubwa sana kwa pacha wangu Joseph Mbilinyi a.k.a Sugu kwa kuhitimu mafunzo ya huko ndani ambayo yameongeza sana ujasili na cv yake ya kisiasa natumaini sasa hivi hatokuwa Rais wa Mbeya bali anaenda kwenye mchakato wa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huko siku za mbeleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa haraka kidogo, kwenye Wizara hii ya Viwanda kama wenzangu walivyosema Mkoa wa Morogoro ulibarikiwa kuwa na viwanda vingi sana ambavyo vingi vilibinafsishwa, na tukiwa tunategemea wawekezaji waweze kuviboresha kwa zaidi, lakini kwa masikitiko viwanda vingi vya Mkoa wa Morogoro vimekufa. Hapo ninavyoongea na wewe viwanda vya Moproco, Komoa, *Canvas, Morogoro Leather Shoes* na viwanda vingine kadha wa kadhaa viko *ICU* na sasa hivi zimekuwa kama Magodauni na vingine vinafugiwa mpaka mbuzi vitu ambavyo kiukweli sidhani kama ni lengo la Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi . *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuombe Waziri kabla hatujaenda kwenye viwanda vipya tuangalie wapi tulijikwaa na viwanda vyetu vilifanywaje ili tuweze kuvirudisha na kuangalia jinsi gani ambavyo tunaweza kuirudisha Morogoro kwenye ramani, kwa sababu sasa hivi pia Serikali ilitangaza kwamba muda si mrefu Morogoro inakwenda kuwa ghala la Taifa la chakula. Kwa hiyo, tunahitaji viwanda

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

vingi, tunahitaji kufufua malighafi nyingi, kwa sababu morogoro imebarikiwa sana kilimo na ina ardhi nzuri na kila sifa ambayo inastahili kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja nijikite katika jimbo langu la Mikumi. Mikumi tumejikita na tuna kiwanda kikubwa sana cha Sukari cha Kilombero, kiwanda hiki kila mmoja anajua kwamba ni moja kati ya viwanda vikubwa sana Tanzania ambavyo vinatoa ajira kubwa na ni tegemeo kubwa sana kwa sukari hapa nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1999 kwenda 2000 wakati kiwanda hiki cha *Kilombero Sugar Company* kikimilikiwa na Serikali kilipunguza wafanyakazi takribani 3000, na ilipoingia Illovo kwenda kama mwekezaji. Hawa wafanyakazi mpaka leo hawajalipwa fidia zao. Kilio hiki cha wafanyakazi ni kikubwa sana na kimeleta taharuki kubwa. Wazee wetu walitumikia kiwanda hiki kwa nguvu zao zote, kwa uwezo wao wote, kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini wengine wamekufa bila kulipwa mafao yao, na wengine wanataabika kupata mafao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, juzi tulikuwa na Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania na nilimuuliza swali hili. Kiwanda hiki ni muhimu sana kwa wakazi wa Mikumi, lakini Jimbo la Kilombero, Jimbo la Mlimba na Wilaya nzima ya Kilosa. Wafanyakazi wengi sana wameajiriwa kwenye kiwanda hiki, ni kiwanda kikubwa tunakipenda na kinaonesha ushirikiano. Lakini tunaomba sana Waziri, Rais alisema kwamba wakati mnabinafsisha kiwanda kwenda Illovo Serikali ilifanya makosa na wawekezaji walifanya makosa, hakusema kwamba wale wafanyakazi wana makosa yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali iwalipe fidia hawa watu walioachishwa kazi zaidi ya watu 3000 ambao kiukweli kabisa inaonesha hii ni haki yao ya msingi. Na niombe kuwaambia kwamba hata Kiwanda cha Makaratasi cha Mgololo na wenyewe walikuwa na kesi hii

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

lakini wenzetu wamelipwa hivi karibuni niwaombe Serikali mtupie jicho na Mheshimiwa Waziri wewe ni rafiki yangu kila nikikutana na wewe unaniambia nakupiga na kiwanda kimoja hapa nina viwanda kama vitatu mfukoni. Siku utakapokuja kule Ruaha watu wanakusubiri wapate majibu kwamba ni lini Serikali inakwenda kuwalipa fidia hawa wazee wetu ambao wametumikia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye Kiwanda cha Sukari Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja hilo, ili tuweze kutunza viwanda vyetu tunahitaji kuwa na mahusiano mazuri tunasema kiwanda cha Ilovo wanafanya vizuri sana wametoa ajira kubwa sana kwa Watanzania pale. Lakini mahusiano yamekuwa mabaya sana kati ya wakulima wa nje pamoja na kiwanda na Ilovo. Bado tunakuwa na matatizo ya mizani, bado wakulima wanalipwa *sucrose* kwa kiwango kidogo, lakini pia tunasema kwamba ili tuweze kuwa na uwiano ni lazima tuwe na mzani huru kwa sababu mpimaji ni huyo huyo, mpanga bei ni huyo huyo wakulima wetu wanaumia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa hivi kumekuwa na taharuki kubwa sana na changamoto kubwa wale wafanyakazi wa kiwanda cha pale cha Ilovo wamekuwa na mgogoro mkubwa sana na mfuko wa jamii wa *NSSF*. Kwa sababu wale wafanyakazi wanafanya kazi ki mikataba na kila msimu wanaweza kuajiriwa kwa miezi nane mpaka 10 na ile baada ya miezi 10 inaahirishwa wanakuwa na mapumziko ya miezi miwili na wanaporudi kwenye msimu mpya kiwanda kinaweza kikawaajiri tena au kisiwaajiri. Kwa hiyo, inasababisha wale wafanyakazi ambao wamefanya kazi na hawarudishwi tena kwenye kiwanda hawawezi kupewa *pension* yao. wengi wanategemea hayo maisha...  
(*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. JOSEPH L. HAULE.** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Anatropia Theonest kwa dakika saba na nusu.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST,** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, kuna msembo mmoja ni maarufu sana kutoka kwa muhenga mmoja anaitwa Napoleon aliwahi kusema; *let China sleep for when the dragon wakes she will shake the world.* Alisema Uchina wamesinzia, lakini siku ikiamka dunia itaona. Nataka hilo swali niimuulize ndugu yangu, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara anaiambia nini Tanzania? Wakati na Napoleon akiiona China na kuiambia dunia msione dunia imesinzia ikiaamka itakuwa balaa yeye anatuambia nini? Anatuambia nini wakati tumekuwa tunaongelea changamoto kadha wa kadha za viwanda zikiwa zinajirudia, wakati tunarudia yale yale na kila bajeti inayokuja tuna *address* yale yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitalia na kitu kidogo sana *EPZA* ninafahamu sisi kama Tanzania tuna *copy* uchumi wa viwanda kwa lengo nzuri la kwenda kuwa Serikali ya uchumi wa kati au nchi ya uchumi wa kati kwa *vision* yetu ya 2025 tukiangalia *Tiger Nations*, tukiangalia Taiwan, Singapore na South Korea, walifanya nini? Wameingia kwenye viwanda ndio, na sisi tunaingia kwenye *system* viwanda tena kwa wazo la ku-*fast track which is good.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tuna - *fast truck* kuingia kwenye viwanda je tunaangalia wao walifanya nini walijikwaa wapi au kipi walifanya vizuri zaidi ili na sisi tukichukie. Wali-*focus* kwenye *export* na mimi ninafurashi kwamba nchi yangu kupitia kwa Waziri Mwijange mnawaza au tunawaza ku-*export*, lakini ni kwa kiwango gani tume-*capitilize* kwenye ku-*export*. Tumekuwa na kitu, nimesema nitasemea kitu kinaitwa *EPZA*, tumefanya nini vya kutosha kuandaa maeneo ya uwekezaji, swali kila wiki swali kila mwezi tunaongelea maeneo ambayo bado madeni ya *EPZA*

lakini pia fedha inayotengwa haitoshi. Nimesoma Fungu 44 katika sera mmeonesha kwamba mmetenga bilioni 1,200,000,000 lakini kwenye kuandaa miundombinu na vitu vingine kadha wa kadha mmeandaa bilioni moja. Nataka mniambie hiyo fedha kidogo itaweza kufanya nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *EPZA* ndio msingi mzima wa biashara, msingi mzima wa biashara kama tunateka kwenda 2025 kama nchi ya uchumi wa kati, ni lazima tu-*export* zaidi. *We have to export more*, ndio *new Tiger's country* walichokifanya. Tuna-*export* nini? Hilo ni swali la pili, maana nchi hizo za Singapore nchi kama South Korea walikuwa *very specific* kwamba tunataka tu-*capitalize* katika moja, mbili, tatu sasa sisi tunataka tu-*capitalize* katika nini. Tunaweza tukawa na viwanda vingi nchini lakini tunataka dunia itufahamu katika nini? Ukiisema Kenya leo, watakwambia katika Afrika, Kenya ni mzalishaji mzuri wa *coffee* na *tea*. Lakini je, Tanzania tuko katika nini? Ni lazima tu-*capitalize* tunataka kufanya nini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarudi tena kwenye *EPZA*, hizo bilioni moja mlizotenga zinatoshwa kutengeneza miundombinu? Kwenye hotuba yako umeonesha hapa, kwamba tunataka tuweze kutengeneza ukuta wa *EPZA* ya Benjamini Mkapa umedondoka; tunataka tuweke miundombinu ya maji ya *EPZA* ya Mkapa kwa sababu haipo. Hivyo ni vitu ambavyo vinaleta ukakasi, ni vitu ambavyo haviwezi kuvutia zaidi wawekezaji. Lakini pia kama haitoshi nimeangalia kwenye *the easy of doing business*. Watu wanavyokuja kuwekeza fedha zao kutoka duniani kitu cha kwanza wata-*google* wewe ndio unasema hapo Tanzania, Tanzania ikoje, bado tuna-*rank 137* hatujafanya vizuri. Kama tunataka ku-*fast track* kama tunataka tuwe uchumi wa kati *by 2025* hatuko mbali na *2025 guys* kama tunadhani tunakaribia huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *report* ya *CAG* ameeleza wawekezaji, niseme *sampling* aliyofanya ya viwanda kumi na moja au ya wawekezaji 11 kati ya 57 ambao wamewekeza kwenye *EPZA* waliahidi wangukuwa na mtaji

## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

wa bilioni 131.5 lakini kwa mwaka uliopita wanaonekana wamewekeza *only 33%* ambayo ni shilingi bilioni 43. Wametudanganya wapi, tumewapokeaje kama wanaleta makaratasi na sio fedha au pengine walikuja na fedha zao wamekutana na vikwazo kadha wa kadha ambavyo tunazidi kuviongelea hapa. Vikwazo kama gharama kubwa ya uzalishaji, gharama ambazo mnatusabibishia leo mnatuambia tunalazimika kununua sukari shilingi 110,000 badala ya shilingi 65,000 kwa lengo la kulinda Viwanda vya ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hatuwezi ku-*compete* kama hatutashuka chini tukapunguza gharama za uzalishaji tukazalisha bidhaa nzuri tuka-*export* nje hicho ndio walichokifanya *New Tigers Contries*, lakini ningeweza kutoa ushauri mdogo wenzangu wamesema, tunaweza kuamua kwamba tunataka ku-*focus* katika kitu gani, umeonesha kwenye kitabu chako hata hivyo uchumi wa viwanda haujachangia kwa kiwango kikubwa sana. Ukurasa wa 185 haujachangia sana katika pato la Taifa. Tunaona asilimia saba, 6.9% mpaka 5.5% *consecutive* ambayo ni ya 2017. Ni changamoto kubwa sana tuna hicho kiwango kidogo ambacho kinachangia katika uchumi wa Taifa kama tungeweza kuwekeza katika sekta zinazowa-*accommodate* watu wengi tungekuwa tunaona mabadiliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungeweza kuona mabadiliko tena kwa macho, umesema kuna uzalishaji wa pamba nchini na viwanda 11 ambavyo ni *processing* lakini havifanyi vizuri. Ukurasa wa 22. Ukasema ni asilimia 30 tu ya pamba inayozalishwa nchini inatumika *instead 70 percent* inakuwa *exported* tukiamua kuji-*reduce* tu kutafuta wawekezaji katika viwanda vya nguo ambao ndio kitawa-*accommodate* watu wengi ambacho ndio kilimo *actually* ndio walichokifanya nchi ambazo tuna-*copy* mfano. Ndio walichokifanya hata South Korea tunayoisema. Walianza kuwa na viwanda vya kawaida baadae waka-*revolutionaries agriculture* yao, sisi bado tuna nafasi nzuri tuna eneo kubwa kwa maana ya ardhi, tuna wakulima, tuna watu wenye hali, tungeweza kuwa tumewafikia watu wengi,

tungeweza kubadilisha Tanzania, tungeweza sasa kuingia kwenye *a mid economic countries* kwa wepesi kushinda nguvu kubwa ambayo tutaenda kuitumia kwa viwanda vya *propaganda*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kikubwa ambacho ninaomba nisisitize hapa ni tunafangamanisha vipi elimu yetu na uchumi wa viwanda? Katika ku-*rank 137* duniani ni wanaangalia na *skills* na watu, wale watu wanaoleta viwanda vyao pia wanaangalia hiyo *labour force* ikoje? Sasa *labour force* ya vyuo ambao *so far* wako *theoretical* na siyo *practical* itazidi kutu-*pull down*. Ni lazima tufungamanishe uchumi wetu na viwanda na elimu yetu na ikiwezekana...(Makofi)

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Mheshimiwa hujaunga mkono. Mheshimiwa Devotha Minja atafuatiwa na Mheshimiwa Mary Muro kwa Dakika tano tano.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niungane na Watanzania wapenda mema, watakia mema Taifa hili, kumpongeza Waziri wangu kivuli Mheshimiwa Joseph Mbilinyi kwa kumaliza kifungo chake, lakini tunamwambia kwamba alipaswa kupitia hayo ili kuleta ukombozi katika Taifa hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunafahamu Mwalimu Nyerere aliamua kuufanya Mkoa wa Morogoro kuwa ni wa viwanda. Tukiacha Mkoa wa Dar es Salaam mkoa wa pili kuwa na viwanda vingi ilikuwa ni Mkoa wa Morogoro. Na kuanzia miaka ya 1960, 1970 kuendelea mpaka ya 1980 kwa Mkoa wa Morogoro huwezi kumkuta *house girl* kutoka Morogoro anaenda kufanya kazi, huwezi kuwakuta vijana wamekaa vijiwani, huwezi kuwakuta hata wazee wanakunywa kahawa vijiwani kwa kuwa watu wote



## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

walikuwa na fursa ya kuingia kwenye viwanda, kufanya kazi kwenye viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Serikali lengo la kubinafsisha viwanda ni kuongeza *efficiency*, lakini cha kushangaza, kwa makusudi mazima watu wale waliihakikisha Serikali kwamba watavichukua viwanda, wataviendeleza na kuhakikisha ajira inaendelea kuongezeka na kuongeza. Sasa badala ya ku-*expand* viwanda, kuongeza ajira watu wamevitumia viwanda kama *collateral* kwenye kukopa na kufanya biashara zao zingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo viwanda vya Morogoro vimekufa kwenye mikono ya watu, watu wamekosa ajira na tunategemea na Waziri wakati anahitimisha atuambie, Serikali imechukua hatua gani kwa watu hao ambao wameua viwanda kwa makusudi kabisa. Serikali imechukua hatua gani kwa watu hao ambao wamewanyima Watanzania ajira? (*Makofi*)

### T A A R I F A

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa!

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa muongeeaji moja ya viwanda ambavyo vimeharibiwa ni kiwanda ambacho alipewa Mbunge mwenzetu kiwanda cha Mang'ula ambacho sasa hivi kimefanywa ni *godown* la kufugia mbuzi. Kile kiwanda kilipewa miongoni mwa Wabunge wenzetu. Kwa hiyo, katika kuhujumu nchi hii na sisi vile vile tunashiriki kuhujumu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Devotha Minja, taarifa hiyo.

**MHE. DEVOTHA MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa na ninaamini Waziri amemsikia vizuri Mheshimiwa Kuchauka alichokisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tegemea Waziri na hitimisha atuambia hivi Morogoro tunahitaji viwanda vingine vipya, kama anavyosema ama tunahitaji kwanza tufufue vilivyoko? Kwa sababu rasilimali ya viwanda tayari tunavyo. Lakini sasa hivi vimekaa tu kwa hiyo tunataka kuona mpango wa Serikali katika kuhakikisha wanafufua viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumza kuhusu viwanda ambavyo vilikuwa vikitengeneza malighafi, nimemsikia Waziri pale wakati anawasilisha, katuonesha na viatu ambavyo vimetengenezwa, hivi Mheshimiwa Waziri nikuulize, ngozi zinaharibikia Morogoro hatuwezi kuzitumia unatuonesha viatu, tunashindwa ku-*export* ngozi pale Morogoro, nilikuwa nauliza lengo lilikuwa ni nini kama kweli tuna ngozi ambazo tunashindwa kuzitumia, unatuonesha *sample* ya viatu vichache. Ungetupa mikakati ni nini Serikali imejipanga kufanya kuhakikisha hata Viwanda vya Ngozi vilivyopo Morogoro ambavyo vimesheheni ngozi ambazo wanashindwa kuziua mpango wako ni nini vitengenezwe viatu kama ulivyotunesha? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kiwanda cha Mbigiri, tumesikia Serikali inataka kuanzisha Kiwanda cha Sukari. Lakini fidia kwa wananchi waliokuwa katika eneo hilo ni kilio mpaka sasa hivi. Kwa kweli watu ambao waliendeleza maeneo haya ambayo yaliachwa na Serikali miaka mingi wanakuja kuambulia patupu, halafu mnawaambia eti mtawafundisha kuwa ni *out growers* ambao hawana maeneo, hii si sahihi kabisa. Na nishukuru nilimuona Mheshimiwa Waziri anajaribu hata kulima kule anawaonesha jinsi ya kulima, lakini watalima wapi Mheshimiwa Jenista? Maeneo mengi yamechukuliwa, hawana pa kulima mnategemea *out growers* watatoka wapi Mbigiri? Kwa hiyo, Serikali inapojipanga ione namna gani yakuwasaidia na wananchi ambao wanazunguka maeneo ya viwanda ambavyo mnataka kufanya kazi ili wale watu waweze ku-*support* viwanda hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia Serikali ikisema ina mpango wa kuweka viwanda 100 kwa kila Mkoa. Hivi

najiuliza, hivi viwanda tunavyovizungumzia ni vipi? Ni viwanda *plant*, tunazungumzia viwanda vidogo au tunazungumzia viwanda vya aina gani? Kwa sababu hivi sasa kuna viwanda vikubwa Dar es Saalam ili kifanye *production* ni lazima umeme ukatike Dar es Salaam nzima. Sasa tunataka kupeleka viwanda vya namna gani kama hatua umeme wa uhakika, hatua barabara zinazoeleweka, hatuna maji ya kutosha, hivi ni viwanda gani mia tunapeleka katika Mikoa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anaelewa kabisa kwamba kuna baadhi ya maeneo wawekezaji wanaombwa leo mzalishe usiku ili Watanzania wengine wapate umeme. Kwa sababu wakizalisha umeme wote unaotumika mkubwa unalazimika kuingia kwenye kiwanda. Kwa hiyo, mimi nafikiria kabla ya kuja na *idea* ya viwanda hakikisheni tuna umeme wa kutosheleza, hakikisheni zipo barabara za kutosheleza zitakazokwenda vijijini kuchukua mazao. Lakini zaidi barabara pamoja na kuhakisha maji yanatosha katika hivi viwanda. Tunaelewa hivi viwanda vinahitaji maji ya kutosha. Kwa hiyo, *idea* ya kusema tu viwanda, viwanda tunaona hii ni kama tu kuwadanganya Watanzania Serikali hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu huwezi kwenda kwenye viwanda huna mipango sahihi ambayo tukitizama tunaona kweli tunaelekea kwenye viwanda. *Unless* utuambie twende kwenye viwanda vya vyerehani, vyerehani havihitaji maji, vingine hata havihitaji umeme tutakuelewa. Lakini *plant* tunazozitaka sisi ziende sambamba na miundombinu ya kuwezesha viwanda hivi viendeleo kutoa ajira kwa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo nakushukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante nakushukuru, lakini siku nyingine usiwe unaongea kwa nguvu namna hiyo unaweza ukaumia.

Mheshimiwa Mary Muro, atafuatiwa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya kwa dakika tano tano tu.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuchangia machache. Kwanza ningependa kusema kwamba Serikali kama ina mpango mkakati wa kuhakikisha sekta hii ya viwanda inafanya kazi vizuri, ningependa ifahamu kwamba kilimo kiwe ni kipaumbele kwa ajili ya kulisha viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ningependa kuzungumzia kwa vile nina muda mchache ningependa kuzungumzia biashara kwa ujumla nikianza na *TRA*. *TRA* imekuwa ni tatizo kwa sababu unapotaka kupata *TIN* kwa mfano *TRA*, utaenda kama unatafuta kazi, kwanza wafanyakazi wa *TRA* ni wachache, ilitokea tangazo hapa wafanyakazi wanaotakiwa kuajiriwa 400 na zikatokea nafasi 56 wakaomba. Wale 400 hatujui kama wameajiriwa au hawajaajiriwa. Wengine wanasema mpaka sasa hivi hawajaajiriwa. Imesababisha *TRA* kuwa na upungufu wa wafanyakazi na hivyo wananchi kupata shida sana kupata mahitaji yao pale *TRA*. Kwa hiyo, *TRA* imekuwa na usumbufu mkubwa sana. Kwa hiyo, naomba Serikali ifanye mchakato wa kuongeza wafanyakazi ili *TRA* iweze kufanya kazi kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kusema kwamba biashara ni matangazo. Nimeona viwanda kwa mfano kuna Kiwanda pale Kibaha cha Viuatilifu. Tangu uzinduzi umefanyika hamna mtu hata wa Kibaha anayejua kiwanda kile kinafanya kazi gani, kwa sababu hamna uzalishaji, hamna biashara kimekaa kama pambo. Tulitarajia watu wa Kibaha kwamba kiwanda kile kikiwepo vijana wetu watapata kazi, lakini kinyume cha hapo ni kwamba kile kiwanda hakifanyi kazi inayotakiwa na biashara ya viuatilifu hatuioni. Na matangazo ya kuonesha kwamba labda kiwanda kile kipo pale kwa sababu kina faida fulani hamna, hamna matangazo yanayoonesha kwamba wananchi wanaweza wakapata hizo dawa labda hata za majumbani kuondoa mazalia ya mbu, hatuoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ningependa kumwambia Waziri hivi viwanda vinavyoanzishwa basi na

matangazo yawepo. Viwanda visaidiwe kufanya matangazo, viwanda vimekaa kama picha hamna kinachoendelea. Pale Kibaha kuna matrekta tunayaona hatujui yapo pale kwa ajili ya nini kwa sababu wananchi hawajatangazia kwamba aidha yale yanauzwa au chochote, sasa biashara za viwanda kama hazitaenda na matangazo ina maana ni sawa sawa na kutwanga maji kwenye kinu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kusema kwamba Tanzania tunashindwa kufanya biashara ya ku-*export*, wananchi wengi wanashindwa kwa sababu Serikali haijatoa elimu juu ya ufungashaji. Unakuta kwamba mazao yanazalishwa hapa halafu yanachukuliwa yanapelekwa Kenya, wanafanya ufungashaji kupeleka nje na yanakuwa *labeled* kwamba mazao haya yanazalishwa Kenya. Sasa kama Tanzania tunataka kufanya biashara basi eneo la ufungashaji liboreshwe ili wananchi wajue akiwa na bidhaa yake anaifungasha vipi ili aweze kuipeleka nje. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia eneo la biashara za nje kuna usumbufu na urasimu mkubwa sana kiasi kwamba watu wakitaka kuuza bidhaa zao nje wanapata usumbufu kiasi kwamba wanakata tamaa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuuongelea juu ya wasindikaji wadogo, wamekata tamaa walio wengi kwa sababu kwa ajili ya zile tozo ambazo ni msululu. Unakuta kuna *TFDA*, kuna *OSHA*, kuna *TBS* kibiashara chenyewe ni kidogo *production* ni ndogo *product* moja unavyotaka kwa mfano ya *spice* anataka kutengeneza viungo unakuta kwamba msululu wa kodi zenyewe zilizoko pale zinamfanya huyu mjasiriamali mdogo ashindwe kufanya uzalishaji. Kama tunataka viwanda vidogo kama tulivyosema kwamba hata anayetwanga tangawizi yake akai-*pack* anaweza kuwa ni kiwanda basi hizo kodi tupunguze ili viwanda vidogo hivi viweze kumudu gharama hizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti ningependa kuongelea juu ya ukaguzi wa Idara ya Viwandani. Tumefurahi kweli viwanda

vimekuja watoto wetu waweze kupata kazi lakini wanapata magonjwa kuliko hata kazi wanayofanya. Kwa sababu unakuta kwamba viwanda havina vitendea kazi mtu anafungasha pale Kibaha kuna Kiwanda cha Sabuni. Siku nzima anabeba sabuni zile, anahamisha, anafungasha lakini hata kinga yake hana. Hana hata ile *mask* ili ya kufunga puani ili angalau asivute yale mavumbi. Sasa kwa mtindo huu kwa maana kwamba tutapata...

*(Hapa kengele illia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Muro, ahsante sana kwa mchango wako. Tunaendelea Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa Musa Mbarouk, dakika tano tano.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kupata hizi dakika tano kuchangia Wizara hii ya viwanda. Kwa sababu mimi Liwale hakufikiki kwa barabara, hakufikiki kwa mawasiliano, hakuna umeme wa uhakika sitaongelea kuhusu viwanda ila nitajadili kitaifa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejadili sana namna ya kulinda viwanda vyetu kwa kulingana na ushindani usio sahihi. Lakini hatujajadili namna ya kulinda wafanyakazi wazawa. Tatizo la wazawa viwandani ni kubwa kuliko tunavyolifikiria, na mimi hapa ni-*declare interest* mimi hapa nimefanya kazi kwenye viwanda vya watu binafsi kwa miaka 25, kabla sijawa Mbunge. Kwa hiyo, ninachoongea hapa ninamaanisha. Nimefanya kazi kwenye viwanda kwa taaluma mimi ni msindikaji wa nafaka. Kwa hiyo, viwanda vyote vya nafaka hapa nchini nimefanya kazi, kwa hiyo ninachokisema namaanisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye nchi za wenzetu mwekezaji anapokuja kutoka nje anapewa *limit* ya wafanyakazi ambao anaweza kuwaajiri, lakini hapa kwetu ni utitiri. Mheshimiwa Waziri hata wafagizi kwenye viwanda vyetu hivi ni ma-*expert*. Hata madereva kutoa bidhaa

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

kupeleka kwenye maduka ya jumla nima-*expert*, hata wasimamizi wa kupakia mizigo kwenye viwanda vyetu ni *ma-expert*. Kazi ambayo Watanzania wanaweza kufanya kwenye hivi viwanda ni ulinzi na ukuli peke yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili kama Taifa hatutaweza kuliangalia kwa upana wake tutaendelea kusema tunazalisha ajira, lakini ajira zenyewe ni ajira ambazo hazina mashiko. Tunasomesha wahasibu, *storekeepers*, tunasomesha Maafisa Utumishi lakini hawa wote hawawezi kupata kazi kwenye hizi sekta binafsi.

Pili, nataka niongelee suala la mazingira wezeshi ya uwekezaji. Mazingira ya uwekezaji Tanzania bado hayajawa sawa sawa na mfano mzuri nataka niwaambie kuna mfanyabiashara moja anaitwa Bakharesa alikuwa anataka kujenga *grain terminal* kwenye Bandari ya Dar es Salaam. Ili mchukua miezi sita kupata kibali, lakini tayari wakati anapata kibali alishakwenda Msumbiji na akapata na kwa nini alitaka kujenga *Grain Terminal* Dar es Salaam kwa sababu yeye ana viwanda karibu Afrika Mashariki nzima na Afrika ya Kati. Kwa hiyo akitaka kuitumia bandari ya Dar es Salaam kwa ajili ya kuagiza ngano zote kwa ajili ya viwanda vyake vilivyopo Barani Afrika. Lakini kwa sababu ya uzembe na urasimu sasa hivi *Grain Terminal* iko Msumbiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, muone namna gani mazingira ya kweli yasivyokuwa rafiki kwa wawekezaji. Lakini sio hivyo tu katika nafasi hiyo hiyo wawekezaji labda hawa wa viwanda vikubwa tutawakosa nchi hii kwa sababu ya sera zetu. Leo hii mwekezaji aliyekuwa kwenye utawala wa Awamu ya Tatu ndio huyo huyo alikuwa fisadi kwenye Awamu ya Nne; mwekezaji aliyekuwa rafiki kwenye Awamu Nne ndio huyo huyo alikuwa fisadi kwenye Awamu ya Tano. Kwa maana hiyo Tanzania hatuaminiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Chama cha Mapinduzi kinatawala tangu uhuru mpaka leo lakini kila tunavyobadilisha uongozi kwa maana ya Rais basi nchi hii inabadilika kama vile chama kilichotawala pale ni

chama kingine. Kwa utaratibu huu hatutawezi kwenda kwa sababu hatuna mwelekeo. Hatuna *goal* moja ambayo kwamba kila atakaye kuja ataendeleza pale ambapo mwenzake ameacha. Kila Rais anayekuja anataka aanze moja. Hii ni sababu hakuna mwekezaji atakayekuja kuwekeza kiwanda cha miaka kumi. Maana yake tunahitaji viwanda, labda hizo cherehani kwamba kila baada ya miaka kumi Rais akibadilika mtu anafunga vyerehani vyake anaenda sehemu nyingine. Lakini kama tunakusudia kupata wawekezaji wakubwa lazima tujenge uaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile naomba niendeleo kwenye *page 185* ya kitabu cha Mheshimiwa Waziri. Mimi takwimu hizi kidogo zinanichanganya. Yaani wakati sekta ya viwanda mchango wake unaporomoka ndio sekta ya viwanda inakua, yaani sijui sijaelewa kuna majedwali pale yaani pato la Taifa mchango wa viwanda unapungua viwanda vyenyewe ndio vinapanda. Viwanda vikipanda mchango wa Taifa unashuka. Mheshimiwa Waziri mimi utakapokuja hebu uje kunieleza vizuri haya mambo yanakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine lazima tukubali kwamba wawekezaji nchi hii wanaondoka kwa sababu ya sera zetu mbovu, kama hamkubali lakini lazima tukubali kwamba wafanyabiashara wakubwa wanahama nchi hii kwa sababu ya mazingira si sawasawa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Asante sana utaendelea kushauri. Mheshimiwa Mussa Mbarouk.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi nishukuru kwa kunipatia nafasi hii.

Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kuweza kukutana na kuchangia Wizara hii ya Viwanda na Biashara. Lakini mara zote nimekuwa nikisema



katika michango yangu kwamba Watanzania sijui tumekumbwa na balaa gani. Kwa sababu hapa viwanda vinazungumzwa kinadharia ziadi, lakini ukienda katika uhalisia mimi nasema hakuna kitu kwa sababu gani? Viwanda vilikuwepo, tulikuwa na viwanda vingi tu kwa mfano katika Jiji letu la Tanga tulikuwa na Kiwanda cha Mbolea, tulikuwa na Kiwanda cha Chuma (*Steel Rolling Mills*), tulikuwa na *Gapex*, tulikuwa na Kiwanda cha Sabuni (*foma*), tulikuwa na *Amboni plastic*, tulikuwa na *CIC*, tulikuwa na Kiwanda cha Mafuta ya Nazi (*Nicoline*), tulikuwa na Viwanda vya Sabuni Gardenia pamoja na *railways*. Tujjulize vitu vyote hivi viko wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nimuweke sawa mchangia aliyechangia Mheshimiwa Devotha Minja katika historia ya Tanzania Tanga ndio ulikuwa mji wa pili kwa shughuli za kimaendeleo kwa sababu ulikuwa ni mji wa viwanda na uliweza kukusanya makabila yote Tanzania mpaka tukaweza kuingiza majirani zetu kama watu kutoka Malawi, kutoka Rwanda na Burundi, Uganda na Kenya wamekuja kufanya kazi Tanga lakini viwanda vyote vile vimekufa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tatizo kubwa ambalo naliona kwanza hatuna umeme wa uhakika, lakini pia umeme ni ghali kuliko dunia nzima na hayo si maneno yangu nafirikiri katika siku za karibuni Mheshimiwa Rais pia aliwahi kuzungumza kwamba Tanzania gharama za umeme ni kubwa ndio maana wazalishaji au wenye viwanda wanashindwa kuja. Hata hivyo hata kama una fedha unataka kuweka kiwanda umeme unakatika mara kwa mara utaajiri watu wakae-*shift* masaa manane mazima, masaa manne umeme hakuna, hilo haliwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nasema kwanza tupate umeme wa uhakika, lakini pili tupunguze utitiri wa kodi. Tanzania kodi zetu sio rafiki wa wafanyabiashara na wazalishaji na wenye viwanda. Kwa hiyo, lazima Serikali hapo ijitathimini na ijilinganishe na nchi majirani zetu. Kwa nini wawekezaji wengi wanakwenda Kenya, wanakwenda

Rwanda, wanakwenda Msumbiji sasa hivi wanakwenda Uganda. Kwetu kuna matatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda lingine ninaloweza kulizungumzia sisi ni wakulima wakubwa wa pamba, lakini tujulize kwa nini Tanzania hadi leo tunaongoza kwa kuvaa mitumba, tena bahati mbaya zaidi hata leo kulikuwa na mjadala katika redio ya Clouds, kwamba kwanini Watanzania mpaka nguo za ndani, chupi, sidiria, soksi, *gloves* pia tunaingiza za mitumba wakati baada ya Sudan katika Afrika tunaongoza kwa uzalishaji wa pamba ni sisi. Sasa lazima Serikali ijiangalie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwijage, usivitaje tu viwanda kinadharia, leo hata vijiti vya kuchokolea meno hizi *toothpicks* pia zinatoka China, *handkerchief made in China* sijui mijiti ya kuchomea mishikika pia *made in China* miaka 57 baada ya uhuru. Sasa tunaposema Tanzania ya viwanda tusizungumze kinadharia na tusizungumze kimisamiati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi kama Singapore, Malaysia, Vietnam hata China katika miaka ya 1970 huko tulikuwa angalau tungalina lingana nazo. Kwa nini sasa hivi wenzetu wametuacha kiasi hiki? Kwa sababu hatuko *serious*, sisi katika kila jambo tunaingiza siasa na hapa ndiyo tunapoharibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri kama tunataka viwanda kweli tumejaza magofu ya viwanda wengine wanafugia mbuzi, wengine wamegeuza *magodown*, kuna viwanda vimebinafsishwa kwa watu binafsi, tujulize hawa tuliobinafsishia viwanda hivi wanafanya shughuli gani sasa hivi? Wameweka yamekuwa ni *magodown* wengine wanafungua mashine zilizokuwa ni vyuma vya pua wanakwenda kuzalisha vyuma vipya au wanatengeneza *scraper*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali iko wapi? Na pia tujulize hivi viwanda baada ya kubinafsishwa hizi fedha zilizopatikana zimefanya shughuli gani? Nashauri ni vyema

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

viwanda vile ambavyo vimekufa vikafungwa mitambo mipya ya kisasa tukapata umeme wa uhakika ili viwanda vyetu viweze kufanya kazi. Lakini pia tunapotamka viwanda tusifikirie kwamba itakayojenga hivyo viwanda ni Serikali maana yake hapa tunalolichukulia ni suala la viwanda kama vile Serikali ndiyo inayojenga viwanda. Tuweke mazingira mazuri ya kodi iwe rafiki kwa wawekezaji, lakini tuwe na umeme wa uhakika, na vilevile pia tuwe na *attraction* kwa hawa wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema hapa Mheshimiwa Kuchauka kuwa leo mtu akitaka leseni au akitaka kibali cha kujenga anasumbuliwa kuna urasimu wa jambo la saa moja Tanzania litachukua siku nne lakini akienda Kenya au Uganda jambo la saa moja ndani ya dakika 20 keshapata kibali...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Umesema Watanzania wote nguo za ndani wanavaa na wewe kumbe umevaa hiyo. *(Kicheko)*

Haya Waheshimiwa Wabunge niseme tu wale wa dakika tano kwa mchana itakuwa Mheshimiwa Sakaya, Mheshimiwa Ahmed Ngwali, halafu nitahamia upande wa Chama cha Mapinduzi ataanza Mheshimiwa Damas Ndumbaro, tutaona tunaendaje.

Baada ya kusema hayo nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja leo jioni.

*(Saa 7.00 Mchanga Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda,  
Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilitangaza mchana kabla ya kusitisha Bunge, wale watatu wa kwanza. Wa dakika tano nilimtaja Mheshimiwa Magdalena Sakaya akifuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Ngwali dakika tano, tano na nilimtaja pia Mheshimiwa Ndumbaro. Mheshimiwa Sakaya hayupo, Mheshimiwa Ngwali.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tu kwa sababu Mheshimiwa Sakaya hayupo, basi nichukue zote kumi.

**MWENYEKITI:** Una dakika zako tano.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka nianze kidogo na ufanyaji biashara baina ya Tanzania Bara na Zanzibar. Wakati anahitimisha Waziri wa Muungano na Mazingira, Mheshimiwa January Makamba alisema kwamba kutokana na kero za ufanyaji wa biashara kuwa nyingi, wanadhamira/wanakusudio kuiunganisha Zanzibar katika mfumo wa *TAVSIS* ili kurasimisha kodi za pamoja baina ya Zanzibar na Tanzania Bara ili kuondoa hilo jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napingana sana na jambo hili kwa sababu unaporasimisha kodi za pamoja, Zanzibar watakuwa katika wakati mgumu sana, itawalazimu washushe kodi zao za ndani na mimi nistaajabu sana Serikali ya Muungano kwa nini watu wanachukua hizi baadhi ya kelele wanataka kuleta jambo ambalo litaongeza tatizo la mzozo wa Muungano kuliko ilivyo sasa. Kwa hiyo, niombe

tu Serikali kwa sababu dakika sina, hili jambo la kuiunganisha Zanzibar katika Mfumo wa *TANSIS* wasilifikirie kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Mheshimiwa Mwijage ni kwa nini Kenya, Tanzania na Zanzibar na nchi nyingine tu zimepiga marufuku kabisa utengenezaji na uingizaji wa mifuko ya plastiki katika nchi. Tuna viwanda 41 tu ambavyo vinatengeneza mifuko ya plastiki ambapo viwanda hivyo vinazalisha asilimia tano tu, asilimia 95 inakuwa *imported* kutoka nje. Sasa kuna tatizo gani? Nyuma ya mfuko wa plastiki kuna nani ambaye anashinikiza viwanda hivi viendeleo na tuendeleo kuharibu mazingira jambo ambalo litatusababisha madhara makubwa kama Taifa, nini nyuma yake kuna kitu gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka niende katika suala zima la viwanda na umeme. Tumebishana na tumezungumza sana kuhusu umeme, wengine wanazungumzia kuhusu *Stiegler's Gorge* lakini na wengine wanazungumzia kuhusu umeme wa gesi lakini *energy mix* ndiyo inayotumika duniani kote, hatuwezi kuwa na umeme wa kutegemea mfumo mmoja tu wa umeme. Lazima tuwe na umeme, huku upatikane na huku upatikane. Lengo letu sote tunajenga nyumba moja, lengo letu ni kupata umeme ambao utafika megawati 5,000 na zaidi. Hizo ndiyo dhamira ya Serikali na mimi nakubaliana nao kwenye *energy mix* kwenye jambo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu Mheshimiwa Mwijage na Ofisi ya Waziri Mkuu, ninyi ndiyo mnaratibu mradi wa Bagamoyo ambao mkatutamanisha, mkatumbia eneo hili ni la *SEZ* tutapata kuweka, tutajenga bandari kubwa ambayo itakuwa meli za kizazi cha nne zitafunga. Wenzetu Kenya tayari meli zinafunga. Meli ya mita 300 karibuni tu ilifunga, sasa sisi meli meli kubwa ambayo *MV Lienna* ambayo ndiyo ina mita 420 tulidhani itakuja kufunga kabla Kenya haijafunga, lakini mpaka leo mradi huu unasuasua. Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo inaratibu kwa sababu jambo hili linaratibiwa na watu wengi, inakuwa shida hamtuelezi,

hakuna maelezo ya kutosha yanayoonesha kwamba jambo hili litamalizika kwa muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne kwa haraka haraka; Mheshimiwa Mwijage, Serikali iseme tu kama imeshindwa kuzuia bidhaa bandia zinazoingia nchini. Tumeanzisha mfumo wa *PVOC* ambao ni *free shipment* kule kuzuia lakini mpaka leo bidhaa *fake* zinaingia. Tumeanzisha hiyo halafu tukasema tutafanya *Direct Inspection (DI)* hapa bandarini lakini bado bidhaa *fake* zinaingia. Lakini polisi ambao unasema, nilikuwa nasoma kitabu chako mnataka kutumia mpaka *Interpol* kuzuia bidhaa *fake*. Polisi hao wenyewe ndiyo wanaoshiriki katika mambo hayo ya kuingiza hizo bidhaa feki, hiyo *Interpol* gani mnayotaka kutumia? Mheshimiwa Mwijage hilo rekebisheni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la tano Mheshimiwa Mwijage suala la *gypsum*. *Gypsum paper* zinaingia kwa asilimia 25, *gypsum board* zinaingia za asilimia 45. *Sorry* ni asilimia 25 kwa 25. Kwa hiyo, zikiingia 25, 25 ushindani ndani ya viwanda vya ndani haiwezekani kwa sababu tuna uwezo, tuna viwanda vinne vya *gypsum* kama sikosei, lakini vinazalisha *gypsum board* milioni 25 kwa mwaka. *Demand* ya Tanzania ni milioni 10 au 12, sasa tunalinda viwanda au tunabomoa viwanda? Kwa hiyo na hilo pia lirekebisheni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo la mwisho, sio la mwisho kama muda utakuwepo lakini kwa mfano teknolojia, tuna *CAMARTEC*, tuna *TEGRO* na kadhalika zinatumiya teknolojia ya kizamani wakati mwendo wa teknolojia sasa hivi umebadilika kwa hivyo...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kuisha muda wa Mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Mheshimiwa Ndumbaro subiri kidogo. Mheshimiwa Wilfred Lwakatare kwa dakika saba na nusu.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana na ningependa kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu ndani ya Bunge lako tukufu na niseme tu kwanza awali niwapongeze Waheshimiwa Madiwani wote kwa ujumla wao bila kujali itikadi zao wa Manispaa ya Bukoba kwa kufanya jambo la kihistoria siku ya juzi kwa kupitisha kwa kauli moja, wakapingana na kauli na njama ambazo zimekuwa zinafanywa na Mwenyekiti wa chama tawala, wa CCM kwa kutaka kudumaza mradi kujenga *stand* ya Bukoba kwa sababu ambazo hazina msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo ambalo ni la kihistoria kwamba sisi Bukoba kwa awamu hii tuliamua kwamba tunaweka siasa pembeni, tunapiga mzigo, wananchi wa Bukoba wanatoka katika historia za malumbano, wanataka mabadiliko ya *Bukoba Town*. Kwa hiyo, nawapongeza kabisa, kabisa na hususana Mwenyekiti wa *caucas* ya Madiwani wa CCM Mheshimiwa Richard, Mungu ambariki kwa kuonyesha kwamba sasa Bukoba imebadilika. Nashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nitoe pole kwa vijana wa bodaboda wawili wa Kata ya Kashai ambao wanatokea maeneo ya Kisindi na Kashenye ambao wameuawa kinyama kwa kupigwa visu na mapanga na hivi sasa tunapozungumza hata wahusika hawajakamatwa, suala hili limewarejesha katika kumbukumbu za watu kutolewa koromeo kwa sababu vijana hao wameuawa, pikipiki haikuchukuliwa, pesa hazikuchukuliwa, *helmet* haikuchukuliwa. Ni jambo ambalo hivi sasa limewafanya vijana kuanza kulala saa mbili na kwamba hivi sasa ikifika saa mbili usiku Bukoba hakuna usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nitoe pole kwa familia ya Mzee Kahigi ambaye ameondokewa na mtoto wake ambaye amepigwa risasi na watu wanaojidai kwamba wanaendesha programu au shughuli ya operesheni ya uvuvi haramu, yaani amepigwa risasi na matukio hayo mpaka sasa hivi polisi hawataki kutoa *statement* rasmi. Sasa masuala kama haya nakumbuka kwa Wizara zilizopita, watu

wamezungumzia suala la amani na utulivu lakini Serikali imekuwa inapata kigugumizi kutaka kukubali hata kuleta *Scotland squad* waje watuambie tatizo liko wapi kwa sababu vyombo vyetu inaonekana vimeshindwa kung' amua matatizo yako wapi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Mheshimiwa Mwijage nimelizungumza hili ili na Mheshimiwa Mwigulu alijue, mazingira ambayo ni mema ya kuwekeza yanategemea amani ya mazingira yenyewe, sio kukata leseni peke yake. Pale ambapo Maafisa wa Ubalozzi wanatekwa na kunyang'anywa kile walichonacho na kuumizwa ujue taswira mbaya inakwenda kwenye nchi za wenzetu na kwa wawekezaji kwa ujumla wao kiasi kwamba hata wawekezaji wataogopa kuwekeza Tanzania kwa sababu hakuna amani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili nataka kuzungumzia senene. Senene ni watamu kuliko nyama na ni kitoweo ambacho hivi sasa ni *international*, ukienda Dubai, London na Washington, sasa hivi senene zinakatiza, wanaliwa na watu wengi, ukienda Tanzania hii kila Mji Mkuu wa Wilaya wa Mkoa machinga hawezi kutengeneza hela kama hajafanya biashara ya senene. (Makofi)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwijage, nimetumwa na wanaumojwa wa wauza senene Bukoba Mjini, wanasema hivi; wao hii biashara walianza tangu mwaka 2000 nilipokuwa Mbunge ya kuanza kuuza senene kwamba ni zao, niliwaelekeza kama ni fursa. Ikaanza kuuza Dar es Salaam kwenye mataa na nini sasa imevuka mipaka. Sasa wanasema, wanaomba uwaunganishe na *TBS, TFDA, Sokoine University* hata na wenzetu wa Ubalozzi wa Canada ambao tumeona katika kitabu chako umesema kuna taasisi zinasaidia wajasiriamali wachanga, ili senene sasa kwanza zitangazwe kama ni zao ambalo lina ladha inayolika Tanzania nzima na nje ya nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili wanataka sasa kuwa na senene ambazo ni *standardized* ambao wana ladha



*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

inayofanana ambayo mtu wa Washington akiwala basi wanafanana na yule aliyeila South Africa.

Kwa hiyo, kwa maneno mengine hizo Taasisi zilizoombwa tunaomba ziende zivasaidie hawa wajasiriamali wa senene kwamba sasa hili zao wafundishwe namna ya *processing*, wasaidiwe namna ya *packaging* kimataifa ili zao hili liendelee kuwa fursa kwa wananchi wa Bukoba na wengine kwenye mkoa ambao wanakuja hawajui namna ya kuwakamata basi watu wa Bukoba watakwenda na kufunga mitambo ya kienyeji iliyoko Bukoba hivi sasa. Sasa viwanda vile vilivyoko Bukoba tunataka mwekezaji apatikane kwa njia yoyote ili aende kwa *local industry* ambayo imeanzishwa na iboreshwe tuweze kupata viwanda vya kisasa, vya ku-*process*, ku-*pack* senene vizuri ili tuanze ku-*export* kwenda nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi, watu wanaofanya biashara ya senene, wanajenga, wanasomesha, yaani senene ni *product* ambayo ni bora kuliko hata kahawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwijage umekuwa maarufu sana kwa hapa ndani ya Bunge kwa kauli zako kwamba mtu yeyote anayehitaji mwekezaji muonane nje ya Bunge umkabidhi mwekezaji aondoke naye kwenda jimboni. Sasa mimi siondoki kwenye Bunge hili, nitakuomba unipe mwekezaji, awe wa Kichina, wa Kijapani, mimi niende naye tuangalie mikakati ya kukamata senene. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa pointi hiyo usemi wa Kireno unaosema *batakusiiima kwiluka ukalabauliemo mwanyu*. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hebu tuambie lina maana gani bwana!

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo maana yake ni kwamba usisifiwe kufanya kazi sana kabla hujaangalia mazingira ambayo yanakuzunguka. Hiyo ndiyo tafsiri, nafikiri ameelewa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda umekwisha. Haya, tunaendelea. Mheshimiwa Damas Ndumbaro, Mheshimiwa Abdallah Bulembo na Mheshimiwa Zainab Katimba ajiandae. Mheshimiwa Bulembo. *(Makofi)*

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi nashukuru kupata nafasi hii lakini awali ya yote kwanza nimpongeze Mheshimiwa kaka yangu Mwijage na Naibu wake *Engineer* Stella Manyanya kwa kazi kubwa wanayofanya, hongereni sana. Mungu awape nguvu ili mfikishe jahazi lenu hili, lakini nimpongeze Katibu Mkuu, Naibu wake wawili, watendaji wakubwa wa taasisi zenu, kule Sabasaba, *TBS*, na kadhalika shughuli tunazona. Endeeleni kuwa na nguvu mtumikie Taifa lenu. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianzie kwenye kupanda bei kwa vifaa vya ujenzi. Kwenye miezi mitano iliyopita, nondo zimepanda kuanzia mwezi wa tisa mwaka jana nondo ya milimita 12 ilikuwa inanunuliwa shilingi 15,000 sasa hivi unanunuliwa kwa shilingi 22,000 na nondo ya milimita 10 ilikuwa shilingi 12,000 sasa hivi ni shilingi 16,000, mabati, *bundle* lilikuwa shilingi 250,000 sasa hivi shilingi 300,000; saruji, ilikuwa shilingi 12,000 sasa hivi ni shilingi 17,500 kuna nini kimetokea? Wanaojenga wanauliza, kuna nini kimetokea? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hebu tupe majibu tuwaambie Watanzania, kuna tatizo gani kubwa limetokea ndani kwenye eneo la ujenzi kwa sababu vifaa hivi ni vya watu wa kawaida ndiyo maisha yao ya kila siku wanaojenga nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili kubwa kuliko vyote, viwanda. Viwanda vingi vilibinafsishwa lakini watu waliobinafsishwa viwanda hivi wameshindwa kuyiendesha.

Serikali kupitia kwa Rais Magufuli nimeshasikia mara mbili Mheshimiwa Mwijage anakwambia wanyang'anye, anakuambia na ndiyo Rais wa nchi lakini kwanini huwanyang'anyi? Hao watendaji wako kwanini hawakusaidii? Mifano hai, kuna watu wamepewa viwanda vina mashine, sasa hivi havina kitu, hivi huyu naye kumnyang'anya ni shida? Tunafanyaje kwa sababu viwanda hivi hawa watu wakinyang'anywa kuna wawekezaji watakaokuja watakuta viwanda vipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Dar es Salaam kuna kiwanda kimoja kinaitwa *Uzi Bora Ubungo Spinning*. Kile kiwanda yule mtu ameng'oa kila kitu, watu wanakodisha mle kuweka mizigo. Ukiweka mizigo, unalipa hela yake, inaendelea. Hivi jamani, tunafanyaje? Mheshimiwa Mwijage na Mheshimiwa Stella Manyanya mnafanya makubwa, hebu waambieni watendaji walioko chini wanaowahujumu hivi navyo vinataka sense gani ili kuwanyang'anya? Mpaka iweje? Yaani ni nini kifanyike? Ukienda Masasi kule kuna viwanda pale vilikuwa vya korosho, watu wameng'oa kila kitu wanafanya maghala, wakulima wa korosho wanaenda kukodisha kwenye kiwanda chao kulipwa wakati wa msimu wa kuvuna korosho. Tufanye nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaheshimu sana hawa ninaowasema lakini naomba mje na majibu, haiwezekani, Rais amesema wanyang'anye viwanda, hamwanyang'anyi kwanini? Kwanini? Kwanini hawanyang'anyi? Kwa nini waende Mahakamani? Ukipanga nyumba ya mtu, ameweka dirisha la nondo, kesho ukiweka mbao si anakufukuza? Sasa hawa wamekuta mashine, wameondoa, wameuza, wakulima wa korosho wanaenda kupanga kwenye viwanda vyao, wanalipishwa hela! *Ubungo Spinning*, MSD mkienda kuangalia kwenye mahesabu alikuwa anapanga kama *store*, MSD ni ya Serikali, anamlipa mtu ambaye ameuza kiwanda. Sasa ni muagize Wakuu wa Mikoa wapo? Wawaletee orodha ya viwanda ambavyo havifanyi kazi na watu walishavunja mikataba, kuna watu wengine wana viwanda wanachechemea kidogo kidogo lakini hawa hawachechemei, wameng'oa kila kitu wanafanya biashara yao na sisi tunawaangalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi mliokaa hapa mnafaa na mnatosha, hebu isaidieni nchi yenu. Tuwanyang'anye vile viwanda, yabaki maghala ya nchi yetu, watakaokuja wana uwezo mpate nafasi ya kuwapa nafasi wafanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihamie Mchuchuma na Liganga. Historia tunayopewa kwamba tunaweza kuchimba yale madini miaka 100 lakini tangu nimesikia utafiti tunajenga, na kadhalika ni kama miaka 12. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilisikia kama kuna mtu aliuliza, kwa nini kama tunaweza, tusiite watu wakaanza kuchimba tukawawekea bei wakapeleka hela Benki Kuu sisi wakati tunaendelea na utaratibu wetu? Si mmetuambia ni miaka 100, kwa nini tuendeleo wakati kitu tunacho, kinatakiwa, hatuuzi, hatujengi, faida yake ni nini? Mwisho tutaondoka huku ulimwenguni hatujaona hata senti tano ya Mchuchuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwenu, hebu waruhusuni wananchi wa nje, wekeni utaratibu pale, waje wachimbe wasafirisha watulipe hela, wakati ninyi mnaandaa utaratibu wenu wa kupata kiwanda. Kigugumizi cha nini? Mheshimiwa Mwijage unaweza, mimi naamini unaweza, kigugumizi kinatoka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watendaji wana urasimu mara mia kwa sababu sisi wanasiasa ni miaka mitano ikiisha, alikuwa Mheshimiwa Mwijage amepita, alikuwa Mheshimiwa Manyanya, amepita. Shukeni huko chini muwaambie, kama hataki kufanya si ufukuze! Si mamlaka mengine mnayo? Wimbo ni ule ule. Alikuwa Mheshimiwa Mzindakaya, ameondoka, sijui wamemweka tena nani Mwenyekiti mwingine. Wenyeviti wanabadilishana tu. Nini kinafanyika NDC kwenye hii Mchuchuma na Liganga? Mnatuficha nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungepata umeme, tungepata pesa, lakini maamuzi hamjafanya. Nawaombeni

sana mwende mfanye maamuzi ili tuone nchi hii inakwenda wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Mara kulikuwa na viwanda vya *ginnery*. Viwanda vile vilikuwa vinafanya kazi, lakini ushirika ulipokufa wakaviweka chini ya mfilisi. Ukienda pale Mgango kidogo kinachechemea, lakini mfilisi, kiwanda kinafilisika kikiwa kwenye mikono ya Serikali. Ukienda *Bunda Ginnery*, kinafilisika kiko pale. Ukienda kule *Ushashi Ginnery*, kiwanda kinafilisika kiko pale pale. Hawa wafilisi nao kwenye Hazina Mheshimiwa Mpango muungane, hawa ni akina nani? Kwa nini mfilisi anapewa mali lakini zinakuwa makopo naye yuko pale pale na ni Serikali? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana, Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi haiko hivyo, watendaji mnaowalea watawapa madhara kwenye kuomba kura, kwa sababu wao wameajiriwa wapo. Vitu vinafia mikononi mwao.

(*Hapa kengele ya kwanza ililia*)

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Dakika tano?

**MWENYEKITI:** Endelea.

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa hiyo, maana yangu ni nini? Leo tunaenda kwenye zao la pamba, watu wanalia hapa. *Ginnery* zipo zilikuwa za Serikali, zinasaidia, lakini watu zimekuwa zao. Yule mfilisi ndio anakodisha kuweka pamba, anakodisha kila kitu, kesho anakwambia imeharibika. Hizi hela huwa zinaenda wapi? Kwa nini tunapata shida namna hii jamani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wakulima pale Bukoba nilikuwa namwuliza *Bukoba Town*, kuna Kiwanda cha *BUKOP*, kile ndiyo kilikuwa kiwanda sisi tunasoma zamani kwenye *KBCU*. Leo kiwanda kile anacho mtu mmoja, *KNCU* hawana mahali pa kukoboa kahawa. Nini kilifanyika, ni shida! Ndugu zangu viwanda hivi tunavitaka sana. Tunawapongeza,

mmefanya sana kazi ya kuleta viwanda, lakini vilivyokuwa vya zamani, cha zamani ni bora zaidi kuliko kipya ambacho hukioni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, turudisheni kwenye ushirika mzuri, viwanda viko chini yako Mheshimiwa Mwijage. Kama teknolojia ya zamani, waambie wang'oe walete ya kisasa, lakini viwanda viwe vyetu. Sasa tunakuwa watumwa kwenye viwanda vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongeze suala la Zanzibar, nataka kulisema kidogo, mnisamehe. Suala la Zanzibar hili, sipingani na Serikali yangu, lakini Mheshimiwa Turkey hayupo hapa, ningemsema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini maji ya Mheshimiwa Turkey yanatoka Zanzibar yanakuja Dar es Salaam yananyweka? Kwa nini sukari ile inayotoka kwenye Kiwanda cha Zanzibar haiji Bara? Kwa nini? Kwa nini haitugusi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mmefanya jukumu kubwa sana kwenye sukari, mnaweka viwanda mnaleta utaratibu, nawapongeza sana...

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** *(Hapa hakutumia kipaza sauti).*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndugulile, haya ahsante. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Bulembo.

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Wizara hii ya viwanda imefanya kazi kubwa sana kwenye sukari, nawapongeza sana. Kwenye sukari kwa sababu kila mwezi wa nne viwanda vinafungwa, mnatoa nafasi kidogo, watu wanaleta sukari hali inakuwa *stable*, lakini kwa nini kwenye sukari hapa kwenye hivi viwanda ikifika mwezi wa kuelekea Ramadhani inakuwa shida? Kwa nini? Mafuta hayapo, sukari haipo? *(Makofi)*

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa Mkulazi inakuja, tunawapongeza, lakini kwa nini tusiwe na *bulk procurement* ya sukari, Serikali ifanye kama inavyofanya kwenye *NRFA*? Wale watu wa vyakula, chukueni miezi ikifika tuwekeeni sukari *tonnage* inatoshia, mafuta yanatoshia, unapokaribia miezi ya Waislamu kuingia, Serikali itoe i-*control*. Leo hii sukari Mheshimiwa Mwijage nakuomba ukimaliza bajeti yako hamia bandarini, ili sukari iweze kushuka kule chini. Tutaingia mwezi wa Ramadhani sukari itafika shilingi 5,000 tutakuwa tunakusema wewe. Nendeni mfanye *operation* kama mlivyofanya ya mbolea, watu wana sukari wanafungia kwenye ma-*godown* sukari inazidi kupanda, kwa nini tunanyanyasika katika nchi yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa 90% samahani kwa kauli hii, ni watu wanaogonga *passport* ndio wanatutesa. Ndio! *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Damas Ndumbaro, atafuatiwa na Mheshimiwa Zainab Katiba na Mheshimiwa Gekul na Mheshimiwa Genzabuke wajiandae.

**MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Kwanza kabisa natoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuja na sera ya viwanda. Pia namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri ambayo anaifanya kuhakikisha kwamba sera hii ya viwanda inatekelezwa kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimshukuru Naibu Waziri, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, kwa kazi nzuri naye ya kumsaidia Waziri kutekeleza sera hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda ni kitu muhimu sana katika uchumi wa nchi. Ni muhimu sana katika kukuza kilimo.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Tunapokuwa wazuri katika kilimo, hasa sisi kule Songea tunalima sana, tunahitaji viwanda ili tuchakate mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda ni muhimu sana katika kuongeza ajira kwa watu mbalimbali, lakini katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri nimeona kuna suala la muhimu sana ambalo limesahaulika. Suala hili ni *research and development*. Kama kweli tuna nia ya kukuza viwanda, hatuwezi kudharau au kuacha suala la *research and development*. Lazima tufanye utafiti wa kitaalam katika kukuza viwanda. Lazima suala hilo litengewe bajeti ya kutosha ili wataalam wa ndani tulionao watuambie teknolojia ipi inafaa kwa viwanda vipi na kwa sehemu gani? La sivyo, tutakuwa tunaleta teknolojia kutoka nje ambayo siyo nzuri na haitusaidii na hatutafikia lengo letu la kukuza viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili ni lazima Wizara ifanye kazi kwa pamoja na taasisi za elimu ya juu. Ifanye kazi kwa pamoja na VETA na SIDO ili kuhakikisha kwamba suala la *research and development* linapewa umuhimu na kwenye bajeti ni lazima liwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu Wizara na Serikali imekuja na mpango wa EPZA, kuweka maeneo maalum ya uwekezaji ili kuinua uchumi. EPZA nayo imekuja na changamoto zake nyingi sana. Mfano mmoja ni katika eneo la EPZA kule Songea, Kata ya Mwengemshindo, wananchi wametwaliwa eneo lao la takribani ekari 5,000 ili kupisha mpango huu mzuri wa Serikali kwa EPZA. Tatizo ni kwamba toka mwaka 2008 mpaka hivi leo, wananchi hao hawajalipwa fidia. Miaka kumi wamezuiwa kuendeleza maeneo yao, lakini hawajalipwa fidia. Serikali imeahidi mara kadhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namwomba Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri katika bajeti ya mwaka huu waje na kauli thabiti kabisa kwamba hili tatizo la fidia katika eneo la EPZA Mwengemshindo, Songea



mtalimaliza. Nisipoliona hilo katika bajeti hii, sitaweza kuwaelewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali hasa Rais, Mheshimiwa Dkt. Magufuli alitoa amri ya kufufua viwanda. Kuna kiwanda cha tumbaku pale Songea Mjini. Kiwanda hiki wakati kinafanya kazi, kilikuwa kinatoa ajira kwa watu zaidi ya 2,000. Kilikuwa kinatoa soko kwa wakulima wa tumbaku wa Mkoa wa Ruvuma, lakini kiwanda hiki hivi sasa kimekufa, hakifanyi kazi na majengo yake yanatumika kama *ma-godown*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema kaka yangu Mheshimiwa Abdallah Bulembo tusifikirie kuanzisha viwanda vipya na tukadharau kufufua viwanda vya zamani. Naomba sana kiwanda hiki ambacho ni muhimu sana kwa Jimbo la Songea, kwa Mkoa wa Ruvuma na Kanda ya Kusini. Lazima kiangaliwe kwa jicho la pekee na Wizara hii na tuambiwe ni lini wataweza kukifufua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyotembelea Songea alitoa amri kwamba kiwanda hiki kiwe kinafanya kazi kufikia Juni, 2018. Sasa Mheshimiwa Waziri tunaomba kwenye hilo hebu tueleze, waambie wananchi wa Songea na Watanzania kwamba je, tumbaku yao itaweza kuwa *processed* katika kiwanda hiki mwaka huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya viwanda ni kitu muhimu sana, lakini tunahitaji kuwa na *coordination* kati ya mkakati huu wa kuwa na viwanda, kuvifufua na kuanzisha vingine pamoja na sekta nyingine ambazo zinasaidia viwanda. Kuwe na *coordination* kati ya mpango wa kufufua viwanda pamoja na sekta ya kilimo. Pale ambapo wananchi wanalima sana zao fulani ndipo viwanda vingi tuhamasishe watu wengi waanzishe viwanda hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingi zinazolima mahindi zinalalamika mahindi yanavunwa mengi, yanaoza, hakuna viwanda vya kuchakata mahindi hayo. Mahindi

yaliyolimwa mwaka 2017 bado yapo na ya mwaka huu tunayoenda kuvuna yapo, tunahitaji viwanda ili vi-*support* suala la kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuwe na *coordination* kati ya hivyo viwanda na umeme. Tunaposema viwanda tuhakikishe kwamba tunapeleka umeme katika maeneo yote na umeme wa kutosha, umeme wa viwanda ili tuweze kwenda vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhimu zaidi ni viwanda na miundombinu hasa barabara na reli. Tunaongelea hapa Liganga, Mchuchuma. Ili usafirisha chuma unahitaji reli, siyo barabara ya kawaida. Tukitegemea tutengeneze chuma Liganga na Mchuchuma halafu tutumie barabara zitakuwa zinaharibika kila mwaka. Hivyo, lazima kuwe na *coordination* kati ya kuendeleza Liganga na Mchuchuma pamoja na ujenzi wa reli ya kutoka *Mbamba Bay* – Liganga – Mchuchuma – Songea mpaka Mtwara. Hili ni muhimu sana kwa sababu bila kuweka *coordination* na hii miundombinu, hivi viwanda vitakuwa *isolated* na hatutavutia watu kwenda kujenga viwanda katika maeneo ambayo hakuna miundombinu ya barabara, hakuna miundombinu ya maji, hakuna miundombinu ya reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ni vizuri Wizara inapoweka mikakati yake iweze kuangalia hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii ni nzuri na nimesoma kitabu hiki, kimeandikwa vizuri. Nawapongeza tena Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara, ila ni muhimu tu haya ambayo tumeyasema yaweze kuzingatiwa katika kuboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Mheshimiwa Zainab Katiba atafuatiwa na Mheshimiwa Josephine Genzabuke.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kufanya kazi kubwa zinazoonekana. Napenda tu kutoa wito kwa vijana wenzangu na Watanzania wote tumwombe Rais wetu, lakini tumpe nguvu na tumpe moyo ili aweze kuendelea kufanya kazi anayoifanya ambayo imedhihirika kwa kipindi kifupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa ambazo wanazifanya. Niseme tuna imani nao, waendeleo kufanya kazi zao na wamuombe Mungu awasimamie ili waongeze juhudi na wafanikishe yale ambayo Watanzania wanayategemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuzungumzia suala la vijana. Sisi tunafahamu kwamba vijana hawapati fursa za kutosha kuajiriwa katika Serikali au sekta binafsi na wanahitaji na kila siku tunasisitiza kwamba vijana waweze kujajiri wenyewe. Kweli sasa hivi vijana wanajitahidi sana kujajiri wenyewe kupitia mifumo ya kufanya biashara. Sasa Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kupitia *BRELA* imeweza kufanikisha kutengeneza *Online Business Registration Platform* yaani ni mfumo wa kielektroniki au wa kimtandao wa kusajili biashara na makampuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo huu umeleta urahisishaji mkubwa sana katika usajili wa biashara na makampuni na umeleta urahisi. Kwa hiyo, tunachooomba ni zile changamoto ambazo mfumo huu umeleta Wizara iweze kuziboresha ili kuleta ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa changamoto ni zipi? Naomba Serikali kwanza mazitambue, lakini mtafute njia ya kuzitatua. Changamoto ya kwanza ni kijiografia tu Tanzania yetu hii ni pana na kwa sababu mfumo huu wa *Online Business*

*Registration* unahitaji matumizi ya mtandao, basi wawasiliane na Wizara husika ili tuweze kuona mtandao unaweza kupatikana hata huko vijijini na katika Tanzania yetu hii yote nzima ili kuweza kuleta manufaa makubwa zaidi ya mfumo huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo hivyo tu, kwenye Dawati la Huduma kwa Wateja (*Help Desk*), ninaiomba sana Serikali iweze kuboresha huduma kwa wateja, kwa sababu mfumo wowote wa kimtandao unahitaji *monitoring*, unahitaji huduma kwa wateja. Katika huduma kwa wateja katika mtandao huu changamoto ambazo vijana wanazipata katika usajili wa biashara na makampuni ni kwamba unaweza ukapiga simu huduma kwa wateja na ile simu isipokelewe au pale pindi simu inapopokelewa bado kunakuwa hakuna utatuzi wa papo kwa hapo kwa changamoto ile ambayo mtu anayetaka kujisajili anakumbana nayo. Kwa hiyo, naomba Serikali itambue kwanza kuna changamoto hiyo, lakini waweze kuifanyia kazi, kuboresha ili tuwe tuna huduma kwa wateja kama vile tunavyoona katika mitandao ya simu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupata leseni ya biashara kumewekwa kigezo cha kuwa na Kitambulisho cha Taifa ili uweze kujisajili katika huu mfumo (*Online Business Registration Platform*) ambayo ipo *BRELA*, ni lazima uwe na Kitambulisho cha Taifa. Sasa sisi tunajua siyo vijana wote wana Vitambulisho hivi vya Taifa, siyo Watanzania wote ambao wana Vitambulisho hivi vya Taifa na wanahitaji kusajili biashara zao, na sisi tunahitaji kurasimisha biashara za Watanzania ili tuweze kupata kodi, lakini wanakosa kitambulisho hiki na wanakosa uwezo wa kusajili hizi biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu naomba Serikali kwa wakati huu ione utaratibu wa kuweza kutumia kitambulisho kama cha Mpiga Kura ambacho sifa ya kuwa na Kitambulisho cha Mpiga Kura ni sifa kama ile ile ya kuwa na Kitambulisho cha Taifa, yaani kwa maana ni Mtanzania ili tusiweze kuwakwamisha vijana wetu au wafanyabiashara

wetu kuweza kusajili makampuni yao na biashara zao.  
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka Watanzania wafanye biashara kwa kufuata mifumo ya kisheria, kwa sheria zetu ambazo tumezitunga wenyewe hapa Tanzania. Kwa hiyo, tuwawekee mazingira mazuri ili waweze ku-*conform*.  
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia imeweka sharti, ili uweze kupata leseni ya biashara lazima upate *tax clearance*, ulipe kodi ile ya *TRA*. Sasa hili ni jambo jema, lakini sasa changamoto yake inakuja kwa ile *startup businesses*, yaani kwa wale wanaoanzisha biashara kwa mara ya kwanza. Kwa sababu hata ukiangalia Sheria ya Kodi (*Income Tax Act*) inataka na inatambua kwamba kodi ya mapato ni ile kodi inayotokana na biashara halisi. Sasa unataka upate leseni uanzishe biashara, kijana anataka kuanzisha biashara yake ajaajiri, unamwambia aanze kwanza kwa kulipa kodi ambayo hajaifanyia biashara akapata faida, hiki ni kikwazo.  
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naishauri Serikali ifanye utaratibu ili kwenye *startup business* kusiwe kuna hii *requirement* ya *tax clearance* kwa ajili ya kupata *business license*.  
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine Serikali imekuwa ina ubunifu wa kuwawezesha vijana na wanawake lakini na makundi mengine katika jamii kwa kutumia mifuko mbalimbali kuwawezesha kimtaji. Hili ni jambo jema sana, tumeona vijana na wanawake wengi wananufaika, lakini sisi wote tunatambua kwamba kumekuwa na changamoto ya kusonga mbele yaani kumekuwa na *vicious circle*. Kwa nini? Kwa sababu wale wanaopewa mikopo, yale makundi ya vijana na wanawake hayajaandaliwa kitaaluma katika uendeshaji wa biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hata kwenye hotuba ukurasa wa 142, utaona wameweka lengo la Wizara

ambalo wamesema kwamba ni kuhamasisha na kuelimisha wajasiriamali namna ya kuanzisha na kuendeleza biashara. Kwa hiyo, hili ni lengo mojawapo la Wizara katika sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo ndogo. Kwa hiyo, kuna uhitaji wa kuweza kuwapatia mafunzo ya kuanzisha biashara (*to start up their own enterprises*) kama ni vijana ama ni wanawake au wajasiriamali wowote waanzishe lakini waweze kuendeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo haya yanaweza yakapatikana kwa kutumia ile *machinery* tuiyokuwa nayo. Hata katika Serikali za Mitaa kuna Maafisa Biashara wa Mikoa, lakini kwenye Halmashauri pia kuna Maafisa Biashara. Wao wanaweza wakatumika, kwa sababu hii sera ni ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Japokuwa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ndiyo inafanya utekelezaji, lakini jukumu kubwa ni la Wizara hii kusimamia utekelezaji wa ile sera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, waangalie ni namna gani watatumia ile mifumo ili hata hivi vikundi, kwa sababu tunategemea vipate faida na ile mifuko ya kuwasaidia vijana na wanawake iwe ina manufaa, kwa hiyo, wapatiwe haya mafunzo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, twende mbele, hii Serikali iwasiliane, kwa sababu katika Wizara ya Elimu, Serikali ione namna ya kuweka katika mitaala ya elimu mafunzo (*Basic Entrepreneur Skills*) kuanzia ngazi ya chini ya elimu, kuanzia *primary* mpaka *secondary*. Kwa sababu tusiwaandae vijana wetu *for white collar jobs*, tuwaandae pia waweze kujajiri. Kwa hiyo, tuwape mafunzo yale *basic* ya kuanzisha *enterprises* zao wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Serikali iweze kuchukua maoni hayo na kuyafanyia kazi. Vilevile tuisahau kwamba katika uchumi wa viwanda tunahitaji sana ku-*invest* katika kilimo. Kwa hiyo, Serikali ione ni kwa namna gani inawekeza katika kilimo, kwa sababu hiki kilimo ndiyo kitakuja kulisha viwanda vyetu.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kule kwetu Kigoma, sisi kumekuwa kuna jitihada za kuanzisha hata viwanda vya mafuta ya mawese ili kusikosekane mafuta. Yaani hatuwezi Tanzania tukasema hatuna mafuta ya kutosha wakati kuna nchi kama Malaysia ambayo ilikuja kuchukua mbegu ya mchikichi Kigoma na leo hii ina-*produce* mafuta ya mchikichi (*palm oil*) kwa wingi sana halafu sisi kama Tanzania tukashindwa kuwekeza katika mbegu bora itakayozalisha kwa kiwango kikubwa na ikaweza kulisha viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Wizara hizi ziweze kufanya kazi kwa pamoja kama Wizara ya Kilimo, Wizara ya Viwanda na Biashara kwa sababu mwisho wa siku tunahitaji kilimo ili kije kinufaishe viwanda vyetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo kupongeza jitihada za Serikali katika viwanda, kwa mfano, mradi huu wa *Stiegler's Gorge* ambao utazalisha zaidi ya megawati 2100 za umeme ambazo ni jitihada zinazoonekana za kuelekea katika uchumi wa viwanda. Ukiangalia mradi kama *standard gauge railway* na...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako mzuri.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Oscar Mukasa na Profesa Norman Sigalla. Mheshimiwa Josephine Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Na mimi nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kufufua viwanda vyetu hasa viwanda hivi vidogo vidogo ni lazima suala la kuwa na mashine au vitendea kazi na wataalam kutazamwa kwa macho mawili. Taasisi hii ya *SIDO* ndiyo taasisi yenye uwezo na taaluma ya kutengeneza mashine ndogo ndogo ambazo zinawasaidia wananchi wetu wenye kipato cha hali ya chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, ni lazima Serikali iimarisha na kufanya shughuli zake za kuhakikisha *SIDO* inaweza kuimarishwa kwa kupatiwa mtaji. Mara nyingi pesa zimekuwa zikitengwa kupelekwa *SIDO*, lakini zikawa haziendi. Kwa hiyo, naomba kabisa *SIDO* iweze kutizamwa kwa macho mawili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa *SIDO* haifanyi vizuri kwa sababu baadhi ya vitendea kazi kama mashine, zimepitwa na wakati. Haziwezi kufanya ushindani na mashine zinazotoka nchi za nje kwa sababu mashine zetu zilizopo sasa hivi ni zile za muda mrefu. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iweze kutoa pesa kusudi *SIDO* iweze kwenda sambamba na mashine zinazoingizwa kutoka nje ya nchi. Hivyo basi, naomba Serikali iweze kuhudumia *SIDO* na kuipa wataalamu wa kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naipongeza Serikali kwa kutambua umuhimu wa kuiimarisha *SIDO*. Katika ukurasa wa 143 wameandika ni jinsi gani watakovyohakikisha *SIDO* inaweza kuimarika na wamesema; "Kutumia *SIDO* kama nyenzo ya kujenga viwanda vidogo vidogo na vya kati kwa kuendelea kulifanyia maboresho shirika hilo la *SIDO* na kuhamasisha ubunifu na matumizi ya teknolojia." Kwa hiyo, ninaomba sana kazi hiyo ya kuhakikisha *SIDO* inaimarishwa iweze kuangaliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka ni lazima maonesho yanakuwepo. Mara nyingi wananchi wa kutoka vijijini wanakuja kuonesha biashara zao kwenye maonesho lakini tatizo ni masoko. Kwa hiyo, naiomba Serikali ihakikishe inawaruhusu wanafanya maonesho, lakini itafute masoko



*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

kwa sababu wanapokuwa wamepeleka kwenye maonesho wanakaguliwa halafu wanakosa maeneo ya kupeleka kuuza bidhaa zao, wanakata tamaa. Kwa hiyo, naiomba Serikali, sambamba na kufanya shughuli ile ya maonesho, lakini izeze kutafuta masoko kwa ajili ya wajasiriamali wadogo wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Mheshimiwa Zainab na Mheshimiwa Zitto Kabwe, katika Mkoa wa Kigoma tunalima zao la michikichi. Tunaiomba Serikali izeze kuja kuwekeza Kigoma ili tuweze kuanzisha viwanda vya mafuta na vilevile viwanda vya kutengeneza dawa kwa sababu zao la michikichi linatoa mafuta, lakini vilevile linaweza likasaidia kuanzishwa viwanda vya dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilikuwa nataka kuzungumzia uwekezaji wa kiwanda katika Wilaya ya Kasulu, Kijiji cha Kitanga. Aliwahi kuja mwekezaji, karibu miaka 10 iliyopita, akaja akaoneshwa eneo, tangu ameondoka hajaweza kurudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naiomba Serikali mpaka sasa hivi eneo hilo lililoko katika Kijiji cha Kitanga, bonde ambalo ni la Mto Malagarasi bado lipo, kwa hiyo, bado tunaihitaji Serikali izeze kututafutia mwekezaji katika bonde hilo ili aweze kulima kilimo cha miwa, lakini vilevile aweze kujenga kiwanda cha sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivyo tutaweza kuimarisha uchumi wetu na viwanda vitaweza kuongezeka. Ni lazima tuhakikishe tunawekeza katika kilimo ili viwanda viweze kupatikana kutokana na mazao ya kilimo chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wamekuwa wakilogopa kuja Kigoma kwa sababu ya miundombinu, lakini naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri, kwa sasa hivi miundombinu Kigoma inaenda kuimarika, barabara zinajengwa, uwanja wa ndege wa Kigoma umetengenezwa na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa juhudi zake,

ndege za *bombardier* zinakuja. Kwa hiyo, wawekezaji watakapokuwa wanakuja Kigoma, hawatapata shida kwa ajili ya kuja Kigoma kwa ajili ya kufanya uwekezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, ninaunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla.

**MHE. PROF. NORMAN A. S. KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza naishukuru Serikali ya CCM na Waziri wa Viwanda na Biashara kwa kazi kubwa waliyonayo mbele yao, lakini pia kwa kazi kubwa ambayo wanafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie tu kidogo, jambo tunalojadili ni muhimu sana kwa mustakabali wa nchi yetu; viwanda na biashara. Lakini duniani kote viwanda, biashara na uwekezaji ukiwemo ndani yake cha kwanza kabisa ni lazima mwekezaji awe anaamini kwamba wewe Serikali unamtazama yeye kama ni muhimu. *Perception on investors* lazima iwe *very very positive*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa lugha rahisi ni kwamba lazima Mheshimiwa Mwijage rafiki yangu na wenzake wakiona watu wana fedha nyingi kwenye akaunti zao, wafurahie. Lazima wafurahie, ndiyo dunia ilivyo. Ni vizuri pia tufahamu mitego ya uchumi na biashara tunayosoma vyuoni na vile tunavyo-*practice*, mara nyingi havioani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii hata wewe mwenyewe ukiwa na shilingi trilion moja, uka-*deposit* kwenye akaunti za US au Switzerland hakuna atakayekunyooshea mkono kwamba hii ni *money laundering*, lakini ukizitoa kwenye uchumi mkubwa ukazileta Tanzania, utaambiwa hela chafu. Nchi changa ni wajibu zijifunze juu ya mtizamo hii. Tukiweka fedha kwenye nchi zilizoendelea, hatuambiwi hela chafu, ukizitoa hizo hizo ulizoweka kwao, ukizileta Tanzania ni hela chafu.

## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda pale Mexico wanalima dawa za kulevya, ukienda China wanalima dawa za kulevya, ukienda Afghanistan wanalima dawa za kulevya na ukienda Colombia wanalima dawa za kulevya. Wakubwa wa dunia hii huoni wanagombana na mataifa hayo juu ya dawa za kulevya. Nini tunajifunza? Maana yake uchumi na menejimenti ya uchumi na biashara duniani ni *tricky*, lazima ufikiri mara mbili kama unataka uwekezaji ukue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba sana Serikali kwa wawekezaji wenye fedha nyingi tuwaelekeze kwa kuwekeza, kwa sababu namna ya kupata fedha kwenye dunia hii ziko nyingi, ni ngumu hata kuzieleza. Siyo *linearly*, yaani ukichukua mtazamo wa *linearity* kwenye kutazama biashara, uta-*fail* kwa sababu biashara haiko hivyo, ina vitu vingi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako watu hapa, tupo ambao msingi wa fedha zetu ni *commission* kwa sababu ni *consultancy*. Mzee Chenge pale Mwenyekiti yule, nguvu yake kubwa ni Mwanasheria mbobezi wa muda mrefu, kwa vyovyote vile anaheshimika ndani na nje ya Tanzania. Fedha zake za *consultancy* huwezi hata kuzitaja, lakini kama Mtanzania akijua kwamba akiweka fedha zake kwenye akaunti za Tanzania atahojiwa, hataweka, ataweka Kenya na kwingineko. Maana yake ni nini? Kutakuwa na homa ya uwekezaji na watu kuikimbia Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, chonde chonde namwomba rafiki yangu Mheshimiwa Mwijage, watu wakizileta fedha, tuhoji sana matumizi yake. Tukiona wameingiza fedha kutaka kuiangusha Serikali yetu, tuhoji. Ila fedha zikiingia, tuwaelekeze, wekeza kwenye minofu ya samaki, wekeza kwenye kiwanda hiki, wekeza kwenye kiwanda kile, ndiyo uchumi wa dunia ulivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie kidogo kuhusu Mchuchuma na Liganga. Chuma dunia nzima sasa uzalishwaji wake unapungua sana. China, Australia na USA ndiyo magwiji wa uzalishaji wa chuma. Mtaji tulionao wa

chuma Liganga na Mchuchuma hakuna mradi; naomba niweke vizuri, hakuna mradi tulionao wa Tanzania leo ambao una uhakika wa fedha kwa maana ya kurudisha fedha kama Liganga na Mchuchuma. Bila kuuma maneno kabisa, hatuna *project* yoyote ya uwekezaji Tanzania ambayo inazidi mradi wa Liganga na Mchuchuma. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu mimi naelewa hata ilipotengwa shilingi bilioni 13 kwa ajili ya *compensation, who is going to be paid?* Ni Mtanzania. *Let them be paid.* Nashangaa Wabunge wanahoji juu ya mtu wa Ludewa kulipwa fidia. Akilipwa mtu wa Ludewa, sana sana anawekeza Ludewa, Songea na Mwanza. Hakuna shida na hilo. *You don't upper the economy* kwa ku-*shift* fedha kutoka *BoT* au Hazina kupeleka kwenye mifuko ya Mheshimiwa Mwijage anayowekeza Mwanza. Hakuna *deterioration* ya *economy* kwenye hilo. *Is just good*, ni jambo zuri kufanya hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Liganga na Mchuchuma ipewe kipaumbele chake, lakini tukisema hivyo ndiyo maana tunasikia hadithi kwamba mafuta yamefika bandarini, *I keep on wondering* kwamba mtu anahoji kwamba *point of origin* hakuna *documents*. Serikali hupati chochote kwa *declaration* ya *point of origin*. Mwisho wa siku Mheshimiwa Mwijage wewe unachopata ni kodi. Kwa nini unauliza kama mafuta yametoka mbinguni au yametoka Kenya? Mafuta yameshafika bandarini, piga kodi, pata pato lako leta mafuta Tanzania. *Simple as that.* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unafahamu leo *Tanzanite* Kenya ni ya pili duniani, kwani Mheshimiwa Uhuru Kenyatta anahoji *Tanzanite* mnatoa wapi? Anauza, anapata kodi yake anaendelea na kujenga uchumi wake. India wanaongoza kwa kuuza *Tanzanite*, Rais na *machinery* ya India haihoji *Tanzanite* mnapata wapi? Siyo kazi yao. Ninyi pigeni kodi, leteni mafuta, kwa sababu sisi tunapata mafuta kwenye kodi, siyo kwenye *documentation*. *Documentation* hatusemi ni mbaya, zinakusaidia ku-*facilitate* upate kodi inayostahiki, siyo ikuzuie sasa kupata hata hela. (Makofi)

## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukishakalisha mafuta bandarini ni wazi yakija mtaani huku bei yake itakuwa kubwa. Kwa hiyo, tutazidi kuumiza wafanyabiashara na sisi wenyewe kujiumiza na Serikali kuiumiza. Kwa hiyo, lazima tuwe na *correct perception* jinsi ya kufanya tunavyoweza kufanya ili kuongeza uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nampongeza sana Mheshimiwa Mwijage, niseme naomba sana aunde Kamati ya kumsaidia kwenye Wizara yake. Kamati ile siyo sisi, wafanyabiashara wamsaidie kufikiri namna bora ya kuwekeza. Mungu akubariki sana Mheshimiwa Mwijage. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

### MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. KABWE R. Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuongelea kuhusu kufungamanisha viwanda na kilimo. Kufunganisha viwanda na kilimo kungeepusha uhaba wa bei kubwa ya sukari nchini. Serikali ingesikiliza ushauri mwaka 2016, nchi isingesumbuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwa mara ya tatu tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani Bunge linajadili na baadae kuidhinisha fedha kwa ajili ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka 2018/2019.

Kwa Serikali ya Awamu ya Tano, Wizara hii ndiyo Wizara mama inayotoa taswira ya kufeli au kufaulu kwa Serikali hii. Maana ahadi ya msingi ya Serikali hii kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 ilikuwa ni kuwa itajikita kujenga Tanzania ya viwanda huku lengo kuu likielezwa kuwa ni kuiwezesha Tanzania kuwa na uchumi wa kati unaongozwa na viwanda ifikapo mwaka 2025. Bunge tunao wajibu wa kuhakikisha tunasaidia Serikali ili itimize ahadi hii.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, azma hiyo ya nchi yetu kuwa nchi ya viwanda ni njema na ni yetu sote, kwa nafasi zetu tunasaidia kuifikia azma hiyo. Tulipitisha hapa Bungeni Mpango wa Pili wa Miaka Mitano wa Maendeleo wa Serikali (FYDP2), kwa miaka ya 2016/2017 - 2020/2021 na kwa hiyo ni mpango wa nchi. Hivyo sote kwa pamoja tunafanya kazi ya kuhakikisha tunafikia malengo ya mpango husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wa upande wa upinzani tuna dhima kubwa zaidi ya Wabunge kutoka Chama Tawala. Tunao wajibu wa kukosoa pale ambapo tunaona walio kwenye Serikali wanakosea, kupendekeza sera bora zaidi za kutumia ili kufikia lengo (Tanzania ya viwanda) na kushauri mbinu nzuri zaidi za utekelezaji wa sera hizo. Naomba nitumie nafasi hii kukumbusha Bunge kuwa sisi upinzani tulitimiza wajibu wetu, ni hivyo tu Serikali haikusikiliza ushauri wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana mengi ya matatizo ya karibuni ya Wizara hii, hasa kwenye suala la uhaba na bei kubwa ya bidhaa za mafuta ya kula na sukari, si mapya, ni zao la uongozi mbovu wa CCM. Serikali ya Awamu ya Tano imerithi, imeendeleza na pia imezalisha zaidi matatizo ya uhaba na bei kubwa ya sukari na mafuta ya kula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016 wakati wa bajeti ya Wizara ya 2016/2017 Wabunge wa Upinzani tulishauri njia za kutatua matatizo hayo. Ushauri wetu haukusikilizwa, tunakumbusha tena leo ili Serikali itatue matatizo ambayo ilipaswa iyatue mwaka 2016. Mchango wangu wa bajeti ya mwaka 2016/2017 ulijikita kwenye kuishauri Serikali juu ya umuhimu wa kufungamanisha sekta ya viwanda pamoja na kilimo ili kuongeza thamani ya mazao ya wakulima wetu na kuhakikisha kuwa aina ya viwanda vyetu tunavyovianzisha nchini ni vile ambavyo vinategemea kwa kiasi kikubwa malighafi kutoka ndani ya nchi yetu hasa bidhaa za kilimo, ikiwemo sukari na mafuta ya kula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa tatizo la sukari nchini, ukurasa wa 140 wa hotuba ya bajeti ya Wizara ya Viwanda ya 2016/2017 unaeleza malengo ya Serikali kwenye

## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

sekta hii ya viwanda. Mambo tisa ya msingi yalipaswa kutekelezwa na Serikali ili kufikia azma ya kuwa na viwanda na katika mambo hayo tisa, hakukuwa na mpango mkakati wa kufungamanisha uzalishaji viwanda na bidhaa za kilimo zenye soko zaidi nchini (sukari na mafuta ya kula).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kurasa za 25 na 44 za hotuba ya bajeti ya Wizara ya Kilimo na Uvuvi kwa mwaka 2016/2017 zinaeleza juu ya mikakati ya kukabilliana na uhaba wa sukari nchini. Kiambatisho namba sita cha hotuba hiyo kilieleza kwa kina changamoto nzima ya sukari na miradi inayopaswa kutekelezwa ili kumaliza kabisa suala la uhaba na kupanda kwa bei ya sukari nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejumlisha miradi ile kutoka kila kona ya nchi na nimekuta ni takribani hekta 300,000 za kulima miwa. Kwa hesabu ya chini ya wastani wa kuzalisha sukari kwa kila hekta, miradi ile kama ingetekelezwa Tanzania ingeweza kuzalisha tani milioni 1.5 za sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiondoa sukari ya kutumia nchini, ziada ambayo ingeuzwa nje ingeweza kuliingizia Taifa fedha za kigeni USD milioni 500, sawa na asilimia 30 ya malengo ya mpango wa maendeleo kwa sekta ya viwanda wa kupata mapato ya fedha za kigeni kiasi cha USD bilioni tatu. Hapo ni bila kutazama kiwango cha ajira zitakazozalishwa, ukuaji wa biashara kwenye sekta nyingine, umeme na kadhalika (*multiplier effect*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bajeti ile ya mwaka 2016/2017 hakukuwa kabisa na mafungamanisho kati ya ulimaji wa hekta hizo 300,000 za miwa na uzalishaji wa tani milioni 1.5 za sukari. Maana Wizara ya Viwanda na Biashara hata haikujua juu ya mkakati huo wa kupunguza uhaba wa sukari wa Wizara ya Kilimo. Wizara mbili zilizo ndani ya Serikali moja hazikuwa zikisomana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishauri mambo matatu kama ifuatavyo:-

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

(i) Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2016/2017 iondolewe na ikapitiwe upya ili isomane na bajeti ya Wizara ya Kilimo ya mwaka husika. Tuliomba Wizara mbili ziwianishe na kuoanisha mipango yao kwa lengo la kuratibu ulimaji wa miwa na uanzishaji wa viwanda vya sukari vya kutumia miwa ile.

Serikali haikusikiliza, Rais akatoa tu matamko ya zuio la sukari kutoka nje wakati hakukuwa na mpango wa Taifa wa namna ya kufidia nakisi ya sukari itokanayo na uzalishaji mdogo wa bidhaa hiyo nchini. Matamko ya zuio ya Rais yaliishia kuleta uhaba wa sukari na kupandisha bei kutoka shilingi 1,800 mpaka shilingi 6,000 katika maeneo mbalimbali nchini na tangu hapo bei ya sukari haijashuka tena, imebaki kuwa shilingi 3,000 kwa kilo.

(ii) Kwenye sukari kuna suala la *low hanging fruits*, kila mwaka miwa yenye uwezo wa kuzalisha tani 50,000 ya sukari huoza huko Kilombero na Mtibwa. Mkoani Morogoro wakulima wanalima miwa mingi zaidi kuliko uwezo wa viwanda kununua, miwa hii inaishia kuoza tu bila kutumika. Bodi ya Sukari ilipaswa kutoa leseni ili vikundi vya wakulima au wawekezaji wadogo wazalishe sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi leo Bodi ya Sukari nchini haijatoa leseni kwa viwanda vidogo vya uzalishaji sukari nchini na wala Serikali haijahasisha Watanzania kuwekeza kwenye viwanda vidogo vya sukari ili kuwezesha miwa yote inayozalishwa nchini itumike kutoa sukari. Kama jambo hili lingefanyika, tungeweza kupunguza nakisi ya sukari nchini kwa zaidi ya tani 50,000.

(iii) Uwekezaji wa bidhaa kama sukari unahitaji vivutio vya punguzo la kodi kutoka Serikalini. Kule Uganda, Rais Museveni tangu aingie madarakani aliweka vivutio maalum kwa viwanda kama *Kakira Sugar* ili wazalishe sukari ya kutosha. Viwanda vya sukari Uganda hata umeme hulipiwa na Serikali kwa asilimia 50 ili kupunguza gharama za uzalishaji na kuvilinda dhidi na ushindani wa sukari kutoka nje.



## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka leo Serikali haijaona kuwa vivutio (*subsidies*) kwa ajili ya kupunguza gharama za uzalishaji ili kuwezesha kuzalisha sukari, kutengeneza ajira na kupata faida ni jambo la lazima. Sisi Kigoma mwaka 2016 kuna mwekezaji alitaka kuzalisha sukari tani milioni moja kwa mwaka kwa kulima miwa Kasulu, Wizara ya Fedha pamoja na Wizara ya Viwanda walibishana kuhusu vivutio (kama wanavyobishana sasa juu ya mafuta ya kula), leo mradi ule wa uwekezaji umekufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti uliofanywa na Bodi ya Sukari Tanzania (*SBT*) kwa kutumia Kampuni ya *LMC International*, ulibaini mahitaji ya sukari kwa mwaka 2016/2017 ni wastani wa tani 590,000 ambapo kati ya hizo, tani 455,000 ni kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na tani 135,000 kwa matumizi ya viwandani. Leo mwaka 2018 nakisi hiyo ya mahitaji ya sukari imekua zaidi, bei ya sukari iko juu zaidi ya shilingi 1,800 iliyokuwepo mwaka 2016 kabla ya Serikali kuweka zuio la kuagiza nje sukari bila kwanza kuwa na mpango wa kuondoa nakisi iliyopo, sasa bei ni wastani wa shilingi 3,000 nchi nzima. Serikali ingetuskiliza mwaka 2016 leo tusingekuwa hapa tulipo, hata miradi inayopangwa sasa kupunguza nakisi, kama ya Mkulazi, ingeanza mapema zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, thamani ya fedha tunazotumia kuagiza mafuta ya kula kutoka nje ni zaidi ya bajeti ya Wizara ya Maji ya mwaka 2018/2019. Serikali ingekubali ushauri wa mwaka 2016 wa kufungamanisha sekta za viwanda na kilimo isingumbuliwa mwaka 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili nchi iendelee, maendeleo ya viwanda yanapaswa kufungamanishwa na sekta nyingine za uchumi kwa sababu kuna kutegemeana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Tanzania ili tuendelee ni lazima kufungamanisha shughuli za uchumi zinazohusisha wananchi wengi zaidi na sekta ya viwanda ili huo uchumi wa viwanda uwe na tija kwa watu. Sekta ya kilimo kwa ujumla ikihusisha uvuvi na ufugaji huhusisha asilimia 75 ya Watanzania.

## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta za viwanda na kilimo kwa pamoja zinachangia nusu ya Pato la Taifa (*GDP*) na nusu nyingine ni sekta ya huduma. Nadharia za uchumi zinatuaambia kuwa tija ikiongezeka kwenye sekta ya kilimo, inawezesha sekta ya viwanda kukua na kisha sekta ya huduma. Hapa Tanzania na nchi nyingine za Afrika, sekta ya huduma iliruka hatua hizi za ukuaji, hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa zaidi kwenye *GDP* kuliko kilimo au viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tunaambiwa uchumi unakua lakini umaskini wa wananchi haupungui, ni kwa sababu ya huduma haiajiri watu wengi kama sekta ya kilimo na hivyo uchumi unaokuzwa na sekta ya huduma hauajiri watu wengi kama sekta ya kilimo na hivyo uchumi unaokuzwa na sekta ya huduma ni nadra kuondoa umaskini. Sekta za kuondoa umaskini ni kilimo na viwanda maana zinaajiri watu wengi zaidi. Hivyo ili tuendelee ni lazima kufungamanisha viwanda tunavyotaka kuvijenga na kilimo chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano tuliieleza haya wakati wa mwaka wa fedha wa 2016/2017, mwaka wake wa kwanza wa bajeti lakini ikashindwa kusikiliza ushauri wetu. Hivyo kushindwa kufungamanisha kilimo chetu na viwanda tunavyotaka kujenga hasa vya bidhaa tunazozitumia zaidi kama mafuta ya kula, bidhaa ambayo ina mahitaji makubwa na sasa bei yake imepanda toka shilingi 55,000 mpaka shilingi 70,000 kwa ndoo ya lita 20 kutokana na masuala yanayohusu uingizwaji wake kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa tatizo la mafuta ya kula nchini na utatuzi wake; suala la mafuta halina tofauti na suala la sukari, ukipanda gari ukapita njia ya Singida unaona wananchi wamepanga madumu ya mafuta ya alizeti wanauza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu Kigoma sisi ndio wazalishaji wakuu wa mafuta ya mawese nchini, lakini bado bei ni haba, uzalishaji wenyewe ni duni na hautoshelezi hata

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

soko la ndani. Kimsingi tarehe 17 Mei, 2016 wakati wa kusomwa kwa bajeti ya Wizara hii kulikuwa na matatizo matatu makuu kwenye sekta ya mafuta ya kula nchini na niliyaeleza katika mchango wangu kama ifuatavyo:-

(i) Suala la unafuu mkubwa wa kodi kwa mafuta yanayoingizwa kutoka nje ambao Serikali iliutoa kwa waagizaji nchini. Unafuu huo ulivunja hamasa ya uwekezaji wa viwanda vya kuzalisha mafuta ya kula ndani ya nchi. Mazingira ya unafuu ule wa kodi yaliwafanya wafanyabiashara waone ni nafuu na kazi rahisi zaidi kuagiza mafuta nje kuliko kuzalisha ndani. Jambo hili la unafuu wa kodi kwa waagizaji wa mafuta ya kula kutoka nje likaua ushindani wa bei na viwanda vya ndani vikashindwa kushindana kwenye soko na hivyo kupunguza uzalishaji, jambo lililoifanya nguvukazi ya wananchi wanaolima mawese na alizeti (mazao makuu ya kuzalishia mafuta nchini) kupotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ule wa bajeti ya mwaka 2016/2017 tuliishauri Serikali iondoe unafuu huu wa kodi inaoutoa kwa waagizaji wa mafuta ya kula kutoka nje ya nchi ili kulinda na kunusuru viwanda vyetu vya ndani na tuchochee uzalishaji zaidi wa ndani wa mafuta ya kula, jambo ambalo lingechangia ukuaji wa kilimo cha mawese na alizeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2016/2017 kodi kwenye mafuta ya kula kutoka nje ni 10% (*imports duty*) na 18% VAT tu. Tukashauri jambo hili libadilike. Mwaka huu ndiyo Serikali imekubali kubadili ushauri wetu wa kuondoa unafuu wa kodi kwa waagizaji wa mafuta ya kula kutoka nje baada ya kuwa tumepoteza zaidi ya mwaka mmoja na nusu wa kuviathiri viwanda vyetu vya ndani.

(ii) Kama ilivyo kwenye sukari, tuna nakisi kwenye uzalishaji wa ndani wa mafuta ya kula. Mwaka jana uzalishaji wa ndani wa mafuta ya kula ulikuwa ni tani 180,000 tu wakati mahitaji yalikadiriwa kuwa ni tani 400,000 mpaka tani 520,000 kwa mwaka.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo wa uzalishaji ndani ukiwa ni asilimia 30 ya mahitaji na uagizaji wa mafuta ya kula kutoka nje ukiwa ni asilimia 70; pia asilimia 55 ya mahitaji ya mafuta ya kula nchini ni mafuta ya mawese (*palm oil*) yanayoagizwa kutoka nje ya nchi. Inakadiriwa kuwa mafuta ya alizeti yanayozalishwa yanatosheleza mahitaji ya ndani kwa asilimia 40 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa katika uzalishaji wa mafuta ya alizeti na mawese nchini inatokana na upungufu wa mbegu zenye ubora stahiki wa kutoa mafuta kwa wingi. Pia uwepo wa viwanda vichache vya kuzalisha mafuta yatokanayo na mazao hayo. Hivyo fursa ya kuwafanya wakulima wetu kuzalisha zaidi na kuziba nakisi hii kukosekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishauri kuwa Serikali inapaswa kuwekeza kwenye uzalishaji wa ndani wa mafuta ya kula kwa kuhamasisha kulimwa zaidi kwa mazao yanayozalisha mafuta ya kula (pamba, karanga, alizeti na mawese) pamoja na kufungamanisha uzalishaji zaidi wa mazao hayo na sekta ya viwanda kwa kuweka unafuu wa kodi kwenye uagizaji wa mashine za kukamulia mafuta ya kula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hamasa ndogo ya Serikali kwa wakulima wawekezaji wa viwanda. Serikali imeshindwa kufanyia kazi ushauri huu tangu mwaka 2016, katika wakati ambao mahitaji ya mafuta ya kula yanapanda nchini, bado uzalishaji wa ndani umebaki ulivyo.

(iii) Kwa lengo la kujazia nakisi ya uzalishaji wa ndani wa mafuta ya kula uliopo, nchi yetu inatumia sehemu kubwa ya akiba ya fedha za kigeni kuagiza mafuta ya kula kutoka nje ya nchi. Kwa wastani kwa mwaka tunatumia USD milioni 340 sawa na shilingi bilioni 782 zaidi ya bajeti yote ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka 2018/2019 ambayo ni shilingi bilioni 727.

## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kigoma ni miongoni mwa mikoa maskini zaidi nchini. Shilingi bilioni 782 tunazopeleka Malaysia kununua mafuta ya mawese kwa ajili ya kujazia nakisi yetu ya ndani zingeweza kabisa kufuta umaskini wa Kigoma. Tuna mradi Kigoma wa kupanda michikichi ili kuzalisha mafuta ya mawese ulio chini ya Serikali ya Mkoa. Mpango wetu ni kila familia kupanda hekta moja ya michikichi, lengo ni kuzifikia familia 100,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa familia hizo za Kigoma kwenye kilimo cha mawese unaweza kuondoa kabisa suala la Tanzania kuagiza mawese kutoka nje maana tutaweza kuzalisha tani 200,000 za *crude palm oil (CPO)* kwa mwaka, kuzalisha ajira nyingi, kupandisha hali ya maisha ya wananchi/wakulima na kukuza biashara nyingine. Uzalishaji ni ndani ya miaka miwili tu tangu upandaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi biashara ya uzalishaji wa mafuta ya kula ni fursa kubwa kwa nchi yetu ambayo ingetumika vyema ingeweza kufuta umaskini wa wananchi wetu. Leo hii ninapozungumza hapa Bungeni bei ya lita moja ya mafuta ya alizeti/mawese ni shilingi 4,000 ikiwa imepanda kutoka shilingi 3,500 na ni bei kubwa kuliko bei ya lita ya petroli kwenye soko la dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutimiza lengo hilo Kigoma wanahitaji watu watakaowekeza kwenye viwanda vya kuzalisha mawese. Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ishirikiane na uongozi wa Mkoa wa Kigoma kuhakikisha tunazalisha mafuta ya kula ya kutosha ili kuondokana na uagizaji huu. Mawese na alizeti ndiyo suluhisho la kudumu la suala la mafuta ya kula. Ni imani yetu kuwa sasa Serikali itabeba ushauri huu ili miaka miwili kutoka leo tusijikite kujadili tena suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu ni kwamba vyuma vitazidi kukaza tukipuuza fungamanisho la miradi mikubwa na ujenzi wa viwanda nchini. Serikali ibebe ushauri wangu wa mwaka 2017.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukumbushia ushauri wangu juu ya namna bora ya kupunguza nakisi na kupunguza bei ya bidhaa za mafuta ya kula na sukari nilioutoa wakati wa bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2016/2017 sasa naomba pia nikumbushie jambo la tatu muhimu nililoishauri Serikali kuhusu hali ya uchumi wa nchi yetu, juu ya sababu ya fedha kupungua nchini (vyuma kukaza) na namna ya kuitumia miradi mikubwa tunayoifanya nchini kuendeleza sekta ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili nilieleza kwa undani wakati wa bajeti ya Wizara hii ya mwaka 2017/2018. Serikali haikuchukua ushauri ule, kwa sababu ya umuhimu wake, naomba niikumbushe tena Serikali juu ya umuhimu wa kuifungamanisha sekta ya viwanda na ujenzi wa miradi mikubwa tunayoifanya nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejipanga kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo kama vile barabara, ndege, madaraja, mabomba ya gesi, mafuta na kadhalika. Fedha nyingi za ndani na za wafadhili zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza miradi hii. Nitajikita kwenye kurudia mfano nilioutoa mwaka jana juu ya mradi wa reli ya kati kwa kiwango cha *SGR*. Kwenye mradi huu wastani wa shilingi trilioni 17 zinahitajika kukamilisha ujenzi wake kati ya Dar es Salaam na Mwanza (kilometa 1,200).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa kilometa moja ya reli unahitaji chuma cha pua (*steel*) chenye ubora wa hali ya juu kiasi cha tani 40 mpaka 60. Sisi tunajenga kilometa 1,200 za reli kwa sasa hivi na baadae zitaongezeka kwa vipande vya Tabora - Kigoma, Kaliua - Mpanda - Karema, Uvinza - Musongati na miradi mingine kama Mtwara - Mbamba Bay, Ruvu - Tanga, Tanga – Musoma - Kigali na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo basi, Tanzania inahitaji siyo chini ya tani 500,000 za chuma cha pua (*steel*) katika kipindi cha miaka michache ijayo. Kwa mipango iliyopo sasa ni kwamba mataruma ya reli yataagizwa kutoka

nje na kuletwa nchini na hivyo kuzalisha ajira huko kwenye nchi za nje ambazo mataruma hayo yatazalishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za miradi hii zitakwenda nje ya nchi, kama ilivyo kwenye fedha za mafuta ya kula na sukari, Watanzania hawatafaidika kabisa. Je, Serikali imeweka mikakati ya kufungamanisha maendeleo ya viwanda na miradi hii? Je, kuna mipango shirikishi ya kuhakikisha utekelezaji wa miradi hii unawasaidia zaidi Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, sekta binafsi ya Tanzania kwa ushirikiano na Serikali imeandaliwa kuzalisha bidhaa na malighafi zinazotakiwa kwenye miradi hii? Hivi Serikali imeambatanisha faida, ajira, mapato ya kodi na mapato ya fedha za kigeni kwenye fungamanisho la miradi hii ya maendeleo na sekta yetu ya viwanda? Maswali haya niliyauliza mwaka 2017 hayakupata majibu, nayarudia hapa ili Serikali ichukue hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mikubwa yote duniani ina mikataba ya ziada iitwayo *Offsets Agreements*. *Offsets Agreements* ni makubaliano maalum kati ya Serikali na mzabuni wa miradi (kwa mfano ubia kati ya kampuni ya Yapi Merkezi ya Uturuki na Kampuni ya *Contrucao Africa SA* ya Ureno uliohinda zabuni kipande cha reli kati ya Dar es Salaam - Morogoro) makubaliano ambayo huweka msukumo maalum wa kisera na kisheria ili kuhakikisha watu wetu wanafaidika wakati wa ujenzi wa miradi mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida husika huwa ni kwa kushirikiana kwenye uzalishaji wa sehemu ya malighafi zitakazotumika wakati wa mradi na pili katika kuhakikisha kuwa sehemu ya utaalum uliotumika wakati wa ujenzi unaachwa nchini ili kuhakikisha tunawajengea uwezo Watanzania wa kufanya miradi ya namna hii siku za usoni (*transfer of knowledge*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina chuma kingi sana kule Mchuchuma na Liganga na pia tuna makaa ya

mawe ya kuchenjua chuma hiki ili kupata chuma cha pua (*steel*). Mradi huu wa reli peke yake ungeweza kuchochea maendeleo makubwa kwenye sekta ndogo ya migodi na viwanda vya chuma. Tungekuwa na mipango thabiti, sisi Tanzania tungekuwa ndio wazalishaji wakubwa wa chuma nchini na hata uzalishaji wa chuma cha kujenga reli kwenye eneo la Mashariki mwa Afrika na Maziwa Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu wa reli unaweza kufungamanishwa na sekta ya kilimo nchini kwa bidhaa za ngozi na mkonge kutumika katika utengenezaji wa vitanda na viti vya mabehewa ya treni. Sekta yetu ya ngozi pamoja na ile ya katani zingeweza kufaidika sana kwa mradi huu mmoja tu wa reli kwa kuhakikisha kuwa mapambo ya ndani ya mabehewa yanakuwa ya bidhaa za ngozi na viti vinakuwa vya bidhaa za katani. Hivi ndivyo namna nchi nyingine zimeweza kuchochea viwanda kwenye mnyororo wa thamani. Najua tunatangaza zabuni ya mabehewa haya, tumetilia maanani jambo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa hizi *Offsets Agreements* kati ya Serikali na Mzabuni kwenye mikataba kungehakikisha Serikali inawakutanisha wakandarasi wa reli na wazalishaji wa bidhaa za ngozi na katani na kungehakikisha uwekezaji kwenye sekta ya uchimbaji madini na viwanda vikubwa vya chuma. Tunaweza kufanya haya kwenye miradi mikubwa ya maji, ujenzi wa bomba la mafuta na kadhalika. Naisihi Serikali itazame hii miradi mikubwa na kuifungamanisha na mkakati wetu wa viwanda ili fedha za miradi hii zibaki zaidi nchini, zitumike kuinua sekta yetu ya viwanda, zitoe ajira kwa watu na zisaidie kuchochea mzunguko wa fedha na kupunguza ugumu wa maisha (vyuma kukaza).

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne ni kwamba tuwe na mkakati maalum ili kuingiza dola bilioni moja kwa mazao ya biashara na India. Mei 2016 tulipokuwa tunajadili makadirio na matumizi ya Wizara hii, viwanda vyetu vilikuwa vinazalisha na kuuza nje ya Tanzania bidhaa zenye thamani ya dola za Marekani bilioni 1.408 (takribani shilingi trilioni 2.6)



na hivyo, kuwa sekta ya pili kwa kuingiza fedha za kigeni nchini kwetu baada ya sekta ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mei 2017 hali hiyo ya uzalishaji na uuzaji wa bidhaa zitokanazo na viwanda haiipo tena, tunaweza kusema kwa uwazi kuwa biashara hiyo imeshuka mno. Kwa mujibu wa taarifa rasmi za Serikali yenyewe, kupitia taarifa ya Benki Kuu ya sasa (*BoT Monthly Economic Review*), sekta ya viwanda inauza nje ya nchi bidhaa za thamani ya dola za Marekani milioni 879 tu (takribani shilingi trilioni 1.962). Hivyo sekta hiyo kushuka na kuwa ya tatu katika kuchangia mapato ya fedha za kigeni baada ya utalii na dhahabu. Ushukaji huu ni wa zaidi ya asilimia 38 yakiwa ni mapato kidogo zaidi tangu mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mei 2018 *BoT* hata hawaweki takwimu za mauzo ya nje ya bidhaa za viwandani maana hali ni mbaya zaidi. Serikali inaona aibu kuwa sera zake mbaya za kiuchumi zimeshusha uzalishaji kwenye viwanda na sasa imeamua kuwakataza *BoT* kutoa takwimu za mauzo ya nje ya bidhaa za viwandani. Ni kilio kwa wakulima wa mbaazi, choroko, dengi na giligilani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauzo ya bidhaa za viwanda kwenda nje ya nchi siyo pekee yaliyoshuka, lipo pia eneo la biashara ya mazao ya kitaifa. Mchango wangu kwenye bajeti ya Wizara hii kwa 2018/2019 utajikita zaidi kwenye eneo la biashara ya kimataifa, hasa biashara ya mazao ya kilimo jamii ya mbaazi, choroko, dengi na giligilani kwenda nchini India.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera mbaya za uchumi, utekelezaji mbaya wa diplomasia yetu na juhudi ndogo za Serikali kutafuta masoko ya bidhaa zetu kimataifa ndani ya miaka miwili na nusu ya Serikali ya Awamu ya Tano vimechangia kwa kiasi kikubwa katika kuanguka kwa biashara ya mazao hayo kimataifa na hivyo Taifa letu kukosa fedha za kigeni. Miongoni mwa biashara za kubwa za mazao nchini ni biashara ya mbaazi tukiwa na soko kubwa nchini India. Mwaka 2015/2016 mauzo ya nje ya mbaazi (kwenda

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

India) yalifikia USD milioni 224 sawa na shilingi bilioni 515 yakiweka rekodi ya juu kabisa ya mauzo yetu ya mbaazi India na pia yakiweka rekodi kwa wakulima kuuza hadi shilingi 3,000 kwa kilo moja ya mbaazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 9 Julai, 2016 Waziri Mkuu wa India, Narendra Modi aliwasili nchini kwa ajili ya ziara yake ya kwanza Afrika, ambapo alitembelea pia Msumbiji, Afrika Kusini na Kenya. Lengo la kuja nchini likiwa ni kuonesha uhusiano mzuri kati ya nchi hiyo na Tanzania na pia kusaini mkataba wa ununuzi wa mbaazi kati ya nchi zetu mbili hasa kwa kuwa Tanzania ilikuwa imeuza mbaazi zenye thamani ya nusu trilioni kwa nchi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mkutano wake na Waziri Mkuu Modi, uliofanyika tarehe 10 Julai, 2016 Rais Magufuli alisema yafuatayo na nanukuu: "Mwaka jana (2015), Tanzania iliuzia India tani 100,000 za mazao ya kunde ambayo yalikuwa na thamani ya USD milioni 200. India inahitaji tani milioni saba za mazao hayo kwa mwaka, kwa hiyo, kuna fursa kubwa ya kufanya biashara katika kilimo hicho." Mwisho wa kunukuu na akawahimiza wakulima wa mbaazi kulima zaidi zao hilo kwa kuwa soko la uhakika liko India.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Serikali yetu kwa zembe tu ilichelewa kusaini makubaliano hayo ya ununuzi wa mbaazi kati ya nchi zetu mbili mpaka muda wa kikomo iliopewa na India ulipopita. Jambo hilo la kuchelewa kusaini makubaliano hayo limetufanya tutolewe miongoni mwa nchi zinazoruhusiwa kuuza mbaazi India na hivyo kusababisha tukose soko la kuuzia mbaazi zetu kwa miaka hii miwili ya Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa haikuwa na mkataba wa kuuza mbaazi India, kwa kuwa ilichelewa kusaini makubaliano, lakini Serikali ilikaa kimya tu na taarifa hizo, haikuwaeleza wananchi waliohamasika kulima zaidi mbaazi kwa sababu ya bei kubwa ya shilingi 3,000 kwa kilo ya mwaka 2015/2016 kuwa haina mkataba na India. Matokeo

yake wakulima na wafanyabiashara wetu wameishia kupata mateso tu na kufilisika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2016/2017 thamani ya mauzo ya mbaazi kwenda India ikashuka mpaka USD milioni 131 sawa na shilingi bilioni 303.3. Mapato yakipungua kwa zaidi ya bilioni 200. Kwa mwaka 2017/2018 mauzo ya mbaazi kwenda India yakishuka zaidi hadi kufikia USD milioni 75 sawa na shilingi bilioni 172.5 na kusababisha ufukara kwa wakulima, kiasi sasa kilo moja ya mbaazi kuuzwa kwa shilingi 150 kutoka shilingi 3,000 ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo baya zaidi ni kuwa Serikali yetu imeshindwa kabisa kutumia mahusiano yetu ya kibiashara, kidiplomasia na kihistoria na India kuhakikisha tunamaliza jambo hili na kunusuru soko letu kimataifa. Katika wakati ambao hatuwezi kuuza mbaazi India, kwa mwaka jana tu India alisaini makubaliano na kununua mbaazi kutoka Nigeria zenye thamani ya USD bilioni mbili sawa na zaidi ya shilingi trilioni 4.6, wakati ambao mbaazi zetu zilibaki kuozea kwa wakulima. Utafiti wa Januari, 2018 uliofanywa na Taasisi za *Tanzania Pulses Network* na *East Africa Grain Council* unaonesha kuwa hasara iliyopatikana kutokana na mbaazi zisizouzwa ni kubwa mno, kipato cha mwananchi kikitajwa kushuka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si mbaazi tu hata giligilani hali ni hiyo, bei yake imeshuka kutoka shilingi 300,000 mwaka 2016 mpaka shilingi 150,000 kwa gunia kwa mwaka 2017 wananchi wa Mkoa wa Manyara wanaumizwa sana na hali hiyo. Hali hiyo ya maumivu na kilio ipo pia kwa wananchi wa Misungwi, Mkoani Mwanza ambao mwaka 2016 waliuza choroko kwa shilingi 300,000 kwa gunia lakini bei hiyo ilishuka mpaka shilingi 150,000 kwa mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao mengine yaliyoshuka bei ni mazao ya jamii ya dengue, mwaka 2016 wakulima wa mazao haya waliuza kilo nne za dengue kwa bei ya shilingi 7,500 lakini tangu mwaka jana bei ya mazao haya kwa hizo kilo nne imeshuka mpaka shilingi 2,500 tu, soko la mazao

haya likiwa ni India. Ukitazama kwa undani, ni dhahiri kuwa mazao haya ya mbaazi, choroko, dengu na giligili, yanao uwezo wa kuliingizia Taifa zaidi ya USD bilioni moja kama tutaweka mipango ya kuongeza uwezo wa uzalishaji pamoja na kutumia diplomasia na historia yetu na India kutatua changamoto ya soko iliyoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kifanyike ili kufikia lengo la kuingiza fedha za kigeni, USD bilioni moja kupitia mazao haya maalum yenye soko India? Baada ya kuonesha upungufu wa Serikali ya CCM katika fungamanisho la kilimo na biashara ya nje, natoa pendekezo la jawabu la hali hii, kama ifuatavyo:-

(i) Tusahihishe mahusiano yetu na India. Tuna faida mbili za kimahusiano na India, ya kwanza ni historia kati ya nchi zetu tangu wakati wa Baba wa Taifa, Mwalimu na Waziri Mkuu Nehru. Pili, ni uwepo wa jamii kubwa ya wafanyabiashara wa Kitanzania wa jamii ya Kihindi wenye asili ya Jimbo la Gujarati ambapo anatokea pia Waziri Mkuu wa India, Narendra Modi. Kuna kulegalega kwenye mahusiano yetu, tusahihishe.

(ii) Tuitumie vyema diplomasia yetu. Kwa vyovyote ni lazima Serikali yetu ifanye diplomasia ya hali ya juu sana na Serikali ya India kwenye suala la soko la bidhaa za *pulses* hasa mbaazi, choroko, giligilani na dengu. Nchi yetu haiwezi na haipaswi kuzidiwa na nchi nyingine za Afrika katika suala zima la soko la bidhaa zake nchini India. Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ambayo inahusika na biashara ya nje, inabidi ifanye kazi ya ziada kwenye eneo hilo, biashara ya nje ni diplomasia, tuitumie.

(iii) Tuhakikishe tunarudisha soko letu. Nguvu yetu ya historia na mafungamanisho na India pamoja na diplomasia yetu vitumike vyema kwa pamoja kuhakikisha tunarudisha soko letu la kuuza mazao haya. Hili la kurudisha soko linapaswa kuwa jambo la kufa na kupona kwa Wizara hii. Ikibidi Waziri, Mheshimiwa Mwijage aende tena kuonana na Waziri mwenzake wa Viwanda na Biashara wa India, Suresh

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Prabhu hasa kwa kuwa alishindwa kuambatana na msafara wa Makamu wa Rais juzi kwenye Mkutano wa Jumuiya ya Madola kule London, mkutano ambao Waziri Mkuu Modi alihudhuria.

(iv) Tuongeze uzalishaji wa mazao haya. Juhudi za diplomasia ya kurudisha soko letu ziende sambamba na kuongeza uzalishaji wetu katika kulima mazao haya. Ni lazima kuongeza uzalishaji wa mazao haya ili kuweza kupata mapato zaidi ya fedha za kigeni kwa mauzo ya nje.

Pia biashara ya mbaazi, choroko, dengu na gilgilani inaweza kuchangia kwenye juhudi za kuondoa umaskini wa wakulima wetu ikiwa tutaweka mkakati maalum wa uendelezwaji wa mazao haya. Mkakati huo unapaswa kuhusisha kuwahamasisha wakulima waliokata tamaa kuanza upya kulima mazao haya, kisha kuwaunganisha kwenye vyama vya ushirika, kuhakikisha vyama hivyo vya ushirika wa wakulima tunaviunganisha na masoko moja kwa moja bila kupitia watu wa kati (madalali wanaowanyonya) na kuongeza tija ya kilimo chao kwa kuwaunganisha kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na kuweka fao la bei kwenye mifuko hiyo ili kuwalinda pale bei ya mazao inapoanguka

Mheshimiwa Mwenyeikiti, tukifanya haya, ni imani yangu kuwa tutaweza kabisa kuongeza uzalishaji hata kwa tani tano tu kutoka sasa ili kufikia mapato ya USD bilioni moja ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kuwasilisha.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tozo mpya imeibuka mpakani Tunduma inaitwa tozo ya uzito wa mizigo inayotokea Zambia ambapo lori moja hulipishwa hadi shilingi 400,000. Hii ni kero mpya na inachangia kuongeza gharama za uzalishaji kwa viwanda vya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni hili la *Kurasini Logistic Centre*. Natambua jitihada binafsi za Mheshimiwa

Waziri lakini sina budi kuliingiza katika rekodi ili nguvu iongezeke katika kulishughulikia suala hili hasa ukizingatia pesa nyingi ya Serikali iliyoingia hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la mwisho ni unyanyasaji wa *TRA* dhidi ya wafanyabiashara kwa kuwakadiria kodi kubwa kuliko hata mitaji yao kimakosa na wanapotakiwa kuhakiki inachukua muda mrefu sana na kuathiri uzalishaji.

**MHE. ALFREDINA A. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namkushukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa hotuba yako nzuri, napenda kupongeza Kamati ya Viwanda na Uwekezaji kwa maoni yao, naomba Serikali iyafanyie kazi maoni hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi ushauri wangu katika Wizara hii naomba katika Mkoa wangu wa Kagera tupatiwe viwanda vidogo vidogo, tunalima maparachichi kwa wingi yanaharibika mashambani, nanasi zinastawi sehemu nyingi, hata ndizi zinaweza kukaushwa na kuwa-*packed* katika mifuko ya plastiki, tukitumia utaalamu tutapata hela za kujikimu shida zetu. Mkoa wa Kagera ni wa mwisho kwa umaskini au ni wa pili kutoka mwisho, Mheshimiwa Waziri ikupendeze utuonee huruma walau tufikirie tuwekwe kwenye *list* ya watakaofikiriwa kuanzishiwa viwanda vidogo vidogo na vya kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatakia kazi nzuri na ya mafanikio, Mungu awabariki sana.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uvunaji wa magadi Engaruka mradi wa kimkakati. Mheshimiwa Waziri anatambua wananchi wa Engaruka - Monduli wameridhia kuachia hekari 75,000 kwa ajili ya ujenzi a kiwanda cha magadi, lakini changamoto kubwa ni barabara. Pamoja na nia ya Serikali kutaka kujenga barabara ya Mto Mbu - Loliondo lakini ujenzi huo utachukua muda mrefu sana. Je, ni nini mkakati wa kujenga barabara hicho, ni lini kiwanda hiki

kitajengwa wananchi waruhusiwe kuendeleza maeneo yao mpaka Serikali itakapokuwa tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda cha nyama Makuyuni kimekamilika lakini tumemkosa mwekezaji wa kuendesha kiwanda hicho. Ni nini mikakati ya Wizara kutusaidia kupati mwekezaji?

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji Wakuu kwa kazi nzuri inayofanyika katika Wizara ya Viwanda na Biashara. Wengi hawakuamini kuwa Tanzania ya viwanda inawezekana hayawi, hayawi, sasa yamekuwa. Nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa viwanda vingi ambavyo vimeanzishwa nchini, viwanda hivi ndivyo vitaipeleka nchi yetu kwenye uchumi wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi wamehamasika kuanzisha viwanda, wanachohitaji ni kuwa karibu nao ili wapate ushauri wa kina. Wanahitaji ushauri/elimu juu ya aina ya viwanda vinavyofaa kuanzishwa katika maeneo yao, viwanda vitakavyotumia malighafi zinazopatikana karibu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawa wanahitaji ushauri wa kitaalam wa hatua za kufuata katika kuanzisha kiwanda (usajili, tozo, kodi, uthibiti na kadhalika) watu hawa wangependa kupata ushauri wa kitaalam wa namna ya kupata masoko. Wanahitaji kujua wapi mitaji rahisi inapatikana. Mheshimiwa Waziri aliwahi kusema kuwa upo mwongozo wa namna ya kuanzisha viwanda, tunaomba huo mwongozo usambazwe na wengi wausome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikoa mingi imeanza kupiga hatua kwa sababu wapo wafanyabiashara wengi wamewekeza kwenye Mikoa hiyo. Mkoa wa Kagera utaendelea kubaki nyuma sababu uwekezaji Mkoani wa Kagera uko chini sana, chini ya asilimia mbili. Wawekezaji wengi wanauona kuwa Mkoa wa Kagera uko pembezoni,

uko mbali na kadhalika. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhamasisha wawekezaji ili wakubali kuja wengi kuwekeza Mkoani Kagera?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na ardhi kwa kuniwezesha kuchangia machache. Ni kweli awamu hii ni ya uchumi wa viwanda lakini tujiulize viwanda hivyo vinavyoongelewa vitajengwa na kumalizika kwa wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inayo nia thabiti ya ujenzi wa viwanda lakini tatizo lipo kwa watendaji. Wapo baadhi ya watendaji ambao hawana nia nzuri na Taifa hili, wanadumaza maendeleo ya Taifa. Hawa watendaji wanakuwa wepesi wa kuomba rushwa kiasi kwamba hata wawekezaji wanahofia kuwekeza nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanga kulikuwa na Kiwanda cha Mbolea ambacho kimeng'olewa mitambo na habari nilizonazo eti kimehamishiwa Minjingu. Namuomba Waziri aeleze ni sababu zipi zilizosababisha kuhamisha kiwanda hicho ukizingatia kilikuwa karibu na bahari, jambo lililosababisha kupata unafuu wa upokeaji wa malighafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kiwanda cha Chuma, kiwanda hiki kimekuwa ni chaka la uhalifu. Kuna watu wanaishi humo kama vivuli vyaoy vya kujificha. Hata mashine zake zilianza kung'olewa. Mheshimiwa Waziri anatuambia nini kuhusu utendaji kazi wa hiki Kiwanda cha Chuma cha Tanga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanga kuna viwanda vya wamiliki wa sekta binafsi, viwanda ambavyo vinatoa ajira kwa wananchi wa Tanga hususani vijana. Tunalalamika kuwa vijana wengi wamejiingiza katika dawa za kulevya hii huenda inasababishwa na ukosefu wa kazi za kufanya matokeo yake wanaamua kutumia dawa za kulevya. Serikali iangalie



umuhimu wa kuanzisha viwanda ili viweze kutoa ajira hususani kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inasema kuwa wanafunzi wanaomaliza masomo wanaweza wakajijiri wao wenyewe, siyo kweli kwa vile mtu hawezi kumaliza masomo kisha akawa ana mtaji wa kufanya biashara yoyote, biashara ni mtaji. Je, anayetoka chuoni atapata wapi mtaji wa kumuwezesha kufanya biashara?

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa jitihada zake za makusudi za kuhakikisha Tanzania inakuwa nchi ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iendelee na mikutano ya mara kwa mara na wadau, wawekezaji na wafanyabiashara ili kubaini changamoto, matatizo na vikwazo vinavyowakabili ikiwemo kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza sekta ya viwanda ni lazima kuiendeleza sekta ya kilimo, uvuvi na mifugo vipewe kipaumbele ili kupata malighafi za kupeleka viwandani, malighafi zitoke hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji wa viwanda vya maziwa wana changamoto ya kodi mbalimbali hivyo ni vema eneo hilo liangaliwe upya. Wafanyabiashara wadogo wadogo kama mama lishe na wajasiriamali wadogo wanasumbuliwa sana kuhusu kodi, hawana uwezo wa kulipa kutokana na faida kuwa ndogo. Serikali iangalie jambo hili ili wananchi wetu wanyonge waweze kujikwamua na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu kwenye hoja hii na mazingira ya uwekezaji. Mazingira ya uwekezaji nchini bado siyo mazuri sana hasa kwa wawekezaji wadogo wadogo

au wazawa. Mazingira haya yanafanya gharama za uzalishaji wa bidhaa nchini kuwa juu kiasi cha kufanya bidhaa zinazozalishwa nchini kushindwa kumudu ushindani wa bidhaa zinazozalishwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utitiri wa mamlaka za usimamizi ni kikwazo kingine kwa wawekezaji wazawa, mfano bidhaa moja husimamiwa na mamlaka zaidi ya tano kama vile kiwanda kidogo cha kusindika nafaka husimamiwa na *TBS, TFDA, OSHA, NEMC* na kadhalika. Taasisi hizi zote zinatoza ada au ushuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa kiwango maalum cha bidhaa (*standard*) kunafanya wazalishaji kukosa ushindani ulio sawa kwenye soko. Bidhaa ya aina moja huzalishwa katika ubora au *standard* tofauti, mfano hapa nchini hatuna kiwango au *standard* ya bidhaa za nafaka kama sembe na unga wa ngano hivyo washindani hushindania rangi ya sembe bila kujali ubora wake ambao unapaswa upimwe kwa *extraction rate* toka kwenye maghali ghafiki. Taasisi kama *TBS* na *TFDA* wana *standard* ambayo ndiyo ingekuwa mwongozo kwa wasindikaji wote wa nafaka hivyo kulinda upotevu wa nafaka unaotokana na wasindikaji kukosa *standard* badala yake wanashindania weupe wa sembe, mchele au ngano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa malighafi kwa viwanda vidogo ni tatizo lingine hasa kwa yale mazao yanayouzwa kwa njia ya mnada. Wawekezaji wadogo hushindwa kuingia mnadani kushindana na wafanyabiashara wakubwa, hivyo viwanda vidogo vidogo hukosa malighafi baada ya kushindwa kuingia mnadani. Mfano, vikundi vya ubanguaji wa korosho hukosa korosho baada ya akina mama hao kushindwa kuingia mnadani, hawaruhusiwi kununua korosho nje ya mnada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo naishauri Serikali ione namna nzuri ya kuwawezesha wawekezaji hawa wadogo namna ya kupata malighafi ikiwezekana waruhusiwe kununua nje ya mnada.

## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji katika viwanda kwa kiasi kikubwa hutegemea mazao ya mashambani kilimo, wako wawekezaji wanaotaka kuwekeza kwenye kilimo kwanza ili kupata malighafi za viwandani na hatimaye waje kwenye viwanda vya kusindika mazao ya kilimo lakini upatikanaji wa ardhi ni mgumu sana, hasa kwenye vijiji ambavyo havijaingia kwenye mpango wa matumizi bora ya ardhi. Jambo hili limekuwa kikwazo kikubwa kwa wawekezaji wa upande wa kilimo hasa kwa mashamba makubwa, urasimu wa upatikanaji wa ardhi ni lazima ukaangaliwa upya ili uwekezaji katika kilimo uwe na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa viwanda nchini kulitegemea kufungua ajira kwa wazawa, lakini kinyume chake ajira nyingi nchini huchukuliwa na wageni hasa kwenye viwanda vya watu binafsi. Wazawa wameendelea kuwa vibarua viwandani. Hakuna namba maalum ya ajira kwa wageni wakati katika nchi za wenzetu mwekezaji anaposaini mkataba wa uwekezaji hupewa idadi maalum ya wafanyakazi wa kigeni lakini hapa kwetu hakuna ufuatiliaji wa sheria hii. Mfano, Uganda mwekezaji wa kigeni huruhusiwa kuajiri wafanyakazi watano tu nje ya nchi yao ili kuwapa ajira wazawa na hao wachache waliopata ajira mishahara yao ni midogo sana na mazingira ya kazi (*job security*) ni ndogo sana, wazawa wananyanyaswa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ambazo zimesahauliwa katika uwekezaji nchini ni sekta ya kilimo. Pamoja na kuwa na ardhi kubwa yenye rutuba kwa mazao mengi, lakini sekta hii haijatangazwa kama ilivyo sekta nyingine. Wawekezaji wa kilimo cha biashara hapa nchini kinafanywa kwa kiwango kidogo sana. Mfano, hapa nchini viwanda vyote vya ngano vinaagiza ngano kutoka nje kwa asilimia mia moja, hakuna mashamba ya ngano nchini tangu kufa kwa mashamba ya *NAFCO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuende na kauli mbiu ya nchi ya viwanda basi ni vema tukaamua kuwekeza kwenye kilimo.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono, nawatakia kila la kheri katika utendaji mzuri uliotokuka. Naomba sana na kwa mara nyingine ulinusuru zao la pamba tumkomboe mkulima wa pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la pamba linaonekana kama zao lisilokuwa na maana, ili kuwakomboa wakulima wa pamba, naomba *Nyambiti Ginnery* ifufuliwe ili ianze kazi ya kuchambua pamba kama ilivyokuwa zamani. Tathmini tayari imeshafanyika kupitia mifuko ya kijamii kupitia Ndugu Bandawe (*PPF*), kinachochelewesha ni uamuzi toka Ofisi ya Waziri Mkuu. Nashauri maamuzi yafanyike ili *ginnery* hiyo ianze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili Mheshimiwa Mwijage unalifahamu, naomba uwasiliane na Mheshimiwa Mhagama ili uamuzi utolewe. Uwepo wa kiwanda hicho utachochea upatikanaji wa ajira za kudumu na muda. Ajira kwa akina mama lishe na kadhalika.

Mheshimiwa Mwijage, najua ukiamua suala hili utalimaliza haraka. Nawasilisha.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kuipongeza Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa kutimiza azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuifanya Tanzania yenye viwanda kutimia. Pia kupongeza kauli ya Serikali iliyotolewa jana na Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu mafuta. Hali iliyopo nje kwa wapiga kura wetu ni mbaya, kwanza mafuta yamepotea, pili mafuta yamepandishwa bei sana. Tuzidi kuiomba Serikali kutatua sintofahamu zilizopo baina ya wafanyabiashara, *TRA* na Wizara ili mwezi wa mfungo wa Ramadhani mafuta yapatikane na kwa bei ya chini kama ilivyokuwa hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili nizungumzie pia hali ya upoteaji wa sukari na upandaji bei. Kumekuwa na tabia ya wafanyabiashara kuficha mafuta, sukari na bidhaa nyingine za chakula na ifikapo mwezi Mtukufu wa Ramadhani wanaviachia na kuvipandisha bei

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

na kuwasababishia Waislamu wanaofanya ibada hii muhimu kupata adha kubwa ya kupata mahitaji yao muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la makontena yaliyozuliwa bandarini kwa kigezo cha kulipia kodi, hii ni hatari sana. Tende hizi zinatumiwa na Waislamu kipindi cha mfungo wa Ramadhani kwa mujibu wa kalenda yetu tunatarajia mfungo kuanza tarehe 17 Mei, 2018 na tende hizi ni kifungua kinywa muhimu sana kwa mwezi huu wa Ramadhani. Tuombe Serikali iliangualie hili suala ili basi *TRA* waweze kuruhusu makontena hayo na hatimaye Waislamu waanze mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhani vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda katika Mkoa wa Kigoma; Mkoa wa Kigoma tunalima zao la michikichi, tuliomba kupitia bajeti iliyopita kwa nini Wizara wasitoe ruzuku kwenye zao la michikichi ili kuwawezesha wakulima wengi ndani ya Mkoa wa Kigoma kulima zao hili kwa wingi tofauti na ilivyo sasa kuna mzungu, raia wa kigeni anavyo vitalu vya michikichi anauza kila mche mmoja shilingi 5,000 na ekari moja inahitajika michikichi 40 hadi 45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo wakulima wengi wanaendelea kutumia michikichi yao ya asili tangu babu zao. Kwa kufanya hivyo hawapati mafuta ya kutosha, lakini wangepata miche ya ruzuku ya michikichi ya kisasa wangeweza kupata mafuta mengi ya kukidhi mahitaji ya walaji na pia kipato chao kingeongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wawekezaji wengi toka nje ya nchi wako tayari kuingia ubia na Watanzania kwenye viwanda vya kuunganisha pikipiki (bodaboda). Tatizo kubwa linalowakuta Watanzania ni kukosa *Government Guarantee*, kuwapa *assurance* wawekezaji kuingia ubia na Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niombe Serikali kupeleka umeme Wilaya ya Uvinza ili kuwawezesha wananchi kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya mafuta ya mawese, mafuta ya mise na utengenezaji wa sabuni sambamba na

viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara kwa jinsi wanavyojituma katika jitihada ya kuusimamia na kuutekeleza kwa vitendo uchumi wa viwanda nchini, pamoja na changamoto zote na utofauti wa uelewa wa nini ni kiwanda kwa wananchi, baadhi ya wenzetu wa upande wa pili, ni vema yakatolewa maelezo ya ufafanuzi kwa lugha nyepesi ya nini ni kiwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Rukwa wananchi wanashughulika wao wenyewe bila ya kusukumwa katika shughuli za kilimo mahindi, mpunga, maharage, ulezi, alizeti, miwa, ufuta na kadhalika. Utaratibu wa kuuza mahindi nje ya nchi, natoa ushauri Serikali kutoa kiasi maalumu na kiasi kikubwa yaongezwe thamani (unga) wa kuuzwa huko. Kuongeza pato kwa mkulima na Taifa letu, mfano asilimia 25 kwa asilimia 75 au asilimia 45 kwa asilimia 55 kwa kuanzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mema yaliyofuatia zoezi la wafanyabiashara ndogo ndogo kutengewa maeneo katika ukurasa 43 - 44 ndani ya hotuba ya Waziri kwa mikoa minne kati ya 26 hii kasi ndogo, kwani wafanyabiashara ndogo ndogo ni eneo pana kwa vijana wetu la kujijiri, hivyo tunahitaji kuongeza kasi, kwani tutawakatisha tamaa vijana na kusababisha wakajiunga na mambo yasiyostahiki kwao na Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali/Wizara kufuatilia zoezi hili ndani ya muda wa miezi sita ya mwaka 2018/2019 kwani ni kero iliyokithiri ndani ya nchi kwa hawa wafanyabiashara ndogo ndogo na ni sehemu kubwa ya wapiga kura wetu ili tuachane na hii changamoto. Pia Serikali

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

kuangalia namna sahihi na rafiki kwa wafanyabiashara kuhusu na malipo ya VAT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa 29 - 30 wa hotuba inazungumzia suala la usindikaji wa mafuta ya alizeti ingawa tuna pamba, karanga, ufuta na kadhalika, kwa mchanganuo wa hizi mbegu zitolewazo mafuta, ndiyo asilimia 30 ndani ya hayo mahitaji yetu ya tani 700,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali kuona umuhimu wa dhati na kulegeza masharti kwa viwanda vya mafuta ya pamba na alizeti ambayo tunayatumia sana nchini kuongeza idadi ya viwanda kutoka 21 na kuongeza idadi ya viwanda vidogo kutoka 750 kwa kuweka lengo hadi tufikapo mwaka 2020 tufikie uzalishaji wa asilimia 45 ya mafuta ya kula, kwani mazao hayo yanazalishwa kwa wingi hapa nchini ni kuwaongezea uwezo wa kilimo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali kuweka mkazo kwa wafanyabiashara wote watakaohusika kwa namna moja au nyingine yaani chakula, mafuta na sukari kwa ndugu zetu wa Kiislamu ili waweze kutimiza ibada ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, urasimu wa kupata leseni ya biashara; wafanyabiashara katika Halmashauri husika wanapata shida kupata leseni ya biashara kwa masharti ya kuwa na *TIN number* ya TRA. Akifika TRA anaambiwa lazima afanyiwe makadirio ya kodi ya biashara yake bila hata kuiona biashara yenyewe. TRA Officers wanakaa ofisini na kufanya makadirio ya mfanyabiashara bila kuona ukubwa wa biashara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfanyabiashara akishakadiriwa kodi ya juu zaidi ya biashara yake anagoma kukata *TIN*, kisha anaendelea na biashara zake bila kuwa na leseni jambo linalopoteza mapato ya Halmashauri kwani

leseni zinakatwa na Halmashauri baada ya kuwa mfanyabiashara amekidhi masharti ya *TRA* ya kuwa na *TIN number*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri, *TRA* wasifanye makadirio ya kodi kwa wafanyabiashaa wakiwa ofisini, wafike *site* wakaone ili wasiwaonee au kuwapendelea wafanyabiashara. Leseni za biashara zitolewe na Halmashauri bila masharti ya kuwa na *TIN number* ili waendeleo na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji, viwanda vikubwa na vya kati hutegemea nishati ya umeme. Kakonko hakuna umeme wa uhakika wa kuwavutia wawekezaji kuja kuweka viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda hutegemea miundombinu ya barabara kwa ajili ya kusafirisha malighafi, Kakonko hadi Kigoma ni kilometa 30 na barabara ni mbovu hivyo haiwavutii wawekezaji kuwekeza Mkoa wa Kigoma na Wilaya zake kama Kakonko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri aliahidi kiwanda cha kuchakata mihogo tangu mwaka 2016 na kiwanda hicho kinasubiriwa Kakonko. Nashauri kiwanda hicho kipatikane ili wananchi waendeleo kuwa na imani naye asije kuonekana ni muongo. Heshima ya Kiongozi ni kutekelekeza ahadi zake anazotoa.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja timu yake kwa kazi kubwa wanayoifanya, kwa kuhakikisha tunafikia uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali iwekeze sana katika kilimo ili tuweze kupata malighafi kutoka kwenye mazao yetu ambayo tunayalima sisi wenyewe, kwani bila kuwekeza katika kilimo tutakuwa tunachelewa sana kuwa na viwanda. Niendeleo kuishauri Serikali yangu tukufu ipeleke pembejeo za kutosha kwa wakulima na kujenga mabwawa



ya kutosha ili wananchi waweze kulima kilimo cha umwagiliaji ili kuongeza tija katika kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia lazima tuhakikishe wananchi wanapata elimu ya ufundi hasa kwa vijana wetu wa Kitanzania ili wawe na uelewa wa kutosha katika suala zima la kusimamia viwanda vyetu tunavyo kusudia kuvijenga. Hivyo basi, Serikali ijenge Vyuo vya *VETA* kila Jimbo na sio kila Wilaya, kwa mfano Wilaya ya Lushoto tangu ianzishwe haina Chuo cha *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kupoteza rasilimali watu na sio hivyo tu pia tunakosa vijana wenye taaluma ambao hawataweza kusimamia viwanda vyetu. Lakini hatujachelewa tuanze sasa kujenga vyuo hivyo ili vijana wetu waende sawa na ajira ya ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali kuanzisha Viwanda Vidogo Vidogo yaani *SIDO* kwani viwanda hivi kwanza vitainua kipato cha mtu mmoja mmoja, pili, uchumi katika sehemu husika kilipowekwa utakuwa na tatu, vijana wengi watapata ajira pamoja na kupata ujuzi hapo hapo. Kwa hiyo, niendeleo kuishauri Serikali kuanzisha viwanda vidogo vidogo hivi katika kila Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanga ulikuwa ni Mkoa wa viwanda lakini sasa viwanda vingi vimekufa. Hivyo basi, niiombe Serikali iweze kurudisha viwanda vile vyote vilivyo kufa hasa kiwanda cha sabuni, nondo na kiwanda cha mbolea. Ni imani yangu viwanda hivi vikifufuliwa Tanga tutakuwa tumepiga hatua kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuongelea uchumi wa viwanda kama barabara zetu ni mbovu, maji hakuna na umeme haupo. Kwa hiyo, hebu tupeleke miundombinu hii, kwani hii ndiyo itatufikisha katika uchumi wa viwanda bila hivyo tutachelewa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lushoto ni Wilaya inayojulikana kwa kuzalisha matunda na mboga mboga

lakini cha kushangaza Serikali haijawahi kufikiria kuweka viwanda Lushoto. Hivyo basi niombe Serikali yangu iweke viwanda Lushoto hasa viwanda vya matunda na mboga mboga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wawekezaji, wapo wawekezaji wazuri na wabaya kwa mfano Lushoto kuna Kiwanda cha Miwati. Lakini kiwanda kile hakifanyi vizuri kwa sababu hakiwalipi mishahara wafanyakazi wake. Kwa hiyo, hili linasikitisha sana, kwani sera ya sasa hivi ni ya viwanda lakini kiwanda hiki kimekuwa hakina manufaa kwa wananchi wa Lushoto. Zaidi ya kuwanyanyasa wafanyakazi wake. Kwa hiyo, niombe Serikali ifuatilie suala hili kwa haraka ili wafanyakazi hawa waweze kulipwa stahiki zao. Pamoja na kujua mwenendo mzima wa uendeshaji wa kiwanda hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali yangu tukufu kwa kuwa tunahitaji wawekezaji kwa wingi na tunawapenda wafanyabiashara wetu. Hivyo basi, ipunguze haya malalamiko yanayo lalamikiwa na wawekezaji pamoja na wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vipimo, maduka yote yawe na mizani ya kupimia bidhaa zinazouzwa. Mizani hiyo iwe na uwezo wa kupima zaidi ya kilo 50 ili mteja akihitaji sukari ya kilo 50, *cement* ya kilo 50, unga wa ngano kilo 50, mbolea ya kilo 50 aweze kupimiwa, maduka mengi yanayouza bidhaa hizo hayapimi na kwa wafanyabiashara wasio waaminifu huwaibia wateja na kuwasababishia hasara wateja hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba za ubavuni kwenye malori ya mchanga Wizara iangalie viwango vya kuandika namba za ubavuni na hasa pale inapokuwa inaandikwa kwa mwaka wa pili, ada hii ni kero na haina uhalisia hivyo inasababisha maudhi na usumbufu kwa wamiliki wa magari hayo, nafahamu fika ni sheria na nia ni kumlinda mlaji, lakini

gharama za kuandika namba hizo inamrudia huyo huyo anayelindwa. Hivyo nashauri Serikali iondoe ada ya kuandika namba ya ujazo kwa mara ya pili ili kuondoa gharama na kero kwa wamiliki. Kama ipo kwenye sheria ya msingi basi iletwe Bungeni na kama ipo ndani ya uwezo wa Wizara basi jambo hili liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshindwa kabisa kudhibiti rumbesa ya viazi mviringo, hii ni aibu kwa wataalam wa Wizara kushindwa kudhibiti jambo la wazi kama hili. Serikali isaidie ujenzi wa *parking house (cold room)* ambazo zitawasaidia wateja wa matunda aina ya parachichi kuweza kununua matunda hayo na kuyaandaa vizuri kwa ajili ya masoko ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo utakuwa umewawezesha wakulima kuuza zao hili na kuisaidia nchi kupata fedha za kigeni kwani parachichi zinazolimwa Njombe zimepata soko nje na hasa Ulaya.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa maandishi. Kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mwijage na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Manyanya, pamoja na timu yao ya watendaji wa Wizara kwa jinsi wanavyosimamia vizuri Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri, ili viwanda vyetu viweze kufanya kazi kwa tija ni lazima kuhakikisha ipo malighafi ya kutosha. Katika mikoa inayolima korosho, msimu huwa unaisha mwezi Desemba, inashangaza sana kuona kwamba wateja wa korosho iliyobanguuliwa wanapoagiza bidhaa hii tena tani 50 tu kwa mwezi. Inakosekana kwa madai kwamba hakuna malighafi wakati ambapo mahitaji yenyewe yametoka mwezi wa pili. Hii inamaanisha kwamba uzalishaji katika viwanda vyetu huwa ni kwa kipindi cha miezi mitatu tu (Novemba, Desemba na Januari).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba jitihada ifanyike kufuatilia tatizo ni nini. Je, ni ukosefu wa mitaji ya kununua

malighafi ya kutosha au ni kukosa mgao wa kutosha ikiwa na maana ya kibali cha ununuzi kimewabana wenye viwanda? Kaeni na wenye viwanda vya korosho na Wizara ya Kilimo ili kujadili namna bora ya kuwezesha upatikanaji wa korosho kwa viwanda vyetu katika kipindi cha mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vyetu vidogo bado vina changamoto kubwa ya kukatikatika umeme hovyona ukosefu wa maji na hivyo kuathiri uzalishaji kwa ufanisi na tija. Wizara ya Viwanda ikae na Wizara ya Maji na Wizara ya Nishati ili kutafuta ufumbuzi wa tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu itolewe kwa wajasiriamali kuhusu namna ya kuanzisha viwanda vidogo. Naunga mkono hoja.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa Serikali itueleze viwanda vilivyobinafsishwa mwaka1992, kati ya156 ni vingapi vinavyofanya kazi na visivyofanya kazi ni vingapi na wale waliopelekea hasara hii wamechukuliwa hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi walio wengi zaidi ya asilimia 80 wanaishi vijijini na kule ndiko kilio kilipo, pamoja na Serikali kupeleka umeme vijijini lakini umeme ule ni mdogo sana hata kuwasha taa. Serikali iliahidi kuwekeza katika viwanda vidogo vidogo lakini vimeshindwa kabisa, lazima pawepo na mgongano wa biashara,vyakula viwe *process* kule kule vijijini na hii itasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana kutokimbilia mjini kutafuta ajira na wengine kuingia katika vitendo viovu. Serikali ije na itueleze nia na mikakati gani ya kuhakikisha mazao yanaongezewa thamani kule kule ili wakulima wapate faida. Hivyo lazima pawepo na viwanda vidogo na vya kati huko vijijini. Wakulima wengi sasa hivi mazao yao yanaozea kwenye maghala kwa kukosa masoko, mfano mahindi na mbaazi wakulima wengi sana wamepoteza mitaji hata ya kuendeleza kilimo chao.

## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mji wa Moshi ulijulikana sana kwa kuwa na viwanda vya misumari, ngozi, makaratasi, viberiti mpaka kiwanda cha dawa lakini sasa hivi kinachofanya kazi tena kwa kuharibu mazingira ya Moshi, harufu mbaya inayochangia afya ya wakazi wa Pasua na Boma Mbuzi ni Kiwanda cha Ngozi. Je, Serikali ina mikakati gani hata ya kufufua *Kibo Match*, viwanda hivi vilichangia sana kupata ajira kwa vijana wetu lakini cha kusikitisha kwa sasa vingi vimeugezwa kuwa stoo za kuhifadhiya vitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda bila kuwa na umeme na maji ya uhakika tutakuwa tunaviongelea viwanda hivi kwenye vitabu na cha zaidi mazingira ya kufanya biashara hapa nchini ni magumu sana, mpaka mfanyabiashara apate kibali cha kufanyia biashara inaweza hata kutumia zaidi ya mwezi. Pia mfumo wa kodi na tozo ni nyingi mno na hii inachangia wafanyabiashara wengi kufanya biashara au kuhama na kwenda kuwekeza kwenye nchi nyingine. Serikali ifanye kazi kwa pamoja kabla *TRA* haijatoa makisio, basi wawapatie leseni wafanyabiashara wafanye kazi nchini wajue wanawapa makisio ya kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei za bidhaa zimekuwa hazipo elekezi Serikali inatoa tu matamko ya kisiasa mfano ilitoa tamko sukari iuzwe shilingi 2,500 kwa kilo lakini sukari inauzwa mpaka shilingi 3,000 kwa kilo sababu hakuna chombo kinachofuatilia bei hizi. Hivi Tume ya Bei (*Price Commission*) haipo? Pamoja na masoko kuwa huria lakini lazima Serikali iangalie ni jinsi gani wataweka *system* ya kufuatilia bei za bidhaa kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitafuta mwekezaji kwa ajili ya kiwanda mama cha *Machine Tools* kilichopo Kilimanjaro. Pamoja na vipuri kupitwa na wakati lakini majengo bado yapo, sasa Serikali imefikia wapi kupata uwekezaji wa kuendeleza kiwanda hiki ambacho kingekuwa mkombozi wa kutengeneza viwanda vidogo na vya kati ili viweze kufanya kazi vijijini?

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika hoja hii ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa viwanda katika Mkoa wa Njombe, kwa vile Serikali ya Awamu ya Tano ina mkakati wa Tanzania ya viwanda, naiomba iandae mazingira wezeshi na rafiki kwa wafanyabiashara wa Mkoa wa Njombe ili wawekeze katika viwanda. Tatizo kubwa ni kwamba inawabana sana wafanyabiashara kwa taratibu ngumu zinazosababisha watu waone vigumu kuanzisha viwanda. Pia zile hatua za uanzishwaji wa viwanda ni ngumu na ni ndefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa jokofu la kuhifadhi matunda (maparachichi), Mkoa wa Njombe unazalisha matunda ya parachichi kwa wingi lakini hakuna jokofu la barafu kwa ajili ya kuhifadhi matunda hayo. Naiomba Serikali itusaidie kutafuta fedha ya kununulia jokofu hilo au kupata mwekezaji mkubwa anayeweza kutufadhili jokofu hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa soko la mahindi; wakulima wa nchi nzima wanahamasika kulima mahindi kwa wingi lakini tatizo kubwa hakuna soko, mfano wakulima wa Mkoa wa Njombe walipata mahindi kwa wingi lakini mahindi hayo yanaoza. Naiomba Serikali ifungue mipaka ili wananchi wa Mkoa wa Njombe wauze mahindi yao nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ya kuchangia katika hotuba hii ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Pili, nampongeza Waziri na watendaji wake wote kwa kuandika na kuiwakilisha ripoti hii kwa umakini mkubwa. Katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali yetu kwa kutangaza na kuweka azma ya kuifanya nchi yetu kuwa nchi ya viwanda. Jambo hili ni jema lakini linahitaji matayarisho makubwa ili kufikia lengo. Lazima tuwe na rasilimali za aina zote hasa rasilimali watu na vifaa (*Human Resource and Materials*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ushauri wangu kwenye kutayarisha rasilimali watu lazima tuwatayarishe vijana wetu kwa kuwapatia taaluma inayohusu viwanda. Haitakuwa vizuri leo tuna vijana waliomaliza vyo wengi, tukatumia wataalam wa kigeni badala ya vijana wetu kwa ukosefu wa ujuzi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutayarisha rasilimali vifaa ni lazima Serikali itilie mkazo kwenye sekta ya kilimo. Kilimo ndiyo msingi wa kila jambo pamoja na viwanda. Hivyo, Serikali ni lazima kuiwezesha kwa maeneo yote sekta ya kilimo kwa kuipatia vitendea kazi na ruhusa zote zitakazo fanikisha azma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya uwekezaji; niishauri Serikali kuangalia jinsi Serikali na watendaji kupunguza urasimu kwa wawekezaji kwani imefikia watu/wawekezaji wanahofia kuwekeza kutokana na sera zetu zinazobadilika mara kwa mara, hivyo kuhofia kupoteza mitaji yao. Pia nizungumzie tozo zilizopita kiasi mfano *TBS, TFDA, OSHA* vitu vyote hivyo badala iwe inalipiwa mahali pamoja na kuhakikisha kodi yake inakuwa ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu leseni la biashara; niishauri Serikali kuangalia mlolongo wa upatikanaji wa leseni. Unatakiwa kulipa *TRA* baada ya kukadiriwa kwa mteja ambaye ndio kwanza anaanza biashara atakadiriwa kwa mteja badala kwa faida baada ya biashara.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, masoko ya uhakika; nizungumzie masuala ya masoko nishauri Serikali kuhakikisha inatafuta soko la bidhaa za watanzania kwani wanazalisha bidhaa lakini hakuna soko la uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali ijitahidi kutafuta masoko hata kwa bidhaa za viwandani kwani kuanzisha viwanda bila soko la bidhaa hizo itakuwa kama viuatilifu vya Kibaha ambavyo hakuna soko na uzalishaji imebidi kupunguzwa. Kutokana na kupungua uzalishaji kiwanda kimeshindwa kuajiri vijana wa Kibaha wa kutosha.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na kwa utekelezaji mzuri wa ilani. Nawapongeza pia Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji kwa utendaji mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais na Serikali ya Awamu ya Tano kwa utekelezaji wa mkakakti wa ujenzi wa viwanda ili Tanzania ifikie hadhi ya nchi ya uchumi wa kati mwaka 2025. Huu ni ukombozi kwa vijana na wananchi kwa ujumla, vijana shida yao kubwa ni ajira na viwanda ni ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Bagamoyo Serikali imetenga eneo la viwanda kwa awamu mbili; *EPZ I* hekta 5,722 (= eka 14,355) na *EPZ II* hekta 4,338; jumla hekta 9,080.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya *EPZ I*, yamethaminiwa mwaka 2008 na hekta 2,399 zimeshalipwa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililopo ni kuwa wananchi 1,025 kati ya 2,180 hawajalipwa fidia zao hadi leo miaka kumi sasa. Namuomba Mheshimiwa Waziri awajulishe wananchi wa Kata za Zinga na Kiromo wanaopisha *EPZ* ni lini watalipwa fidia zao?



## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la *EPZ II* - hekta 4,338 linajumuisha maeneo yenye makazi ya wananchi katika vijiji vya Zinga, Kondo, Mlingotini na Kiromo. Vijiji hivi vina jumla ya kaya 3,381 (sensa ya zoezi) zenye watu 12,797. Maeneo haya hayajathaminiwa wala watu hawajalipwa fidia. Suala kuu ni kwamba, wananchi hawaridhii kuhamishwa maeneo yao ya makazi hasa kwa kuzingatia kuwa tayari wameshatoa hekta 5,742 kwa ajili ya *EPZ*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu tukufu kuwaachia wananchi maeneo yao ya makazi, wananchi hawa hawana hamu wala hawana nguvu ya kuhama na hawana mahali pa kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kijiji cha Pande wanaopisha bandari mpaka sasa hawana eneo la makazi mbadala. Ni utaratibu wa kawaida duniani kwa wananchi wanaopisha miradi mikubwa ya kitaifa kupatiwa makazi mbadala. Wananchi wa Vijiji vya Pande na Mlingotini waliahidiwa na Serikali makazi mbadala. Naiomba Serikali tukufu iruhusu wananchi hao kupatiwa eneo la makazi mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, zuiu la mifuko ya *plastic*; nchi jirani zote katika kutekeleza *the so called EAC Polytene Material Control Bill* ilipitishwa baada ya muda wa karibu miaka mitano, zimezuia kabisa uzalishaji, usambazaji na matumzi ya mifuko ya *plastic*. Sisi Tanzania mpaka sasa tumeendelea kuzalisha mifuko ya *plastic* kwa namna ambayo imejaa ujanja mtupu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kenya na Uganda kuzuia, sasa sisi tumegeuzwa soko. Kati ya tani zaidi ya 1,500 zinazosambazwa kwa mwaka ni tani 100 tu ndo zinazalishwa hapa nchini, maana yake ni kuwa chini ya asilimia kumi ndio inazalishwa hapa nchini. Hivyo hoja ya kuwa tunalinda viwanda sio kweli kwa sababu asilimia 90 ya mifuko inatoka nje na zaidi nchi jirani.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira wanasema Viwanda, Biashara na Uwekezaji ndio kikwazo, wao hawana tatizo. Ni matumaini yangu kuwa kwenye hitimisho, Wizara itakuja na maelezo ni kwa nini mpaka sasa haijazuia uzalishaji kama inavyodaiwa wa mifuko ya *plastic*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *BRELA* na usajili wa kimtandao; wananchi wengi siku za nyuma waliliwa fedha zao na *middle men*, lakini toka usajili kuanza kufanyika kwa njia mtandao (*online*) kumekuwa na ufanisi wa hali ya juu, ni suala la kupongeza, ushauri, *BRELA* ifanye semina nyingi kadri iwezavyo ili elimu hii ienee maeneo mengi hasa yenye uzalishaji, kwa mfano Mafinga ina shughuli nyingi za mazao ya misitu, kuna mbao lakini wengi wa wafanyabiashara bado hawana elimu ya kutosha kuhusu umuhimu wa kuwa na kampuni na faida zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michezo ya kubahatisha; hii ni biashara inayokuwa kwa kasi sana. Hata hivyo taratibu zinazotawala biashara hii hazileti matunda bora, kwa mfano ilivyo sasa katika *Sports Betting*, mchezeshaji analipa asilimia sita ya mauzo ghafi. Hii iliwekwa kwa ajili ya kuvutia wawekezaji, baada ya kukua kwa hii biashara, ni wakati sasa kuzingatia yafuatayo:-

(i) Kuonesha uhuru/kodi ya mauzo kutoka asilimia sita hadi asilimia 20. Maana yake katika kila shilingi 100 Serikali itapata shilingi 20 badala ya shilingi sita ilivyo sasa.

(ii) Ili kuvutia wachezaji wengi ambao sasa baadhi yao wameanza kupendelea kucheza *Sports Betting* za nje kwa hoja kuwa makato ya asilimia 14 ya zawadi ya mshindi ina-*discourage*. Ni afadhali kanuni ikawa kwa mfumo wa *capital gain* asilimia kumi. Hii itachochea wengi kucheza na Serikali kupata nyingi katika ile asilimia 20 ya mauzo ghafi maana washindi ambao hutupatia asilimia 18 ni wachache kuliko wachezaji.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vilivyobinafsishwa; ushauri wangu kama ambayo Serikali inatutajia idadi ya viwanda, ituambie *status* ya viwanda vilivyokuwa vimebinafsisha ikoje, vingapi vinazalisha na kwa *capacity* gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya mazao ya misitu; nimeshaiomba Wizara na Waziri tufanye kongamano tukihusisha vyombo vyote muhimu kama vile *BRELA, OSHA, TIC, TIB, TRA, TFS, NEMC* na Wizara ili wawekezaji wa mazao ya misitu waweze kuelezwa fursa zilizopo, lakini pia kueleza changamoto wanazokabiliana nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya mazao ya misitu ni eneo lenye *potential*/kubwa. Ni masikitiko yangu kuwa jitihada za kumuomba Waziri kutembelea Mafinga ili kujione uwekezaji lakini pia kujionea changamoto zinazowakabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanga viwanda vingi vimekufa kifo kitakatifu, Viwanda vya Chuma, Viwanda vya Mbolea, Viwanda vya Mafuta ya Kujipaka na kadhalika. Katika hotuba yako hakuna mkakati wowote wa kufufua viwanda mkoani Tanga. Naomba utakapohitimisha nipate maelezo kuhusu masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Matunda Tanga ambacho kilipangwa kujengwa Segera ili kiweze kukusanya matunda ya Muheza, Lushoto na Handeni, je, ni lini na wapi Kiwanda cha Matunda kitajengwa Tanga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Muheza Kata Magorofo kuna shamba kubwa la michikichi ambalo linakufa kwa kukosa kiwanda cha kukamua. Je, ni lini Serikali itafufua kiwanda cha kukamua mawese kwa ajili ya upatikanaji wa ajira kwa wananchi na bidhaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mkakati gani wa kushughulikia matatizo ya wafanyakazi, viwandani ambayo

nayo kwa asilimia fulani yanachangia kufa, mfano wafanyakazi wa viwanda vya chai, Tarafa ya Amani.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika hapa na mimi nashiriki kikao hiki kujadili hotuba hii ya bajeti ya Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka 2018/2019. Hotuba hii imeandaliwa kwa kuzingatia mwelekeo wa nchi hivi sasa kuwa Tanzania ya viwanda. Napenda kuipongeza Wizara kwa kuandaa bajeti nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali inazoendelea kuzichukua hasa kusimamia na kaulimbiu ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kujenga uchumi wa Taifa unaotegemea viwanda. Kwa maelezo ya Serikali ni kwamba hadi kufikia mwezi Februari 2018 viwanda vipya 3,306 vimeanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali inaendelea kuhamasisha uwekezaji katika viwanda kwa kutoa vivutio vya kodi na visivyo vya kodi kwa wawekezaji mahiri, hii itasaidia kuongeza hamasa kwa wawekezaji wa ndani na wa nje. Hata hivyo naipongeza Serikali kwa kuendeleza na kuboresha miundombinu wezeshi kama vile barabara, reli, bandari, umeme na maji, haya ni maandalizi rafiki na ya kuvutia kwa wawekezaji watakaokuja na kuwekeza. Lakini haikuishia hapo, Serikali imeendelea kuhuisha sera, sheria na kanuni pamoja na kufuatilia utendaji wa viwanda vilivyobinafsishwa na kuchukua hatua stahiki kwa wamiliki walioenda kinyume na mikataba ya mauzo, ni hatua nzuri kwani kuna baadhi ya wawekezaji wasiokuwa waaminifu wamekuwa wakitumia viwanda hivyo vilivyobinafsishwa kwa matumizi tofauti na yale yaliyokusudiwa na Serikali wakati wa sera ya ubinafsishaji. Mpango wa Serikali kwa Mikoa na Halmashauri zote nchini kuwaelekeza kutenga maeneo ya uwekezaji wa viwanda ni mpango mzuri wenye tija na malengo chanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imehakikisha Sekta ya Hifadhi ya Jamii inashiriki kikamilifu katika ujenzi wa uchumi

## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

wa viwanda, pamoja na miradi mingine, *NSSF* na *PPF* kwa kushirikiana na Jeshi la Magereza wanatekeleza mradi mkubwa wa uzalishaji wa sukari Mkoani Morogoro, ni mpango mzuri na wa kupongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo hasa la mradi huo ni kuzalisha tani 250,000 za sukari na umeme MV 40, ni mkakati mzuri na wa kupongezwa hasa katika kipindi hiki ambacho Serikali ina mpango wa kufanya nchi yetu kuwa ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa viwanda unaendana hasa na masuala mazima ya kisayansi, hivyo ni budi Serikali kuendelea kufanya tafiti mbalimbali ili kuwezesha kugundua changamoto zilizopo na kukabiliana nazo. Viwanda vina faida kubwa sana kwa maendeleo ya nchi, viwanda hukuza ajira na kuleta maendeleo chanya, nchi kubwa duniani zenye uchumi mkubwa ziliwekeza zaidi katika viwanda na kuweza kuzalisha bidhaa mbalimbali na kuziua nje ya mipaka yao na hivyo kupata fedha za kigeni. Dhana nzima ya viwanda isibezwe kwani ni mpango wenye malengo mazuri kwa maendeleo ya Taifa letu na ni mpango endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuwa karibu na sekta binafsi, ni jambo la kupongeza kwani sekta binafsi ina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi nchini, kushirikiana kunaiwezesha Serikali kujua changamoto inazokabiliana nazo sekta binafsi na kuja na suluhisho la kitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Wizara kuendelea kuwa walezi wa sekta binafsi na kupokea ushauri ili uchumi wa nchi yetu uweze kuwa endelevu katika ukuaji. Kuna changamoto mbalimbali ambazo sekta binafsi inakutana nazo hasa katika masuala mbalimbali ya kikodi na kadhalika, lakini Wizara inatakiwa kuwa karibu na wadau hawa ili changamoto hizo ziwezekutatuliwa. Nampongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kukaa na sekta binafsi na kuwapa nafasi ya kuwakilisha kero zao, maoni na ushauri na kwa baadhi ya changamoto kuzifanyia kazi.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina fursa nyingi sana za kiuwekezaji, tuna maeneo mengi ambayo yanavutia kwa wawekezaji, tunahitaji wawekezaji wa ndani na wa nje, ni wajibu wa Wizara kuendelea kuwavutia wawekezaji kuweka mazingira rafiki ili tuweze kupata wawekezaji wengi zaidi kuja kuwekeza katika nyanja mbalimbali na kuzalisha ajira kwa wingi kwa watu wetu. Naishauri Wizara kuendelea kuwachukulia hatua wawekezaji ambao wamekalia baadhi ya maeneo kama viwanda, kuvifunga au kubadilisha matumizi, wanyang'anywe na kupewa wawekezaji wengine wenye nia njema na kuendeleza maeneo husika. Kibaha Vijijini tuna maeneo yaliyopimwa kwa ajili ya uwekezaji, maeneo ni mazuri na ukizingatia Kibaha Vijijini ni mji unaokuwa sasa na hata mazingira ya kiuwekezaji ni mazuri, miundombinu ipo vizuri, hivyo naomba Wizara itupe kipaumbele pale inapopata wawekezaji basi waje Kibaha Vijijini kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na mimi niweze kuchangia kwenye Wizara hii nyeti ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Sukari cha Illovo – Kilombero; kumekuwa na malalamiko makubwa sana ya wafanyakazi waliokuwa wanafanya kazi kwenye Kiwanda cha Sukari cha Kilombero kilichobinafsishwa na Serikali mwaka 1999-2000 ambapo wafanyakazi zaidi ya 3000 mpaka leo hawajalipwa fidia zao na wanapigwa danadana na hawapewi majibu ya kueleweka ya fidia zao, wengi ni watu wazima wengine wanakufa bila kulipwa haki zao na wengine wanategemea fidia hiyo ili waweze kusomesha watoto wao na pia kujiendeshea maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Waziri atakapokuja atupe majibu ni lini wananchi hawa waliokuwa wanafanya kazi Kiwanda cha Sukari Kilombero watalipwa fidia zao ambazo ni haki yao ya msingi? Pia kwenye Kiwanda cha Sukari cha Illovo kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu sana ya wakulima wa miwa kuhusu upimaji wa *sucrose*,

upimaji wa mzani na bei ya miwa yao wanayokipeleka kiwandani kutokuwa ya uwazi kabisa, maana vitu vyote muhimu vinafanywa na kiwanda yaani upimaji uzito, utamu na upangaji wa bei wote unafanywa na kiwanda na kuwabana sana wakulima wa nje (*out growers*). Je, ni lini Serikali itawaamuru wawekezaji hawa kuwapa wakulima mzani huru wa tani za miwa, utamu na ni lini wakulima hawa wataanza kulipwa kutokana na *buggers* na *sprit* ambapo sasa hivi wanalipwa utamu wa muwa peke yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda kidogo cha sukari cha Mufilisi – Mikumi; Serikali kwenye bajeti ya 2015/2016 ilikuja na bajeti na kusema wametenga pesa za kuanzisha Kiwanda cha Sukari cha Mufilisi. Je, zoezi hili limeishia wapi? Maana sasa kwenye bajeti hatuoni tena likizungumzwa na halipo kabisa. Je, Serikali inaweza kutuambia tumekwama wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya kusindika nyama, nyanya, ngozi, maziwa, viazi na matunda na mboga mboga, mbaazi; Mheshimiwa Waziri Wilaya ya Kilosa tumebarikiwa mifugo mingi sana na wingi huo wa mifugo unasababisha changamoto kubwa sana ya mapigano ya wakulima na wafugaji, kwa sababu wafugaji wamezidiwa sana na mifugo mingi na hawana pa kuwapeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali iangalie umuhimu wa kuanzisha viwanda vya kusindika nyama, ngozi, maziwa ili wafugaji hawa wapate uhakika wa soko la kuuza mifugo yao na kupunguza mifugo yao tofauti na sasa ambapo tunawaambia wafugaji wapunguze mifugo yao. Je, waipeleke wapi wakati hawana masoko ya uhakika ya kuuza mifugo yao, naomba Waziri uliangalie sana hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya kusindika nyanya, viazi, mbogamboga, mbaazi na matunda; wakulima wengi wa Wilayani Kilosa wanalima sana mazao haya na mengine mengi, kitendo cha kukosa soko la uhakika kinawapa umaskini mkubwa sana na kuwakatisha tamaa ya kuendelea kulima wakati wote, tunajua kilimo ndio uti

wa mgongo wa Taifa letu. Tunaomba sana Serikali itusaidie jimboni Mikumi tupate viwanda vya kusindika mazao haya ili tuweze kumkomboa mkulima wa Mikumi na Wilaya ya Kilosa kwa ujumla hasa kwenye kata zinazoongoza kwa kilimo kama Kata za Kisanga, Tindiga, Mabwerekwere, Vidunda, Malolo, Kilangali, Mhenda, Zombo, Ulaya, Masanze, Ruaha, Mikumi, Kidodi, Ruhembe na Uleling'ombe. Hili naomba majibu ya Waziri ni lini watatujengea viwanda vya kusindika mazao jimboni Mikumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *COSOTA*; bajeti inayopelekwa na kutengwa kwenye taasisi hii muhimu ni ndogo sana na inapelekea *COSOTA* kushindwa kutimiza wajibu wake sawasawa. *COSOTA* ni chombo muhimu sana kinapaswa kiangaliwe kwa jicho la kipekee sana maana ndicho chombo kinachoweza kuwasaidia wanamuziki wetu wa Tanzania kwenye wizi wa kazi zao ambacho kimsingi wizi wa kazi za wasanii ndicho kilio kikubwa sana cha wasanii wetu Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Sheria ya Hakimiliki na Hakishirika Namba 7 ya mwaka 1999 imepitwa sana na wakati na imekosa meno kabisa, niombe sana Serikali kama kweli ina nia thabiti na dhamira ya kweli ya kuwasaidia wasanii wa nchi hii basi ilete muswada wa sheria hii Bungeni ili tuweze kuirekebisha na kuipa nguvu ili tuweze kuwakomboa wasanii wetu wengi waliojijiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji, Jimbo la Mikumi lina ardhi nzuri na bora tena kubwa sana na tumebarikiwa sana kuwa na vyanzo mbalimbali na vingi vya maji kwenye mito mbalimbali na ardhi yetu maji yapo juu kabisa kwa maana ya *water table*. Tunaomba sana Serikali iweze kutupatia ardhi kubwa sana ambayo imetekelezwa na wawekezaji ambao wanahodhi mashamba hayo makubwa bila kuyaendeleza. Kurudishwa kwa mashamba hayo kutawezesha sana wawekezaji wengi kuweza kuja jimboni kwetu Mikumi na Wilayani kwetu Kilosa ili tuweze kutoa ajira zaidi kwa Wanamikumi na pia kuweza kuleta maendeleo kwa wanakilosa kwa ujumla.



Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho tunaomba sana Serikali itupie macho kwenye Jimbo la Mikumi ili waweze kutuletea wawekezaji maana Mikumi inajitoshleza katika kila sifa inayotakiwa na wawekezaji ili waje na kufanya uwekelezaji hasa kwenye masuala ya kilimo, utalii na viwanda. Ahsanteni sana na karibuni sana.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tafsiri na upotoshaji wa maana halisi ya viwanda vidogo. Tunaomba kupata tafsiri sahihi, maana ya viwanda na aina ya viwanda vinavyozungumziwa na Wizara husika ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo yana viwanda vingi na kuna maeneo ambayo hayana viwanda kabisa. Napenda kujua kigezo kinachotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wawekezaji kukata tamaa ni vyema likaangaliwa upya kuhusiana na mazingira ya wawekezaji ili kukuza uchumi wetu. Aidha, ni vyema kama Taifa kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji wetu wanaotaka kuwekeza nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema umeme uwe na uhakika ili kuendesha viwanda na kuwapa wawekezaji nchini kuwa na uhakika na uwekezaji wao kwa kuwa kila mtu anawekeza ili apate faida, inapotokea changamoto ya umeme na maji wawekezaji wanaweza kukata tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishwaji wa kiwanda cha dawa ni muhimu sana kwani kukiwa na viwanda vingi vinavyozalisha dawa za binadamu kutasaidia Taifa na wananchi wa kawaida kwani bei itakuwa nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu kuanzisha Kiwanda cha Mbolea. Mbolea inahitajika sana nchini lakini kumekuwa na changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kutolewa semina elekezi kwa wafanyabiashara na *TRA* juu ya kulipa kodi

badala ya hii hali ambayo inajitokeza sasa kwa kuonekana uadui mkubwa kati ya wafanyabiashara na TRA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya sasa kiuchumi katika nchi yetu ni tete mno hasa kwa wananchi wa chini kabisa. Ni vyema kukawa na mazingira rafiki kwa wafanyabiashara wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wafanyabiashara kuhama kutokana na changamoto wanazokutana nazo Serikali iweke utaratibu mpya utakaosaidia wafanyabiashara wetu.

**MHE. SUZANA C. MGONUKULIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1992 Tanzania ilikuwa na viwanda 156. Viwanda hivi Serikali iliposhindwa kuviendesha ilivibinafsisha, lakini haviendelezwi. Kwenye hotuba ya Waziri hakuna mahali popote alipozungumzia chochote kuhusu waliobinafsishiwa viwanda na kutokuviendeleza. Tunaomba anapohitimisha hoja aje na majibu yanayoelekeza hatua zilizochukuliwa juu ya tukio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imesemwa Tanzania ni nchi ya viwanda, je, ni viwanda vya kuchuja alizeti na kutengeneza pipi? Mbona sioni juhudi ya Serikali juu ya viwanda vya kutengeneza nguo ukizingatia tunahimiza zao la pamba lilimwe kwa wingi? Nafikiri ni wakati muafaka wa viwanda vyote vya nguo mfano Urafiki, *Mwatex*, *Mutex* na kadhalika vifufuliwe kwa kuwa tunahimiza Watanzania kulima pamba ili malighafi yetu itumike na hapa kwetu kwa wingi pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti yote inayopitishwa kwenye Bunge lako juu ya viwanda haionekani utekelezaji wake. Je, Tanzania ya viwanda itakuja kihawahewa? Tunaomba majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Waheshimiwa Wabunge tunapoishauri Serikali hoja zote zichukuliwe, zifanyiwe kazi ili kuleta tija ya maendeleo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Mbunge yeyote asiyetaka maendeleo katika Taifa lake, ndiyo maana wote huchangia hoja kwa hisia. Hivyo hoja zifanyiwe kazi.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukaguzi wa *TBS, NEMC, TFDA*; Serikali kupitia mamlaka mbalimbali imekuwa ikifanya ukaguzi wa maeneo ya viwanda, bidhaa za viwanda na kutoa vibali au kuteketeza mali za wajasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa la mamlaka hizi ni rushwa, urasimu na kutumia *standards* za Ulaya kwa kuwafanya Watanzania wengi kukwama kuanza biashara, kuchelewa kuanza biashara na kufilisika kutokana na matumizi mabaya ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kama tunataka viwanda viongezeke, nchi yetu lazima iondoe rushwa, urasimu na *Europe Standards* kwenye vigezo vya kufanya biashara au ubora wa bidhaa za Watanzania. Kwa sababu duniani kote kuna *export quality* na kuna *internal consumption quality*, lazima tuondoe masharti yanayokwamisha kuanza biashara na kujenga viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutumia *TIC* imekuwa ikihamasisha wawekezaji kutoka nje kuwekeza Tanzania. Wawekezaji wengi wanaokuja na mitaji yao na kununua ardhi na kumiliki kwa asilimia mia moja; nchi kabla ya kuingia kwenye mkakati huu wa viwanda haikuandaa sera itakayolinda wazawa na kuzuia utoro shaji wa faida zote kwenda nje. Mfano, viwanda vyote vikimilikiwa na wageni, maana yake faida yote ya uwekezaji mkubwa itakwenda kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni kwamba tulitakiwa kuwa na sera ya kulinda maslahi ya nchi ili kuepuka matatizo tunayopata sasa kwenye uwekezaji mkubwa wa madini kumilikiwa na wageni watupu na kuruhusu wizi mkubwa, udanganyifu mkubwa kupitia *transfer pricing* na *cheating* kwenye *contracts*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kutazama upya Sera ya Uwekezaji kwenye viwanda ili kuruhusu mgeni kuuza sehemu ya haki zake kwa wazawa, suala ambalo litasaidia kupunguza *profit export* kurudi kwao na kuiacha Tanzania maskini.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa maendeleo katika Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji hauendani kabisa na kaulimbiu ya Tanzania ya viwanda. Utekelezaji wa bajeti ya viwanda licha ya ukweli kwamba suala la viwanda lilikuwa halipigwi upatu na wala halikuwa kipaumbele cha Serikali ya Awamu ya Nne, mara tu baada ya Serikali ya Awamu ya Tano kuingia madarakani, utekelezaji wa bajeti ya maendeleo katika Wizara hii umeyumba sana licha ya kwamba ni Serikali inayojenga uchumi na viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano ilianza utekelezaji wa bajeti ya maendeleo katika Wizara ya Viwanda, Biashara na Utekelezaji kwa kutoa asilimia tano tu ya fedha zilizokuwa zimetengwa kutekeleza miradi ya maendeleo. Katika fedha hizo hakukuwa na hata senti moja ya fedha za ndani. Ni vizuri Serikali ikatoa fedha za kutosha ili kuchochea ukuaji wa sekta ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuporomoka vibaya kwa sekta ya viwanda vidogo na vya kati, ukweli ni kwamba viwanda vidogo ndiyo chimbuko la mapinduzi makubwa ya viwanda. Sekta hii imekuwa haipewi kipaumbele na Serikali jambo ambalo limesababisha sekta hii kuporomoka vibaya na kufifia kwa ndoto za kufikia uchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile sekta ya viwanda vidogo vidogo ni dhaifu na imeshindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa. Sekta hii ya viwanda vidogo vidogo haikui kwa kiwango cha kuridhisha. Kumekuwa na utekelezaji mdogo sana wa bajeti za maendeleo kwa viwanda vidogo vidogo katika ngazi zote za Serikali. Ni vizuri viwanda vidogo vidogo wapewe huduma za mafunzo ya kuridhisha. Vilevile

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

hakuna maendeleo ya teknolojia katika sekta ya viwanda vidogo vidogo na vya kati, kwani sekta hii ya viwanda inaporomoka kwa kasi kuliko ukuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya viwanda vidogo vidogo na vya kati ndiyo moyo wa maendeleo ya viwanda hata katika nchi zilizoendelea, lakini Tanzania sekta ya viwanda vidogo ni dhaifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu idadi ya viwanda na masoko nchini, Serikali ya Awamu ya Tano imekuwa ikijinasibu mara kwa mara kuwa inajenga uchumi wa viwanda na imekuwa ikitoa takwimu mbalimabli zikionesha idadi ya viwanda vinavyoanzishwa nchini kwa lengo la kutoa taswira nchi inaendelea vizuri kiviwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji hajawahi kuwasilisha kwenye Bunge lako tukufu mpango wa ujenzi wa viwanda na uzalishaji masoko ya bidhaa utakavyofanyika. Aidha, yapo maelekezo yaliyotolewa kwa Wakuu wa Mikoa kuhakikisha kuwa kila Mkoa unajenga viwanda 100 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haijielezwa ni viwanda vya namna gani vinaenda kujengwa na kwa tafiti zipi za masoko ya bidhaa zitakazozaliwa na viwanda husika; japokuwa Serikali imeeleza kwenye mpango wa miaka mitano kuwa itajikita kwenye uchumi wa viwanda na kutengeneza ajira? Vilevile ongezeko la kodi na kubadilika kwa ghafla kwa mifumo ya usimamizi wa biashara inayofanywa na Serikali yameathiri ukuaji wa biashara nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pato la Taifa kuonekana kukua, mazingira ya biashara nchini siyo rafiki kwa uwekezaji na maendeleo ya biashara. Kutokana na hali hiyo, kuonekana dhahiri kuwa shughuli za kiuchumi ni dhaifu, hivyo kutopelekea kuzalisha ajira na kupunguza umasikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kumekuwa na ongezeko kubwa la mikopo isiyolipika kwenye mabenki,

jambo ambalo linaathiri mazingira ya ufanyaji biashara kwa sababu udhaifu uliopo katika mfumo wa sasa wa kodi na maelekezo ya kiutawala yasiyoangalia maslahi ya wafanyabiashara, hii inapelekea wafanyabiashara kushindwa kulipa mikopo kwenye mabanki ya ndani, hivyo kuathiri mazingira ya biashara katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizingumzie kuhusu suala la kodi na urasimu yanavyoathiri biashara nchini. Serikali inawahimiza wafanyabiashara nchini kulipa kodi ya maendeleo (jambo ambalo ni jema) lakini haijaweka mazingira mazuri kwa ukuaji wa biashara hizo. Ukweli ni kuwa mazingira ya kuanzisha biashara nchini ni magumu. Mfano, kuanzisha biashara ya kawaida unaweza ukatakiwa kupitia kwenye mamlaka na wakala zaidi ya tano na sehemu zote hizo kuna gharama ambazo lazima uzilipe kama mfanyabiashara ili kupata vibali au leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapato (*TRA*) siyo rafiki kwa wafanyabiashara. Hii ni kutokana na maafisa kuambatana na vyombo vya ulinzi na usalama wakati wa ukusanyaji na ufuatiliaji wa kodi, jambo ambalo linatia hofu wafanyabiashara na kuamua kufunga biashara zao. Ni vizuri Serikali isijikite zaidi kwenye ukusanyaji wa kodi bila kuweka mazingira wezeshi kwa wafanyabiashara nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi ya rasilimali ya makaa ya mawe na chuma katika maendeleo ya viwanda; Shirika la Maendeleo la Taifa lilishakamilisha tathmini ya kufahamu wingi na ubora wa makaa ya mawe, pamoja na chuma cha Liganga na kubaini kuwa tuna makaa ya mawe ya kutosha, kwa kuwa tathmini ya mazingira ilishafanyika na Serikali kueleza kuwa ujenzi wa miradi hiyo ulitarajiwa kuanza mwaka 2016 na uzalishaji kuanza mnamo mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali itumie chuma cha Liganga katika kujenga reli ya *standard gauge* badala ya kutumia vyuma vya Uturuki, kwani tuna chuma cha kutosha kwa matumizi ya ndani na akiba ya kuuza nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendelea kuchelewa kulipa fidia ili kupisha miradi ya biashara na viwanda, kuna athari kubwa kiuchumi. Kwanza muda unavyozidi kwenda ndiyo thamani ya ardhi inazidi kupanda. Hivyo kuchelewa zaidi ni kuongeza kiwango cha fidia kitakacholipwa kwa wanaodai. Vilevile huu ni unyanyasaji mwingine wa Serikali dhidi ya raia wake, lakini pia ni kurudisha nyuma maendeleo katika sekta ya viwanda na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kazi rahisi kuanzisha viwanda kama ambavyo Serikali hii imekuwa ikisema na kutangaza kwenye vyombo vya habari. Pamoja na gharama kubwa za kuanzisha na kuviendesha hivyo viwanda, bidhaa zitakazozalishwa ili kuingia kwenye soko na kukubalika katika jamii ya watumiaji huwa mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Serikali ikaanzisha viwanda vya uunganishaji kama wenzetu wa Kenya walivyofanya au kama inavyofanyika kwa matrekta ya ASUS yanayounganishwa hapa Tanzania, lakini kiwanda mama kipo nchi za nje. Kwa njia hii tutakuwa tumeepuka gharama kubwa ya matumizi ya nishati ya umeme na gharama ya kutangaza bidhaa husika na hivyo bidhaa husika zitakuwa shindani katika soko la ndani na nje.

**MHE. ZAINAB M. AMIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji chini ya Waziri Mheshimiwa Charles J. P. Mwijage, pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya kwa kazi kubwa wanayofanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naishauri Serikali ifufue viwanda vilivyopewa wawekezaji mfano, Kiwanda cha Nguo cha *Karibu Textile Mills (KTM)* ili kiweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naishauri Serikali kupitia upya viwanda vilivyo katika Mkoa wa Morogoro, mfano *Morogoro Shoes Company, Polyester, Magunia, Tannaies, Ceramic, Canvas, Moprocco* ambapo katika miaka ya 1980 vilikuwa vinazalisha bidhaa mbalimbali, pia vilikuwa vinatoa

ajira kwa Watanzania na pia kuongeza pato la Taifa letu. Hivyo wawezeshaji ambao wameshindwa kuviendeleza viwanda hivyo wapokonywe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Serikali ijenge Kiwanda cha Matunda (*juice*) ili wakulima wa Mkoa wa Tanga waweze kuuza matunda katika kiwanda hicho. Hivyo ni muhimu Serikali ijenge kiwanda katika Mkoa wa Tanga kwa sababu Mkoa wa Tanga wananchi wake hulima kwa wingi matunda ya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, naishauri Serikali iishauri Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) iwakadirie wafanyabiashara mapato mara baada ya miezi mitatu (*grace period*) ndipo *TRA* wafanye makadirio ya mapato na siyo kuwakadiria kabla ya kuanza biashara. Hii hupelekea wafanyabiashara hao kushindwa kuendelea na biashara na kufunga na kulikoshesha Taifa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, naishauri Serikali ikutane na watendaji wa taasisi ya *Fair Competition Commission (FCC)* ili iwashauri *FCC* watoe elimu kwanza kwa wafanyabiashara kabla hawajaagiza bidhaa kutoka nje ya nchi. Siyo *FCC* kusubiri wafanyabiashara walete bidhaa kisha kuanza kuwatoza faini kubwa na mara nyingine kuziteketeza na kuwasababishia hasara kubwa wafanyabiashara hao na pia kulikoshesha Taifa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, naishauri Serikali ionane na kikosi cha Zimamoto cha Mkoa wa Dar es Salaam ili kuondoa bugudha iliyopo, maana wafanyabisahara wanalazimishwa kununua *fire extinguisher* kilogramu tano kwa shilingi 200,000 kisha kila mwaka kulipia shilingi 40,000.

Mheshimiwa Mwenyekitik, ushauri wangu ni kwamba Zimamoto wawaelekeze wamiliki wa majengo ya biashara Dar es Salaam (Kariakoo), waweke *fire extinguisher* katika *corridor* za nyumba hizo na siyo ndani ya maduka, sababu moto ukitokea usiku *fire extinguisher* limefungiwa ndani ya duka halitasaidia kuokoa mali za mfanyabiashara.



*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba, naishauri Serikali itenge maeneo maalum kwa wafanyabishara ndogo ndogo (Wamachinga) wa Mkoa wa Dar es Salaam na siyo kuweka biashara zao mbele ya maduka ya wafanyabishara. Hii itasaidia Wamachinga kuweza kulipa pato la biashara zao, huduma za jiji, huduma za usafi kwa urahisi na kuweza kulingizia pato Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nawatakia kazi njema na Mwenyezi Mungu awape afya njema na umri mrefu katika kuyaenda majukumu yenu ya kila siku.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa mchango wangu kwa Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni upi hasa mkakati wa Wizara kuhakikisha viwanda vyetu vya ndani vilivyojengwa, vinavyojengwa na vitakavyojengwa baadae vinalindwa ili viweze kukua na kuweza kuhimili ushindani wa viwanda vya wenzetu wa Ulaya, Asia na Amerika ambao viwanda vyao vimejiimarisha? Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri hakuna mahali popote alipotaja kulinda viwanda dhidi ya ushindani usio haki kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenye viwanda vya nguo, nyama, maziwa, nyanya na kadhalika wanalalamika juu ya ushindani usio haki unaotokana na waagizaji wa bidhaa toka nje kutolipa kodi stahiki kwa Serikali kwa sababu waagizaji hao wana-*under declare* ama kwa kushirikiana na watumishi wasio waaminifu wa *TRA* wanafanya *under-valuation* ya bidhaa walizoagiza na hivyo kulipa kodi isiyo stahiki. Nini nafasi ya Tume ya Ushindani katika hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kuwa sisi bado ni nchi changa sana, tusipokuwa na mkakati wa uhalisia wa kulinda viwanda vyetu, tusahau kabisa kuwa na uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naitaka Serikali ilete mpango mkakati wa kulinda viwanda vyetu ili ndoto ya Tanzania ya viwanda iweze kukamilika na kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Waziri, lakini lazima uzingatie kulinda viwanda vyetu.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango wa maneno, naomba pia kuchangia kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2017 nilichangia na kuitaka Serikali ianze kutoa leseni kama sheria inavyotaka ili wananchi waweze kupata fursa ya kuweza kujiongezea kipato, kwa kuuza pombe ya Nipa ambayo ni *by product* ya mazao ya korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Nipa tumeweza kupata *ethanol*, *methanol* na *alcohol* ambayo inaweza kutumika viwandani. Haya yanafanyika sana nchi jirani ya Mozambique. Hivyo, Watanzania wanavusha hiyo Nipa na kupeleka nchi jirani ambayo wanatumia kujiingizia pesa za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la Viwanda vya Korosho Masasi na maeneo mengine. Taarifa ya mwisho inasema kuna kesi Mahakamani, lakini katika hali ya kushangaza, viwanda hivyo sasa hivi vinatumika kama maghala na watu hao wanajipatia kipato wakati Serikali inasubiri kesi Mahakamani. Sasa ni wakati muafaka kesi hizi ziishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho kabisa ni kuhusu stakabadhi ghalani na *commodity exchange*. Kila mara taratibu hizi huwa zinaanza mikoa ya Kusini. Ni kwa nini? Kwa mfumo wetu wa sasa, *commodity exchange* kwa Tanzania kwenye mazao ya kilimo ni bado kabisa. Hivi karibuni watu wa *TMX* wamewaandikia barua wamiliki wa maghala ili waje kukutana nao. Kimsingi watu hawa wanataka kulazimisha wakati maandalizi hayajafanyika. Kwa hiyo,

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

tunaomba suala la *commodity exchange* likafanyike kwenye mazao mengine. Sasa naelewa kwa nini Mzee Nandonde (Mbunge wa zamani wa Tandahimba) aliomba Mtwara ijitenge. Kwa nini hakuna mikakati ya uhakika na kuwekeza viwanda?

**MWENYEKITI:** Namwita sasa Mheshimiwa Waziri wa Nishati atafuatiwa na Waziri wa Fedha na Mipango kila mmoja dakika kumi. Mheshimiwa Waziri wa Nishati.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nashukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi nitoe mchango katika Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara hii kwa hotuba yao mahiri na ni nzuri yenye kueleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nawapongeza sana Serikali kwa kuweka mikakati mizuri ya kutupeleka kwenye kujenga uchumi wa viwanda. Katika Wizara yetu yako mambo mawili ya msingi ambayo nadhani katika Wizara hii ni muhimu sana tukayafafanua vizuri kama mikakati ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti pamoja na Waheshimiwa Wabunge, lipo suala la kuzalisha umeme wa kutosha, wa uhakika na unaotabirika. Njia pekee ni kuwa na umeme mchanganyiko. Kuwa na umeme mchanganyiko maana yake utumie rasilimali zote ulizonazo, ukusanye nguvu zote upate umeme mwingi, wa uhakika na wenye gharama nafuu ili kujenga uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya Serikali hadi sasa ni kuzalisha umeme upatao megawati 5,000 ifikapo mwaka 2020 na megawati 10,000 mwaka 2025. Sasa huwezi kuupata umeme huu kwa chanzo kimoja. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kusema kwamba tunayo rasilimali nzuri sana ya gesi asilia kuzalisha umeme.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa katika umeme tulionao, kama malengo yetu ni kupata megawati 5,000 mwaka 2020, hivi sasa tuna jumla ya megawati 1,513. Kwa hiyo, bado safari ni ndefu. Kwa hiyo, lazima tuzalishe umeme wa kutosha ili kujenga uchumi wa viwanda vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika umeme huo hadi sasa, tuna takribani megawati 783 zinazotokana na rasilimali ya gesi asilia, lakini umeme wa maji ni megawati 567.7. Kwa hiyo, bado tupo mbali. Umeme wa mwisho wa kuzalishwa katika miradi ya maji ni huu mradi wa Kihansi wa mwaka 2000. Mradi kabla ya hapo ulikuwa ni umeme wa Kidatu wa mwaka 1975 na 1980. Kwa hiyo, ni miaka mingi tangu tumezalisha umeme wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika rasilimali ya gesi mwaka 2008 tulizalisha megawati 102 *Ubungo I* na mwaka 2012 tulizalisha megawati 129, mwaka 2016 megawati 150 *Kinyerezi I* na mwezi Aprili tumezalisha megawati 168 za gesi asilia. Kwa hiyo, ni lazima tuendelee kuzalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, katika gesi asilia bado kuna miradi mikubwa mitano ijayo. Mradi wa kwanza ni wa Somanga – Fungu wa megawati 330 tunaoanza kuzalisha na kuujenga mwaka huu wa fedha na mradi mwingine wa Mtwara megawati 300 za gesi asilia. Mradi mwingine utakaoanza mwakani ni mradi wa *Kinyerezi III*, megawati 300 na *Kinyerezi II* megawati 300 na hatimaye *Kinyerezi IV* megawati 330. Hayo malengo lazima tuyatimize. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fursa nyingine ya kutumia rasilimali ya gesi ni pamoja na matumizi ya viwandani. Tuna takribani trilioni 4.6 zitakazotumika kwa ajili ya kutengeneza viwanda vya mbolea na *petrochemicals*. Kwa hiyo, hayo ni matumizi ya gesi asilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kutumia rasilimali hiyo katika kusambaza mbolea lakini pia kwenye

## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

ujenzi wa viwanda vinavyoendelea ambavyo matumizi yake ni trilioni 3.6. Hayo ni matumizi ya gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuna mpango wa kusambaza gesi majumbani na katika magari ambayo itatumika trilioni 1.2 kama gesi asilia ya kutumia kwenye matumizi yetu nyumbani na bado trilioni 1.2 itatumika kwa ajili ya viwanda vya vyuma. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kusema kwamba matumizi ya gesi asilia bado ni mengi kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mpango wa kujenga kiwanda kikubwa cha kusindika gesi kwenda kwenye kimiminika na matumizi hayo kila mwaka kiwanda hicho kitatumia tani milioni 10 kwa ajili ya kujenga kiwanda hicho cha gesi asilia. Kwa hiyo, manufaa ya gesi asilia bado ni mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia nafasi hii wananchi wa Mtwara, Lindi na maeneo mengine bado tutanufaika na hii rasilimali ya matumizi ya gesi asilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *potential* tuliyonayo, tunavyo vyanzo vingi. Hivi sasa *potential* tuliyonayo kwa upande wa kuzalisha umeme wa maji, tukizitumia vizuri, tunayo *potential* ya kuzalisha megawati 4,700 ya maji ambayo hatujaitumia. Hivi sasa tumetumia asilimia 12 tu. Wakati kwenye gesi, niweke sahihisho kidogo, jana nilisikia imesemwa kwamba ni 5%, siyo kweli, tumeshafika asilimia 10 ya matumizi ya gesi asilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya gesi ambayo nimeisema, ukiangalia kwenye matumizi ya maji, kati ya megawati 4,700 tumetumia megawati 567 tu. Kwa hiyo, ni lazima tuendeleo kuzalisha umeme wa maji ili rasilimali ya maji tuliyonayo ambayo ni kubwa ilete manufaa makubwa kwa ujenzi wa uchumi wa viwanda vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kusema mradi wa maporomoko ya maji ya Mto Rufiji na wala siyo

*Stiegler's Gorge*; maporomoko ya Mto Rufiji ni muhimu sana tukiujenga sasa kuliko kuuacha. Maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama malengo yetu ni kufikia megawati 5,000 mwaka 2020 na 10,000 mwaka 2025, umeme unaokwenda kutukombo kwa mkupuo, kwa mchapuo, mara moja, ni megawati 2,100 wa maji ya maporomoko ya Mto Rufiji. Kwa hiyo, naomba sana Waheshimiwa Wabunge kwamba tuunge mkono juhudi za Serikali ili kusudi tuweze kupata umeme huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo vyanzo vingine ambavyo nazungumza mbali na kusema Mradi wa Mto Rufiji, ipo miradi ya *geothermal* na makaa ya mawe. Hivi sasa tuna *potential* ya makaa ya mawe tani bilioni tano hatujawahi kuzitumia. Tunayotumia sasa ambayo ni *proven* ni asilimia 25. Kwa hiyo, ni vema sana Waheshimiwa Wabunge tuendeleo kuhamasisha *energy mix* katika kujenga uchumi wa viwanda yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuna *potential* ya *geothermal* ambayo inafikia pia megawati 5,000, hatujaanza kuitumia. Ni vizuri sana Waheshimiwa Wabunge tukiunga mkono juhudi za Serikali kutumia umeme mchanganyiko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitumie nafasi hii kusema Mradi wa Maporomoko ya Mto Rufiji ni muhimu sana kwa kuzalisha umeme lakini pia kwa utalii pamoja na shughuli za umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo napenda kulizungumza ni kupata umeme wa uhakika na unaosafirishwa. Ni kweli kabisa tunazungumza hapa suala la umeme kukatika. Kwa sasa umeme tulionao, hali halisi ya umeme inaendelea kuimarika kwa kiasi kikubwa, changamoto tuliyonayo kidogo ni katika miundombinu. Lakini kama Serikali tumejipanga na tuna miradi mahususi ya kufanya ukarabati wa miundombinu ili kuhakikisha umeme tulionao haukatiki. Hiyo inaenda sambamba na kuwa na

umeme wa kutosha ikiwemo na miradi mikubwa niliyoitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nziungumze kidogo kuhusu juhudi za Serikali ya kusambaza umeme vijijini kama juhudi za kuunga mkono ujenzi wa viwanda. Ni dhamira ya Serikali kwamba ni lazima sasa viwanda tunavyovizungumza vianze kujengwa kuanzia vijijini na wala siyo mijini tu. Ndiyo maana kama Serikali tunapeleka umeme katika vijiji vyote mwaka 2020/2021. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa katika nchi yetu, kati ya vijiji 12,268 ni takribani vijiji 4,878 vimeshapelekewa umeme na vijiji vingine 500 vipo katika kuunganishwa umeme. Ni matumaini yetu kwamba mara baada ya miradi hii ya umeme vijijini kukamilika viwanda sasa vitarejea kuanzia vijiji. Ni matumaini yetu mihogo inazalishwa vijijini, hivyo tukiwapelekea umeme vijijini wananchi wote, viwanda vya kusaga na kukoboa unga vitaanzia vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono juhudi za Mheshimiwa Waziri wa Viwanda kuhamasisha viwanda, uchumi wa kati ili kujenga uchumi wa Taifa letu. Kwa hiyo, nishati ndiyo mhimili pekee tunapokwenda kwenye uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati kwa mchango wako. Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa dakika kumi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Na mimi nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Naibu wake, Mheshimiwa *Engineer* Manyanya; timu nzima ya uongozi wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisisitize kwamba viwanda ndiyo njia pekee ambayo ilifanya nchi zote ambazo tunaziita zimeendelea kuendelea. Kwa hiyo, hii ni njia sahihi, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na timu nzima kazaneni, mkaze buti, hii ndiyo njia sahihi ya kwenda kadri ya uongozi wa Serikali yetu inavyotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia niseme mapema kabisa kwamba naunga mkono hoja na nitachangia kwa kutoa ufafanuzi wa mambo machache na mengine tutaendelea kuyafafanua kadri mjadala wa bajeti unavyoendelea mpaka huko mwishoni mwa mwezi Juni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ambalo napenda kulitolea maelezo, pamekuwepo hoja hapa kwamba watu wanateseka sana kwa fedha zao ambazo zimekwama kwenye iliyokuwa benki ya *FBME* ambayo tuliweka chini ya ufilisi. Naomba tu niseme kwamba Serikali inawajali watu wake na imekuwa inalishughulikia jambo hili inavyopaswa na kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfilisi ambaye ni *Deposit Insurance Board (DIB)* imeendelea kulipa amana za wateja na tulianza hiyo kazi toka tarehe 1 Novemba, 2017. Mpaka kufikia tarehe 8 Mei zimeshalipwa shilingi bilioni 2.31 kwa kiwango kile cha juu ya shilingi milioni moja na nusu ambayo imefikia sasa takriban asilimia 53 kati ya shilingi bilioni 4.3 ambazo zilitarajiwa kuwa zimelipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliolipwa ni wenye amana takribani 3,203 ambayo ni asilimia 48.1 ya wateja wa iliyokuwa hiyo benki. Malipo yalibaki tutaendelea kuyalipa, hususani yale ambayo yanahusu amana yatafanyika baada ya kuwa tumefanya uhakiki wa mikopo mbalimbali ya wadaiwa na madeni ya hiyo benki. Kwa hiyo, hilo naomba niliachie hapa kwa sasa, nikisisitiza tu kwamba Serikali inawajali wananchi wake na itahakikisha kwamba haki yao inapatikana baada ya taratibu kukamilika.



*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala la *export levy* ya ngozi. Sasa hili, ngozi ghafi ni muhimu sana. Ule uamuzi wa kuweka *export levy* ulikuwa ni wa makusudi. Ni lazima tulinde ajira, tuuze nje kile ambacho kimeongezewa thamani ndiyo wananchi wetu wataweza kufaidika. Tusipofanya hivyo, maana yake tunawapatia ajira huko ngozi zitakapokwenda. Kwa nini tufanye hivyo wakati tunalia na ajira ya vijana wetu?

Pia kulikuwa na hoja juu ya rai kwamba wafanyabiashara wetu wanapo-*declare* zile fedha kwenye mipaka, hali inakuwa ngumu kweli! *It is very risk* na wengine hata wanauawa.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kidogo.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kidogo.

**T A A R I F A**

**MWENYEKITI:** Taarifa. Hebu subiri Mheshimiwa Waziri, taarifa.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza niendeleo kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango. Namwomba tu ndugu yangu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa toa taarifa.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Taarifa, kuna watu wanaweka shilingi milioni 600 au shilingi milioni 300 wanapewa shilingi milioni moja na nusu. Si sawa sawa na kuchukua sukari kuitia kwenye maji ya chumvi utegemee kupata maji matamu? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, endelea.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri wala sitahangaika na hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali ilivyoshauriwa, tutaendelea kuliangalia hili jambo la namna ambavyo watu wetu wana-*declare* fedha walizonazo pale mpakani. Napenda kutumia nafasi hii kuvitaka vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kuimarisha usalama katika maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitumie fursa hii kuikumbusha Mamlaka ya Mapato/watumishi wetu wa Mamlaka ya Mapato ni marufuku kutoa siri za wananchi/wateja wetu wanapo-*declare* fedha zile. Nitumie nafasi hii kumwagiza Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato kuandaa...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** ...kuandaa viapo vya watumishi wetu waliopo pale mipakani kuhakikisha kwamba atakayekiuka vile viapo, basi anapata habari yake. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nadhani ni muhimu niseme kwamba hatua hii ni muhimu kwa ajili ya kuzuia utakatishaji fedha, lakini hata ufadhili wa ugaidi. Kwa hiyo, hili jambo ni *international practice* na lazima na sisi tuendeleo kufanya ili Taifa letu liendeleo kuwa salama. Pia wananchi wenyewe husika ni muhimu wakachukua tahadhari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya Mamlaka ya Mapato kupuuza *invoices* za wateja na kuzikadiria upya. Kiini cha shida hii kwa kweli ni udanganyifu. Watu wanatoa *value* ya hizi *invoices* zisizo sahihi na ni kwa makusudi kwa sababu kama ingekuwa ni *human error*

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

unategemea kwamba basi *invoice* zilizozidishwa au zile zilizopunguzwa ziwiane, lakini daima sivyo, *under invoicing* ndiyo kubwa. Kwa hiyo, ni muhimu sana kwamba wananchi nao wanaohusika, wote tunawataka watoe *invoices* ambazo ni sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja watumishi wetu wa *TRA* kudai rushwa. Hili napenda nitumie nafasi hii kulikemea kwa nguvu zote. Hili ni kosa kubwa na Serikali ya Awamu ya Tano imejitabanaisha kwa kupambana na rushwa. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi ambao wanatusikiliza, watupatie taarifa pale ambapo pana mtumishi yeyote wa *TRA* ambaye anadai rushwa, nasi tutamtumbua, wala hatutanii. Tupatieni taarifa tutawafanyia kazi ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala pia kuhusu *research and development*. Ni kweli tunapokwenda kujenga uchumi wa viwanda, *research and development* ni jambo la msingi sana. Rai yangu ni kwamba Watanzania tushikamane, tuendeleo kukusanya mapato zaidi na zaidi kadri inavyowezekana na kupanua wigo... (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea, ngoja nitoe matangazo ya wageni waliopo Bungeni jioni hii. Kundi la kwanza tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Wageni wa Mheshimiwa Antony Mavunde, Mbunge na Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira ambao ni wanafunzi 80 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Mko wapi? Karibuni sana. (*Makofi*)

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Daimu Mpakate ambao ni Waandishi wa Habari kutoka Songea, Mkoani Ruvuma. Waandishi wa Habari hao hapo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Kundi la pili ni wageni waliokuja Bungeni kwa ajili ya mafunzo. Tunao wanafunzi 21 kutoka Chuo cha Utumishi wa Umma, Magogoni Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Ally Mtoro, Makamu wa Rais wa Chuo hicho. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaendelea. Sasa namwita Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya kwa dakika 20. Karibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia afya na baraka tele zinazotuwezesha kutekeleza majukumu tuliyokasimiwa kwa maendeleo ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake kwangu na kwa kunituua kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Nathamini sana dhamana aliyonipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru pia Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwongozo wao thabiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Charles Mwijage, Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwongozo na ushirikiano wake mkubwa unaoniwezesha kutekeleza vizuri majukumu niliyopewa. *(Makofi)*

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu pia kuishukuru sana familia yangu kwa sala na ushirikiano wao...

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** ambao ni Baraka na nguvu ya kipekee kwamba...

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MWENYEKITI:** Kuhusu Utaratibu. Mheshimiwa Naibu Waziri, hebu subiri kidogo. Kuhusu Utaratibu, Mheshimiwa Bilago. Kaa kidogo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anavunja...

**MWENYEKITI:** Nieleze kifungu bwana!

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 99(14); "Bila kuathiri masharti ya Kanuni ya 154, yoyote ya utangulizi, utambulisho, salamu za pole, pongezi na shukrani pamoja na kutaja majina ya Wabunge waliochangia hoja havitaruhusiwa kwa Mbunge au Waziri wakati wa kujadili hotuba ya bajeti." (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba ajielekeze kwenye hoja iliyopo. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bilago, na mimi nasikiliza hayo yote, nakushukuru. Yeye alikuwa anapongeza familia yake kuruhusu muda wote anapokuwa hapa.

Mheshimiwa Waziri, endelea. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa hekima zako na ndiyo maana tulikuchagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru tena, narudia, Mheshimiwa Charles Mwijage, Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, kwa mwongozo na ushirikiano wake mkubwa unaoniwezesha kutekeleza vizuri majukumu niliyopewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu kuishukuru sana familia yangu kwa sala na ushirikiano wao ambao ni baraka na nguvu ya kipekee kwangu katika kutekeleza majukumu haya mapya. *(Makofi)*

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua pia fursa hii adhimu kuwashukuru sana wapiga kura wangu wote...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** ...na wananchi wa Jimbo la Nyasa...

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** ...kwa kuendelea kuniamini na kunipa ushirikiano kama Mbunge wao. Hapa kazi tu. *(Makofi)*

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

**MWENYEKITI:** Kuhusu Utaratibu. Kaa kidogo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MBUNGE FULANI:** Mama, jibu hoja zetu.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MWENYEKITI:** Sasa Mheshimiwa Bilago, usimchezee chatu. Twende tu kwenye Kanuni, niambie sasa ni Kanuni ipi imekiukwa.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni nimemaliza kuisoma sasa hivi ambayo...

**MWENYEKITI:** Kama ni hiyo, nimeshafanya *ruling*, *please* naomba ukae chini.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ameendelea...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ameendelea kuvunja Kanuni kwa makusudi kabisa.

**MWENYEKITI:** Nakuomba ukae chini. Mheshimiwa Naibu Waziri, endelea. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumelelewa kwa nidhamu kwa upande wa kambi hii...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** ...ndiyo maana Mwenyekiti akisema neno tunaheshimu. Kwa sababu maelekezo ya Kiti ndiyo ya

mwisho. Naomba uheshimu Kiti. Wewe usiteseke, uendelea kuomba. *(Kicheko)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, endelea tu kwenye hoja. Jibu tu hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Tulia, endelea.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unapojenga hoja, kuna namna ya kuvuta pumzi. Mimi ni Yohana, ndiyo naanza utangulizi hapa, kwa hiyo, usiniletee vurugu. Ninachosema ni kwamba Tanzania sasa tunajenga viwanda, endelea kusikiliza hoja. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** ...na kamanda wetu mkuu mnamfahamu, ni Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, namshukuru na tunashukuru kwa mwongozo anaoutoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, hoja zetu zitajibiwa zaidi kwa kadri tunavyoenda, lakini nikianza na hoja ya tafsiri ya viwanda na suala hilo lilitolewa na Mheshimiwa Aida Joseph. Napenda niseme kwamba kiwanda ni eneo ambapo shughuli ya kiuchumi hufanyika ikihusisha uchakataji wa malighafi (*value addition*) kwa lengo la kuzalisha bidhaa ambazo hutumika moja kwa moja kwa mlaji au viwanda vingine. Hotuba ya bajeti ya mwaka 2018/2019 ukurasa wa tano, aya ya 15 mpaka 16 imeeleza hayo na imeainisha viwanda hivyo kwa kadiri ya ngazi zake na imefafanua kwa uwazi kabisa. *(Makofi)*



## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nikiunganisha na suala ambalo lilijitokeza kwa upande wa hoja ya Mheshimiwa Cecil Mwambe, viwanda hivyo vinavyozungumzwa ni viwanda gani na ni vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Mheshimiwa Waziri alipokuwa akitoa hotuba yake, alionesha kitabu ambacho tuliamua kwa makusudi kuorodhesha viwanda vyote. Hiyo ipo katika *soft copy* ambayo imekabidhiwa kwa ajili ya gharama, lakini pia muda, tumesema kitabu ni hiki. Kama kweli Mheshimiwa Cecil unatoka kwenu Ndanda na unawajua watu wako wote, njoo chukua kitabu hiki upitie, watu wa Ndanda utawaona wako humu, wale wote wenye viwanda vidogo sana, vidogo, vya kati na vikubwa kwa kadri ya utaratibu uliopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba viwanda ni sawa na binadamu, vinazaliwa, vinakua na vinakufa. Kwa hiyo, usishangae kuona kwa *data* hizi ambazo zilitengenezwa na kuhakikiwa na *NBS* toka mwaka 2014 na pia kuongezeka kwa idadi hii ambayo tunasema kufikia sasa, vingine vinaweza visiwe kwenye kazi kwa sababu hatufanyi uhakiki kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba nikimaliza, njoo uchukue, kama unawafahamu watu wako utawaona humu, mimi wa kwangu nimewaona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kuhusu kuwezesha taasisi za tafiti na teknolojia kuchochea maendeleo ya viwanda. Niseme tu kwamba ni kweli kuna umuhimu mkubwa sana wa kuziwezesha taasisi hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa taasisi hizi, hasa katika kufanya tafiti zinazolenga uongezaji thamani, ubora na kupunguza upotevu wa mazao na malighafi mbalimbali kwa kutumia teknolojia sahihi. Vilevile kupitia tafiti hizi, taasisi hizi zinaainisha maeneo ya uanzishwaji wa viwanda (*industrial mapping*) ili kuweza kutoa ushauri kwa Serikali na sekta binafsi, kuanzisha viwanda

shindani na endelevu. Tafiti hizi zitawezesha kuwa na matumizi bora na yenye tija ya rasilimali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitenga fedha kuziwezesha taasisi hizi. Kwa mfano tu, kumekuwepo na ongezeko la fedha za maendeleo zilizotolewa kutoka shilingi milioni 678.95 mwaka 2016/2017 hadi shilingi bilioni 7.511 mwaka 2017/2018 likiwa ni ongezeko la asilimia 1,006 ya fedha zilizotolewa na Serikali kwa taasisi hizi. Jitihada za Serikali za kuwezesha zaidi kifedha zitaendelea kutokana na umuhimu wa taasisi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna suala lilikuwa limezungumzwa kuhusiana na Kiwanda cha Viuadudu. Kiwanda cha Viuadudu cha Kibaha kilianza uzalishaji wa kibiashara kuanzia tarehe 3 Februari, 2017. Kiwanda hiki kina uwezo wa kuzalisha lita milioni sita za viuadudu kwa mwaka. Hadi sasa kiwanda kimezalisha jumla ya lita 449,503 ambazo zimeuzwa ndani na nje ya nchi kama vile Niger na Angola. Ni kweli kabisa jumla ya Halmashauri 84 zilikuwa zimechukua dawa, yaani viuadudu katika kiwanda hiki na Halmashauri tisa ziliweza kulipa nyingine tunaendelea kuzihamasisha. Kiwanda hiki ni muhimu sana katika vita yakutokomeza ugonjwa wa malaria nchini na hasa katika hili eneo la malaria, tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ambaye alitoa fedha kwa ajili ya kupeleka kwenye Halmashauri ambazo zilikuwa zina maambukizi makubwa ya Malaria na fedha hizo zililipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala kuhusiana na utekelezaji wa Mkataba wa C2C. Katika hotuba ya mwaka 2017/2018 tulieleza kwa kirefu mikakati tuliyoundaa kwa ajili ya uendelezaji viwanda ikiwepo ya sekta ya pamba hadi mavazi. Hotuba hii imejielekeza katika utekelezaji wa kipindi cha mwaka mmoja, mfano katika aya ya 50 inaeleza uanzishaji Kiwanda cha Vifaatiba vinavyotumia Pamba Simiyu, aya ya 52 inaeleza juu ya ufufuaji wa *Morogoro Canvas Mill* na vinu kumi vya kuchambua pamba. Aidha, aya ya 51, tumeleza jinsi tunavyoshughulikia changamoto zinazokabili sekta ya pamba hadi mavazi, jambo ambalo

limebainishwa kwenye Mkakati ya C2C. Mambo hayo yaliyotekelezwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mkakati wa C2C.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulijitokeza suala la ulipaji wa fidia kuhusiana na maeneo tunayotegemea ya uwekezaji, EPZA. Na mimi nikiwa natoka Mkoa wa Ruvuma, niseme tu kwamba ukienda katika kitabu cha randama kama unacho kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbo, utakuta pale tayari kuna fedha zilizotengwa kwa ajili ya kulipa fidia. Kwa upande wa Ruvuma, Songea, nafahamu Mheshimiwa Waziri Mkuu tarehe 23 Desemba alikuwa pale na wananchi walilalamika sana juu ya suala hilo. Jumla ya shilingi 2,624,990,000 zimetengwa kwa ajili ya shughuli hiyo. Pia kuna maeneo ya mikoa mingine ambayo wanaweza wakapata taarifa hizo kupitia ukurasa huu wa 210.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu Serikali kuiwezesha *Tanrade*, kuhakikisha kwamba bidhaa za Tanzania zinaingia katika masoko ya Kimataifa na kwamba Serikali iwezeshe *TanTrade* kuwekeza katika miundombinu ya masoko, maghala na viwanja vya maonesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2017/2018, Serikali ilitenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya uendelezaji wa miundombinu ya Uwanja wa Maonesho ya Mwalimu Nyerere na kwa mwaka 2018/2019 *TanTrade* imetenga shilingi 2,376,400,000 katika bajeti ya maendeleo ikiwa ni ongezeko la shilingi 1,876,400,000. Ongezeko hili linatarajia kuongeza ufanisi katika utafutaji wa maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya kujenga ofisi za kanda, viwanja vya maonesho, miundombinu ya masoko katika kanda mbalimbali nchini, kuongeza huduma karibu na wananchi na kuongeza tija katika biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulijitokeza pia suala la Sheria ya FCC na hali halisi ya mazingira ya biashara. Sheria ya FCC inaonekana inakinzana na mazingira halisi ya kufanya biashara. Tulishauriwa kuhusu Serikali kuwa na teknolojia bora ya kutofautisha kati ya bidhaa bandia na bidhaa halisi na Sheria ya FCC ifanyiwe marekebisho.

## NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia FCC imekuwa ikifanya utambuzi wa baadhi ya bidhaa bandia kwa kutumia teknolojia miongoni mwa bidhaa ambazo utambuzi wake unatumia teknolojia. Ni bidhaa za kielektroniki na wino wa kurudia (*cartridge*). Serikali inaendelea kushirikiana na wazalishaji wa bidhaa mbalimbali ili kupata teknolojia za utambuzi katika bidhaa wanazozalisha. Utambuzi wa bidhaa bandia hufanyika kwa kuzingatia Sheria ya Alama za Bidhaa ya mwaka 1963 kama ambavyo ilirekebisha mwaka 2007 na 2012 na Kanuni zake za mwaka 2008.

Vilevile kwa kutumia TEHAMA pamoja na kushirikiana na taasisi za utafiti wa elimu ya juu kuimarisha usimamizi vitumike kuhawilisha (*commercialization*) matokeo ya tafiti kutoka vituo hivyo ili matokeo ya tafiti hizo yaweze kutumika kutengeneza mifumo, huduma na bidhaa hiyo kusaidia kukuza uchumi. Hiyo ipo katika hotuba ya mwaka 2018/2019 ukurasa wa 161 aya ya 327.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuuza ufuta kwa kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani, maandalizi yameshafanyika ambapo kikao cha wataalam kimefanyika Mkoani Dar es Salaam tarehe 30 Aprili, 2018. Maandalizi ya kikao cha wadau yamekamilika ambapo kinatarajiwa kufanyika Mkoani Dodoma pia tarehe 15 hadi 16 Mei, ili kupata maoni ya mwisho kabla ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la kulinda viwanda vya ndani, eneo hilo limechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi na naomba radhi, sitaweza kuwataja wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Serikali inafanya juhudi kubwa katika kulinda viwanda vya ndani. Juhudi hizo ni pamoja na kuhakikisha kunakuwepo mazingira bora ya uzalishaji viwandani ikiwa ni pamoja na kupunguza gharama za uzalishaji, yaani andiko la *blueprint* limebainisha masuala yote ya kushughulikia, kuimarisha udhibiti wa bidhaa kutoka nje ya nchi na kuhakikisha kodi stahiki inalipwa na hivyo kutoa suluhisho la *under-invoicing, under-declaration, tax evasion*

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

na pia masuala ya njia ya panya, kuongeza kodi kwa bidhaa kutoka nje ambazo viwanda vyetu vina uwezo wa kuzalisha hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na haya ambayo nimeyaeleza, niseme tu kwamba kuna mambo mengine ambayo yalijitokeza. Mfano, suala la lumbesa. Katika suala hili kumekuwa na manung'uniko mengi kutoka kwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kukamatwa magunia yakiwa yamebeba viazi na bidhaa za aina hiyo. Tunachosema ni kwamba gunia linaweza likawa limewekwa lumbesa, liwe gunia dogo au kubwa, lakini tunachosisitiza ni umuhimu wa kuwa na mizani itakayopima kwa kilo. Ukishapima kwa kilo, ina maana kilo 50 itajulikana ni kilo 50. Kama utakuwa hauna mzani, kwa vyovyote vile itakuwa ni vigumu mtu kutambua kwamba hizi ni kilo 50 na hivyo kupelekea kuwaibia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitoe rai kwa Watanzania wote kuhakikisha kwamba wanapofanya shughuli zao zote za kibiashara za kuuza bidhaa zao, wahakikishe bidhaa zile ambazo zinahusika katika upimaji wa kilo, basi watumie kilo na siyo kutumia magunia pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa upande wa Wizara tunaangalia namna ya kufanya marekebisho ya sheria, hasa kuhusiana na suala la ujazo wa magunia yenyewe. Kama unavyofahamu, ni kwamba gunia la kilo 100 hata kulibeba bado linaweza lisilete afya kwa mbebaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo, kwa kuzingatia kwamba tunaenda na viwango, tunasema kwamba tuwe na ujazo tofauti tofauti utakaowezesha hata wale ambao wanahusika katika shughuli za ubebaji mizigo, wafanye hivyo katika vipimo ambavyo ni sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kulijitokeza pia suala la Mheshimiwa Mariam Kisangi kuomba juu ya watoto au akina mama kuweza kufanyia shughuli zao za kibiashara katika uwanja wa pale Sabasaba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi suala hilo baada ya kujadiliana, Mheshimiwa Waziri wangu kwa ridhaa yake, lakini pia taasisi ya *TanTrade*, tumeona ni jambo jema sana kwa sababu litawezesha akina mama hao katika hizo siku watakazoweza kwenda kufanya shughuli zao pale kwanza kupata mapumziko, lakini pia kuwa jirani na familia zao na kufanya biashara ndogo ndogo zitakazowawezesha wao kupata kipato zaidi. Kwa hiyo, utaratibu rasmi utawekwa ili kuwezesha namna bora zaidi ya kushughulikia jambo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu ujenzi wa uchumi wa viwanda kwamba liendane na kutengeneza ujuzi. Ni kweli kabisa kwamba hilo ni suala muhimu sana. Serikali imekuwa ikifanya jitihada hizo katika kuhakikisha kwamba kupitia Wizara nyingine, kama ambavyo inaeleweka kwamba ujenzi wa uchumi wa viwanda siyo wa Wizara moja, ni wa Wizara mbalimbali; kupitia Wizara mbalimbali ikiwemo Wizara ya Elimu lakini pia TAMISEMI, kuhakikisha kwamba mafunzo ya aina mbalimbali yanatolewa, lakini hata Vyuvo vyetu Vikuu vimekuwa pia vikitoa mafunzo ya ujasiriamali.

Vilevile kwa upande wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji tunacho Chuo cha Biashara (*CBE*) ambacho kinatoa mafunzo ya ujasiriamali, lakini pia mafunzo ya vipimo, hayo yote yanawezesha wananchi kufanya shughuli zao kiukamilifu lakini pia kufanya shughuli zao kwa tija. Kwa hiyo, mchango huo ni mzuri na tutaendelea kuufanyia kazi ili kuhakikisha kwamba wananchi wengi zaidi wanaelimika na kuweza kufanya shughuli zao inavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la kwamba biashara nyingi kushindwa kufanya vizuri, ilizungumzwa kwamba kutolewe elimu siyo tu katika miji ni mpaka vijijini zitolewe elimu. Nakubaliana kabisa na suala hili, ni kwamba biashara ni sawa na binadamu, biashara zinaumwa kama binadamu, mtu anapokuwa hajui namna ya kufanya biashara inamfanya hata hiyo biashara ikianzishwa isiweze kuendelea. Kwa hiyo, Wizara yetu tumeona kwamba kuna kila sababu

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

ya kuanzisha vituo ambavyo vitasaidia katika kuwezesha kutoa tiba (*business clinics*) kwa ajili kusaidia viwanda hivyo vidogo vidogo, pia na biashara ndogo ndogo kusaidia katika kuleta uongozi wa masuala ya kiuwekezaji. Tupo katika mkakati huo na tutapokuwa tumekamilisha taratibu zetu basi tunaamini kwamba masuala hayo yatakuwa yamekaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo, kuna ambao walizungumzia ili tuweze kuwa na biashara vizuri au uwekezaji vizuri suala la amani ni suala muhimu sana, naunga mkono hoja hii ambayo ililetwa na Mheshimiwa Lwakatare, amani itaanzia humu Bungeni, mwenzako akiongea lazima umskilize, uwe na uhimilivu, lakini kama hatutakuwa na amani ya kusikilizana hata kama kuna jambo la msingi mtu unakuwa kama tunafanya mchezo wakati watu tunakuwa tumefikiria tunafanya mambo ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa wote tuna dhamira moja ya kumuunga mkono Rais wetu kuhakikisha kwamba uchumi wa ujenzi huu wa viwanda unakua, basi tumuunge mkono kwa dhati na tuhakikishe kwamba tupitie vizuri vitabu hivi vilivyoandikwa na Wizara yetu ukurasa kwa ukurasa mtapata mambo mengi sana ambayo kwa hakika yatajenga na kuhakikisha kwamba tunajenga vizuri uchumi wetu, tusaidiane.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Waheshimiwa Wabunge naomba utulivu Bungeni, tumeanza hii tabia ambayo siyo ya Kibunge, nawaombeni sana, hapana sitaki lugha hiyo. Sasa namuita mtoa hoja aweze kuhitimisha hoja yake, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, unazo dakika 40. karibu sana Mheshimiwa Mwijage.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuhitimisha hoja ya Wizara yangu. Hoja zangu ziko kwenye makundi makuu mawili, kundi la kwanza ni hoja kama zilivyowasilishwa na Wabunge kupitia kwenye Kamati inayosimamia Wizara hii, niwashukuru kwa kuleta hoja zao na ninawaahidi kwamba nitazitekeleza. Kundi la pili ni Waheshimiwa Wabunge ambao ama walizungumza ama walikuja kwa maandishi wakichangia bajeti hii. Waheshimiwa Wabunge 50 wameweza kuchangia kwa kuongeza hapa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge 39 walichangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi Mheshimiwa Spika wakati alipokuwa hapa nawasilisha alitupa dira na nadhani ndiye aliyewapa hamasa Waheshimiwa Wabunge kwamba muijenge upya, mui-*shape* upya hii bajeti. Hiyo yote yaliyosemwa nakwenda kuandika upya utekelezaji wangu wa mwaka unaokuja. Kwa kukubali kwangu huko niko mbele yenu nikiwaomba mpitishie bajeti yangu nitaitekeleza kama mlivyonishauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongozwa na Dira ya Taifa 2020/2025 ambayo kama Taifa tunalenga ifikapo mwaka 2020/2025 Taifa letu liwe Taifa la uchumi wa kati. Uchumi wa kati Watanzania wenye kipato cha kati tungetamani Mtanzania wakati huo 2020/2025 awe na kipato kwa wastani wa dola 3,000, hicho ndicho kipato tunachokitaka ili kufikia hapo kwenye uchumi wa kati uliojumuishi chombo cha kutupitisha mpaka hapo ni uchumi wa viwanda. Dira yetu ya Taifa inajengwa katika mipango mitatu ya miaka mitano mitano iliyoanza mwaka 2011 inayoisha 2026. Mpango wa kwanza ulilenga kuondoa vikwazo, mpango wa pili ni ujenzi wa uchumi wa viwanda na mpango wa tatu kujenga uchumi shindani (*the capacitive economy*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufika hapo tunaongozwa na mkakati (*Integrated Industrial Development Strategy*) wa 2011 unakwenda mpaka 2020/2025 unaelezea yote ambayo



NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Waheshimiwa Wabunge mlikuwa mnanikumbusha yote yameandika mle. Huo ni mkakati mkubwa, ndani ya mkakati mkubwa kuna mkakati mdogo, mkakati mdogo wa kwanza unazungumzia kutoka pamba mpaka mavazi, mwingine unazungumzia fursa ya kutumia mafuta ya kula kutoka kwenye mbegu tuzalishayo hasa hasa alizeti. Kama mlivyosema Waheshimiwa Wabunge mafuta ya kula ni bidhaa ambayo inachukua pesa zetu za kigeni ikiwa namba mbili ikifuatiwa na mafuta ya jamii ya petroli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati mwingine kama mlivyosema Waheshimiwa Wabunge upo unazungumzia namna gani tutengeneze ngozi na bidhaa za ngozi. Wakati mwingine mdogo ni wa madawa, mkakati mwingine ni wa kujitosheleza chakula, mikakati yote hii inajengwa ndani ya mkakati mkubwa wa *Integrated Industrial Development Strategy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunapojenga uchumi wa viwanda kwa maandiko ya mipango hiyo mitatu na kwa maelekezo ya viongozi wakuu, tunaambiwa tulenge mambo matatu, tujenge viwanda ambavyo vinaajiri watu wengi. Tujenge viwanda ambavyo bidhaa zake zinatumika sana, lakini tujenge viwanda ambavyo vinategemea malighafi zinazozalishwa na Watanzania walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazotumika kwa wingi tumebakiza *item* moja na mimi na Waziri wa Afya tumeweka kipaumbele kuhamasisha ujenzi viwanda vya madawa. Tutakapokuwa tumefanikiwa kujenga viwanda vya madawa sekta ya bidhaa zinazozalishwa kwa wingi tutakuwa tumevuka. Kama nilivyoeleza tunajitosheleza kwa nondo, lakini Mheshimiwa Bulembo amehoji inakuwaje nondo zinapanda bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika soko la dunia chuma kimepanda bei hatujafika Bajeti Kuu ya Serikali tutaangalia namna gani ya kufanya, lakini mtoto mzuri Dangote ambaye mimi namuita mtoto mzuri, alipoharibikiwa mitambo yake

ya *clinker* kutokuwepo kwa Dangote ambaye yeye anazalisha tani milioni tatu kwa mwaka hawa wazalishaji wadogo wakashindwa kulihimili soko. Kwa sababu Dangote alipoleta *industry shakeout* hawa wazalishaji wengine walikuwa wamerudi nyuma wakizalisha kwa kujikimu, sasa alipoondoka kwenye soko tukabaki na *vacuum*, lakini Dangote wakati wowote atamaliza mtambo wake wa *clinker* na wakati huohuo anafungiwa gesi kila kitu tayari atarudi *troublemaker*, tuweze kurudi kwenye bei zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naelezea viwanda ambavyo bidhaa zake zinatumika kwa wingi ndiyo tuko hapa, tumebakiza madawa, pili tumebakiza mafuta ya kula ambayo nitaelezea suluhisho lake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachofanya siyo kufika uchumi wa kati, ni kufika uchumi wa kati ulio jumuishi na uchumi wa kati ulio jumuishi unaupata kwa kupitia viwanda vinavyotegemea mali za wakulima na ndiyo maana tunazungumza viwanda kuanzia vijijini, ndiyo maana tunazungumza viwanda vinavyochakata malighafi za wananchi, yule anayelima pamba anapata keki yake, anayeivuna anapata keki yake, anayeichakata kwenye *ginnery* anapata keki yake, anayetengeneza nguo anapata kipande cha keki na anayekwenda sokoni kuuza nguo ndiyo uchumi jumuishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilibidi niliendeleze hivyo, ili kujenda uchumi jumuishi ambapo Wizara yangu inakuwa ni kitovo na muhimili nahitaji watu wa kuniwezesha. Nichukue fursa hii kumpongeza Waziri wa Nishati amezungumza, bila nishati huwezi kujenga viwanda, unahitaji nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru Waziri wa Nishati umezungumza *power mix* sipaswi kuirudia, tunahitaji umeme wa kutosha. Hatuwezi kuuza mawese ya Kigoma, Kigoma inaweza kuzalisha mawese lakini soko liko Dar es Salaam, asilimia 50 mpaka asilimia 70 ya bidhaa zote ziliwazo Tanzania huliwa Dar es Salaam. Hivyo mawese ya Kigoma bila usafirishaji mzuri hamuwezi kuyauza Dar es Salaam, ndiyo

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

maana tunajenga *standard gauge*, kumbe reli miundombinu wezeshi, barabara ni miundombinu wezeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mliyosema bila maji hatuwezi kwenda popote, namshukuru Mwenyezi Mungu Bwawa la Kidunda litawezesha *Bagamoyo Special Economic Zone* na Dar es Salaam kufanya kazi. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge niwaeleze, tunachofanya tunataka kuwa Taifa lenye uchumi wa kati ifikapo 2025, tuna miaka miwili, tunaweza kuwa tumechelewa, lakini msikate tamaa, *your on right truck*. Unapokuwa na mashaka na kule uendako umeshajua njia, haya mashaka mnayoonesha ina maana mmeshaiona njia, kazi mliyoifanya kwa siku mbili imeshanionesha namna gani niendeshe kwa kasi. Nimeona nizungumze hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda vilivyobinafsishwa; kazi niliyopewa moja ni kuhakikisha viwanda vyote bila kujali mmiliki vinafanya kazi vizuri. Viwanda vyote bila kujali mmiliki binafsi na vya Serikali vinafanya kazi vizuri. Ndiyo maana tunazungumza mazingira wezeshi, natambua *concern* yenu, natambua maelezo yenu katika mazingira wezeshi. Hatuko vizuri kwa muhtasari wa namba, kwamba sisi ni wa 137 kati ya 190, lakini *distance to frontier* tuko *above 50 percent*. Sitaki kujivuna na hiyo nitafuata maelekezo yenu na ndiyo maana tunakuja na *regulatory reform* ya *blueprints* ambayo hizi taasisi mnazozilalamikia zitalazimika kufanya kazi, inaanza na bajeti mpya kwa sababu ina bajeti *implication*. Hatukuianza jana kwa sababu ina mambo ya kibajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vilivyobinafsishwa na nimshukuru Shangazi yangu Mheshimiwa Lulida alisema Mwigaje asiwe kondoo wa kafara. Lakini hili la viwanda niko tayari kuwa kafara! Nitahubiri viwanda anayetaka kunipiga risasi anipige risasi, lakini Mheshimiwa Lulida unajua mtoto hakui kwa shangazi yake, mimi nilipoelekezwa suala la viwanda, viwanda vilivyobinafsishwa vilikuwa ni 156, tulipokuja kufanya *snap shot* wakati naambiwa nikiwa Tanga

na Mheshimiwa Rais kwamba nimemkwana, viwanda vilivyokuwa vinafanya kazi vizuri vilikuwa 62, vilivyokuwa havifanyi vizuri tatizo langu vilikuwa 56, vilivyokuwa vina suasua ni 28, vilivyozwa *by stripping* (engine peke yake, *godown* peke yake) vilikuwa kumi. Nikaanza kazi, taarifa niliyowaletea mwezi Machi ndiyo kazi niliyofanya. Katika viwanda 56 *troublesome*, viwanda 18 vimeshaanza kukarabatiwa na vimekarabatiwa tayari kufanya kazi. Katika kipindi cha mwaka mmoja nawaomba Wabunge mnikubalie muwe na uhakika kwamba nikibaki hapa kufikia mwaka kesho viwanda vinatakuwa vimekwisha vyote. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja nikuambie viwanda 35 vilivyobaki na nitawasilisha kwa Mheshimwa Spika haya ni mambo ya kitaalam, Waheshimiwa Wabunge viwanda 35 vingine havina sifa ya kuwa viwanda, lakini kwa mamlaka niliyonayo siwezi kuvifuta, inabidi niende kwenye ngazi zinazohusika niwaambie jamani mlichonionesha kama ni viwanda 156 hiki haki-*qualify*. Mfano, lilikuwepo eneo la kiwanda cha kuunga matrekta, nimeambiwa na kiwanda, nikaenda kufanya *survey* nikakuta wamejenga *shopping mall* nzuri kabisa, inaajiri watu inaitwa *Quality Center*, mimi *mall* naipenda kwa sababu inazalisha ajira, kumbe tumekosa eneo la matrekta sasa nimetengeza maeneo mengine ya matrekta, ugomvi utoke wapi? Mnanishauri nikabomoe ile *shopping mall*? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna viwanda vingine vilikuwa vya kupasua mbao, nilipokwenda kuangalia misitu imekwisha, sasa huyo mtu nimfanyeje, nimuue huyo mtu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna viwanda vingine ni mali ya Serikali, kuna eneo kiwanda cha maziwa ni mali ya *NHIF*, sasa kiwanda cha Serikali siwezi kukichukua nimemwambia *NHIF* pesa unazo unijengee kiwanda cha madawa, yuko kwenye mchakato ajenge kiwanda cha madawa, ndiyo *story* za viwanda hivi navimaliza kabla ya asubuhi. Waheshimiwa Wabunge mniamini, wengine wanasema *Mwigaje he is not serious*, siwezi kujua! (Makofi)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze suala la sukari, mimi ni mcha Mungu na mcha Mungu yeyote ni lazima atii na aheshimu dini ya mwezake. Mbali na kuwa mcha Mungu mama yangu ni Muislamu apumzike kwa amani, mama yangu aliitwa Mariamu, nikalelewa na bibi yangu anaitwa Mwamini na Zuhura. Kwa hiyo Uislamu ninao, Mjomba wangu anaitwa Sadiki, kwa hiyo siwezi kuhujumu Uislamu. Mama mdogo wangu mwingine yuko pale, sina tatizo, lakini Watanzania niwaambie tunayo sukari ya kutosha. Tunapozungumza sasa kuna tani 43,000, kwenye *stock*, lakini Tanzania tunatumia tani 40,000. Bandarini nimeshamwagiza Meneja wa *TFDA* na *TBS* sukari iliyoko bandarini inaondoka, ninyi Wabunge ndiyo mnawaonea huruma wale wanaokwenda kufunga na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge yeyote, Mbunge wa kwanza ameshaniambia nimpe tani 1,000 nimemruhusu achukue, njooni mchukue sukari, tuna sukari ya kutosha. (*Makofi?Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bandarini tani 22,000 ziko tayari. Mbali na sukari hiyo viwanda vya sukari vyote vimebakiza wiki tatu mpaka wiki nne baada ya *dry season* vinaanza kuzalisha. Kwa hiyo, asitokee suala la uadimikaji wa sukari ilikuwa ni *propaganda* na katika *propaganda* mimi nilisomea *propaganda* mpaka China ilikuwa ni *propaganda* sukari ipo, kama ni *propagandist* mwenyewe ni mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kingunge angekuwepo ungemuuliza *propaganda* alinifundisha Kingunge Ngombale Mwiru. Kwa hiyo, hakuna tatizo la sukari, Wabunge niko hapa na tunafunga kwenye mwezi mtukufu wa Ramadhani atakayekuwa na tatizo aje aniulize tunasambaza sukari kwenda mikoani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzue suala la sukari nchini, suala hili halikuanza leo na linaenda na mfungo wa Ramadhani, linaendana na *rain season* viwanda vinapofungwa tumekuwa na haja kama nilivyowafahamisha

kwenye sababu tatu za viwanda tulenge viwanda vinavyoajiri watu wengi, kama ilivyo pamba sekta ya sukari inaajiri watu wengi. Sekta ya sukari, kwa mfano kiwanda cha *Kagera Sugar* kinachozalisha tani 75,000 kinaajiri watu 5,000, lakini Tanzania kama nchi ndiyo wale Wabunge mnasema halafu mnakasirika mnasema *shame*, wakati mwingine mna haki ya kusema hivyo. Tanzania tuna fursa ya kuweza kuzalisha tani milioni mbili za sukari kwenye mabonde yetu, lakini upaunuaji wa mashamba hayo *financiers*/wanaotoa fedha walikuwa wanakataa kwa sababu ya uingizaji wa sukari holela na *substandard*. Tatizo lililompata Kenya, uingizaji wa sukari wa Kenya, sukari wanayozalisha imeshuka kwa *40 percent*, sasa tulichoamua Serikali ni kwamba *gap sugar* tani 135,000 wailete wale wenye viwanda ambao wanalalamika kwamba kuna watu wana-*dump* sukari halafu wale wenye viwanda tukawapa masharti watuoneshe *acreage*, eneo watakalooonze la kuweza kulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwaeleze kwamba Kiwanda cha Mtibwa wanaongeza, *British Food* walikuwa hapa kwenye Mei Mosi wakija kutangaza mbele ya Mheshimiwa Rais, wame-*commit* bilioni 500 Kilombero kuwekeza, pamoja na kuongeza Profesa Jay nikuambie, nitahakikisha maslahi ya wafanyakazi waliopunguzwa wanalipwa pesa zao. Watu wa Mtibwa wanatengeneza bwawa *la irrigation 29 square kilometres*, Mwenyekiti wa Kamati ni shahidi wameanza *system ya irrigation* na Kagera vilevile. Mheshimiwa Rais amewapa daraja kuvuka kwenda upande wa Kitengule, tunataka kujitosheleza kwa sukari na ninawahakikishia utaratibu huu ni mzuri, atakayekiuka tunamchukulia hatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze alizeti, mawese na karanga ili kuziba lile pengo. Nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Munde Tambwe, amesema kwao Tabora na Wabunge wote wa Tabora na Halmashauri zenu eti mje kwangu niwape trekta, nina matrekta 148, mimi ndiye nawajibika, hizo *tractor* tatu mlizoomba kila Halmashauri mniletee barua ya Mwenyekiti wa Halmashauri, Mkurugenzi

wa Halmashauri, Mkuu wa Mkoa asaini, mlete kwangu kwa mamlaka niliyonayo matrekta zikaanzie kule hamuwezi kutoroka ninyi ni Watanzania. Ngoja tukafanye mazoezi Tabora, Mheshimiwa Munde tukafanye mazoezi Tabora tuta-*leverage* kwenye Mikoa mingine. Maksud yake ni nini? Tumeshakubaliana na *SAGCOT* walete mbegu zenye *high yield* na ninyi Wabunge najua, kuna Wabunge mnalima alizeti, msilime alizeti ilimradi alizeti, kuna alizeti ambazo ukikamua unapata mafuta mengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SAGCOT* wameshafanya utaratibu, Waziri wa Kilimo ataelezea, tutawapa mbegu lakini ngoja niwaambie na mimi nitakwenda kukamata shamba Tabota nitaanzia Tabora nikikosa Nzega nitakwenda Igunga tulime alizeti, nitahakikisha si mmesema viwanda nilivilindwe, nitavilinda viwanda vinavyozalisha mafuta yawe ya pamba, yawe ya alizeti tuondoe hiyo mliyoniambia *shame*. Nilikuwa naangalia kwenye *dictionary*, *shame* ni neno baya mtu akikwambia *shame* nikamuuliza mwanangu anasema *shame* maana yake ni nini. Kwa hiyo, nitawahakikishia tunazalisha alizeti na tunapokuwa na alizeti tunaweza kujiokoa na mafuta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze suala la kulinda viwanda, suala la la kulinda viwanda ni wajibu wangu, lakini Watanzania tukubaliane, waliochangia wengine wamehoji utamaduni wa *TBS* na *FCC*. Ukienda bandarini haya mambo ya *under invoicing* na *over invoicing* kuna nguo zinapita wakishonewa wanafunzi *uniform* baada ya wiki tatu nguo inakuwa kama chandarua. *FCC* akizichoma ndiyo hayo maneno ya Mheshimiwa Munira anasema mnachoma nguo za watu, mningoza nifanye nini. Sasa kwa sababu mmeniruhusu, atakayeleta bidhaa yoyote, *TBS* nakwambia na *FCC* wewe choma usisikilize kilio cha huku kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wameniruhusu wenyewe. Hiyo ndiyo namna ya kulinda viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, linahusu *valuation* ya *TRA*. Suti niliyovaa mimi hii thamani yake ni dola 600, mtu wa *TRA* akii-*value* dola 50 unapigwa *25 percent* na

*18 percent, sasa wewe unataka ipigwe vipi? Mheshimiwa Mpango wametupa ruhusa atakayeleta suti kama hii niliyovaa akasema dola 50 nakuomba tu-uplift kusudi tuipege bei kubwa, tulinde viwanda vya ndani, nadhani ndivyo mlivyonieleza! Ndivyo mlivyotueleza, ndivyo nilivyo waelewa na ndiyo maana viwanda vyetu vinakufa. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumza *Mwatex*, *Mwatex* ilikufa kwa sababu tulipenda kanga za China ambazo Mheshimiwa Zainabu Mwamwindi anasema akijifunga haiwezi kumfika vizuri, lakini ukiziangalia watoto wa Pwani wanasema zile ndiyo nzuri wanaziita sijui nini zile, ndiyo wanazozipenda sasa tutahakikisha kwamba *substandard product tunazi-control*, nitalinda viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la tata la Mchuchuma na Liganga. Waheshimiwa Wabunge mradi wa Mchuchuma na Liganga upo, Serikali ilishaingia makubaliano na mbia kampuni ya China. Kampuni ya China imewekeza pesa karibu dola milioni 60 wamemaliza, wakasaini kitu kinaitwa *performance contract*, baada ya kusaini *performance contract* ikabaki kuanza, ndiyo tukaja na sheria yetu ya kuangalia mara mbili tukakubaliana kwamba tupitie ule mkataba tuboreshe vifungu. Wataalam wakaanza kufikia, sasa wataalam kwa maelekezo wao walitumwa kuangalia kama kuna ukakasi au maslahi mapana ya Taifa, ikakutwa kuna vifungu tunavyojadiliana, lakini mwekezaji yuko tayari. Vifungu vya kujadiliana huu ni mkataba wa siri na silazimiki na siyo vizuri kwa wanaojua sheria kuujadili, lakini mimi ni ninyi, ngoja niwaambie mambo mawili na msiwaambie watu. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule mkataba wa kwanza, ngoja niwaambie, mkataba wa kwanza mwekezaji alikuwa anataka akusanye VAT, aichukue VAT aitumie baada ya miaka 20 atulipe, akasema baada ya miaka 20 niwalipe, sasa ukikutana na watendakazi wa leo wanataka VAT wakatoe elimu bure, wanataka VAT wakanunue madawa wanapata ukakasi. Kwa hiyo, tukakaa nao, kitu kingine na niwashukuru



NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Wabunge waliochangia chuma cha Mchuchuma na Liganga. Watalaam wa uchambuzi wa migodi wanasema katika ule mgodi *deal* siyo chuma, kuna madini mengine ambayo kitarakimu yanatija zaidi, wakatuonesha kwa namba na mimi nikawa m dogo kama *piriton*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mradi niliupigia kampeni mimi tukamwambia mbia mwenzetu atulettee *financial modal*, amekwenda kutafuta *financial modal* ya ku-*recognize* madini yale na madini haya halafu tutakaa chini na namwambia huyo mbia alipo haraka sana alete *financial modal* tuanze. Katika utaratibu wangu tukakubaliana kwamba twende tukatengeneze barabara za ndani ramani tunajua, kiwanda kitawekwa hapa, barabara ya kutokea, mlima uko hapa ndiyo nikaomba pesa ambazo ziko mbele yenu shilingi bilioni tano, lakini kuna shilingi bilioni tano nyingine kama walivyosema, ninakwenda kutathmini upya nijue anayepaswa kustahili kulipwa, kama bilioni moja ndiyo fidia, bilioni nne nitazileta nina Kamati inanisimamia, nina CAG ananisimamia ndiyo Mchuchuma na Liganga, ipo na tutaitumia.

Waheshimiwa Wabunge niwaambie, kuna kitu kinaitwa *kulila masimanda*, unachukuakitu chako unakiuza, unakuja kwa Kiswahili wanakwambia umeuza kwenye *throw price*. Kuna nchi moja nilioona kwenye *clip* walifanya mkataba na wawekezaji, mwekezaji akawaambia *we will break even after 30 years*, huyu akakubali akasema nipata *employment*, walipoanza kazi miezi sita aka-*break*, mwaka wa pili madini yamekwisha, wananchi wakamrudia kiongozi huyo. Nisingependa kuliona hilo na naogopa na nilishawahi kuwaambia sitashiriki kwenye maamuzi yoyote ambayo wajukuu wangu watafunga kaburi langu minyororo, ndiyo hiyo Mchuchuma na Liganga, mnamini, niko *serious*, watu wengine wanasema Mwijage hayuko *serious*, hivi sura hii iwe *serious* itafananaje, mtaiangalia? *I am serious (Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze suala lililozungumzwa sana la mkakati wa pamba mpaka mavazi.

Nimewaita wenye viwanda vya nguo, wenye *ginneries* nimekaa nao watu wenyewe wa kwenye *field*, wameeleza maeneo wameeleza maeneo ambayo yana ukakasi, nilikuwa na watu wa Wizara ya Fedha tunayashughulikia, lakini Mheshimiwa Waziri wa Nishati amezungumza, tunapeleka umeme. Kwa hiyo, tunathamini *cotton to clothing* kama mlivyo sema siwezi kusema tena, ndiyo sekta yenye ajira nyingi. Kwa mfano, Kanda ya Ziwa nimeeleza kwenye *speech* yangu kwamba *Social Security Funds* wamekwenda kufufua *ginneries*, tunapambana zinunuliwe zaidi lakini kuna *ginneries* za sekta binafsi, muulize Mheshimiwa Kishimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua kuna watu wengine anamiliki lakini hataki kujulikana anamiliki, Kishimba anamiliki na anasema anamiliki. Sasa kuna *ginneries* za Tanzania, uzoefu tulio nao hakuna *ginnery* ilikuwa inaweza kufanyakazi kwa siku 90, sasa pamba imezalishwa kwa wingi, tunakwenda kuiunganisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuzungumza kidogo kwa heshima na taadhima, watu waliosema *The Government is not coordinated, No! tuko coordinated*. Mfano, ni *cotton to clothing*, ilipopigwa baragumu ya pamba mpaka mavazi, Waziri Mkuu alikuwa Kiranja wetu Mkuu, alikuwepo Charles John Tizeba, Waziri wa Kilimo, alikuwepo Waziri wa TAMISEMI, Jafo tukakimbia wote na Mheshimiwa Selemani Jafo, tukaanza kuzunguka nchi nzima, ndiyo matokeo haya tukisaidiwa na ma-DC, tukigawa kamba, tukapanda, Mungu atatusaidia pamba itavunwa nyingi, lakini tutavilinda viwanda vilivyopo ili viweze kuchakata pamba yetu. Ndiyo nataka kujibu hilo kwamba mniamini. *Cotton to clothing* tunaijua na nimezungumza kwenye mikakati midogo kwamba na yenyewe ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaeleze Waheshimiwa Wabunge, kuna Mbunge mmoja kazungumza vizuri kwamba haya mambo yanabadilika, yatakapobadilika wote tupo Tanzania mnieleze. Mimi napatikana, kwa simu napatikana, hata kwenye kahawa nakuwepo tuzungumze. (*Makofi*)

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la kukwamisha Wawekezaji na nizungumze kesi ya Hanang'. Mimi ndiye niliyepewa dhamana na nitahukumiwa kwa kutoakuanzisha viwanda. Kama nilivyowaambia, kufufua viwanda vilivyokufa na vile vilivyopo kuzalisha ukomo lakini kuanzisha vipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mamlaka niliyonayo nitamtuma Naibu Katibu Mkuu wa Viwanda aende Hanang amtafute yule mwekezaji aliyetaka kutengeneza kiwanda cha saruji nije nisikie mtu anayekataa nitampandia juu, nitampandia juu kwenye mamlaka iliyotuteua! Haiwezekani, huwezi kuchelewesha mwekezaji. Mbunge wa Hanang usiwe na wasiwasi, kiwanda cha saruji tunakihitaji, atakayetaka kujenga kiwanda afanye utafiti na utafiti utafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo *TIRDO*, nimewaambia ndugu zangu, ukitka kuenga kiwanda kama wewe ni mwenzangu nenda *SIDO*, kama inafikiri una ubavu nenda *TIRDO*. Hata uki-*hire consultancy*, niwaambie tahadhari enyi wawekezaji na Wabunge muwe wawekezaji na niwashukuru wale Wabunge ambao mnakuja kuwekeza na mnaanza kujenga, mnaniletea picha kwa *whatsapp*, msiniletee picha mnialike mimi nina gari nzuri, nitakuja nifungue viwanda hivyo. Tunadanganyana, kuna watu wanafungua viwanda vidogo, wanapata tija halafu wewe unabaki viwanda vidogo mimi sivitaki, wenzako wanakula ,wewe unasusa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la mazingira ya biashara. Nawashukuru mlinishauri vizuri, lakini siyo kwamba nchi hii siyo ya uwekezaji. Ninawaahidi nitaboresha zaidi, *regulatory reform* ikija mtaona mambo yanakuwa mazuri, mambo yatakuwa mazuri.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Lucy Mayenga uliyozungumza yote kuhusu mazingira ya biashara, najua watoto tunawazaa wenyewe. Mimi mtoto wangu anaweza akapata kazi *Fair Competition* au *TBS* akikosea siyo mimi. Sasa kama nilivyowaeleza, Mheshimiwa Lucy Mayenga yote mnayoyaona mje mtuambie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *brother* umezungumza mambo ya ukaguzi wa bidhaa kule Dubai, njoo uniambie, umekuwa kwenye Wizara hii ukisimami sekta hii unajua vizuri njoo uniambie. Mabadiliko unayoyasema kama SGS anaongeza gharama nitayatekeleza. Sina maslahi binafsi mtu kukwamisha wawekezaji. Kwanza wawekezaji wanapokuja wengi ujiko unakuja kwangu, mnasema Mwijage umejenga viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze suala la kujenga viwanda. Serikali haijengi viwanda ila inaweka mazingira mazuri kwa sekta binafsi kuwekeza. Tuko vizuri, soma hotuba yangu nimeeleza nafasi yangu na *Tanzania Private Sector Foundation*, muulize Mzee Mengi.

Nimezungumza na Mzee Mengi wakati nahamasisha viwanda vya madawa ilikuwa juzi tu tumeweka jiwe la msingi kiwanda chake. Tunazungumza na biashara ni kuzungumza kama mikono miwili ilivyo, mikono miwili ni kunawishana, kwa hiyo hatuna tatizo na *private sector*. Hii migongano iliyopo mtu anapopata matatizo aje atueleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Chumi alizungumza suala la mifuko. Hilo suala la mifuko ya *plastic* ni suala la kiutawala. Katibu Mkuu wangu usimame, angalia hiyo mifuko inakwendaje na uanze utekelezaji bila kuchelewa.

Tumezungumza suala la fidia za EPZA, Mheshimiwa Kawambwa, Kaka yangu twende tukae chini, tuangalie Bagamoyo tutakavyoweza kuiweka vizuri na niwaeleze kuna watu waliandika wakihoji kuhusu *Bagamoyo Special Economic Zone*. *Bagamoyo Special Economic Zone* ninavyozungumza sasa mwekezaji yuko Dar es Salaam na timu ya Serikali wanajadiliana. Upande wa viwanda wamemaliza, sasa wanajadiliana upande wa bandari ndiyo taarifa niliyonayo, mambo yanakwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko mwaka wa pili katika safari ya miaka kumi ya kufika uchumi wa kati. Watu

wangependa kufika leo lakini naona muende taratibu tutafika lakini muendeleo kunielekeza na kunikosoa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la Mheshimiwa Mariam Kisangi. Tumekubaliana na Meneja wa *TanTrade* kwamba siku za sikukuu wenye biashara mtaingia kuuza bila kujali kama ni Sabasaba au siyo Sabasaba wale wananchi wa Dar es Salaam na watoto wataingia bure. Mheshimiwa Mariam Kisangi amependekeza bembea, sasa tunatafuta nani aweke bembea na atafute mtu binafsi aweke mabembea mtoto kipanda weka shilingi 50, msiwa-charge pesa nyingi, mkitaka *profit* nitawafukuza, watoto waende kuburudika na watoto hawana pesa au wacheze bure kwa sababu hawana pesa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Benardetha Mushashu umezungumzia suala la viwanda Kagera, namsubiri Waziri wa Mifugo, tumepata mwekezaji ambaye atatengeneza kiwanda cha maziwa, shamba la kutengeneza maziwa kuanzia maziwa kwenda kwenye *UHT* mpaka maziwa unga. Mheshimiwa Lwakatare anasema Mwijage usikimbie ukapita kwenu. Bibi yangu aliyenilea, alinimbia Mwijage ukiamka unawe uso na uso ni Jimbo langu, uso ni nyumbani, lakini mimi najenga Tanzania. Kwa hiyo, usiwe na wasiwasi Mama Mushashu nitakuja kuwaelekeza namna gani ya kujenga viwanda. Wewe shangazi yangu unielewe, usiogope kuanza na kiwanda kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la kiwanda kidogo sana nilizungumze, mwenzangu mimi hujawahi kumiliki hata milioni moja, unakwenda kutafuta bilioni 100 utaanguka nayo, anza kidogo. Siri ya kiwanda kidogo maana yake ni nini? Tunataka kurithisha utamaduni wa kumiliki biashara.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri muda.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie hili, tunataka kujenga utamaduni wa kupenda viwanda. Nimetoa mfano huu siyo wa kibaguzi. Wenzetu Wahindi na Waarabu watoto wao

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

tunasoma nao, lakini kwenye kazi hatuombi na wao. Nilikwenda Manyara kwenye kiwanda cha sukari, nimekuta watu mle wana historia ya viwanda, wameanza kwenye kiwanda kile cha sukari mpaka kinakua, mtoto na watoto wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza maelezo hayo nitayafafanua zaidi nikipata nafasi, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante, hoja imetolewa na imeungwa mkono, tunakushukuru sana na ama kweli upele umepata mkunaji, tunakushukuru sana. Katibu. *(Kicheko/Makofi)*

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 44 – Viwanda**

Kif. 1001 - *Admnistration & HR Mgt.....Sh.11,675,416,448/=*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hapo ndipo kwenye maneno. Orodha ya kambi zetu za vyama nimeletewa hapa. Naomba tuwe na maelezo mafupi kwa sababu ya muda mnauona wenyewe siyo rafiki, tutatenda haki tu. Tunaanza na Mheshimiwa Hawa Chakoma.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ili kufanikisha dhana ya uchumi wa viwanda, suala la maeneo maalum ya uwekezaji na uzalishaji kwa ajili ya kuuza nje *(Export Processing Zone)* yameainishwa kuwa ni njia nzuri na ya haraka kuelekea uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imefanya jambo jema sana kuanzisha *EPZA* ambayo kimsingi iliangaliwa kwamba kuna malighafi ya kutosha, kuna nguvu kazi ya kutosha, kuna ardhi ya kutosha, isipokuwa jambo la kusikitisha yapata miaka 15 sasa maeneo tofauti ambayo kimsingi yalitengwa kwa ajili hiyo wananchi wake wanadai fidia hajalipwa mpaka hivi sasa. Pia maeneo hayo hayajawekewa miundombinu mizuri ya kumvutia ama kumshawishi huyu mwekezaji. Kwa maana hiyo, ni wazi kabisa hakuna mwekezaji atakayekuja kwenye eneo la namna hii ambalo wananchi wanadai fidia, lakini hakuna miundombinu wezeshi.

Sasa nitaomba kupata kauli ya Serikali kwamba ni uchumi gani wa viwanda tunaoenda nao katika mazingira kama haya? Kama sikuridhishwa na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nakusudia kutoa shilingi. Ahsante. (*Makoff*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi tu.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu Mheshimiwa Hawa Chakoma, ni kweli tunayo maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za kiuchumi hizo *EPZA* na *Special Economic Zone*, kama alivyosema kweli kiuchumi nchi zilizokwenda haraka sana ambazo tunajifunza kwake kama China wamewekeza kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitenga maeneo kwenye bajeti yangu humu inajieleza. Pesa nilizotengewa kwa mwaka kesho nitamaliza yale maeneo, pesa zile zikiletwa nitamaliza maeneo. Iko Kigoma, iko Ruvuma, kwa kutaja baadhi. Tatizo sugu ilikuwa ni Bagamoyo. *Bagamoyo Special Economic Zone* maamuzi yalishatolewa kwamba lile eneo watu ambao hawajafidiwa basi wawekezaji wale watatu Tanzania, Oman na China ule utatu waweze kuwalipa fidia. Kwa kutambua nafasi ya haya maeneo Wizara yangu imehamasisha sana *Stand Alone special Economic Zone*, kama kwenye kitabu changu kilivyooneshwa. *Stand Alone*

*special Economic Zone 77* zinazokuwa *owned* na *private sector* na *individual* zimeanzishwa, ukisoma kitabu changu utaweza kuona zile *stand alone* zimekwenda namna gani, sekta binafsi na Serikali tunakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo inategemea na pesa tunazozipata lakini msiwe na wasiwasi *stand alone* zimekuja na ndiyo mkakati ambao unahimiza zaidi wakati namalizia Ruvuma NA Kigoma, kama nilivyoeleza kwenye bajeti yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo maelezo yangu.  
(Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Chakoma.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi upo yapata miaka 15 sasa, hilo la Bagamoyo lapata miaka 11 sasa, naomba kutoa hoja ili wenzangu wapate kuniunga mkono.

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa, imeungwa mkono wamefika zaidi ya kumi. Waheshimiwa Wabunge mnafahamu ninahesabu, *don't play with me*. Sasa tunaorodhesha Mheshimiwa Dkt. Kawambwa, Mheshimiwa Vulu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mbene na Mheshimiwa Mhagama na Mheshimiwa Jitu Soni. Tunaanza na Mheshimiwa Kawambwa.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchagua hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Hawa Mchafu na kwamba Serikali ijitahidi kuhakikisha kwamba tunatenga pesa kwa ajili ya maeneo haya maalum ya *EPZA* na *SEZ*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda mrefu sana umepita tumeyatenga haya maeneo na ni mifano mizuri ya uwekezaji katika nchi ambazo tunazingalia zimepiga hatua kubwa, moja ya nchi hizo ni nchi ya China ambayo imetumia



*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

maeneo haya ya *SEZ* kwa ajili ya kufanya uwekezaji mkubwa viwanda na uwekezaji ambao upo katika mpangilio mzuri, unajua viwanda vipi, unaviweka wapi na wanajali mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wetu tumewatupa sana, kwa Bagamoyo peke yake ni takribani miaka 11 sasa hawajui namna gani wataishi, rasilimali walizokuwa wanazitegemea mashamba yao na nyumba zao ndizo ambazo wameambiwa subirini haya maeneo yanachukuliwa, lakini mwaka hadi mwaka imetimia miaka 11 sasa hatujaweza kuzigomboa hizi ardhi ziwe *free*. Ni kweli Mheshimiwa Waziri anazungumza lakini imekuwa muda mrefu sana, kwa hivyo sasa hivi tunapenda kuona vitendo kwamba Waziri aji-*commit* kwamba Serikali itawekeza hela kuwalipa wananchi fidia zao ambazo imekuwa *pending* kwa miaka mingi ili sasa tujue kweli sasa tunaenda kwenye uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbene.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Na mimi ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Hawa kwa kutaka kujua, kwa kweli muda ni mrefu na kila mwaka tunapewa majibu haya haya. Haya maeneo kwa kutengwa kwake ina maana wananchi hawawezi kuyatumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *there is an opportunity cost there*, kuwa wananchi hawawezi kutumia maeneo haya *and therefore* wao pia kiuchumi wanaathirika. Sasa tukiwa tunaambiwa tu itakuwa hivi hela imetengwa, kutengwa pesa kwenye bajeti hii ni *indication, this is a just a plan*. Je, hizi pesa zipo kwa ajili ya kwenda kufidia? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisema kwa mfano baada ya bajeti Julai wataanza kwenda kuzi-*disburse* hizi pesa kwa ajili ya kufidia haya maeneo au wanaanza na lipi? *At least* tujue hata ile *action plan* ya hili jambo, itupe *comfort* kuwa

kwa kweli sasa *we are moving ahead*. 15 years ni lifetime ya mtu bado hatuja-*compensate* watu na wamekaa na ardhi yao wanangojea tu *indefinitely*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nafikiri *it is high time* Serikali itupe jibu, kwa sababu uchumi wetu unategemea sana hivi viwanda na *this is very easy way* na ya haraka zaidi kufanya viwanda kuliko hayo mambo mengine tunayofikiria. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Vulu.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja, lakini sina mengi mengine wamezungumza wenzangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida yangu ni kwamba nataka kujua Serikali imefikia wapi, Taifa la Oman na China wako tayari kufidia na kujenga, sasa tatizo liko wapi? Tumesimama viwanda havijengwi, wananchi hawajiendelezi na tuko kwenye mfumo wa viwanda. Tunachokitaka hapa tupate kauli ya Serikali, je, tatizo ni nini na lini litakwamuliwa? Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Mhagama.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, na mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kulielewa hili jambo vizuri upate nafasi ya kuwatembelea wale wananchi wanaoishi katika maeneo haya ambao kwa zaidi ya miaka kumi wameahidiwa. Hawa watu wanaishi nyumba ambazo hazina hadhi na maisha ya Mtanzania. Kwa miaka zaidi ya kumi hawa wananchi wameambiwa wasiendeleze makazi wanayoishi na fedha za fidia hawajapata. Akitaka kujenga

kibanda cha kuku haiwezekani, akitaka kubadilisha bati zinavuja haiwezekani, naomba tukavae viatu vya hawa wananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwijage ni mtu muadilifu sana, mzalendo, mpenda Watanzania na ni mtu mcha Mungu. Atafute nafasi hii kwenda kukutana na watu wanaoishi Mwingemshindo ataelewa nini maana yake, kwa nini Serikali isiende kuwatua mzigo wananchi hawa? Ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jitu Soni kama hoja ni hiyo ya pesa *commitment* ya Serikali *please don't over play, deliver the point* ili twende mbele.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli naona labda Serikali ingekuja na tamko tofauti. Hizi *Special Ecomic Zones* na *SEZ*. Naona kwamba tutaingia kwenye changamoto moja kama walivyosema wengine fidia. Mwaka jana tumepitisha Sheria ya Fidia hapa, *six month* ina maana tunatakiwa kwenda kufanya tathmini upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuwa na mipango kwa miaka yote hii, hivi mipango yote hii tunapeleka umeme vijijini, *densification*, tunapeleka barabara, tunapeleka miundombinu mbalimbali, hivi kote kule maji na kadhalika, tulishindwa kupangilia baadhi ya *ecomic zones* tupeleke miundombinu ili ziwe zinafanya kazi? Pia *incentive* ya kodi kwa mfano, mtu akitaka kuwekeza pale kama yale mamlaka tulishayafuta leo mtu anawekeza pale ili apate nini wakati nchi za jirani ukiwekeza kule kuna *incentive* wanayopata ya kikodi kwamba *export* atakuwa na *incentive* ya kutokuwa na kodi ili aweze kuzalisha, hapa kwetu hizo *incentives* hatuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni vizuri tujue kwamba suala la *EPZ* na *SEZ* tunai-*phase out* taratibu ili wananchi waliopo kwenye yale maeneo wafanye shughuli zingine za

maendeleo, kwa sababu sioni kabisa mpango huu umekaaje. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaelewa Waheshimiwa Wabunge, hoja kubwa ya Waheshimiwa Wabunge ni kuharakisha kulipa fidia. Ninawaelewa kwamba wahapingi mpango wa kuzitenga hizi *economic zones* kwa ajili ya kuendeleza mpango mkakati wa uchumi wa viwanda katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge wamuelewe Mheshimiwa Waziri, waiachie Serikali iendelee na huu mpango kama unavyojionesha kwenye ukurasa wa 210 wa randama hii ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipitia hiyo randama unaona kabisa kwa mara ya kwanza Serikali imelipa uzito sana suala hili kwa kutenga fedha katika maeneo mbalimbali ambayo yamekuwa na migogoro hii ya fidia katika nchi yetu.

Kwa hiyo, kama sasa tumeweza kuonesha dhamira hiyo ya dhati kama Serikali, kuona umuhimu wa kutenga fedha na kulipa maeneo haya ili yaweze kweli kuanza hiyo kazi iliyokusudiwa ya uchumi wa viwanda. Ninawaomba sana, nimuombe sana Mheshimiwa Hawa Chakoma, kwa kusudio hili linalojidhihirisha wazi kwenye randama ya kitabu cha bajeti cha Waziri sina shaka, sasa tumepiga hatua ya kutosha. Waheshimiwa Wabunge ninaamini kabisa tukitekeleza hili safari yetu sasa ya uchumi wa viwanda inaweza ikafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia unaikuta

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Dodoma, Kibaha, unayakuta haya maeneo ya Tanga, unaikuta Ruvuma, unakuta Manyoni, maeneo yako mengi fidia zimeoneshwa na zinajionesha katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri namuomba Mheshimiwa Hawa aiachie shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri Mwajjage.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Hawa kwa maelezo yaliyotolewa nia nzuri ya Serikali iko, maeneo yaliyokuwa na matatizo makubwa nimeyaeleza, lakini kuna kazi nyingine labda sikuisema ndiyo maana wanasema labda Mheshimiwa Mwijage kitabu chako hakijajitosheleza. Juzi tumemaliza kulipa shilingi bilioni tatu za Makambako. Makambako alikuwa kwenye *list* nimemlipa, nikitoka Makambako orodha ni hiyo maeneo yote yanakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bagamoyo ambapo tumekuwa na *bill* kubwa, nimesema wale watatu wabia wameshakubaliana na Mheshimiwa Zaynabu Vulu anauliza tatizo ni nini? Tumemaliza mambo ya fidia sasa hivi kinachojadiliwa ni *tariff* za bandari. Kwamba huyu anapochimba bandari *tariff* zitalipwaje, ndiyo kitu kinachojadiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Hawa mnikubalie mnipe shilingi nikachape kazi, hili suala litaenda kutekelezwa na fedha zitatoka mara moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Chakoma mwenye hoja.

**MHE.HAWA CHAKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru randama yangu inaonesha ni maeneo Sita kati ya maeneo mengi ambayo yana hiyo changamoto ya fidia hapa naona maeneo sita na hiyo Bagamoyo haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba mambo mawili, kitu cha kwanza ambacho naiomba Serikali hizi hela ambazo mmeziainisha hapa muende mkazi-*ring fance* zisije zikaguswa zitumike kwa kusudio hilo maana ni kilio cha muda mrefu sana. Jambo la pili, maeneo ya kule Bagamoyo ambayo kimsingi Serikali inashinikiza wale watu kuondoka pale, watu wamegoma baadhi bado wako pale wameamua kutumia njia...

**MWENYEKITI:** Kwa kifupi.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa ndiyo namalizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wameamua kutumia njia ya kuondoa miundombinu ya kijamii ikiwemo shule na zahanati ikiwa ni njia ya ku-*force* ili watu wapishe pale. Tunaomba tusaidiwe ile shule iendelee ifanye kazi na ile zahanati iendelee kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru na narudisha shilingi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea Mheshimiwa Kiteto Koshuma.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vingi ambavyo vimebinafsishwa ambavyo ni hivyo viwanda 156 viwanda vyote hivyo .....

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa subiri kidogo, kaa kidogo tu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mamlaka nilionayo kwa mujibu wa Kanuni ya 104 (1) ikisomwa na Kanuni ya 56(8) naongeza muda usiozidi dakika 30 ili tuendelee na shughuli hii. Mheshimiwa Koshuma endelea.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda 156 ambavyo vilibinafsishwa hapa nchini Tanzania vyote havifanyi kazi. Kwa maelezo ya Waziri viwanda 62 vinafanya kazi, lakini kwa mtazamo wangu na mtazamo wa Wabunge wengi ambao watakuwa ni mashahidi viwanda ambavyo vinafanya kazi ni viwanda vya bia, viwanda vya sigara na viwanda vya sukari. Hivyo ndiyo viwanda ambavyo vinafanya kazi lakini viwanda vingine vyote vilivyobaki na hata ukikumbuka mchango wangu wa jana hususani viwanda vya nguo vyote havifanyi kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tunataka kuwa na nchi ya viwanda, nitahitaji majibu mazuri ya Serikali kwamba ina mkakati gani wa makusudi wa kuhakisha viwanda hivi vyote 156 ambavyo ni viwanda vya kimkakati vilivyoanzishwa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwamba vinaanza kufanya kazi vizuri, la sivyoyote nisipopata majibu ya kuridhisha ya Serikali juu ya viwanda hivyo vilivyobinafsishwa nitashika shilingi na leo nitaondoka nayo naenda nayo Mwanza kabisa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri wa Viwanda.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimuombe Mheshimiwa Koshuma asinikatalie shilingi hii kwa maslahi yangu binafsi na maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaeleze Watanzania kama nilivyowaeleza, mimi kazi yangu ni kuhakikisha viwanda visivyofanyakazi vinafanyakazi. Lakini viwanda 156 vilivyobinafsishwa ninawahakikishia siyo kweli kwamba viwanda 156 vyote havifanyi kazi. Kama ulivyosema Mheshimiwa Mbunge umeniambia kwamba viwanda vya saruji vyote vinafanya kazi? Kwa hiyo katika 156 umeshapunguza vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kiwanda cha Bora

kinafanya kazi ninayo orodha hapa, *ALAF* kinafanya kazi, *Mufindi Paper Mill* inafanya kazi ingawa ina matatizo na watu, *21st Century* kinafanya kazi, orodha ninayo hapa nilisema nitaiwasilisha. Viwanda 61 vipo vinafanyakazi, lakini viwanda 18 ambavyo nimehangahika navyo mwaka mmoja vimeanza ku-*import machine*. Kiwanda cha Korosho Kibaha wame-*import machine* mpaka tumewawezesha kwenda kuzitoa, nilikwenda mpaka *customs* kuhakikisha mashine zinatoka, viwanda 18 vile vinafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna viwanda ambavyo hazifanyi kazi, utaratibu wa vile viwanda kuvitoa ni kwamba, hii ni nchi ya sheria, mimi namuandikia *TR*, *TR* anamuandikia *AG* na *AG* anampa *TR* na *TR* ina *issue notice*. Katika mkataba ule, imeandikwa kwamba majadiliano ya sisi kupeana *notice* siyo *public*. Kwa hiyo, kuna viwanda niwaeleze taratibu na msiwaambie watu vimeshapewa *notice* lakini hawawezi kuja hapa kutangaza, ndiyo utaratibu wa kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnaposema tuwe na utalawa bora ndiyo utawala bora wenyewe, Mimi Mwijage nikikamata kiwanda nitakifanyaje? Lakini kuna viwanda vingine vinatafuta waendeshaji, *Mwanza Tanneries* kinatafuta wawekezaji kiko pale hakijawahi kubinafsishwa, kiwanda cha *Triples S* kinatafuta mwekezaji. Kwahiyo, vipo ndyo kazi nnayofanya kutafuta wawekezaji. Nitafute mwekezaji wa *Mwanza Tanneries*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge naomba shilingi yangu airudishe, viwanda 61 vinafanya kazi, viwanda 18 na wenye navyo wanajulikana, mojawapo ya viwanda 18 ambavyo vimefufuka ni pamoja ni Moprocco. Katika viwanda hivi mnavyovisema, vingine tumeipa Mifuko ya Hifadhi. Mifuko yetu ya Hifadhi tumeipa viwanda iendeshe. Sasa Mifuko ya Hifadhi ni ya kwetu ndiyo wanapaswa wafanye hizo mnazoziiita *RND* ili kusudi pesa za wananchi zisizame. Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Koshuma hiyo ndiyo taarifa ya viwanda. Viwanda vyenu vinafanya kazi 61 na 18 nimevifufua, nimewaahidi nakwenda kwenye mamlaka



*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

inayohusika, mimi siwezi kufuta kiwanda mpaka Baraza la Mawaziri liniruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kiwanda sasa kimebadilisha hakitatengeneza nguo kitakamua mahindi kupata *starch* badala ya ku-*import starch* kutoka nje kitatengeneza *starch* kutoka kwenye mahindi *tu-consume* mahindi, lakini kitakamua mafuta ya kula kutoka kwenye mahidi, kazi zinaendelea yote hayo mimi nafuata taratibu za mamlaka ambayo ni *cabinet*.

Mheshimiwa Mbunge ningeomba kwa heshima na taadhima unrudishie hii shilingi ndiko uliko mshahara wa shangazi zako. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Koshuma baada ya maelezo ya Serikali hayo sahihi bado unaendelea nayo?

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kwa sababu moja. Viwanda 62 ambavyo vinafanya kazi kama nilivyotangulia kusema vinafanya kazi kwa kusuasua kwa sababu vinatumia teknolojia ya zamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliweka pesa nyingi sana katika viwanda hivi, tukaviuza kwa bei rahisi watu hawa wametupotezea uchumi wa Tanzania na unazidi kudorora naomba Wabunge wazidi kuishauri Serikali namna bora ya kufanya ili viwanda hivi viweze kutumiwa.

**MWENYEKITI:** Usihutubie, nenda *straight* kutoa hoja yako.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Natoa hoja Wabunge waweze kujadili ili kuishauri Serikali.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono, tunachukua majina, Mheshimiwa Flatei, Mheshimiwa Ulega, Mheshimiwa Getere, Mheshimiwa Dkt. Ishengoma,

Mheshimiwa Omary. Waheshimiwa Wabunge tutende haki, haiwezekani tukajiorodhesha wote, mimi nitachukua upande huu na huu. *Already* kabla ya serikali huku tunao watano. Mheshimiwa Maftaha na Mheshimiwa Jaku. Sasa tuanze na Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti nikushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba ukiangalia viwanda ambavyo vipo katika *list* ya kitabu hili nimekisoma, viwanda vingi vya Serikali ni vya zamani kwa kweli havifanyikazi. Mheshimiwa Waziri angeeleza nia yake ya kutosha kabisa ukitaka kuonesha nia njema, onesho katika yale yaliyopita vingapi unavyo sasa na umefufua vingapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, viwanda vile vya zamani akina *Mwatex*, Urafiki, viwanda vya viatu kama Bora na kadhalika hata *General Tyre*, viwanda vile vyote havipo. Sasa ukitaka kuongeza viwanda ni lazima uoneshe kwanza unafufua vile vya kwako. Kwa hiyo, naona Serikali inapaswa kuja na mbinu mbadala ili kushawishi kwamba tumefufua vya kwetu hivi hapa na vinafanya kazi ili watu wengine waweze kuwekeza katika viwanda hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kiteto vizuri sana na ninamuomba ashikilie hiyo shilingi mpaka mwisho ili Waziri ajue kwamba Watanzania wana-*pinch* na jambo hili. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea Mheshimiwa Jaku.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jina jingine unajiita reli ninakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ninamshukuru sana Waziri aliogelea sana mpaka kima kirefu cha maji hapa kuhusu kulinda viwanda. Hoja yangu tunalinda viwanda vya Tanzania, ninakata kujua kiwanda cha Mahonda cha Sukari hakipo Tanzania? Tumetimiza miaka 54 ya Muungano wetu

na kile kiwanda kimefanya kazi kubwa sana kufufuliwa na wao wako katika kuhangaika kutafuta biashara. Sababu gani ya msingi ikiwa tunalinda viwanda vya Tanzania na najua Zanzibar ipo Tanzania, ni sababu gani Waziri wale wasiweze kuuza mali yao na ukizingatia tupo katika Muungano wetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jaku unafahamu *sometimes* tunavumiliana tu, lakini hoja ya Mheshimiwa Koshuma ni viwanda ambavyo vilibinafshwa ambavyo havifanyikazi, sasa hivi Mahonda inafanya kazi. Tutafika kwenye hoja hiyo unayoitaka wewe, naamini tutafika tu. Naendelea Mheshimiwa Getere Boniphace.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahasante na naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kiteto Koshuma na nimwombe Waziri wa Viwanda unajua yapo maneno yanayozungumzwa na watu walioenda huko mbinguni, moja ilizungumzwa na Mwalimu alisema unaweza ukawadanganya watu kwa muda lakini huwezi kuwadanganya kwa muda wote. *(Makofi)*

Sasa Waziri amekuwa na maneno matamu mengi lakini kadri siku zinavyoenda za kwake zinahesabika. Nasema ni vizuri akagundua haya maneno ya Wabunge yanavyoenda, ukweli ni kwamba ufufuaji wa viwanda vya zamani kasi yake ni ndogo sana. Nikitolea mfano, Kanda ya Ziwa kule Musoma kuna *Mutex*, kuna *Mwatex*, kuna *Ginnery* za Guramba, kuna *Ginnery* ya Ushasi, kuna *Ginnery* ya Mgango, tumezungumza hapa Bungeni hapa muda mrefu sana kwenda kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwamba kuna hoja ya kujua kwamba kitu gani kinafanyika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja ya

Mheshimiwa Koshuma kwa sababu Mheshimiwa Waziri ndiyo unafanya kazi nzuri lakini Morogoro ni Mkoa ambao ulikuwa na viwanda vingi ni kweli umefufua vichache, lakini bado tuna viwanda vingi kama vya Magunia ambapo magunia yanatakiwa kwa wakulima. Tuna viwanda vya ngozi ambapo tunataka viatu vya Tanzania, kwa kweli naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Koshuma naomba Mheshimiwa Waziri ukaze buti, kusudi na Serikali iwe na mkakati wa wazi wa kufufua viwanda na Morogoro irudi tena kuwa Morogoro ya viwanda. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Maftaha.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kiteto Koshuma.

Suala hili la kuuzwa kwa viwanda kulienda sambamba na uuzaji wa Mashirika mengine ya Umma ambayo kwa kiasi kikubwa hayafanyi kazi ambayo tulikusudia na mimi naungana na Waheshimiwa Wabunge kwa sababu viwanda hivi vilikuwa vinatoa ajira sana, kule kwetu kwa mfano Mtwara tulikuwa na Viwanda vya Korosho, Viwanda vya *TANITA* ambavyo vilikuwa vinatoa ajira sana kwa wananchi wa Mikoa ya Kusini, lakini viwanda vile vyote viliuzwa, vingine vilikufa, lakini mkakati wa Serikali ni upi hasa wa kufufua viwanda hivi ambavyo vinatoa ajira kubwa kwa wananchi wetu wa Tanzania. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Omary Mgumba.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi hii. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kiteto Koshuma kwa sababu sijaona *commitment* ya Serikali, haya makampuni binafsi yaliyopewa viwanda hivi yaliingia mikataba kwa miaka 20 wamekiuka mikataba hiyo, wengine wamegeuza maghala, wengine wameuza *machine stools* kama *scraper*, wengine wametumia viwanda vyetu kwenda kukopea na kufanya biashara tofauti na ile walioyokuwa nayo. Lakini Serikali miaka

yote 20 hawajachukua jukumu lolote pamoja na hawa watu kukiuka mikataba inavyosema. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano upo hai kama alivyosema imewapa sasa Mifuko ya Jamii, kwa mfano ya *NSSF* umetaka kufufua kiwanda cha kuchakata mazao ya mahindi na mpunga pale Mwanza, umeshatoa zaidi ya bilioni 8.9 tangu mwaka jana mpaka leo Bodi ya Mazao Mchanganyiko haijanunua hivyo. Tunaitaka Serikali ituambie ina mkakati gani wa kuwanyang'anya hawa viwanda na kuwapa watu wengine badala ya kubembelezana? Ninashukuru. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Ulega.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri na ningemuomba kwa heshima kubwa na taadhima rafiki yangu Mheshimiwa Kiteto Koshuma baadae amrudishie Mheshimiwa Waziri shilingi yake ili aweze kwenda kuhakikisha anaendelea kuhamasisha shughuli hii ya ujenzi wa viwanda katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili la kuhakikisha kwamba tunalinda viwanda vyetu vya ndani ni jambo kubwa sana, Mheshimiwa Waziri ameeleza juu ya hatua ambazo yeye Mheshimiwa Kiteto ametaka kuzijua, Serikali inafanya hatua gani.

Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba unafanyika uthamini, kwa mfano pale Mwanza kuna kiwanda kile cha ngozi cha *Mwanza Tanneries*, Shinyanga kuna Kiwanda cha *Triple S*, Mbeya kuna *Tanganyika Packers* ya zamani na kwingineko. Tayari *TR* anafanya kazi yake, siyo kazi ndogo ya kusema kwamba leo na kesho itakuwa tayari. Ni kazi ambayo inazungumzia mali tena ni mali kubwa. Kwa hivyo, lazima tuwape nafasi ili miradi inapokuja kutangazwa tena tisiingie mkenge ule ule ambao mwanzo tulishaingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ni muhimu sana

Waheshimiwa Wabunge watuunge mkono ili lile wanalolisema tusiendeleo kuhakikisha kwamba tunaagiza maziwa, tusiendeleo kuhakikisha nyama.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

**WAZIRI WA VIWANDA BIASHARANA UWEKEZAJI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie tena kumuomba Mheshimiwa Koshuma, naiona *concern* ya Wabunge, kinachotakiwa hapa ni kasi, najua *concern* ya watu wa Morogoro lakini kila kiwanda kina maelezo yake. Watu wa Morogoro wanazungumzia kuhusu *Ceramic*, *Ceramic* alipewa mtu, yule mtu akakopea alipokopea *TIB* akaenda Mahakamani, mali ikakamatwa ikauzwa *by stripping*, huyo aliyenunua jengo ndiyo tunamzungumza, aliyenunua mashine akaondoka nazo kwenda Nigeria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyozungumza Shangazi Lulida hii tunazungumza miaka 20 iliyopita ambapo tulifanya *privatization*, sasa kinachofanyika ni kwamba tuna tafuta mtu wa kuweza kuwekeza mle. Washemiwa Wabunge mlilikubaliana na Mheshimiwa Koshuma pamoja na kuvichukua vile viwanda nafanya zoezi la nani aviendeshe hata hao wamiliki wengine waliouziwa walishakufa. Unakuta kesi ziko mahakamani, kuna kesi nimezitoa mahakamani lakini unakuta mama mjane anakuambia usininyang'anye kiwanda lakini hawezi kukiendesha na kwenda kumtafuta mbia ambaye mimi simju.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema viko viwanda ambavyo kwa sheria siwezi kuvitaja, viwanda hivyo *Treasurer Registrar* baada ya ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali wameshapewa *notice* na nyaraka hizo naweza nisiseme lakini hili *file* nitalipeleka kwenye Ofisi za Bunge ili kila mtu aende kuangalia kiwanda kinachomsumbua aweze kukieleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Koshuma unisaidie kama una mwekezaji unamjua *Mwanza Tanneries*

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

tumemaliza tathmini, *Triple S* tumemaliza tathmini, nitafutie mwekezaji nitahakikisha viwanda vyote nafuata taratibu ili kusudi viweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapomalizia nina majukumu matatu, niliagizwa kuhakikisha viwanda vyote vinafanya kazi, niliagizwa viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo vilikufa vifanye kazi na niliagizwa kuhamasisha viwanda vipya. Kwa hiyo, nitaendelea kuhamasisha viwanda vipya na hivi mniruhusu nivifufue na wafanyabiashara vifanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo yangu mojawapo ni kwamba tulipovibinafsisha tulianzisha soko huria, likawa soko holela, huwezi kushindanisha *infant industry* na *matured industry*, mmeniruhusu kwamba nikavilinde viwanda, nakwenda kuvilinda. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Koshuma kwa kifupi tu.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama itakupendeza ninashauri kwamba Kamati ya Viwanda na Biashara ya Bunge iende ikavitembelee vile viwanda 62 ambavyo Mheshimiwa Waziri anasema kwamba vinafanya kazi ili Kamati iweze kuja na tathmini iweze kuishauri vizuri Serikali namna gani viwanda hivi vinaweza vikafanya kazi kwa sababu Mheshimiwa Waziri amekuwa akishauriwa na Kamati. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa umeanza kuhutubia hapana, hapana! Hatuendi hivyo, kama hurudishi shilingi tu iamue.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini busara zitakuongoza kwamba ninajitahidi kuishauri Serikali namna ya kufanya kwamba Kamati ya Bunge iende ikavitembelee vile viwanda, kwa sababu Mheshimiwa Waziri amekuwa akizungusha Kamati ya Bunge anawapeleka kwenda kufanya ziara kwenye...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Koshuma twende na utaratibu tu, rejsha shilingi, twende mbele.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo hayo ambayo nimeyatoa ninaamini kwamba Serikali imesikia na itaifanya kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa. Nakushukuru sana kwa busara yako. Tunaendelea na Mheshimiwa Mashimba Ndaki.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaenda haraka kwa sababu ya muda wetu. Suala la kulinda viwanda vyetu ambavyo Serikali ya Awamu ya Tano imeamua ili tuende kwenye uchumi wa kati wa viwanda ni la muhimu sana. Lakini ukijaribu kuangalia na hata kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, sijaona kabisa mkakati mahsusi wa kulinda viwanda vyetu ili viweze kukua na hatimaye viweze kujitegemea na kushindana na bidhaa zingine zinazotoka kwenye nchi za wenzetu walioanza viwanda muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni tatizo kubwa kwa sababu tusipokuwa na mkakati ambao ni wazi, mkakati ambao ni shirikishi, mkakati ambao unajulikana kwa watu wanaowekeza kwenye viwanda, bado tutarudi kwenye tatizo lile lile ambalo tulikuwa nalo miaka ya 1970 viwanda vilipoanza, lakini kwa sababu ya matatizo ya kutokuvilinda na kutokuwa wazi juu ya ulinzi wake vilikufa na leo tunaanza kung'anga'nia ni namna gani vitarudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, nataka maelezo ya Serikali juu ya mkakati mahsusi wa kulinda viwanda vyetu ili tuweze kulinda ajira, tuweze kulinda bidhaa zetu nasi tuweze kuzalisha zaidi na kuuza nje zaidi. Nisipopata maelezo ya kutosha juu ya mkakati huo nakusudia kuchukua shilingi.

**MWENYEKITI:** Ahasante sana. Mheshimiwa Waziri anataka mkakati wa Serikali kulinda viwanda vya ndani.



**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali upo, imeandikwa kwenye kurasa za kwanza wakati nazungumzia ujenzi wa uchumi wa viwanda nilipozungumza miundombinu wezeshi, mojawapo ya sababu za viwanda kufa ni kukosa umeme. Mheshimiwa Waziri wa Nishati ameelezea, sababu nyingine ni miundombinu mibovu, tunatengeneza barabara ili kusudi *cost of production* na *operational cost* ziweze kupungua, lakini tunazungumza namna ya kutumia *tariffs* kulinda viwanda vyetu *against* bidhaa za kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna kampeni nitaanzisha ya kipende chako, ipende Tanzania, nunua bidhaa zako ndiyo falsafa ambayo itaweza kulinda viwanda vyetu. Mheshimiwa Ndaki naomba unisaide unipe shilingi kusudi nikatekeleze niliyoyapanga. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ndaki.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua maneno na vitendo ni tofauti sana, kama tutaenda hivyo sio sawasawa. Wenye viwanda vya pamba wanalalamika...

**MWENYEKITI:** Hapana Mheshimiwa Ndaki.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mimi natoa hoja, Bunge lisaidie kujadili suala hili halafu tupate uamuzi.

**MWENYEKII:** Hoja imeungwa mkono, sawa. Nachukua majina ya wanaotaka kuchangia, Mheshimiwa Kiswaga, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mheshimiwa Shangazi. Sasa nachukua Serikali, Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Jitu Soni na Mheshimiwa Bulembo. Tunaanza na Mheshimiwa Bulembo.

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuunga mkono hoja ya Serikali na nimuombe rafiki yangu suala hili liko wazi. Waziri amejieleza vya kutosha, ni kweli anaenda kufufua na anakwambia anatafuta wabia, wabia wasipopatikana itakuwaje? Hawezi

kutenda yeye na Serikali ni watu wengi wanaokutana kuamua jambo. Tumpe nafasi, tumepitishie bajeti yake, tutampata kwa maswali na majibu. Kwa hiyo, kaka yangu nakuheshimu sana ndugu yangu wa Maswa, nakuomba sana, tumuunge mkono, tumpe nafasi ili tuendelee kutenda. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nishauri tu maana hili jambo nimeskiliza maelezo ya Serikali na Mheshimiwa Ndaki nimeona iko sehemu ndogo tu ambayo tunatakiwa tuiweke sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, nafikiri kubwa zaidi linalozungumziwa hapa ni mpango mkakati wa kuona jinsi gani tunalinda viwanda vyetu vya ndani, hakuna mbwembwe nyingine hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako nikupe mfano mmoja tu, Kiwanda kile Viuadudu pale Kibaha hakifanyi kazi vizuri kwa sababu hakuna mkakati wa kibiashara wa kuwezesha bidhaa ile inayotengenezwa viwandani iuzike. Mheshimiwa Rais juzi amekwenda pale, ametoa maagizo Halmashauri zote ziende zikachukue, lakini hakuna mpango mkakati wa kutoka ndani ya Wizara au ndani ya kiwanda kile cha jinsi gani zile *product* zinakwenda kuwafikia walengwa ambao ni wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani Mheshimiwa Rais ikawa shughuli yake kwenda sehemu na kutoa maagizo, wakati mwingine tuwe wepesi wa kutengeneza mikakati ya kibiashara ili tuweze kuuza bidhaa zetu za ndani, ndiyo tutafanikiwa kulinda viwanda vyetu na siyo kwa njia nyingine. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Kiswaga.

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba tu nishauri kwamba ili tuvilinde

viwanda vyetu ni vizuri Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Fedha wakae kwa pamoja watazame namna ambavyo wanatoza kodi bidhaa inayotoka nje, kwa sababu bidhaa ianyotoka nje ikitozwa kodi kidogo viwanda vyetu haviwezi ku-*compete* na bidhaa hiyo iliyotoka nje. Tunapolinda viwanda tutawawezesha wakulima wetu kuzalisha vizuri, wale wakulima wa pamba, mbegu pamoja na wale wakulima wa miwa ili sukari iweze kutengenezwa vizuri zaidi. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Shangazi kwa kifupi tu.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni kweli nami niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Mashimba kwamba tunataka Serikali iwe na *incentives* kwa viwanda vya ndani, ivilinde ili viweze kushindana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua hata *cost of production* ni kubwa lakini tunataka Serikali itazame kwa jicho la kutoa *incentive* kwa viwanda vya ndani ili kuvijengea uwezo wa kushindana na viwanda vingine, lakini pia na suala zima la kodi liangaliwe kwa makini sana ili bidhaa za kutoka nje zitozwe kodi kubwa kulinda viwanda vya ndani. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jitu Soni kwa kifupi tu.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi namuunga mkono ndugu yangu Mheshimiwa Ndaki kwa sababu tumeona na hapa wakati Waziri anatoa maelezo hapo mwishoni alizungumza suala la *blueprint* kwenye masuala ya *regulatory authority*, lakini *blueprint* hiyo kama ipo katika hizi Wizara ambazo tumepitisha ambazo kuna *regulatory bodies* si tungeona mmeitengea angalau bajeti? Sasa kama haijatengewa bajeti mkaja na hiyo sheria kwenye huo mwaka mpya ambao mnasema mtatekeleza, bajeti itajiendeshaje? Kwa hiyo, bado nakuwa na wasiwasi kwamba hatuna mkakati wa uhakika wa kulinda viwanda

vya ndani ni vizuri tujipange, bado tuna muda tukija kwenye *Finance Bill* ifanyiwe kazi. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa kifupi wape matumaini Wabunge hawa.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namsihi sana Mheshimiwa Ndaki muachie shilingi ndugu yangu huyu na nikuhakikishie kwamba wakati wa Bajeti Kuu ya Serikali, Serikali itaeleza hatua mahsusi za kikodi kwenda kulinda viwanda vyetu humu ndani ili tuende mbele. (Makofi)

Vilevile kwa upande wa hizi tozo na *regulatory forms* tuna hatua ambazo tunachukua kupunguza adha hasa kwa viwanda vyetu vya ndani, pia kuna maelekezo mahsusi ili kuwahakikishia bidhaa za ndani zinapata soko hususan kutoka kwenye sekta ya umma. Mheshimiwa Ndaki tafadhali. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ndaki kwa kifupi tu hiyo ndiyo *commitment* ya Serikali, bajeti ni hii tunakuja keshokutwa.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaheshimu sana Viongozi wa Serikali lakini pia na Serikali yenyewe. Nakubali kurudisha lakini ni vizuri sana tusifanye vitu kwa matukio. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisikiliza maelezo mazuri kabisa ambayo Mheshimiwa Waziri alikuwa anayatoa juu ya suala la Mchuchuma na Liganga utaona ni namna gani jambo hili limeigharimu sana nchi yetu hasa zaidi kwenye suala la pesa za kigeni.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakusudia kushika shilingi kama hatutapata maelezo ya kina kwa sababu ukiangalia hata kwenye kitabu chake Mheshimiwa Waziri pamoja na maelezo marefu aliyoyatumia wakati ule, suala hili limeandikwa kwa mistari 12 tu, wakati huo huo tunasema hili ni suala la viwanda mama na miradi ya kielelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaposema suala mama na miradi ya kielelezo lakini tukumbuke shida wanazozipata wakazi wa kuanzia Mtwara mpaka kufika huko Liganga. Kwa hiyo tunaomba Serikali itupe maelezo watu wale wanatakiwa walipwe fidia na vitu vingine hapa katikati. Kwa hiyo, tunaomba Serikali itupe maelezo vinginevyo nitashika shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, toa *assurance* kabla sijaenda kwenye *guillotine*.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawahakikishia ndugu zangu wa Njombe, Mtwara, Ruvuma kote kwamba mradi wa Mchuchuma na Liganga upo na ni ukweli kabisa. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaingia katika *guillotine*, zege halilali.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 – *Finance and Accounts* ... .. Sh. 356,844,589/=

Kif. 1003 – *Policy and Planning* ... .. Sh. 1,327,146,130/=

Kif. 1004 – *Gvt. Comm. Unit* ... .. Sh.137, 177,684/=

Kif. 1005 – *Internal Audit Unit* ... .. Sh. 220,808,825/=

Kif. 1006 – *Legal Services Unit* ... .. Sh. 130,349,184/=

Kif. 1007 – *Mgt Information System*... .. Sh. 268,722,549/=

Kif. 1008 – *Procurement Mgt. Unit* ... .. Sh. 217,504,036/=

Kif. 2001 – *Industry* ... .. Sh. 4,988,501,885/=

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Kif. 2002 – <i>Small &amp; Medium Enterprises Division...</i>	Sh. 4,940,011,670/=
Kif. 3001 – <i>Commerce</i>	Sh. 0
Kif. 4002 – <i>Commodity Market Dvt</i>	Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 60 – Biashara na Uwekezaji**

Kif. 3001 – <i>Commerce Division</i>	Sh. 1,213,045,437/=
Kif. 3002 – <i>Investment Division</i>	Sh. 1,649,542,013/=
Kif. 4002 – <i>Commodity Market Development Division.....</i>	Sh. 16,184,558,198/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 44 – Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji**

Kif. 1001 – <i>Administration &amp; HR Mgt.</i>	Sh. 700,000,000/=
Kif. 1003 – <i>Policy &amp; Planning</i>	Sh. 2,874,525,000/=
Kif. 2001 – <i>Industry</i>	Sh. 61,115,918,000/=
Kif. 2002 – <i>Small and Medium Enterprises Division...</i>	Sh. 28,334,082,000/=
Kif. 4002 – <i>Commodity Market Development</i>	Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 60 – Biashara na Uwekezaji**

Kif. 4002 – <i>Commodity Market Development Division..</i>	Sh. 7,000,000,000/=
--	---------------------

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

**NDG. BAKARI KISHOMA - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

*(Bunge lllirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja taarifa.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, Kanuni ya 104(3)(a) na (b) kwamba Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.  
*(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja lilitolewa lamuliwe)  
(Hoja lliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2018/2019 –  
Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji  
yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, natamka rasmi kwamba Bunge limekubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Tumefika mwisho wa hoja hii. Ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kazi nzuri mliyoifanya tangu jana. Kwa namna ya pekee nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji na Naibu wake, lakini na nyuma yao, Katibu Mkuu na timu yote ya wataalam wa Wizara hii, mmetufikisha hapa vizuri. Mmesikia ushauri

wa Waheshimiwa Wabunge katika maeneo mbalimbali. Bunge limekubali kuwawezesha mkayafanye hayo mliyoomba kwa mwaka ujao wa fedha. Kilio cha wengi, utitiri wa tozo na kodi. Umetoa maelezo mazuri, tutayaona ndani ya Mkutano huu maana tunakuja kwenye Bajeti Kuu ya Serikali na kwenye *Finance Bill*.

Waheshimiwa Wabunge, wameomba sana kasi ya maamuzi ndani ya vyombo vya Serikali iende haraka kwa sababu ya uwekezaji. Pesa hizi zinatafutwa na wengine siyo Tanzania tu, tufanye hayo maamuzi kwa haraka na pale ambapo tunaona kuna mahitaji ya kufanya marekebisho ufanye *tuning* ya sheria, Bunge lipo, tusiogope! Ndiyo maana Serikali iko Bungeni. Tunataka tu-*facilitate* mambo yaende haraka. Kwa hiyo, hatuko mbali sana kufika mwaka 2025, lakini tunaenda vizuri, hongereni sana na naamini mtaenda kujipanga vizuri. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo mawili, kwanza kuna simu imekutwa kwenye *desk* la Waziri wa Nishati Mheshimiwa Dkt. Kalemani, bahati mbaya wamejaribu kuiwasha *battery* iko chini, kwa hiyo inawezekana ikawa ya Mheshimiwa Mbunge, lakini wajue kwamba tutaiacha kwa wasaidizi wa Katibu wa Bunge.

Tangazo la pili, Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba asubuhi hapa mnakumbuka nilitangaza semina mbili sasa kuna mabadiliko kidogo. Tangazo hili ni kwamba semina ya Wabunge wote kuhusu shughuli za Idara ya Usalama wa Taifa iliyokuwa ifanyike kesho sasa imeahirishwa hadi hapo itakapotangazwa tena. (*Makofi*)

Aidha, semina kuhusu mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja iliyopangwa kufanyika siku ya Jumapili tarehe 13 Mei, 2018 kuanzia saa tano asubuhi itaendelea kama iivyopangwa. Kwa hiyo, kesho utawala binafsi, lakini kesho kutwa semina hiyo itaendelea kuwepo, semina hiyo ya kwanza imeahirishwa tu hadi hapo tutakapojulishwa vinginevyo. (*Makofi*)



*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo niliyoletewa hapa sina la ziada.

Baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatatu, saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.15 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu  
Tarehe 14 Mei, 2018 Saa Tatu Asubuhi)*